# USAWIRI WA WAHUSIKA WA KIUME KATIKA RIWAYA ZA KISWAHILI ZILIZOANDIKWA NA WANAWAKE

**NA**

**OLIVIA KANWA**
**C82/27647/2013**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMIFU KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**MEI, 2022**

# UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mimi mwenyewe na halijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine.

Sahihi:.............................. Tarehe: 30/05/2022

**Olivia Kanwa -** C82/27647/2013

Idara ya Kiswahili

Tasnifu hii imetolewa kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa idhini yetu kama wasimamizi.

Sahihi:.............................. Tarehe: 30/5/2022

**Prof. Catherine Ndungo**

Idara ya Kiswahili

Sahihi:.............................. Tarehe: 30/5/2022

**Dkt. Richard. M Wafula**

Idara ya Kiswahili

## TABARUKU

Kazi hii naitabarukia dada yangu mpendwa Lidia Kanwa, kaka yangu Jordan Kanwa. Watoto wangu wapendwa Peace na Samwel.

## SHUKRANI

Kwanza ninamshukuru mwenyezi Mungu kwa kunijalia neema ya kukamilisha kazi hii. Nawashukuru pia wasimamizi wangu Profesa Catherine Ndungo na Dkt. Richard. M. Wafula kwa kutenga muda wao ili wanielekeze katika kila hatua na hivyo nikaimaliza kazi hii. Mola awabariki sana. Aidha,namshukuru mwanafunzi mwenzangu Charles Nyanduru Magati, tulisoma pamoja shahada ya uzamifu, kuombeana na kutiana moyo katika safari hii ndefu ya kuisaka shahada ya uzamifu. Nawashukuru pia wazazi wangu wapendwa Reina Francis Musimba na Petro Kanwa Katura, hata kama mmeishatoweka katika uso huu wa dunia, naamini mmekuwa mkiniombea huko mliko kwani mliithamini sana elimu, enzi za uhai wenu. Mungu awajalie pumziko la milele. Aidha,namshukuru kwa dhati dada yangu Lidia Kanwa kwa kunitia moyo na kunitimizia mahitaji ya kifedha wakati nilipopungukiwa. Mwisho nawashukuru wanangu Peace na Samwel kwa maombi na uvumilivu mwingi wakati wa masomo yangu.

# YALIYOMO

**UNGAMO** ..... ii
**TABARUKU** ..... iii
**SHUKRANI** ..... iv
**YALIYOMO** ..... v
**UFAFANUZI WA DHANA MUHIMU** ..... ix
**VIFUPISHO** ..... xi
**IKISIRI** ..... xii
**ABSTRACT** ..... xiii
**SURA YA KWANZA** ..... 1
**UTANGULIZI WA UTAFITI** ..... 1
1.0 Usuli wa Mada ..... 1
1.1 Suala la Utafiti ..... 6
1.2 Malengo ya Utafiti ..... 7
1.3 Maswali ya Utafiti ..... 7
1.4 Sababu za Kuchagua Mada ..... 7
1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti ..... 10
1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ..... 11
1.7 Misingi ya Nadharia ..... 35
1.7.1 Nadharia ya ujifunzaji wa Kijamii ..... 37
1.7.2 Nadharia ya Mwanaume Mpya ..... 39
1.7.3 Nadharia ya Uhalisia ..... 42
1.8 Mbinu za Utafiti ..... 49
1.8.1 Mahali pa Utafiti ..... 50
1.8.2 Muundo wa Utafiti ..... 51
1.8.3 Uteuzi wa Sampuli ..... 51

1.8.4 Ukusanyaji wa Data ....................................................................54

1.8.5 Uchanganuzi wa Data ..................................................................55

1.8.6 Uaminikaji na Utegemewaji wa Utafiti ...........................................56

1.8.7 Uwasilishaji wa Matokeo...............................................................58

1.8.8 Maadili ya Utafiti..........................................................................58

1.8.9 Hitimisho.....................................................................................59

**SURA YA PILI..................................................................................60**

**DHAMIRA ZILIZOWASILISHWA KUPITIA KWA WAHUSIKA WA KIUME..........................................................................................60**

2.0 Utangulizi......................................................................................60

2.1 Dhana ya Dhamira na Wahusika.....................................................60

2.2 Dhamira katika Riwaya za Kipimo cha Mizani, Hiba ya Wivu, Dago wa Munje na Tumaini..........................................................................61

2.2.1 Dhana ya ndoa katika Riwaya Teule ............................................61

2.2.2 Uchapakazi au Bidii ya Kazi katika Riwaya Teule ..........................72

2.2.3 Maadili ya Kazi katika Riwaya Teule.............................................82

2.2.4 Urafiki wa Kweli katika Riwaya Teule ..........................................91

2.2.5 Ukosefu wa Haki katika Riwaya Teule .........................................100

2.2.6 Umuhimu wa Elimu katika Riwaya Teule.....................................110

2.2.7 Malezi katika Riwaya Teule ........................................................116

2.2.8 Migogoro katika Riwaya Teule ....................................................123

2.3 Hitimisho.....................................................................................142

**SURA YA TATU...............................................................................144**

**TASWIRA ZINAZOTUMIWA KUWASAWIRI WAHUSIKA WA KIUME KATIKA RIWAYA TEULE.........................................................144**

3.0 Utangulizi....................................................................................................144

3.1 Taswira ya Mwanaume katika Riwaya ya *Kipimo Cha Mizani*..............146

3.2 Taswira ya Mwanaume katika Riwaya ya *Dago Wa Munje*....................163

3.3 Taswira ya Mwanaume katika Riwaya ya *Hiba ya Wivu* ........................175

3.4 Taswira ya Mwanaume katika Riwaya ya *Tumaini*................................197

3.5 Hitimisho.......................................................................................................212

**SURA YA NNE .............................................................................................214**

**MITAZAMO INAYOIBULIWA NA WAHUSIKA WA KIUME KATIKA RIWAYA TEULE..................................................................214**

4.0 Utangulizi....................................................................................................214

4.1 Mtazamo katika *Kipimo Cha Mizani* ......................................................215

4.2 Mtazamo Katika Riwaya ya *Hiba ya Wivu*..............................................230

4.3 Mtazamo Katika Riwaya ya *Tumaini* .....................................................240

4.4 Mtazamo Katika Riwaya ya *Dago Wa Munje* ........................................251

4.5 Hitimisho.......................................................................................................260

**SURA YA TANO ............................................................................................262**

**ULINGANISHI NA ULINGANUO WA WAANDISHI WA KIKE WA KENYA NA TANZANIA .............................................................262**

5.0 Utangulizi....................................................................................................262

5.1 Kulingana kwa waandishi wanawake wa Kenya na Tanzania................262

5.1.1 Kumsifu Mwanaume..............................................................................263

5.1.2 Kumdunisha Mwanaume .......................................................................272

5.1.3 Mfanano wa Mwanaume katika Kukabiliana na Mitihani ya Maisha ..283

5.2 Kutofautiana kwa Waandishi Wanawake wa Kenya na Tanzania..........286

5.2.1 Kukabiliana na Mitihani ya Maisha.....................................................286

5.2.2 Mtazamo wa Waandishi kuhusu Ushujaa wa Wahusika wa Kiume.....287

5.3 Hitimisho........................................................................................290

**SURA YA SITA........................................................................................292**

**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ..............................292**

6.0 Utangulizi........................................................................................292

6.1 Muhtasari ........................................................................................292

6.2 Matokeo ya Utafiti ..........................................................................294

6.3 Mchango kwa Utafiti ......................................................................298

6.4 Changamoto ....................................................................................302

6.5 Hitimisho.........................................................................................303

6.6 Mapendekezo ..................................................................................304

**MAREJELEO ..........................................................................................307**

## UFAFANUZI WA DHANA MUHIMU

**Chanya:** Inayopendeza, inayofaa, kinyume cha hasi, -enye kuleta matumaini.

**Dhamira:** Ni suala linalokuzwa na kuendelezwa na msuko pamoja na mahusiano ya wahusika mbalimbali katika kazi ya fasihi.(Wamitila 2003b)

**Hasi:** Isiyofaa, iliyokosa matumaini na isiyopendeza.

**Itikadi:** Mfumo wa mawazo na maadili yaliyopendekezwa na jamii ili kuwaongoza wanajamii katika hali zao za kisaikolojia na kijamii (Eagleton, 1986).

**Jinsia:** Ni hali ya kimaumbile ya mtu kuwa mwanamke au mwanamume.

**Mafunzo ya kijamii:** Huu ni uendelezaji wa kijamii. Ni utaratibu ambao hutumiwa ili watu wajifunze tabia na mitazamo inayoafiki majukumu yao katika jamii. Ni utaratibu wa maingiliano ambao binadamu hupata thamani, mitazamo, ujuzi na maarifa ya jamii yao. Mafunzo ya jamii huhusu kwanza, kujifunza majukumu haya ya kijamii na pili, kutiwa ari ya kuyatekeleza (Merton, 1985).

Maudhui: ni yaliyomo au jumla ya masuala yanayozungumziwa katika kazi ya kifasihi yoyote. Maudhu yanaibuka katika uendelezaji na ukuzaji wa dhamira ya riwaya fualni. (Wamitila 2003)

**Mtazamo au Mitazamo**: Jinsi ya kuangalia, namna ya kufikiria na kazingatia. Ni mawazo ya mtu juu ya suala fulani.

**Uana:** Ni utaratibu wa kijamii unaotumiwa kuimarisha tofauti za majukumu ya kijamii yaliyotengewa wanaume na wanawake katika jamii zao.

**Ubabedume:** Hutumiwa kueleza mfumo wa jamii ambao unamtukuza mwanamume huku ukimdhalilisha au kumdunisha mwanamke. Ni mfumo unaomfanya mwanamume msingi mkuu wa kaida kuu ya jamii. Mfumo wa ubabedume huzichukulia amali za kiume na mawazo yao kama kaida ya kufuatwa katika jamii nzima (Wamitila, 2003).

**Unyanyasaji:** Ni aina mbalimbali za maonevu ya kimwili, kihisia na kimawazo yanayotendewa binadamu yeyote katika jamii. Maonevu haya yanaweza kujitokeza katika hali tofauti kama kupigwa, kutukanwa, kunyimwa chakula miongoni mwa mengine ambayo humnyima anayedhulumiwa haki za kibinadamu na hudidimiza hashima yake kama mwanajamii.

**Usawiri:** Uumbaji wa wahusika/mhusika, kuchora kitu au jambo akilini mwa msomaji wa kazi. Kitendo cha kumpa mhusika au wahusika sifa katika kazi.

**Wahusika**: Viumbe wa kifasihi wanaoumbwa na mwandishi wa kazi ya fasihi ili wawe wasemaji wake katika kuufikisha ujumbe kwa hadhira lengwa.

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| K.h.j | - | kama hapo juu |
| SUZA | - | State University of Zanzibar |
| TUKI | - | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| UDOM | - | University of Dodoma |
| UDSM | - | University of Dar es Salaam |
| Uk. | - | Ukurasa |

# IKISIRI

Utafiti huu ulishughulikia usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake. Utafiti umechunguza kazi za waandishi wa kike wa Kenya na wa Tanzania kwa kutumia mkabala linganishi. Malengo manne ya utafiti huu ni: kubainisha dhamira zinazowasilishwa na wahusika wa kiume, kuchanganua taswira zinazotumiwa na waandishi kuwasawiri wahusika wa kiume, kujadili mitazamo inayoibuliwa na wahusika wa kiume katika riwaya teule na kulinganisha na kulinganua waandishi wakike wa Kenya na Tanzania katika usawiri wao wa wahusika wa kiume. Riwaya mbili za waandishi wa kike wa Kenya ni *Tumaini* iliyoandikwa na Clara Momanyi, *Dago wa Munje* iliyoandikwa na Sheilla Ryanga na za kutoka Tanzania ni *Kipimo cha Mizani* ya Zainabu Burhani, *Hiba ya Wivu* ya Zainabu Mwanga zilihakikiwa kwa kufuata utaratibu. Sanjari na hilo, tasnifu hii imeonesha kuwa nadharia ya uhalisia, ujifunzaji wa kijamii (imejikita kwenye uana) na mwanaume mpya zimekuwa nadharia faafu zilizoongoza utafiti huu. Uhalisia umefafanuliwa kama msingi wa usawiri katika jamii kwa maana hutofautiana kulingana na hali na baina ya jamii moja na nyingine. Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii huona tabia kama kitendo ambacho mtu hujifunza kutoka katika mazingira ambayo ndiyo hupelekea umuhimu wa majukumu ya kiuana. Mwisho, utafiti ulitumia nadharia ya mwanaume mpya, nadharia inayojaribu kuelezea kwanini baadhi ya wanaume hukaa na wake zao kwa usawa bila tabia za mfumo dume ambazo huashiria kuwepo kwa taasubi ya kuumeni. Nadharia hizi tatu zilitumika kujibu sehemu mbalimbali za maswali ya utafiti. Mbinu za utafiti zilizotumika ni usomaji wa riwaya teule kwa kina na kuhakiki. Kutokana na uhakiki, wahusika wa kiume wamesawiriwa chanya na waandishi wanawake. Wachache walikuwa hasi. Wameonesha pande mbili za wahusika kwa kuwachora hasi na chanya. Utafiti huu umesaidia kuongeza maarifa katika eneo la kijinsia na tahakiki za kifasihi.

## ABSTRACT

The dissertation entitled "The Portrayal of Male Characters in Kiswahili Novels" written by women writers investigated female writers' works from Kenya and Tanzania through comparative approach. The objectives of this study were: to identify different themes presented by male characters in the selected novels, to describe imagery that is employed by novelists to portray male characters, to discuss the perceptions revealed by male characters in selected novels and to compare and contrast selected women novelists from Kenya and Tanzania. Two novels written by female writers from Kenya, *Tumaini* by Clara Momanyi and *Dago wa Munje* by Sheila Ryanga and two from Tanzania, *Kipimo cha Mizani* and *Hiba ya Wivu* by Zainabu Burhani and Zainabu Mwanga were analyzed respectively. Moreover this dissertation demonstrated that realism, social learning (gender based) and new manism proved to be viable theories that guided this study. Realism was constructed as a subjective portrayal of society. Reality varied from situation to situation and from one society to another. Social learning theory saw behavior as action which is learned from the environment and consequently influenced gender roles significantly. Finally, the study applied new manism, a theory which tried to explain why some men treat their women counterparts equally and without a chauvinistic attitude that characterizes the partriachal male. These three theories were used to respond to the various elements of the research questions. The research techniques which were used in this study were close reading of the primary text and content analysis. From the analysis, most male characters as portrayed by female characters were positive. A few were negative. They showed negative and positive sides of characters. This study has contributed significantly to knowledge in the area of gender and literary criticism.

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA UTAFITI

## 1.0 Usuli wa Mada

Stratton, (1994) anaeleza kuwa anapendelea kusoma kazi zilizoandikwa na wanawake kwa kuzilinganisha na za wanaume kutokana na historia ya fasihi iliyojikita katika kazi zilizoandikwa na wanaume. Kwa kujikita katika dhana ya uhakiki, alianza kutathmini mapokezi hasi ya kazi zilizoandikwa na wanawake wa Kiafrika na alitoa dhana ya uhakiki katika uandishi wa wanawake wa Kiafrika katika utamaduni wa kiuandishi wa Kiafrika. Ulianzishwa mjadala juu ya waandishi wanawake na wanaume wa Kiafrika katika mada ya utaifa na jinsia na ilichambuliwa kwa mapana. Anaendelea kueleza kuwa kazi zilizoandikwa na wanaume zilichukuliwa na jamii kwa jicho pevu na kumakinikiwa kwa upana. Wanaume kama Leopold Sedar Senghor, Okot P'Bitek, Nuruddin Farah, Mongo Beti, Wole Soyinka na Ngugi Wa Thiong'o waliwagawa wanawake katika makundi makuu mawili: wale walioegemea katika utamaduni kwa kulinganishwa na wale waliojikita katika historia.

Kazi hii imetusaidia kuelewa namna ambavyo wanawake wamekuwa wakigandamizwa na kubaguliwa katika nyanja mbalimbali ikiwemo taaluma. Imefafanua kwa kina jinsi ambavyo kazi zilizoandikwa na wanawake hazikupewa kipaumbele na hata kuthaminiwa. Japo kazi hii imejikita katika fasihi ya Kiingereza imetupa mwanga kuhusu masuala ya kiuana. Kazi hii imejikita kwenye baguzi mbalimbali zinazotokana na utamaduni dhidi ya

wanawake ambalo si lengo la utafiti wetu. Utafiti wetu unahusu usawiri wa wahusika wa kiume katika kazi zilizoandikwa na wanawake.

Stratton (k.h.j) anaendelea kueleza kazi za fasihi ya Kiafrika zimekuwa za kimaigizo zaidi badala ya kueleza maisha halisi ya Waafrika na ulimwengu wa Waafrika kwa ujumla wakati kipimo cha kazi ni ukweli unaowasilishwa na kazi hiyo. Anaendelea kutoa wazo la kupinga kazi zinazoandikwa na wanaume kuhusu wanawake. Akimrejelea Rita Felski ambapo alisisitiza kuwa si lazima kazi za fasihi zieleze mazuri juu ya wanawake au kuwapa uwezo wa hali ya juu bali ielezwe hali halisi. Anakubaliana na Chielo katika utunzi wa Achebe katika kueleza uzito na uzuri wa utamaduni wa Mwafrika. Stratton (k.h.j) amehakiki namna Achebe *katika Things Fall Apart* kuwa ni kazi mojawapo. Mfano, Ezinma kutekwa nyara inaonesha kuwa wanawake hawana uwezo wa kimadaraka ipasavyo. Hata Ekwefi kutoka kwa mumewe wa kwanza na kwenda kwa Okonkwo na akaendelea kupata kipigo, Inaonekana kuwa ni mwanamke wa kupigwa tu. Suala hili la kutafuta sababu ya kijinsia si kwa waandishi wanawake wala wanaume bali hawakuona kama ni tatizo katika jamii hiyo. Utamaduni huwabana wanawake katika minyororo ya tamaduni na kuwatenga na usasa. Walio katika historia huchukuliwa kama waandishi wa mlengo wa kushoto na hufikiriwa kuwaonea huruma watetea maslahi ya wanawake. Hii inaonesha jinsi unyanyasaji na ugandamizaji kwa wanawake lilivyoonekana ni jambo la kawaida.

Kazi hii imekuwa faafu kwa utafiti wetu maana imetupa maarifa ya kiuana na vipengele mbalimbali ambavyo mwana mke amekuwa akigandamizwa ingawa si lengo la utafiti wetu.

Kazi hii ya Stratton japo imejikita katika kazi zisizo za Kiswahili, imeonesha ni kwa vipi waandishi wa kiume wanavyowachora wanawake kwa mtazamo hasi zaidi kuliko chanya. Hii ni kutokana na jamii zilivyotawaliwa na ubabe dume. Kutokana na uibukaji wa wanaharakati wa kijinsia kulipelekea jamii kubadilika kwa kiasi fulani. Hivyo basi, msimamo huu wa Straton umepelekea kufanyika kwa utafiti huu ili kujadili namna waandishi wa kike wanavyowasawiri wahusika wa kiume katika riwaya wanazoziandika. Je, wanalipa kisasi au wanaandika kwa mtazamo mwingine? Hili limechunguzwa na utafiti huu.

Zulfiqar, (2016) anaeleza kuwa katika tamaduni za Kiafrika, wanawake hawakuonwa kama watendaji tu ila watoa elimu kwa kujikita katika fasihi simulizi inayoonesha umuhimu wa wajibu wa kimaadili. Watafiti katika tamaduni simulizi, wameweka kumbukumbu ya uwajibikaji wa wanawake katika utunzaji na usambazaji wa fasihi simulizi. Anafafanua kuwa Nnaemeka anadai; wanawake wamekuwa na umaarufu katika majukumu ya utaalamu wa ushairi kwa ujumla. Vilevile, Finnegan, (2007) anaeleza kuwa kila mwanamke wa Kiakan anategemewa kuwa na uwezo wa nyimbo za majonzi au kilio ingawa waimbaji baadhi hufidiwa kuliko wenzao. Hata hivyo kila mwanamke anayeomboleza katika msiba hupaswa kuimba la sivyo atakutana na

vipinzamizi vya kutuhumiwa kifo hicho. Hii hudhihirisha ulazima wa mwanamke kushiriki bila kupenda kwani ni muhimu sana katika ibada na maandiko. Finnegan anapambana katika sehemu ya Afrika katika usimulizi wa kinathari ambao hauunganiki moja kwa moja na mizunguko ya maisha unatawaliwa na wanawake.

Carole, (1986) anaeleza kuwa uwepo wa wanawake wachapakazi na wenye nguvu katika tamaduni za Kiafrika imekuwa ni chanzo muhimu cha msukumo wa wanawake wa Kiafrika.

Kazi hii imekuwa faafu kwa utafiti wetu maana imeeleza uwepo wa wanawake wachapakazi licha ya kugandamizwa na tamaduni za jamii zao. Vile vile imetoa hamasa ya kufanyika kwa utafiti huu ili kubainisha namna wahusika wa kiume wanavyosawiriwa na waandishi wanawake maana waandishi wanaume wameelezwa wanavyowasawiri wanawake hivyo kulikuwa na umuhimu wa kujua jinsia hii inavyoisawiri jinsia ya kiume. Mwanamke katika jamii anafanya mengi mazuri kama kuchapa kazi za nyumbani, kilimo, kutunza familia, na mengineyo mengi ila tamaduni haziyapi nafasi ya kihadhi katika jamii. Hii imedhihirishwa na waandishi wanaume namna wanavyowachora katika kazi zao.

Riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na wanaume huwasawiri wahusika wa kike kwa mitazamo hasi zaidi kuliko chanya ambapo wahusika wa kiume huchorwa kwa mtazamo chanya zaidi kuliko hasi, Momanyi (2001), Ndungo

(1998), Chesaina, (1987), Matteru, (1982). Kutokana na usawiri huu wa mwanamke katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na wanaume, waandishi hao wamekuwa wakibadilika katika kumsawiri mwanamke kulingana na jamii inavyobadilika. Vile vile, Momanyi, (keshatajwa) amemrejelea Reed, (1970), ambaye anadai kuwa tangu enzi za umwinyi hadi ubepari wanawake wamekuwa mbioni katika mashindano ya kuwanasa wanaume ili wajinasue katika manyanyaso. Wanawake walifanya jitihada za kujinasua katika utabaka uliowagandamiza kiasi cha kupoteza ushirikiano kati ya mwanamke na mwanaume. Katika jamii hizo za kitabaka mwanamke alidunishwa kiasi cha kulazimika kumtenga mwanaume kiuchumi, kutokana na hali hii wanawake walilazimika kujirembesha ili kuwanasa wanaume ambao walionekana kuwa mbali na wanawake.

Tafiti zilizotafitiwa kuhusu wahusika wanawake kwa kazi zilizoandikwa na wanaume kwa wanawake zimetoa hitimisho linaloleta hamasa ya kutaka kujua ni kwa vipi wahusika wanaume wanasawiriwa katika kazi za fasihi zilizoandikwa na wanawake, ambapo suala hili limeshughulikiwa na utafiti huu.

Kutokana na maelezo hayo mtafiti amejikita katika usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake maana tafiti nyingi zinajikita kuwatafiti wahusika wa kike wakati na wanaume wamo katika kazi hizo zinazoakisi matendo mbalimbali ya kijamii. Utafiti unahusu

usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili za Tanzania na Kenya zilizoandikwa na waandishi wanawake.

**1.1 Suala la Utafiti**

Watafiti waliotangulia kama vile Momanyi, (2001), Ndungo, (1998), Chesaina (1987), Matteru, (1982), Mnenuka, (2011) na Stratton, (1994) wamechunguza kazi mbalimbali zilizoandikwa na wanaume na kubaini namna wahusika wa kike walivyosawiriwa katika kazi mbalimbali za Fasihi hasa katika Tamthiliya na Ushairi na pia kuchunguza namna jamii zinavyowachukulia wahusika wa kike kama vyanzo vya maovu, wahalifu, vyombo vya starehe kwa wanaume na pia ni tegemezi kwa wanaume kama alivyoainisha Momanyi, Balisidya na Ndungo. Je wakati wahusika wa kike wakisawiriwa katika hali hiyo na waandishi wa kiume, wahusika wa kiume wamesawiriwaje na waandishi wa kike? Swala hili halijatafitiwa kwa kina. Kuna pengo linalostahili kuzibwa. Pengo hili limezibwa na utafiti huu. Kazi zinazoandikwa na waandishi wanawake zimeanza kupewa hadhi katika ulimwengu wa fasihi; katika taaluma ya uhakiki wa fasihi kama zile zinazoandikwa na wanaume. Mambo si kama vile yalivyofafanuliwa na Stratton zaidi ya miaka mingi iliyopita (1994) kwa maana alijikita katika lugha za kigeni ambazo si za Kiswahili. Hata hivyo wako waandishi wa kiume wanaowasawiri wahusika wanawake chanya kama vile Alamini Mazrui, Ngugi Wa Thiongo na Mugyabuso Mulokozi. Je wahusika wa kiume wanasawiriwa vipi na waandishi wanawake. Hata kwa hivyo, suala hili ni muhimu pale ambapo tumeweza kulinganisha

uandishi wa waandishi wa kike wa Kenya na Tanzania kwa namna walivyowasawiri wahusika wa kiume.

## 1.2 Malengo ya Utafiti

i. Kubainisha dhamira zinazowasilishwa kupitia wahusika wa kiume.
ii. Kuchanganua taswira zinazotumiwa na waandishi kuwasawiri wahusika wa kiume katika riwaya za waandishi wa kike.
iii. Kujadili mitazamo inayoibuliwa na wahusika wa kiume katika riwaya teule.
iv. Kulinganisha na kulinganua waandishi wa kike wa Kenya na Tanzania katika usawiri wao wa wahusika wa kiume.

## 1.3 Maswali ya Utafiti

i. Je, ni dhamira zipi zinazowasilishwa kupitia wahusika wa kiume katika riwaya teule?
ii. Wahusika wa kiume wamesawiriwa kwa kutumia taswira zipi?
iii. Ni mitazamo gani ambayo inaibuliwa na wahusika wa kiume katika riwaya teule?
iv. Waandishi wa kike wa Kenya na Tanzania wanalingana na kutofautiana vipi katika usawiri wao wa wahusika wa kiume?

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Kwa miaka mingi, watafiti wa kazi za fasihi wamekuwa wakijikita kuwachunguza wahusika wa kike waliobuniwa na waandishi wa kiume namna

wanavyonyanyaswa na kudhulumiwa katika jamii mbalimbali za Kiafrika. Kwa mfano, Mnenuka, (2011), Mavisi, (2007), Matteru, (1982), Momanyi, (2000), Chesaina, (1987) na wengineo ambapo kazi zao zimejikita kuwa jadili wanawake kama sehemu ya jamii inayoonewa na kugandamizwa kutokana na mitazamo na tajriba ya kuumeni.

Hata hivyo kazi za waandishi wa kiume, zimekuwa zikichunguzwa kwa namna wanavyowasawiri wanawake ila kazi za waandishi wanawake namna wanavyowasawiri wahusika wa kiume kumekuwa na pengo hivyo ni wakati sasa wa kuelewa kuwa wanaume nao wanasawiriwa kwa namna tofauti na waandishi wa kike kwa wa kiume na hivyo ni muhimu kuchunguzwa. Jambo hili limeshughulikiwa kwa kina katika utafiti huu. Ni muhimu pia kuelewa taswira mbalimbali ambazo jamii imewapa wanaume na nafasi mahsusi walizonazo katika jamii zao kwa kupitia uwasilishi wa waandishi wa riwaya teule. Hii imedhihirishwa katika dhamira na taswira wanazoziwasilisha wahusika wa kiume.

Utafiti huu utakuwa na mchango mkubwa kwa tafiti ambazo zimeshughulikia masuala ya wanawake. Utafiti huu utakuwa muhimu ili kuelewa jinsi wanaume wanavyoathiriwa kama wakimu familia na mabadiliko ya kijamii na ya kiuchumi. Vilevile, kazi hii itasaidia kupiga msasa harakati za kuwakomboa wanawake kutokana na mila, desturi na njia zingine zozote zinazowadhalilisha. Bila kuwabadilisha wanaume, mabadiliko ya wanawake wa kisasa hayatapatikana kwa ukamilifu wake. Ni muhimu kuwa nafsi mpya

na majukumu mapya ya wanawake yaende sambamba na nafsi mpya na majukumu mapya ya wanaume.

Kwa vile utafiti huu umehakiki riwaya teule za Kenya na Tanzania zilizoandikwa na waandishi wanawake, utasaidia wasomaji kuelewa masuala ya kijinsia katika riwaya hizo. Utafiti huu pia umeonesha namna wahusika wa kiume wanavyojishughulisha au kutojishughulisha na mambo mbalimbali katika jamii na mambo wanayoyawakilisha kwa ujumla kulingana na itikadi za jamii. Vilevile, utafiti huu utatumika kama chanzo cha jamii kuliangalia na kulichunguza kwa undani suala la wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na waandishi wanawake pamoja na kazi nyinginezo za fasihi. Kazi hii itachangia katika taaluma ya elimu jamii kuwahamasisha kuhusu masuala ya mahusiano mema ya kiuana.

Isitoshe, baadhi ya wasomi walipendekeza utafiti ufanywe ili kuangalia upande wa pili wa masuala ya uana kwa sababu mengi yametafitiwa kuhusiana na jinsi ya kike, jambo ambalo limewekwa wazi katika utafiti huu. Wasomi hawa ni kama Momanyi, (1998), Kimani, (2003), King'ei, (2002) na Wandera, (2002) ambapo anaeleza kuwa tafiti za kijinsia katika fasihi ya Kiswahili zitaendelea kuwepo katika maisha ya mwanadamu kwa maana binadamu anaendelea kuwepo. Vile vile, zitabadilika kutokana na mahitaji ya kijinsia ya jamii husika kulingana na nyakati za kihistoria za jamii hiyo. Kwa hiyo utafiti huu ni muhimu ili kulitekeleza hilo.

## 1.5 Upeo na Mipaka ya Utafiti

Kuna waandishi mbalimbali wake kwa waume ambao wamesawiri wahusika wao wa kike na wa kiume kwa njia tofauti tofauti. Utafiti huu umejikita katika riwaya nne ambapo mbili ni za waandishi wanawake wa Tanzania na mbili za kutoka Kenya. Riwaya hizo ni: *Hiba ya Wivu* (1997), *Kipimo cha Mizani* (2004) *Tumaini*, (2006) na *Dago wa Munje*, (2008).

Riwaya hizi tulizozichagua zina mawanda mapana ya kutosha kuwakilisha mtazamo wa mwandishi wa kila riwaya kuhusu swala la mwanaume. Riwaya hizo ziliteuliwa kwa kuzingatia kigezo cha nyakati za kuchapishwa maana zilihitajika zilizoandikwa na wanawake za nyakati za karibuni kuanzia miaka ya 1990 kuja mbele. Kigezo hicho ni muhimu kwa maana mambo hubadilika kulingana na nyakati yaani matendo ya wahusika katika jamii.

Hill, (1977) anatoa maoni kuwa usawiri bora wa wahusika huhitaji hali ya juu ya ubunifu ili kuwafanya wahusika hao wadhihirishe hali halisi zipatikanazo katika mazingira halisi ya kijamii na ya kawaida. Riwaya mbili kwa kila nchi zilizoteuliwa zina mawanda mapana kuhusu wahusika wa kiume, ya kutosheleza malengo ya ufafiti huu.

Watunzi hawa wa Tanzania na Kenya wamewasuka wahusika wa kiume katika kazi zao kiasi cha kutosha kutupa data za kuichanganua mada hii. Utafiti huu kwa waandishi wa Kenya na Tanzania umekuwa ni wa tofauti kutokana na vigezo vya kijamii vya waandishi hawa maana wanatoka jamii

tofauti, vile vile wameandika kazi kwa nyakati tofauti na mambo waliyoyaandikia ni tofauti. Utafiti huu umejikita kuangazia kazi tajwa zilizoandikwa na waandishi wanawake ili kuchunguza namna walivyowasawiri wahusika wa kiume.

## 1.6 Yaliyoandikwa kuhusu Mada

Marejeo yanayohusu usawiri wa wahusika wa kiume na wa kike yamechambuliwa ili kubaini jinsi wataalamu walivyouchambua usawiri huo kwa mikabala mbalimbali. Wanawake wanahusishwa katika sehemu hii kwa sababu mtafiti ameona kazi zinazohusu mwanaume na mwanamke peke yake kwa nafasi zao, jinsi jamii inavyowatazama pamoja na majukumu yao, pia kuna kazi zinazohusu mwanamke kwa kumhusisha na mwanaume. Ndiyo maana zimetumika kazi zinazohusu jinsia zote mbili wakati mada inahusu mwanaume namna alivyosawiriwa na waandishi wanawake. Marejeo na machapisho mbalimbali yamehakikiwa ili kujenga mkabala uliotumika katika utafiti huu. Tumeangalia kazi zilizoshughulikia wahusika wa kiume zilizoandikwa na waandishi wa kike wa Kenya na wa Tanzania.

Balisidya, (1982) anadai kuwa mwanamke anachukuliwa kwa mtazamo tofauti katika fasihi simulizi za Kitanzania kulingana na jamii husika. Kuna wanaomwona kama mzazi na mlezi wa familia, wengine wanamchukulia kama mali ya mwanaume. Vilevile ameonekana kama chombo cha starehe kwa mwanaume pamoja na mambo mengine yanayomuonesha mwanamke kama kiumbe dhaifu kwa mwanaume.

Kazi hii imesaidia kuonesha uhasi ambao wanawake wamesawiriwa na njia mbalimbali zilizotumika kumgandamiza mwanamke katika jamii, je ndivyo ilivyo hata kwa wanaume waliosawiriwa na wanawake? Kazi hii imeandikwa kitambo kidogo. Je kwa nyakati za karibuni ndivyo wanaume wanavyosawiriwa na wanawake kama kulipa kisasi au ni tofauti? Hili ndilo lengo la utafiti huu.

Kiango, (1992) anaeleza kuwa wanawake ni kundi muhimu kama walivyo wanaume katika maendeleo ya kijamii katika nchi zetu ambazo zinategemea kilimo, sehemu kubwa ya watu inaishi vijijini, mwanamke ana mchango mkubwa katika maendeleo kwani ndiye huwajibika zaidi katika shughuli za kilimo. Kwa ajili ya teknolojia ya nchi hizi kuwa nyuma, mgawanyo wa kazi unamwumiza zaidi mwanamke ambaye zaidi ya kwamba anakwenda shamba, vilevile karibu kazi zote za nyumbani zinamuangukia yeye mwanaume anapokuwa anapumzika.

Katika makala hii ya Kiango (k.h.j) ameeleza juu ya taswira ya mwanamke katika tamthiliya za Kiswahili za Kenya ingawa aliyoyajadili yanaakisi jamii mbalimbali za Kiafrika juu ya wanawake. Amejadili tamthiliya za *Nakupenda Lakini……*, *Nimelogwa Nisiwe na Mpenzi*, *Jirani Kanyolewa*, *Mwana Mpotevu*, *Bibi Arusi*, *Kilio cha Haki*, *Uasi*, *Mke Mwenza*, *Malimwengu Ulimwengu*, *Thamani Yangu*, *na Tazama Mbele*. Tamthiliya hizi zina mandhari ya Kenya japo zinaakisi jamii nyinginezo nje ya Kenya.

Kwa hiyo, katika hali kama hii inayoelezwa na Kiango kwenye kazi hii, mwanamke wa kijijini anaonekana kuwa anafanya kazi zaidi ya mwenzi wake yaani mwanaume. Ingawa wanawake wana mchango mkubwa sana katika maendeleo lakini hawamiliki mali sawa na wanaume ambao wanamiliki sehemu kubwa ya mapato na kumwacha mwanamke na sehemu ndogo sana. Mgawanyo wa mali kiuana hauko sawa, unampendelea mwanaume.

Mtafiti ameonyesha namna ambavyo wanawake wamesawiriwa na waandishi wa kiume na hasa wanavyowasawiri kwa mtazamo hasi zaidi. Utafiti umeonesha namna wanawake  wanavyogandamizwa mno kwa kazi nyingi huku waume zao wakila raha. Utafiti huu umetoa mwanga mkubwa kuhusiana na masuala ya kiuna na hasa usawiri wa wahusika wa kike katika tamthiliya za Kenya. Hili si lengo la utafiti wetu kwani utafiti wetu umejikita katika kuwajadili wahusika wa kiume namna walivyosawiriwa na waandishi wanawake ili kubainisha muono wa kiuana miongoni mwa waandishi wanawake wa Kenya na Tanzania.

Stratton, (1994) amemwelezea Ama Ata Aidoo kuwa alitafiti matatizo yanayowakumba waandishi wanawake wa Kiafrika ambayo aliyaeleza katika mkutano wa pili wa waandishi wa Kiafrika uliofanyika Stockholm mwaka 1986. Katika andiko lake ambalo liliitwa "Mwandishi mwanamke wa Kiafrika-maelezo ya jumla na ya kina". Aidoo alikumbusha kuwa kazi za tahakiki juu ya waandishi wanawake zimekuwa chache hasa katika vitabu vya mada maalumu vilivyoitwa Mambo Muhimu ya Majarida machache ya

tahakiki, kwa mfano toleo la kumi na tano la fasihi ya Kiafrika juu ya wanawake katika fasihi ya Kiafrika iliyochapishwa mwaka 1987. Aidoo anaeleza kuwa ufadhili wa kitaaluma umeonesha hakuna nia kabisa na umejaa dharau kwa wanawake ambayo haiko wazi. Anaendelea kueleza kuwa kama waandishi wanawake wa Kiafrika wana haki ya kuchukuliwa sawa kwa kutegemea kuwa tahakiki zinajitahidi kuzipa umakini baadhi ya kazi na kuzipa uzito kama zilivyo kazi zilizoandikwa na wanaume. (Tafsiri yetu). Kazi hii imetufaa sana kuelewa namna ambavyo wanawake walibaguliwa katika uwanja wa taaluma ikiwemo kufadhiliwa kimasomo na kuandika kazi za fasihi, wanawake hawakupewa nafasi. Hili si lengo la utafiti wetu japo limetupa ari ya kiutafiti katika kuangazia wahusika wa kiume namna wanavyosawiriwa na waandishi wanawake.

Kazi hii imeeleza kwa ujumla kuhusu mwandishi mwanamke wa Kiafrika kazi zake zisivyokuwa na nafasi sawa kihadhi na zile zinazoandikwa na mwanaume. Andiko hili halijazungumzia namna wahusika wa kiume wala wa kike wanavyochorwa na waandishi hao wanawake na hivyo kutoa mwanya wa kufanya uafiti huu ambao umejikita katika wahusika wa kiume namna wanavyochorwa na waandishi wanawake katika riwaya zao kwa kulinganisha waandishi wawili wanawake wa Kenya na wawili wa Tanzania.

Ndungo, (1998) anaeleza baada ya kufanya utafiti katika jamii za Kikuyu kuwa; katika jamii ya Kikuyu na jamii nyingine za Kiswahili, wanawake wamechorwa kichanya katika majukumu yao kama wawakilishi, walimu na

mfano wa kuigwa kwa watoto wao. Kwa ujumla wanawake wamechorwa hasi katika jamii ya Kikuyu na ya Waswahili kwa kutazama ubinafsi wao. Wanawake wameoneshwa kama wategemezi, wasio wakweli, wasio na akili, wategemezi, wasio na maono na hekima.

Alihitimisha kuwa, jamii hizi mbili kuwachora wanawake chanya kama mama na sehemu nyinginezo hasi, hapa lazima kuna sababu nzuri tu. Inaweza kuwa kiashiria kuwa mwanamke kama kikundi cha kijamii huogopa kizazi cha kiume. Inapaswa kubainishwa kwanini wanawake wanatazamwa hasi na ni kwa vipi mwono hasi unatafsiriwa katika maisha halisi.

Kazi hii imezungumzia taswira ya mwanamke katika fasihi simulizi. Pamoja na kwamba imeeleza namna mwanamke anavyochorwa hasi zaidi katika jamii ya Kikuyu na ya Kiswahili kwa ujumla ila haijaeleza anayesawiri hivyo mwanamke ni mwanaume au mwanamke mwenzake. Hata hivyo kazi hii imejikita katika fasihi simulizi yaani methali. Utafiti huu unahusu fasihi andishi yaani riwaya zilizoandikwa na wanawake na namna wanavyowasawiri wahusika wa kiume.

Wafula, (1999) anaeleza kuhusu mtazamo-kike katika tamthiliya ya *Mama ee* iliyoandikwa na Mwachofi. Inazungumzia mahusiano ya ndoa kati ya mwanamke (Mwavita) na mwanaume (Kinaya) ambapo mwanamke anagandamizwa kwa kila hali katika ndoa. Mwanamke anapoenda mahakamani ili kujinasua katika minyororo ya ukandamizwaji bado sheria

zinampendelea mwanaume. Kutokana na hayo Mwavita anaungana na mwanamke mwenzie Tenge katika kujitetea na kupigania haki zao kwani waliona ndio njia pekee ya kuwakomboa.

Lengo la utafiti huu si kujikita katika kuchunguza mtazamo-kike katika masuala ya kindoa bali ni kuchunguza namna waandishi wa kike wanavyowasawiri wahusika wa kiume katika miktadha mbalimbali na siyo katika asasi ya ndoa tu. Kazi hii inaonesha namna mwanamke anavyosawiriwa na mwandishi wa kike ila hazungumzii namna wahusika wa kiume wanavyosawiriwa kwa kina, jambo hili limechochea uhitaji kufanya utafiti juu ya usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya teule.

Momanyi, (2001) amedai kuwa wanaume ndio chanzo kikuu katika kumdunisha mwanamke katika sekta mbalimbali ndani ya jamii na jamii haioni kama kuna shida kwa maana maisha yanaendelea vizuri bila kujali masuala ya kiuana. Hata hivyo mwandishi huyu ametumia mashairi yaliyoandikwa na mwanaume jambo ambalo si lengo la utafiti huu.

Momanyi, (keshatajwa) amefafanua kuwa suala la mwanamke katika fasihi ya Kiswahili limeshughulikiwa na waandishi mbalimbali wa kiume na wa kike. Kazi hii imezungumzia wahusika wa kike namna wanavyosawiriwa katika kazi mbalimbali zilizoandikwa na wanaume kwa wanawake ambapo mwanamke bado anaendelea kuonekana ni mtu wa chini kwa kugandamizwa katika masuala mengi ndani ya jamii ambali si lengo la utafiti wetu. Utafiti

huu umeshughulikia wahusika wa kiume namna wanavyosawiriwa na waandishi wa kike.

Mogere, (2003) anaeleza kwamba usawiri wa wahusika wa kike katika kazi nyingi za fasihi ya Kiswahili limekuwa ni jambo lenye utata mwingi hadi leo. Inaelezwa kuwa wanawake wanachorwa hasi zaidi katika kazi nyingi zilizoandikwa na waandishi wa kiume. Waandishi wa kiume huwachora wanawake hasi na kuonesha kuwa ni viumbe wanaofaa kuonewa kwa kila nyanja na vile vile huandika kwa kuwapendelea wahusika wa kiume. Wahakiki wengine hueleza kuwa vigezo vya kitamaduni ndivyo huchangia katika kuwasawiri wahusika wa kike kwa namna hiyo inayowadunisha.

Amehitimisha kuwa wanawake wanapaswa kupambana wenyewe ili wajitoe katika minyororo gandamizi ya kitamaduni kwa kuelimika wao kwanza na kuielimisha jamii kwa ujumla kuhusu umuhimu wa mwanamke katika jamii pamoja na madhara ya kumgandamiza mwanamke. Utafiti huu umetusaidia sana kwa kubaini kuwa kazi zinazoandikwa na wanaume zinamchora mwanamke hasi. Hii imetujengea msingi wa kutafiti kazi zinazoandikwa na wanawake ili kuchunguza namna wanavyosawiriwa wanaume katika kazi teule.

Burgess, (2007) anafafanua kuwa wanaume wanasawiriwa kwa kujitokeza mara nyingi katika mchezo wa filamu kuliko wanawake. Wanawake husawiriwa zaidi katika masuala hasi ya kingono ambapo wahusika wa kiume

hutokeza mara nne zaidi ya wanawake  na upewa nafasi muhimu zaidi kuliko wanawake. Wanawake pamoja na kutokeza kwa uchache, huchorwa kwa kutia chumvi matendo wayafanyayo hasa ya kingono. Masuala ya uvurugaji na ngono hutiwa chumvi kwa wahusika wanawake tofauti na mwonekano wa wahusika wa kiume ambao huonekana wababe. Huu usawiri hasi wa wahusika wanawake ni muhimu kujadiliwa kwa kulinganishwa na wahusika wanaume wanavyosawiriwa. (Tafsiri yetu). Utafiti huu umetufaa kwa kutupa maarifa juu ya nafasi wanazopewa wanawake katika filamu ambazo zinaonesha ugandamizi na uonevu juu yao. Hili si lengo la utafiti wetu.

Utafiti huu haujazungumzia kazi za filamu kama zinaandaliwa na waandaaji wa kike wala wa kiume bali ni filamu kwa ujumla wake. Hata hivyo kazi hii imemsaidia mtafiti kupanua uelewa juu ya wahusika wa kike na wa kiume katika filamu na utokezaji wao kiuwiano baina ya wahusika wa kiume na wa kike. Kazi hii imetoa hamasa kwa mtafiti kuangazia usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya zilizoandikwa na wanawake.

Matundura, (2007) anaeleza kuwa mkabala wa kiuana unajishughulisha na maswala ya kimahusiano katika jamii. Mahusiano yanabainishwa katika jamii kutokana na sababu za kijinsia ambazo zimejikita katika misingi ya kitamaduni. Pia ametumia mkabala wa nadharia ya ufeministi ambao ulilenga kuleta usawa wa kijinsia katika jamii. Masuala ya kiuana yamekuwa ni tatizo katika jamii nyingi ulimwenguni kwa maana hakuna usawa wa kiuana katika majukumu ambayo yamejikita katika tamaduni za jamii husika. Kazi hii

imetusaidia sana kwa vile imeeleza masuala ya kiuana yanayoegemea katika fasihi ya watoto. Mambo hayo ndiyo yanadhihirisha pengo ambalo linazibwa na utafiti huu katika wahusika wa kiume maana lilikuwa halijazibwa. Vilevile Matundura (keshatajwa) amefafanua dhana za uana na jinsia ambapo anaeleza kuwa jinsia ni dhana ya kibayolojia na uana ni dhana ya kitamaduni. Dhana hizi zimetusaidia katika kujadili usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake kwa maana majukumu mbalimbali katika jamii hugawanywa kwa kujikita katika dhana hizi.

Kanwa, (2011) amejadili kazi ya Gabriel Ruhumbika, *Miradi Bubu ya Wazalendo* inayoakisi kipindi cha kabla ya uhuru, kipindi cha uhuru na baada ya uhuru ikilinganishwa na riwaya ya Ndyanao Balisidya, *Shida* inayoakisi kipindi cha azimio la Arusha. Waandishi hawa wawili wameonesha namna wahusika wa kiume walivyokuwa wakichukuliwa katika nyakati hizo ambapo jamii iliwatwisha mizigo mizito ikiamini kuwa mwanaume hashindwi, jambo lililowapelekea wakati mwingine kuanguka katika sehemu zao za kazi.

Mtafiti alihitimisha kuwa watunzi wote wa kazi teule wameathiriwa na mfumo wa jamii zao hasa ujamaa kwa maana wahusika wa kiume katika kazi hizi wamewasawiri wahusika wa kiume wakiwa mstari wa mbele kuhamasisha na kutenda shughuli za kisiasa na kiuchumu. Kwa mfano Nzoka ambaye amekuwa mwanasiasa mwanzo mpaka mwisho na kuhamasisha jamii kuipenda siasa kwani ilionekana ndiyo imepeba mifumo mingi ya kimaisha kama vile kijamii na kiuchumi. Mhusika mkuu Nzoka anapewa kila aina ya

cheo kwenye uchumi, siasa katika kada mbalimbali ilhali shule yake haikumwezesha kuzibeba nyadhifa zote hizo bali ni kutokana na mfumo wa nyakati hizo.

Kazi hii imemsaidia sana mtafiti kubaini usawiri wa wahusika wa kiume nyakazi hizo kwa kulinganisha mwanamke na mwanaume ambao wameandika kwa kujikita katika mwono wa kiulimwengu uliojaa unaynyasaji na uonevu wa hali ya juu ambao ulifanywa na wanaume kwa wanaume wenzao na pia kwa wanawake. Kazi hii imejikita sana huko japo hili si lengo la utafiti wetu maana utafiti wetu. Nadharia ya uhalisia iliyotumiwa na mtafiti wa kazi hii imekuwa faafu kwa utafiti wetu kwa kuielezea historia ya nadharia yenyewe na kuitumia kwa ujumla wake. Hata hvyo namna nadharia ilivyotumika ni kwa ujumla mno na wala haielezewi mhasisi wala mihimili haijaainishwa na namna ilivyotumika katika uchambuzi haijawekwa bayana. Hili limefanywa na utafiti wetu. Kazi hii pia haibainishi masuala ya kiuana katika kazi teule. Utafiti wetu unalenga kuujadili na kuuchambua kwa kuulinganisha usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake wa Kenya na Tanzania.

Jick na Nkweteyim, (2016) katika makala yao inayoitwa “Maono mbadala ya kiuana katika fasihi ya Kingereza ya Afrika: Tathmini ya mchezo wa Bole Butake” wanaeleza masuala mbalimbali ya kiuana. Katika makala yao wanaeleza masuala hayo ya kiuana yanayoelezwa katika fasihi ya leo, lengo ni kuchunguza kama kuna maono mbalimbali ya kijinsia. Pamoja na mchango

mkubwa wa waandishi wa kike katika fasihi, bado inatawaliwa na mfumo dume. Ni kutokana na mtazamo huo, wameamua kuleta mwamko kupitia mdahalo wa Bole Butake, kutathmini mchango wake katika muono wa kiuana katika fasihi ya Kiafrika ya sasa. Bole Butake ni mwanamaigizo wa kiume Mkameruni anayeandika kwa umakini masuala ya kiuana (wanawake na wanaume) wa Kiafrika na wanawake wa Kikameruni kwa umahsusi.

Wameonesha katika kazi yao kuwa mbali na mchango mkubwa sana wa Bole Butake katika masuala ya kiuana, majukumu ya wanawake hayazingatiwi kabisa na kutotiliwa maanani na kile wakitegemeacho wanawake. Bole Butake ni mwanaume mwandishi wa tofauti katika kuyajadili maswala ya kiuana hasa kuhusu wanawake maana anakuwa na mawazo ya kuwaleta wanawake kwenye uchanya zaidi tofauti na wanaume wengine katika fasihi.

Jamii nyingi, mbali na mambo haya, wanawake katika nchi nyingi wana haki ya kupiga kura, kwenda vyuo vikuu na kusoma kozi wazitakazo. Wengi wamejiunga na siasa na wengine kuongoza serikalini. Mfano, Margaret Thatcher wa Uingereza na Corazon Aquino wa Ufilipino. Huu wote ni uthibitisho kuwa mwanamke anashika nafasi ambazo awali alifikiriwa kutoziweza. Haya mageuzi ya wanawake kutoka katika desturi za kitamaduni hasi na kwenda zilizo chanya na za maana, yanamfanya sasa mwanamke atambulike na kuthaminiwa.

Katika jamii za mfumo dume, wanawake wako juu ya wanawake. Matendo yao hasa ya kimajukumu huwafanya waonekane duni ila bado wanawake wanafaa na wakati mwingine huonekana wa thamani na wanaowafaa wanaume. Mgawanyo huu huwafanya wanaume kuwa na mamlaka kuwamiliki wanawake.

Mfumo dume humpa mwanaume muktadha wa masuala ya ngono kuonekana kuwa ni jambo la msingi kwa mwanaume na ndiye analimiliki bali halimlengi mwanamke. Kazi hii inaonesha kuwa tamaduni mbalimbali zinazomgandamiza mwanamke zinabadilika siku hadi siku. Hata wanaume wanaowachora vibaya wanawake na kuwa na mitazamo hasi tu wanabadilika polepole kwa kuanza kuwachora wahusika wa kike kwa uchanya kama vile wenye mafanikio, mwamko na mengineyo mazuri. Hii ni kutokana na mwamko wa waandishi wanawake katika kutoa maoni yao juu ya mwamko wa wanawake katika masuala ya kiuana. (Tafsiri yetu).

Wahakiki wachache wameeleza kazi mbalimbali za waandishi wa kike kwa namna walivyowasawiri wahusika wa kiume katika kazi zao. Kwa mfano, Wafula, (1999) anaeleza kuhusu mwandishi Mwachofi katika tamthiliya ya *Mama ee* mwanaume amechorwa kwa mtazamo hasi zaidi kwa namna Kinaya anavyomnyanyasa mke wake Mwavita, kumpiga na kumsemea lugha ya ukali kila wakati. Mwanaume amechorwa kama mnyanyasaji, mlevi asiyekuwa na utu kwa mwanamke na hapendi maendeleo.

Mwanaume ni mbabe na mjeuri kupita kiasi, hata anapokalishwa vikao vya shauri hataki kumtii mtu hata wakubwa waliomzidi kisa yeye ni mwanaume. Mwanaume amechorwa kama mgomvi kwa familia yake na hasa kwa mkewe. Kinaya anampa vitisho Mwavita wakati hata kuwajibika kama mume ndani ya ndoa hakuna. Kinaya alimpiga sana mkewe na kumng'oa meno ila bado alipoenda kwao aliamriwa kurudi kwa mwanaume baada ya shauri. Wazee walimlaumu sana Mwavita kugoma kurudi kwa mumewe ila akaamua kukaa peke yake na maisha yanakuwa mazauri kuliko alivyokuwa kwa Kinaya. Kinaya amechorwa kama mhusika wa kiume asiyetambua wajibu wake kama kichwa cha familia kwa maana alidai kabisa na kuzua ugomvi akitaka atunzwe na mkewe kwa kununuliwa kila kitu kwa maana yeye ni mume wa ndoa.

Vilevile, Wafula (keshatajwa) anahakikia tamthiliya ya *Hatia* ya Mlama namna ilivyomsawiri mhusika wa kiume. Tunaona wahusika wa kiume kama walaghai, wasaliti, waongo na wenye ujasiri. Mfano, Juma anampa mimba binti mdogo Cheja ila anapomjuza habari za ujauzito anakuwa mkali sana na kumpa wazo la kumsingizia Sembuli. Cheja anarejea kijijini kwao na kumtaja Sembuli kuwa ndo kampa ujauzito. Kijiji kizima kinamlaumu Sembuli kwa tukio hilo na kumwita mara moja kijijini ili akaapishwe kama kafanya kweli aadhibiwe kimila. Kwa hili Sembuli alikuwa jasiri sana na alikuwa na msimamo kwa maana alijua hajampa mimba Cheja. Jambo lilizua tafrani na ukaibuka ugomvi mkubwa uliopelekea watu kuumizana kwa mapigano kisa Sembuli kagoma kufanya kiapo. Baada ya mapigano makali Cheja aliamua kusema kweli kuwa Sembuli hahusiki. Katika tamthiliya hii, mtunzi

amemchora mhusika wa kiume hasi na chanya ingawa matendo ya hasi yanakuwa na mguso zaidi kwa kuigusa zaidi jamii kuliko chanya.

Kazi hii inahusu masuala ya kiuana hasa kuhusu namna wanawake wanavyochorwa hasi na waandishi wanaume kwa kupelekewa na tamaduni za jamii za mfumo dume. Hata hivyo wahakiki ndio wameandika kuhusu waandishi wanawake wanavyowachora wahusika wa kiume katika taaluma ya uhakiki kazi zilizoandikwa na wanawake zimeanza kupewa hadhi kama zile zilizoandikwa na wanaume kama ambavyo tumeeleza hapo awali. Katika uwanda huu bado kuna pengo ambalo limezibwa na utafiti huu kwa kuhakiki riwaya zilizoandikwa na waandishi wanawake wa Kenya na wa Tanzania kubaini namna walivyowasawiri wahusika wa kiume katika kazi zao.

Wanjiku, (2018) ameeleza kuwa mabadiliko na nafasi ya mtazamo wa wahusika wa kiume unasababishwa na mabadiliko ya mazingira alimokulia na alimoishi mwandishi, mabadiliko ya kisiasa, kijamii na hata tajriba na ukuaji wake kama mwandishi. Amechambua riwaya za S.A. Mohammed ambazo ni *Utengano,* (1980) na *Dunia Yao,* (2006). Ametafiti juu ya mtazamo wa wanaume kuhusu wanawake na kubaini kuwa mtazamo wa wanaume kuhusu wanawake na wanaume wenzao unabadilika siku hadi siku.

Kazi hii imemsaidia mtafiti kubaini vipengele vinavyoleta mabadiliko ya mtazamo wa wahusika wa kiume kwani mtazamo wa wahusika wa kiume ni kipengele kimojawapo katika kuujadili usawiri wa wahusika wa kiume ingawa

kazi hii imejikita katika kazi za mwandishi mmoja wa kiume ambalo si lengo la utafiti wetu. Kazi hii imekuwa faafu kwa utafiti wetu maana imezungumzia masuala ya mtazamo kwa undani pamoja na nadharia ya uhalisia iliyoasisiswa na Gustave Flaubert na wengine ambayo pia imekuwa na nadharia mojawapo katika utafiti wetu.

Wanjiku (k.h.j) anaendelea kufafanua kuwa katika kila jamii huwa kuna nafasi au majukumu ambayo kila mtu anatarajiwa kutekeleza hasa kulingana na jinsia yake (Blackstone, 2003). Jamii nyingi za Afrika zimejikita katika mfumo wa kuumeni ambao huhakikisha, huhifadhi na kuendeleza mamlaka ya mwanamume katika nyanja zote za maisha. Mabadiliko ya nafasi na mtazamo wa wahusika wanaume yanadhihirika wazi kwa kulinganisha riwaya ya *Utengano* na ya *Dunia Yao.*

Aidha mabadiliko ya nafasi Nafasi ni jukumu au matumizi ambayo mtu au kifaa huwa nayo au hutarajiwa kuwa nayo (Kamusi ya Cambridge, 2008). Hivyo katika sehemu hii, nafasi ni jukumu alilonalo mtu au analotarajiwa kutekeleza katika kundi, jamii au uhusiano fulani. Kwa mfano, mtafuta riziki mhusika mkuu wa kiume katika riwaya ya Utengano ni Bwana Maksuudi Kambe. Ana mke kwa jina Tamima na watoto watatu, Mussa, Maimuna na kitoto kingine kichanga. Bwana Maksuudi ndiye mwenye kufanya kazi ili kupata riziki. Yeye ni mkurugenzi wa shirika la Bima la Taifa na pia ananuia kuwania ubunge. Mkewe Bi. Tamima hafanyi kazi bali anaishi ndani ya kasri lililo na watumishi wengi. Hata hivyo, katika riwaya ya Dunia Yao,

mabadiliko yanadhihirika kwa kumzingatia mhusika mkuu wa kiume Ndi-. Huyu ana mke kwa jina Bi. M na watoto sita, watatu wa kike kwa majina Mtima, Yungi na Kilua na watatu wa kiume wanaoitwa Dubwa, Bori na Jitu. Bi. M ndiye mtafuta riziki katika familia hii. Yeye ana biashara ya kuuza vyakula ofisini. Anamweleza mumewe: Nakuletea chakula hiki. Kutokana na dondoo hizo inadhihirika wazi kuwa nafasi ya mwanamume ya kutafutia familia yake riziki imebadilika katika karne ya ishirini na moja. Sasa wanawake pia hutekeleza jukumu hilo iwapo mume ameshindwa au amepoteza kazi aliyokuwa nayo. Kwa upande mwingine, kutokana na utaratibu wa mfumo wa kuumeni kuwa kutafuta riziki ni kazi ya mume pekee; mwanamume anaonekana kuathirika hasa kisaikolojia. Kutokubali mabadiliko haya kunamfanya amuwazie mwanamke mabaya kwa kuamini kuwa mwanamke ameshiriki ukahaba ili alete riziki nyumbani. Mwanzoni, haamini kuwa mwanamke anaweza kufanya kazi yoyote halali na ya heshima ili apate riziki. Haoni ni vipi mwanamke anaweza kutekeleza jukumu ambalo tangu zamani ni la mume. Mume ndiye anafaa kuajiriwa au kufanya biashara ili apate pesa za kununua chakula na mavazi, kulipa karo na kugharamia mahitaji yote ya mke wake na watoto. Jambo hilo la mwanamume kutoamini kuwa sasa mwanamke anaweza kufanya kazi kama mwanamume na kuleta riziki nyumbani linaendelea kushadidiwa kupitia kwa maneno ya rafiki ya Ndi- kwa jina Sakarati anayeongea kumrejelea mkewe. Kwa maoni ya mtafiti, majukumu ya kiuana yamebadilika sana katika karne ya ishirini na moja. Wanawake wameendelea kielimu na kiuchumi na hivyo wanaweza kuchangia katika kutafutia famila zao riziki.

Inadhihirika kuwa familia zilikuwa chini ya uongozi wa mwanamume kulingana na mfumo wa kuumeni. Kando na kutafuta riziki, mwanamume ndiye alitunga sheria na kumdhibiti kila mtu katika familia. Kwa maoni ya mtafiti, jamii ilimtarajia mume ahakikishe kuwa maadili mema yamefuatwa na mkewe na watoto wote. Maadili haya yalikuwa ni yale yaliyokubalika katika jamii kwa mfano heshima ya watoto kwa wakubwa, unyenyekevu wa mke kwa mume wake na kadhalika. Mwanamume alikuwa amepewa mamlaka mengi juu ya watoto, wafanyikazi na hata mke wake. Wanaume wengine hata walizidisha mamlaka yao na kuwatawisha watoto wa kike na pia wake zao. Mwanamke alinyenyekea na kuishi kwa woga mwingi kwani wakati mwingine alipigwa na mumewe hata kwa makosa yasiyokuwa yake. Kwa upande mwingine, mume alikuwa na uhuru wa kufanya lolote alilotaka na wengine hata walifanya lile lisilolingana na maadili tarajiwa ya jamii.

Kutokana na nafasi ya mwanamume ya kutunga sheria na kudhibiti familia, wanawake wengi waliogopa hata kuchukua hatua muhimu kuhusu maisha yao. Kwa namna hiyo, walionekana kuwa tayari kuhatarisha maisha yao ilimradi wasitende kinyume na sheria za waume wao. Aidha, watoto walipofanya makosa wanaume waliwaadhibu vikali ili wasirudie makosa hayo.

Kazi hii imemsaidia mtafiti kulielewa kwa undani suala ya mitazamo pamoja na mabadiliko ya kijamii kuhusu masuala ya kiuana. Mtafiti katumia nadharia ya uhalisia ambayo imekuwa faafu kwa kumwezesha mtafiti wa kazi hii kuielewa sawa sawa nadharia ya uhakiki pamoja na mihimili yake kulingana

na kile kinachotafitiwa. Imehitimishwa kuwa suala la mabadiliko ni la muhimu hivyo haliepukiki. Nadharia ya uhalisia imemsaidia mtafiti katika kuyachambua mawanda mapana ya kifasihi katika ulimwengu halisi. Imefafanuliwa katika utafiti huu kuwa mabadiliko ya mtazamo ni ya muhimu sana katika kuifanya jamii iende na wakati.

Hata hivyo kazi hii imejikita katika masuala ya kimabadiliko peke yake ilhali kubadilika wakati mwingine ni kwa kiasili mfano, kukua ni jambo asili ambalo ni muhimu. Jambo hili halionyeshi namna wahusika wa kiume wanavyochorwa na waandishi wa kiume katika riwaya za Kiswahili, jambo hili limefanywa na utafiti huu.

Mutungi, (2019) anaeleza kuwa kuna unyanyasaji wa kiusemi katika vijana wanaokuwa katika mahusiano ya kutongozana. Unyanyasaji huu unawaathiri vijana wanapokuwa katika mahusiano hayo na baadae huyaendeleza wanapokuwa katika ndoa. Mtafiti amezungumzia mamlaka au nguvu za kijinsia, kilongo cha unyanyasaji wa kiusemi ambapo kinajikita katika madaraka ya kiumri na ushupavu maalumu wa mhusika au kundi mahususi. Misingi hiyo ya kimamlaka imemwezesha kijana wa kiume kumpuuza, kumkanganya, na hivyo kumdhibiti kwa urahisi kijana wa kike. Vijana wa kiume hutumia usemi kuwalaghai wasichana na baadae kuwatenda mambo mabaya na kuwakimbia. Kazi hii imemsaidia mtafiti kuelewa mbinu mbalimbali wazitumiazo vijana wa kiume katika kuwatongoza wasichana na kuwatia mtegoni.

Mtafiti ameeleza namna ambavyo vijana wa kiume wanakuwa na mbinu mbalimbali za kuwalaghai wasichana kwa kuonesha kuwa wanawapenda sana. Wanakuwa na maneno mazuri yaliyopakwa mafuta na kuwafanya waaminike kwa wasichana. Wakitimiza walichokihitaji basi huwaacha wasichana kwenye mataa na kuwafanya waishi maisha magumu. Cheja alilaghaiwa na Juma na kweli wakaanza mahusiano kwa siri huku wakiaminiana na kuwekeana ahadi kemkem. Cheja anapopata ujauzito ndipo Juma anadhihirisha kuwa hakuwa mkweli kwa yale waliyokubaliana awali. Utafiti umemsaidia mtafiti kuyaelewa maneno mbalimbali wayatumiayo vijana wa kiume katika kuyatimiza yale yanayokuwa kiu cha maisha yao. Hili limeelezwa kwa upana sana na kumfanya mtafiti aielewe vizuri tamthiliya inayojadiliwa. Mkabala uliotumika umeonekana kuwa mpya kwa mtafiti hivyo umemwezesha mtafiti kuuelewa na kupata maarifa mapya. Ni Mkabala wa uchanganuzi tunduizi kilongo wa kifeministi ambao umeelezwa kwa kina katika utafiti wake.

Hili si lengo la utafiti wetu japo kazi hii imemsaidia mtafiti kupanua wigo katika masuala ya kiuana na kupata ari ya kuzitafiti riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake ili kubaini namna waandishi hao wanavyowasawiri wahusika wa kiume.

Mooka, (2019) katika utafiti wake wa shahada ya uzamifu ametafiti masuala ya ubabe dume katika riwaya zilizoandikwa na vijana wa Kenya. Amefafanua kuwa katika riwaya hizo ubabe dume unatokana na mila na desturi pamoja na tamaduni nyinginezo ambazo zinampa kipaumbele mwanaume katika jamii

pamoja na mambo ayafanyayo ikiwemo kumiliki mali pamoja na mamlaka walizo nazo katika masula mbalimbali ya kijamii.

Kazi hii imeendelea kufafanua udume nchini Kenya umetafitiwa mara nyingi na kuonekana kuwa unapewa kipaumbele kiasi cha kuufanya uendelee kukua na kuonekana una umuhimu katika mambo mbalimbali na nyanja tofauti. Umuhimu wa udume katika jamii za Kenya humfanya mwanamke aendelee kuwa chini ya mwanaume na kunyimwa haki mbalimbali kutokana na tamaduni zao.

Amemrejela Wilkinson, (2017) ambaye ametafiti katika uzamifu wake kuhusu mau mau na udume:rangi,jinsia na mwili katika nchi ya Kenya kipindi cha ukoloni. Matafiti kaonesha namna wakenya walivyobaguliwa kirangi, jinsia na mwonekano wa mwili. Wengi walinyanyaswa na kunyimwa haki zao. Athari hiyo iliendelea hadi kipindi cha baada ya uhuru mpaka sasa bali ubaguzi unakuwa ukibadilika sura kulingana na nyakati.

Mfumo dume unachukua nafasi katika jamii za Kenya na Afrika kwa ujumla kutoka na athari ya ukoloni pamoja na tamaduni zetu zinazoinyima jinsia moja haki na nyingine kupendelewa. Kazi hii ya Mooka (keshatajwa) imetumia nadharia ya mwanaume mpya kuonesha kuwa masuala ya ubabe dume anayepaswa kubadilishwa ni mwanaume ili aachane na kujiona yeye ni wa juu sana kuliko mwanaume. Ubabe na dhana nyingine zinazofanana nazo

zinapaswa kukomeshwa kwa kuanza kumbadilisha mwanaume ambaye anaona ni haki yake kupendelewa na mwanamke kuwekwa chini.

Kazi hii imemsaidia sana mtafiti kuielewa nadharia ya mwanaume mpya pamoja na mihimili yake. Kazi nzima imekuwa ya manufaa sana kwa mtafiti maana inahusu masuala ya mwanaume katika kazi halisi zilizoandikwa na vijana wa Kenya. Kazi hii haikubagua vijana wa kike au wa kiume walioandika bali imejikita katika masuala ya mfumo dume. Imekuwa ya manufaa kwa kumsaidia mtafiti kuelewa masuala ya mfumo dume na aina zake na mambo yanayopelekea mfumo dume katika nchi ya Kenya na Afrika kwa ujumla.

Hili halikuwa lengo la utafiti wetu bali kazi imetupa upana wa uelewa wa mambo ya kijinsia. Ametumia nadharia ambayo ni faafu kwetu ila hajazungumzia usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake kwa maana haikuwa sehemu ya utafiti wake. Hili ndilo lengo la utafiti wetu.

Mutungi, (2021) anaeleza kuwa mila na desturi za kijamii zinazowezesha au kufaninikisha unyanyasaji wa kiusemi baina ya wanandoa katika tamthilia teule za Kiswahili. Mila na desturi za kijamii kwa ujumla zinarejelea mienendo, tabia, mazoea au mfumo wa kanuni za jamii.

Anaendelea kufafanua kuwa mienendo ya kiutamaduni ni msingi maalumu wa shughuli na mambo ya kibinadamu katika jamii. Hivyo, muktadha wa kiutamaduni ni jambo muhimu sana katika uchanganuzi na uelewa wa unyanyasaji wa kiusemi baina ya wanandoa. Muktadha wa kiutamaduni umehusisha mila na desturi mbalimbali za kijamii ambazo huonesha ugandamizaji wa jinsia moja na kuikweza nyingine. Unyanyasaji hujidhihirisha katika vipengele vifuatavyo:

**Mume ndiye mkuu wa nyumba**.

Utamaduni huu kwa kujikita katika mila na desturi mila na desturi katika jamii nyingi za Kiafrika zinamwonesha mume kama mwenye nyumba/mkuu wa nyumba au kichwa cha familia ambapo anatumia nafasi hiyo kumtawala na kumkandamiza mke wake. Hivyo, mila na desturi hizo ambazo zinaonekana kumpa mume aula na hadhi kubwa katika mahusiano ya ndoa zinawezesha na kufanikisha unyanyasaji wa kiusemi baina ya wanandoa.

**Mke kumtii mume wake**

Hii nayo ni mila inayopewa nafasi katika jamii zenye mfumo dume ambapo mwanaume hupewa mamlaka ya kutawala na kulinda wanafamilia wengine ambao wanatarajiwa kuheshimu na kutii utawala wake, na hali hiyo inadumisha utaratibu na utulivu katika familia (Odimegwu, 2006). Imani na tabia kama hizi zinathibitisha kuwa ndoa ni asasi ya kijinsia ambayo inambagua mwanamke.

**Ulipaji wa mahari**

Mila ambazo zinaendelea kumgandamiza mwanamke katika jamii ni kulipiwa mahari katika mchakato wa ndoa. Hii humfanya mwanaume aone kuwa amepewa haki ya kummiliki mwanamke. Muthengeki, Kule na Neemah, (2012) wanaeleza kwamba mahari ni mojawapo ya mambo yanayochagiza udhalilishaji na unyanyasaji wa wanawake katika mahusiano ya ndoa. Mathalani, mume aliyelipa mahari anathibitisha mamlaka kwa kuhisi kwamba alilipia mke huyo, na hilo linamnyima mke haki na usawa.

**Mume kuoa wake wengi**

Mila na desturi hizi pia huendeleza mfumo dume kwa kuwafanya wake walioolewa na mume mmoja kuishi kimashindano katika kumteka huyo mwanaume aliyewaoa. Mutungi, (2018) na Maitaria, (2019) wanaonesha kwamba utamaduni wa Kiafrika unampa mwanamume uhuru wa kuoa wake wengi, lakini mke hatarajiwi kujihusisha na mwanamume yeyote mwingine isipokuwa mume wake. Maelezo haya yanaionesha ndoa kama asasi iliyoundwa kwenye msingi wa ubaguzi wa kijinsia ambapo mwanamume anapewa kipaumbele, yaani ndiye ‘anaoa’ na mwanamke anashirikishwa tu kwa ‘kuolewa’.

**Mgawanyo wa majukumu kati ya mke na mume**.

Majukumu ya kijinsia yanarejelea tabia na shughuli ambazo wanawake na wanaume wanatarajiwa kutekeleza au kufanya kulingana na jinsi zao, huku wakizingatia imani za jamii maalumu (Eagly, 2009; Urlich na Cosell, 2009;

Eisenchlas, 2013). Majukumu ya kijinsia katika jamii hudhibiti tabia na mienendo ya wanawake na wanaume kwa kutofautisha hadhi na shughuli zao maalumu. Mfano, majukumu ya wanaume yanadhihirisha mamlaka na uwezo mkubwa ilhali majukumu ya wanawake yanawaonesha kama binadamu wa hadhi ya chini ambao hawafai kupewa haki na heshima sawa na wanaume katika jamii (Joro, 2016).

**Watoto kumilikiwa na baba**

Katika utamaduni unaozingatia mfumo dume, watoto humilikiwa na baba kwa niaba ya ukoo na/au kabila husika. Kanu, (2014) anaeleza kwamba katika jamii za Kiafrika zinazoongozwa kwa misingi ya mfumo dume, watoto humilikiwa na baba ili kudumisha uhai wa baba katika familia, na kuendeleza ukoo katika kabila kwa ujumla. Hii ni tabia au mila nyingine ya kijamii ambayo inawadhalilisha wanawake na kuwafanya wabaguliwe na wanyanyaswe katika mahusiano ya ndoa. Tamaduni hizi huupalilia mfumo dume na wala jamii haioni kama kuna tatizo lolote la kiuana miongoni mwa wanajamii.

Utafiti huu wa Mutungi (keshatajwa) umefafanua masuala ya kiuana namna ambavyo husababishwa na mila na desturi ambazo husisitizwa na jamii husika na kutoleta usawa wa kijinsia. Utafiti huu umejikita katika muktadha wa unyanyasaji wa kiusemi baina ya wanandoa. Kazi hii imemsaidia mtafiti kubaini masuala ya kitamaduni ambayo yanauendekeza mfumo dume na

kuwanyanyasa wanawake kwa kuanzia katika usemi na baadae katika matendo.

Vilevile umejikita katika masuala ya ndoa na matendo yatendwayo ndani ya ndoa na kupelekea ubaguzi wa kijinsia kwa kuikweza jinsia mojawapo na nyingine kugandamizwa katika ndoa. Kazi hii imemsaidia mtafiti kuyabaini masuala hayo katika ndoa japo hili si lengo la utafiti huu. Utafiti huu umejikita katika usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake.

Kutokana na udurusu na tafiti za awali kuhusu mada, imebainika kwamba kuna tafiti nyingi zilizofanywa kuhusu usawiri wa wahusika wa kike na waandishi wanaume kwa wanawake kuliko tafiti zilizoandikwa kuhusu usawiri wa wahusika wanaume kwenye kazi za waandishi wanawake na ndio maana utafiti huu umehitajika kufanywa ili kuziba pengo hili.

## 1.7 Misingi ya Nadharia

Kulingana na Wafula na Kimani Njogu, (2007) wasema kwamba nadharia ni istilahi ya kijumla inayomaanisha miongozo inayomwelekeza msomaji wa kazi za fasihi kuifahamu kazi anayoshughulikia. Aidha ni maarifa ya kumwelekeza mtafiti katika kuchunguza suala fulani. Dhima kuu ya nadharia ni kuwezesha uchunguzi na ufasili mwafaka utimie na mchanganuzi aidha mtafiti asionekane kama aliyejitungia dhana au mawazo katika utafiti wake. Hivyo yanayotafitiwa hayataonekana chapwa maana nadharia ziliyokubalika

zinatosheleza kuhimili maelezo yanayotolewa. Utafiti wetu utaongozwa na nadharia zinayoakisi masuala mbalimbali ya kijamii pamoja na maoni pendekezwa.

Kutokana na usomaji wa mtafiti wa nadharia mbalimbali za uhakiki wa kazi za fasihi amebainisha kwamba katika utafiti huu nadharia zilizotumika ni nadharia ya Ujifunzaji wa kijamii, nadharia ya mwanaume mpya na uhalisia. Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii imeshughulikia chanzo cha mtu kujua masuala ya kiuana kimajukumu kulingana na jinsia ya kike na kiume. Nadharia hii inaeleza chanzo cha tabia za binadamu kulingana na jinsia hivyo haiwezi kujadili masuala ya usawa wa jinsia na hivyo nadharia ya mwanaume mpya ni muhimu kutumika. Nadharia ya mwanaume mpya imeshughulikia mwanaume ambaye anakubali mabadiliko kwa kumuona mwanamke kiumbe sawa na mwanaume,hana ubabe kwa mkewe na kumsaidia aina mbalimbali za kazi bila ubaguzi. Kutokanana mihimili ya nadharia ya mwanaume mpya, haiwezi kujadili masuala ya kimabadiliko katika ulimwengu halisi hivyo nadharia ya uhalisia ndiyo ya kuyafafanua haya. Nadharia ya uhalisia inadhihirisha jinsi dunia inavyobadilika katika masuala mbalimbali na kuonesha kama masuala hayo yanaendana na hali halisi ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kitamaduni kulingana na ulimwengu uliopo. Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii na ya mwanaume mpya zinaonesha masuala mahsusi ya kiuana katika dunia halisi wakati nadharia ya uhalisia inatoa picha ya jumla ya matendo ya watu na dunia jinsi ilivyo.

Nadharia zimemsaidia mtafiti kuainisha mihimili, kupata mawazo yaliyomo katika nadharia tajwa, kuwaelewa waasisi wa nadharia husika namna wanavyozijengea misingi nadharia zao. Vile vile mtafiti anapata nafasi ya kutoa maoni kwa kila nadharia kila baada ya uchambuzi wa kazi teule zinazoongozwa na mihimili ya nadharia katika kuyajibu maswali ya utafiti huu.

### 1.7.1 Nadharia ya Ujifunzaji wa Kijamii

Hii ni nadharia ya hatua za ujifunzaji na tabia za kijamii ambayo inapendekeza kuwa tabia mpya, mtu huzipata kuangalia na kuiga wengine. Inasisitiza uchunguzi na utengenezaji wa vielelezi na kuiga tabia au mienendo, mielekeo na hisia za wengine. Inachunguza jinsi mazingira na utambuzi vinavyotangiza na kuathiri ujifunzaji wa mtu na tabia yake.

Inaeleza kuwa ujifunzaji ni hatua ya kiakili yaani kumbukumbu ambayo hutokana na kuangalia au maelekezo ya moja kwa moja au hata vishawishi vilivyomo katika jamii yake. Kwa kuongezea, ujifunzaji hutokana pia na tuzo pamoja na adhabu zinazomfanya mjifunzaji kuweza kung'amua mambo. Tabia inayotuzwa mara kwa mara hiyo huota mizizi na inayoadhibiwa mara kwa mara basi hiyo huachwa. Nadharia hii hupanuka kwa kujikita katika nadharia za kitabia katika utamaduni ambapo tabia hudhibitiwa kwa vishawishi ambavyo husisitiza majukumu muhimu katika hatua za ujifunzaji (Bandura, 1972).

Nadharia hii imeasisiwa na Albert Bandura mwaka 1963 kutoka katika nadharia za kisaikolojia za ujifunzaji katika kupanua uwanda wa ujifunzaji ambao hutokea katika ulimwengu halisi. Imefanyiwa maboresho na Albert Bandura akishirikiana na Walters 1977 kwa kuainisha mihimili yake Nadharia ilichukuliwa katika saikolojia na kuletwa katika uana kwa maana tabia anazokuwa nazo binadamu hazaliwi nazo bali huzikuta katika jamii ambamo anajifunza kutoka kwa watangulizi wake au wazazi na jamii kwa ujumla wake (Bandura, 1977).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii inatumika kwa sasa kuweka bayana nadharia ya utambuzi ya utamaduni. Nadharia tete ya tambuzi wa kitamaduni inaeleza kuwa binadamu huwa na tabia na ujuzi ambao humruhusu kubadilishana mawazo ya kitamaduni (Hermann, 2007). Hii hufungua mwanya wa kujifunza ambapo ujifunzaji wa kijamii ndiyo dira ya kumfanya apate nafasi kubwa ya kujifunza mambo mengi ya kijamii. Kutokana na mawazo haya ya Bandura inaonekana kuwa huu ni ushahidi wa kuthibitisha kuwa binadamu huiga tabia nyingi kuliko wanyama kama nyani katika hatua za ujifunzaji. Baadhi ya wataaluma wamependekeza kuwa utayari wetu binadamu katika ujifunzaji kijamii na kitamaduni umepelekea kufanikiwa (Rear, 2014).

Mihimili ya nadharia. Imeainishwa na Pfohl, (1994) kama ifuatavyo:

i. Ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia.

ii. Ujifunzaji unahusu kuchunguza, kupata habari kutokana na ule uchunguzi na kuunda maazimio kuhusu utendakazi wa tabia hiyo.
iii. Vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote.
iv. Mwanafunzi si mpokezi tulivu wa habari, utambuzi wa mazingira na tabia vinaathiriana katika upataji wa habari wa mwanafunzi.

### 1.7.2 Nadharia ya Mwanaume Mpya

Hii ni nadharia mojawapo kati ya nadharia tatu za uanaume zilizoainishwa na Judith Buttler ambazo ni mwanaume mbabe, mwanaume mtekelezaji majukumu ya kiuana na mwaume mpya (Mooka, 2019).

Nadharia hii imeasisiwa na John Beynon mwaka 2002 ambapo alifafanua kuwa mwanaume siyo mbabe nyakati zote na kwa kila jamii bali wapo wananaume ambao wanajali sana, wasikivu na wanatii maagizo ya kiuana. Kuna wanaume ambao kwa muonekano ni wapole sana ila wanatawaliwa na mfumo dume. Kwa maana hiyo jamii ina wanaume mchanganyiko wakiwemo wanaume wapya yaani walioondokana na mfumo dume na ambao wanaushikiria. Nadharia inalenga kuwaonesha wanaume wapya ambao wamebadilika na kuwa katika utendaji mpya ikilinganishwa na mfumo uliotekelezwa na wanaume awali (Segal, 1990).

Mikondo mbalimbali ya uanaume inategemea elimu rasmi, vyombo vya mawasiliano na utamaduni wa Kimagharibi, kwa mfano wanaume wanaobadilika kuusheheni upya wa tabia wanakubali tabia majukumu yoyote ya kiuana kwa kutojali jinsia, hawaonyeshi udikteta na wanawajibika kufanya majukumu ya kinyumbani. Pamoja na haya wanaweza kuzikosoa nafasi zao na mazoea yao  (Morell, (2002).

Wanaume wapya huwasaidia wake zao kujiendeleza kielimu na kikazi. Vilevile wanaweza kufanya kazi za jikoni kama kuosha sahani, masufuria na kulinda watoto bila kuogopa kuwa watafanyiwa masihara na wanaume wenzao au jamaa walioko karibu nao. Kulingana na Gill, (2003) anaeleza kuwa mwanaume mpya ana hisia chanya, anawaheshimu wanawake na anawaona wanaume kwa wanawake kuwa viumbe sawa. Lakini pia ni mtu anayejipenda kwa kuzingatia jinsi hulka yake ilivyo. Ana hisia za kike za kulinda watoto kama baba mwema.

Nadharia hii imeungwa mkono na Newman, (2012) ambapo ameeleza kuhusu mtazamo huu mpywa wa uana kuhusu mwanaume wa kisasa au anayetarajiwa kuwa wa kisasa kwa kumsaidia mkewe kama kiumbe sawa. Mkondo huu umesaidia kumchanganua mwanaume anayeelekea kuwa chanya kwa mwanamke tofauti na wanaume walio wengi katika jamii za Kenya na Tanzania kama ilivyobainishwa na waandishi wanawake katika nchi hizi mbili.

Nadharia ya mwanaume mpya imetumika katika utafiti huu kwa kuchunguza utamaduni, historia, dini, mielekeo na amali za kijamii zinazobainika kupitia uhakiki wa taswira za kiuana katika riwaya zilizoandikwa na waandishi wanawake wa Kenya na Tanzania ili kulinganisha namna wanavyowasawiri wahusika wa kiume katika kazi hizo. Nadharia hii inasaili, kuelekeza na kudadisi misimamo na itikadi ya kiume na kupendekeza namna ya kuiondoa ili kuweza kuwa na wanaume wanaouchukia unyanyasaji na ugandamizaji wa wanawake. Inaelekeza pia katika jamii kuwa ni muhimu kuwa na udadisi wa fasiri za kiume za fasihi pamoja na mikabala yakibabedume pamoja na athari zake zinaendeleza matabaka katika jamii na kufanya jinsia moja kuwa chini ya nyingine ilhali zinaishi kwa kutegemeana.

Mihimimili ya nadharia: Imeainishwa na Beynon, (2002) kama ifuatavyo:

i. Kusaidia wake zao na wanawake wengine katika jamii katika kujiendeleza kielimu na kikazi.
ii. Kukubali majukumu yoyote ya kiuana bila kujali jinsia bila kujali watu waliowazunguka.
iii. Kutoonesha udikteta katika familia zao pamoja na jamii inayowazunguka.
iv. Kuwaona wanawake kama viumbe sawa na wanaume kwa kuwaheshimu na kuwapenda katika kila nyanja wanazokuwepo.
v. Kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume.

### 1.7.3 Nadharia ya Uhalisia

Uhalisia ni mkondo unaosisitiza usanii wa matukio katika maisha ya kila siku. Holemann, (1972), anaeleza kuwa uhalisia ni ukweli kama ulivyo katika mazingira. Kazi inayotungwa yapaswa kuiga kwa karibu zaidi hali ilivyo katika ulimwengu halisi, Drabble, (1993). Kwa mujibu wa Qusby, (1988), neno uhalisia lilitumiwa kwa mara ya kwanza huko Ufaransa katika mwaka wa 1850 ili kuelezea kazi za sanaa zilizojikita katika kuusawiri ulimwengu kama ulivyo wala sio kama unavyofikiriwa kuwa.

Uhalisia huzingatia namna ukweli unavyosawiriwa katika nyakati mbalimbali. Jinsi ya kuusawiri na kuuelewa uhalisia hutofautiana kutokajamii moja hadi nyingine. Kwa hivyo ni bayana kuwa kila kizazi huwa na 'uhalisia' wake. Tapo hili liliwekewa msingi na mwanafalsafa Hegel katika kitabu chake. cha Aesthetic. Mtaalamu huyu alipendekeza matumizi ya neno hili kuelezea kazi ya kifasihi ambayo inauwasilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii ambako kuna wahusika au mhusika anayetenda mambo kwajinsi inayochochewa waziwazi na hali aliyomo. 10 Msingi mkubwa wa tapo hili ni usimulizi wa kimuhakati, unaosimulia matukio kama yanavyotokea katika ulimwengu halisi au kwa namna inayokaribiana sana na hali iliyoko katikajamii.

Kwa hivyo, mwandishi anapaswa kutunga kwa kuyaakisi maisha ya kijamii katika ngazi za kijamii, kiuchumi, kitamaduni na kisiasa. Mtazamo huu unatia mkazo kwenye uwasilishi wa mambo ambayo yanaonekana katika jamii. Waandishi wanatarajiwa kutoa picha za wahusika, matukio na mandhari

ambayo yanaoana kwa kiasi kikubwa na uhalisia wa jamii ya mwandishi anayehusika. Mchango mkubwa wa nadharia hii ni kuchora maisha kama yalivyo.

Uhalisia unapinga au kukataa aina yoyote ya majaribio. Mwandishi analazimika kuuteua mtazamo wa kisimulizi ambao utamwezesha kuyawasilisha maisha kwa 'usahihi'. Mwandishi hutilia mkazo wahusika katika hali za kawaida za maisha, matukio au mandhari ya kawaida na yanayoweza kuonekana katika jamii. Huu ndio msingi wa kauli ya Lenin kuwa 'fasihi ni kioo cha jamii'. Uwasilishi huu wa maisha ni dhana ya ushabihikweli. Msisitizo upo katika kuukaribia ukweli uliopo katikajamii inayohusika. Lukacs, (1972), anauona uhalisia kama lengo kuu la msanii au mwandishi.

Anaamini kuwa mwandishi anasukumwa na nia ya kuusawiri uhalisi katika ukamilifu wake katika wakati fulani maalum. Mwandishi anapaswa kupenya chini ya picha ya kijuujuu na kuidhihirisha mifanyiko ya mabadiliko iliyoko. Hivyo, kazi ya msanii au mwandishi ni kuusawiri ulimwengu kama changamano na wenye ukamilifu fulani unaobadilika na wenye sheri a au kanuni maalum.

Chomba, (2018) wanaeleza kuwa nadharia ya uhalisia iliasisiwa katika karne ya kumi na tisa na kufafanuliwa zaidi na Goffman, (1952) aliyeishi kati ya mwaka (1922-1982). Baadhi ya wataalamu wengine waliotoa mchango wao ni Gustav Flaubert, (1850). George Lukacs, (1972), Rene Wellek, (1960),

Macdowell Arthur, (1918) na Hegel G. (1971. Lukacs, (1963) anaeleza kuwa mwandishi anasukumwa na njia ya kuusawiri uhalisia katika ukamilifu na wakati wake maalumu. Tukio, mhusika au mandhari huelezwa kama vya kihalisia ikiwa vinafanana na sura fulani ya maisha.

Wamitila, (2003) anasema kuwa uhalisia ni dhana inayotumiwa katika fasihi kuelezea hali ilivyo katika jamii kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni. Anaendelea kusema kuwa uhalisia ni dhana muhimu katika uhakiki wa kifasihi na ina historia ndefu.

Uhalisia ulizuka kama vuguvugu la kuupinga mtazamo wa kiromansia. Ni mkondo unaosisitiza usawiri wa matukio au maisha katika fasihi kama yalivyo katika maisha ya kila siku. Mmoja kati ya wataalamu wanaohusishwa na dhana hii ni mfuasi wa Marx, Georg Lukacs mwaka 1972 ambaye anaamini kuwa, usawiri wa uhalisi katika ukamilifu wake na kuchunguza undani wa picha inayoonekana ya uhalisi na kugundua sheria za mabadiliko ya kihistoria zinazoisababisha hali fulani.

Mutua, (2017) ametafiti kuhusu mitazamo ya waandishi wa kike na wa kiume kuhusu usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili na kubaini kuwa waandishi wa kiume wanawasawiri wahusika wa kike chanya zaidi kuliko hasi na wa kike wanawasawiri hasi zaidi kuliko chanya. Hali hii inaonyesha kuwa asilimia kubwa inawakilisha mtazamo hasi wa mwandishi kuhusu wahusika wa kike. Kwa hivyo, mwandishi huyo wa kike ana mtazamo

hasi kwa wahusika wa kike. Yamkini mtazamo wa mwandishi unatokana utamaduni na athari ya wakoloni barani Afrika kama inavyodaiwa na nadharia ya ufeministi wa Baada-ukoloni.

Anaendelea kueleza kuwa waandishi wa kike wanafanana kimtazamo katika kuwasawiri wahusika wa kike. Anaendelea kueleza waandishi wanawake wamewapa jumla ya sifa sita (6). Miongoni mwa hizo sifa sita, moja (1) ni chanya na tano (5) ni hasi. Sifa chanya zimechangia asilimia 83.3% nazo tano ni hasi na zinachangia asilimia 16.7%. Kiwango cha kufafana ni asilimia 66.6%. Kiwango hiki cha kufanana kimechuliwa kumaanisha ya kwamba waandishi wa kike wamekubaliana kwa kiwango kidogo mno kuhusu sifa chanya za wahusika wa kike. Kwa upande mwingine, wamekubaliana kwa kiwango kikubwa kuhusu sifa hasi. Hali inasisitiza mitazamo hasi kuhusu wahusika wa kike katika tamthilia zao.

Vile vile, mtafiti ameonyesha jinsi waandishi wa kiume walivyowasawiri wahusika wa kike katika tamthilia za Posa za Bikisiwa (Said Mohamed na Kitula King'ei) na Sudana (Alamin Mazrui na Kimani Njogu).

Mtafiti amebaini kuwa sifa chanya zimechukua asilimia kubwa ya jumla ya sifa zote nane (8). Sifa chanya ni 62.5% nazo hasi ni 37.5%. Hali hii inaonyesha kuwa waandishi hao wamewasawiri wahusika wa kike kwa mtazamo chanya. Kwa mujibu wa utafiti wake imebainika kuwa, licha ya kwamba waandishi wa kiume wameathiriwa na utamaduni wa jamii zao

wanaelekea kuwa na mtazamo chanya kwa wahusika wa kike. Hali hii huenda imechangiwa na mabadiliko ya mtazamo wa jamii katika karne hii ya ishirini na moja.

Mtazamo huu unadhihirika katika katiba ya Kenya 2010 ambayo imempa mwanamke nafasi kubwa katika uwakilishi wa kisiasa. Hali hii ya kuwakweza wanawake inadhihirika katika siasa kote ulimwenguni kama njia ya kubadilisha hali ya makundi ya watu wanaodhaniwa kuwa wametekelezwa duniani. Waandishi wa kiume wamewasawiri wahusika wa kike kwa kuwapa sifa nne (4) za kufanana, yaani waandishi hao wawili waliwapa sifa sawa. Sifa hasi ni moja (1) na sifa chanya ni tatu (3) ambazo zimechangia asilimia 75% ilhali hasi ni asilimia 25%. Kiwango cha kufanana cha waandishi wa kiume ni asilimia 50%. Ulinganisho huu umeonyesha kuwa waandishi wa kiume wameafikiana kwa kiwango kikubwa kuhusu sifa chanya za wahusika wa kike. Hali hii inasisitiza mitazamo chanya ya waandishi wa kiume kwa wahusika wa kike.

Kazi hii imemsaidia mtafiti kuelewa masuala ya mitazamo ya waandishi wa kike na wa kiume kuhusu wahusika wa kike. Vile vile,  kazi hii imemsaidia mtafiti kupata maarifa juu ya ufeministi wa ubada-ukoloni. Hata hivyo hili halikuwa lengo la mtafiti kwani utafitibwetu unajikita katika usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake.

Njogu na Wafula, (2007) wanaeleza kuwa uhalisia ulianza katika karne ya 19-20 na pia uliendelea kuathiri karne ya 21 ambapo mapinduzi ya viwanda yalikuwa yamefikia kilele kutokana na kuendelea kiteknolojia, na hivyo miji kupanuka haraka haraka na matatizo kuibuka na tabaka la wafanyakazi lilizuka. Karl Marx alianza kuzungumzia jamii kisayansi huku akibashiri ya kwamba mapinduzi ya makabwela yangetokea baadaye kama hatima ya historia. Hivyo uhalisia ulitokana na matatizo yaliyokuwa yakiwakabili watu. Matatizo haya yaliwafanya wanasanaa kuutuhumu uromansia.

Wamitila, (2002) anaeleza kuwa uhalisia huelezea aina ya mtazamo au tapo la kifasihi ambamo kazi za kifasihi huhifadhiwa na kueleza mambo ya msingi yanayohusu masuala ya kweli yaani uhalisia kama ulivyo katika jamii husika. Anafafanua kuwa waandishi wanaojikita katika msingi wa uandishi huu uakisi mambo halisi yaliyomo katika jamii kiuaminifu kwa kuibua wahusika, matendo pamoja na matukio halisi ya kijamii. Hata mambo wanayoyatungia katika kazi zao kama hayajatokea basi yanakuwa mbioni kutokea katika jamii lengwa. Vile vile, uhalisia unahusu nyanja mbalimbali kama vile uchumi, historia, jamii na mapinduzi. Uhalisia una msisitizo mkubwa kwenye msingi wa hali ya kiyakinifu ya maisha kama mazingira ya kuishi kuliko mawazo katika maisha ya binadamu.

Hivyo uhalisia ni uelezaji wa jambo fulani kiukweli kama linavyoonekana au kuchukuliwa ndani ya jamii. Kama ni jina linakuwa na maana ile ile inayotumika ndani ya jamii au kitu kina ukweli wa kuwepo kama

kilivyotumiwa na mwandishi wa kazi ya fasihi hata kama mwandishi ataweka ubunifu wake ila uhalisia unakuwa palepale. Mwandishi anaweza kutumia wahusika wa kubuni kuuelezea ukweli huo au anaweza kutumia wahusika halisi kama ataona haina madhara kwake.

Hata hivyo nadharia ya uhalisia ni nadharia iliyotokana na wahakiki wa Kimagharibi kama akina Aristotle na Plato na baadae akina Hegel. Katika utafiti huu mtafiti ameeleza namna wahusika wa kiume walivyosawiriwa katika riwaya teule kwa kuhusianisha na hali halisi ya sasa yaani dunia ilivyo kulingana na usawiriwaji huo katika riwaya teule.

Mihimili ya nadharia; kama zilivyoainishwa na Ntarangwi, (2004):

a) Uyakinifu: kuelezea mambo kulingana na hali halisi ya maisha.
b) Wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii
c) Usadikifu; yale anayoyaibuliwa katika jamii yawe yanasadikiwa na wasomaji
d) Mshikamano
e) Itumie sajili ambazo ni za kawaida

Nadharia hii imemsaidia mtafiti kuyabaini mambo ya kweli ya kiuana yanayowahusu wahusika wa kiume. Uhalisia unajidhihirisha kwa kutumika wahusika halisi na wa kubuni katika kueleza mambo halisi yanayotokea Tanzania na Kenya kama yalivyoainishwa na Zainabu Mwanga, Zainabu Burhani, Sheila Ryanga na Clara Momanyi katika riwaya zao.

Nadharia hii pia ni muhimu kwa kuwa inasisitiza juu ya ubunifu ambao ndio huongoza usawiri wa wahusika. Kwa kuwa riwaya ni sanaa inayotumia lugha kiubunifu, usawiri bora wa wahusika sharti uhitaji ubunifu wa hali ya juu. Kwa jumla, inaitambua riwaya kama sanaa isiyofua kuwekewa mipaka ya kiutunzi, na badala yake kuutambua ubunifu kama nyenzo muhimu ya kumwongoza mtunzi.

Kwa kufanya hivyo, nadharia hii inaupa uhakiki wa riwaya za Kiswahili mwongozo wa kitaaluma na kwa kuwachora wahusika katika misingi halisi inayojidhihirisha katika ulimwengu halisi ambapo ndipo hujenga mijadala ya kiusomi.

Ufaafu wa nadharia hii pia unatokana na misingi kuwa inaipa riwaya uwanda mpana wa kihakiki unampa mtunzi uwezo wa kuyapambanua ayaonayo katika jamii. Ni nadharia inayojaribu kujenga uwiano wa kitaswira katika mambo yawasilishwayo na waandishi katika kazi zao.

**1.8 Mbinu za Utafiti**

Ili kufanikisha malengo ya utafiti ni lazima mtafiti akusanye data zinazowezesha kujibu maswali ya utafiti husika. Kothari, (2008) anadahili kwamba mbinu za utafiti ni mwongozo uliopangwa kufuatwa katika kukusanya na kuchambua data ili kujibu maswali ya utafiti husika. Sehemu hii iliainisha mbinu mbalimbali ambazo zilitumika njeo katika ukusanyaji na uchambuzi wa data ili kujibu maswali ya utafiti.

### 1.8.1 Mahali pa Utafiti

Utafiti huu ni wa maktabani ambapo mtafiti amefanya Uchambuzi Matini ili kubainisha namna wahusika wa kiume walivyosawiriwa katika riwaya za Kiswahili. Yaani kufanya uchambuzi wa riwaya teule. Uchambuzi umehusisha riwaya za *Kipimo cha Mizani* na *Hiba ya Wivu* kwa upande wa Tanzania na Kenya zitatumika riwaya ya *Tumaini* na *Dago wa Munje* kama vyanzo vya kukusanyia data na taarifa za msingi katika utafiti huu. Data fuatizi zimekusanywa kutoka maandiko mbalimbali ambayo yamepatikana katika vitengo vya makusanyo ya 'East Africana' na makusanyo ya sayansi za jamii vya Maktaba Kuu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na maktaba kuu ya Chuo Kikuu cha Kenyatta. Maktaba nyingine ambazo zimetumiwa ni Maktaba Kuu ya Taifa pamoja na ile ya Taasisi ya Taaluma za Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na maktaba ya idara ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta.zimetumika hata maktaba za mtandaoni katika kusoma kazi na mbalimbali zilizoko mtandaoni juu ya wahusika wa kiume na wa kike pamoja na waandishi wa kike. Maktaba hizi zimechangia sana katika kutupatia data na taarifa zinazohusiana na nadharia ya riwaya kwa ujumla na mahususi kwa riwaya za Kiswahili. Si hivyo tu bali tahakiki mbalimbali zimesomwa kuhusu waandishi wa kike na pia kutuwezesha kupata maandiko mbalimbali yenye kueleza na kufafanua dhana ya wahusika wa kiume ili kushadidia usawiri wa dhana hiyo kama inavyosawiriwa katika riwaya teule.

Maktaba na taasisi zote zilizoainishwa kutumika katika utafiti wetu zinapatikana katika jiji la Dar es Salaam na jiji la Nairobi hivyo imekuwa

rahisi kufikika kwa gharama nafuu kwa kuzingatia kuwa mtafiti anasoma Chuo Kikuu cha Kenyatta akitokea Dar es Salaam. Data ambazo zimekusanywa kutoka maktaba na taasisi tajwa hapo juu zimesaidia kukazia dhana ya Usawiri wa wahusika wa kiume kama inavyosawiriwa katika riwaya teule na kuwezesha kujibu maswali ya utafiti.

### 1.8.2 Muundo wa Utafiti

Muundo uliotumiwa katika utafiti huu ni wa kimaelezo. Utafiti wa kimaelezo ni mtazamo ambao huchunguza sifa zinazobainika katika jambo linalochunguzwa. (Kothari, 2004). Kusudi lake ni kuchunguza jinsi mambo yalivyo katika mazingira fulani. Lengo kuu katika muundo huu ni kukusanya data na kueleza uhusiano wa vipengele mbalimbali vya data hiyo. Kwa kutumia muundo huu, namna mbalimbali kuhusu usawiri wa wahusika wa kiume kutoka riwaya teule zimebainishwa kwa kuzingatia misingi ya tamaduni za jamii husika. Na mwisho maelezo juu ya utafiti kwa jumla yametolewa.

### 1.8.3 Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli ni utaratibu anaoutumia mtafiti kupata idadi ya watoa taarifa (sampuli) kutoka katika idadi ya watu lengwa wa utafiti (Kothari, 2008). Katika kupata sampuli ya kufanyia utafiti, mtafiti ametumia usampulishaji kusudio ambapo mtafiti ameweza kupata data kwa kuzingatia malengo ya utafiti.

Babbie, (1999), anaeleza kwamba ni vigumu kwa mtafiti kushughulikia idadi kubwa ya wanajamii inayohusika katika utafiti wake hata kama anavutiwa na idadi hiyo ya vitafitiwa. Hivyo basi mtafiti hulazimika kuchagua au kuteua idadi maalumu ya watafitiwa/vitafitiwa ya kushughulikia katika utafiti wake. Idadi hiyo maalumu huitwa watafitiwa lengwa/vitafutiwa. Hivyo basi vitafitiwa lengwa katika utafiti huu ni riwaya nne ambazo ni; *Kipimo cha Mizani,* (2004), *Hiba ya Wivu,* (1997), *Tumaini,* (2006) na *Dago wa Munje,* (2008).

Mtafiti alitambua kuwepo kwa riwaya nyingine zilizokuwa na ukuruba wa kimaudhui na zile zilizohakikiwa lakini aliteua nne tu ambazo ndizo zililenga suala la wanaume kikamilifu. Riwaya hizi nne ziliteuliwa kama sampuli inayowakilisha nyingine zilizowasawiri wahusika wa kiume kwa mitazamo mbalimbali. Pamoja na hayo, mapitio ya maandishi yalidhihirisha kuwa idadi waandishi wa kike wa riwaya za Kiswahili ni wachache kuliko waandishi wa kiume. Mtafiti alikumbana na waandishi wa kike wachache sana kwa Kenya na Tanzania ambapo mmoja wa Kenya na mmoja wa Tanzania wote wameandika riwaya moja moja yaani Zainabu Mwanga na Sheila Ryanga japo wameandika kazi za tanzu nyingine mbali na riwaya. Wengineo mmoja akiwa wa Tanzania mwingine wa Kenya wameandika riwaya zaidi ya moja yaani Clara Momanyi na Zainabu Burhani.

Riwaya hizi zimechaguliwa kwa kutumia Usampulishaji Lengwa; yaani mtafiti ameteua vitafitiwa akitarajia kwamba vitampatia data na taarifa

zinazosaidia kujibu maswali ya utafiti wake. Riwaya hizi zimetumika kama vyanzo vya data na taarifa za msingi ambazo zimemwezesha mtafiti kujibu maswali ya utafiti kwa maana waandishi hawa ni wabobezi wa riwaya na wametumia utaalamu katika kuwachora wahusika wa kiume.

Sampuli lengwa, ni sampuli inayoteuliwa na mtafiti akiwa na imani kuwa, sampuli hiyo itampatia data anazohitaji na hivyo, akiteua sampuli tofauti na hiyo basi hatoweza kupata data anazohitaji kwa namna alivyolenga (Creswell, 2009). Mtafiti alichagua mada anayohitaji kuitafiti kulingana na uhitaji wake baada ya kusoma kazi mbalimbali. Baada ya kupata kazi zilizoandikwa na wanawake maana zilizoandikwa na wanaume hazihusiki kwa mujibu wa mada. Kwa vile mtafiti alilenga kutafiti kazi zilizoandikwa miaka kuanzia 1996 na hivi karibuni ndipo akajikita katika riwaya teule maana zilionekana zinakidhi vigezo kwa kuwa vitafitiwa kulingana na mada ya utafiti.

Waandishi wa riwaya teule wanatoka katika jamii tofauti na pia kazi zao zimeandikwa nyakati tofauti na mambo waliyoyaandikia ni tofauti ambayo ndiyo yalimpa mtafiti mawanda mapana ya kupata data za kukamilisha malengo na kujibu maswali ya utafiti. Mtafiti amezingatia matukio yaliyofanywa na wahusika wa kiume katika hizi riwaya ili kuweza kuchunguza namna waandishi walivyowasawiri wahusika hao.

Data ambayo imechanganuliwa mahsusi inahusu vifungu vinavyoeleza taarifa zilizotupa dhamira za riwaya husika kwa kuzingatia mtazamo ya waandishi wa

kike kuhusu wahusika wa kiume, vifungu vinavyohusu usawiri wa wahusika wa kiume kupitia yanayoelezwa na mwanandishi yanayosemwa na wenyewe wahusika na yanayosemwa na wahusika wengine juu ya wahusika lengwa. Isitoshe, data ya kimsingi imetokana na jinsi ambavyo wahusika wa kiume wamechorwa kwa kutumia lugha, ishara na vipengele mbalimbali vya mawasiliano ambavyo waandishi hawa wametumia.

### 1.8.4 Ukusanyaji wa Data

Mbinu za kukusanya data Ili kupata maelezo ya kimsingi kuhusu yaliyoandikwa juu ya mada na nadharia iliyoongoza utafiti huu, mtafiti alisoma vitabu, makala na tasnifu mbalimbali zilizoandikwa na wataalamu na watafiti mbalimbali. Upekuzi wa majarida na vitabu mbalimbali maktabani ulimwezesha mtafiti kufichua maoni na mawazo ya watafiti wangine kuhusiana na masuala ya wanawake pamoja na kukadiria nadharia iliyofaa kuongoza utafiti huu. Mtafiti pia alidondoa na kuainisha sifa mbalimbali za wahusika wa kiume kama walivyosawiriwa na mwandishi katika kila riwaya. Vifaa vya kukusanyia data. Mojawapo ya vifaa vilivyotumiwa kukusanyia data ni usomi. Mtafiti alisoma riwaya nne zilizoteuliwa pamoja na vitabu vya maelezo kuhusu nadharia. Upekuzi ulitumika kutafuta makala katika maktaba na kwenye mtandao wa tovuti kuhusu nadharia na usawiri wa wamaume katika fasihi. Udurusu ulitumika katika kutafuta yale yaliyokuwa yameandikwa kuhusu usawiri wa mwanaume na wataalamu mbalimbali. Aidha, mtafiti alitumia uandishi kama kifaa cha kumwezesha kuyanakili yale yote ambayo yameandikwa katika utafiti huu.Kifaa kingine kilichotumiwa na

mtafiti ni uchunguzi. Mtafiti alichunguza usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya zilizoteuliwa.

Ukusanyaji wa data katika utafiti huu umehusisha mbinu ya Uchambuzi Matini ambapo riwaya teule zimesomwa na kuchambuliwa na kupata data ya kujibu maswali ya utafiti na malengo yake. Pia makala na tasnifu mbalimbali kuhusu waandishi wa riwaya teule pamoja na mada zinazohusu masula ya kiuana zilisomwa na kupata hoja mbalimbali zilizohusu utafiti huu. Kupitia mbinu hizi tumepata kuelewa ni kwanini waandishi wa riwaya teule wamewasawiri wahusika wa kiume kama walivyowasawiri, taswira zinazotumiwa kuwasawiri wahusika wa kiume, dhamira zinazowasilishwa na mitazamo inayoibuliwa na wahusika wa kiume katika riwaya teule.

### 1.8.5 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data iliyotokana na uchambuzi wa riwaya nne pamoja na maandiko yaliyochangia kuimarisha utafiti huu yalichunguzwa kulingana na madhumuni ya utafiti. Data hiyo ilichanganuliwa katika hatua zifuatazo; kwanza, mtafiti alisoma riwaya za waandishi wa kike kisha akadondoa na kuorodhesha sifa mbalimbali kwa mujibu wa kila mwandishi. Hatua ya pili ilikuwa ni kuainisha sifa zilizodondolewa kutoka katika kila riwaya.

Mtafiti alipanga data katika makundi ya upande mmoja hasi na upande wa chanya. Aidha idadi ya sifa hizo hasi na chanya zilitumiwa kama kigezo cha kuamulia mtazamo wa mwandishi anayehusika katika kumsawiri mhusika wa

kiume. Sifa hasi zilitumiwa kuashiria kuwa mwandishi husika alikuwa na mtazamo hasi kumhusu mhusika wa kiume. Kwa mujibu wa utafiti huu, mtazamo hasi ni ule uliomwangalia mwanaume kama mtu dhalili akilinganishwa na mwanamke na pia kumuumba aonekane kama mtu mbaya au aliyechukiza kwenye macho ya jamii. Hali kadhalika, pale ambapo mwandishi alikuwa amempa mhusika wa kiume sifa zilizomjenga kama mwenye hadhi sawa na mwanamke au kupewa sifa zilizopendeza na kutompunguzia heshima yake, huo ulichukuliwa kuwa mtazamo chanya kwa mhusika aliyerejelewa.

Kwa kiwango kikubwa, kigezo cha kuamulia uhalali wa sifa ziwe mbaya (hasi) au nzuri (chanya) kwa mhusika fulani kulitegemea tathmini na ukadiriaji wa mtafiti. Awamu ya mwisho ilikuwa ni kulinganishwa kwa sifa chanya na hasi ili kubainisha mitazamo ya kila mwandishi juu ya wahusika wa kiume.

### 1.8.6 Uaminikaji na Utegemewaji wa Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanaaminika kwa sababu zifuatazo; kwanza, mtafiti amesoma riwaya nne zilizochunguzwa na kuthibitisha kila maoni aliyotoa kwa kudondoa au kunukuu mifano kutoka kwenye matini pamoja na kuonyesha ukurasa unaohusika. Vile vile, utafiti huu ulisimamiwa na kuelekezwa na wasimamizi wawili ambao waliusoma na kuhakikisha kuwa maoni yaliyotolewa na mtafiti yanaweza kutegemewa.

Kwa kuwa usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili umechunguzwa kutoka katika riwaya nne teule, riwaya hizo zimesomwa na habari zinazohusu wahusika wa kiume zimepatikana na kunakiliwa ili ziweze kutumika katika uchanganuzi wa data. Data iliyokusanywa imechanganuliwa kwa kutumia mihimili ya nadharia zilizoainishwa yaani nadharia ya ujifunzaji wa kijamii, nadharia ya mwanaume mpya na ya uhalisia. Hata hivyo zimeainishwa kulingana na mwandishi husika. Taswira mbalimbali za mwanaume zilizojitokeza katika kazi za fasihi zimeelezwa wazi kulingana na tofauti za kitamaduni za waandishi.

Vile vile, data zilizokusanywa zimeainishwa katika makundi kwa kufuata vipengele vilivyoainishwa na waandishi katika usawiri wa wahusika wa kiume kama ilivyotafitiwa. Vipengele hivyo ni pamoja na dhamira zinazowasilishwa na wahusika wa kiume, taswira zinazotumiwa na waandishi kuwasawiri wahusika wa kiume na mitazamo inayoibuliwa na wahusika wa kiume pamoja na kufanana na kutofautiana kwa waandishi wa riwaya teule.

Aidha, data hizo zimechanganuliwa kimakundi kwa kuzingatia tafsiri ya vipengele hivyo vinavyohusu wahusika wa kiume katika maisha halisi katika jamii. Hapa inamaanisha kumekuwa na matukio yanayohusu maudhui ya kiutamaduni, ndoa, kielimu na kimaadili. Uchanganuzi ulizingatia ulinganisho katika matumizi ya vipengele tajwa katika waandishi wanawake walioteuliwa katika nchi ya Kenya na Tanzania.

### 1.8.7 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo yamewasilishwa kwa njia ya mkabala wa maelezo katika maandishi ambapo utafiti umefanyika maktabani. Maelezo yametumiwa kuweka bayana na kushadidia yale yaliyojitokeza kwenye riwaya teule.

Mkabala huu unaelezwa na Young, (1984) kuwa ni mbinu ya uchambuzi wa data ambayo haihusishi mahesabu bali maelezo tu ndio hutolewa kuhusiana na data za utafiti zilizokusanywa. Matokeo yaliwasilishwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti kwa namna data zake zilivyokusanywa. Njia hii humwezesha mtafiti kurahisisha uwasilishaji wa matokeo na kwa kutumia muda mfupi katika kukamilisha malengo ya utafiti.

### 1.8.8 Maadili ya Utafiti

Mtafiti alipata kibali kutoka kwa kamati ya Chuo Kikuu cha Kenyatta inayoshughulika na utathmini wa maadili ya utafiti kabla ya kuanza kazi ya kutafiti. Pia, alianza utafiti baada ya kuandika pendekezo la utafiti ambalo liliidhinishwa na wasimamizi wawili walioteuliwa rasmi na Chuo cha Kenyatta. Utafiti huu haujavunja au hata kuingilia haki za waandishi wala kazi zao zilizochunguzwa. Aidha, mtafiti aliwatambua wataalamu wote ambao aliwanukuu na kushirikisha mawazo yao katika utafiti wake. Halikadhalika, aliorodhesha marejeleo na viambatisho mwishoni mwa sura ya sita ili kukidhi kigezo cha maadili ya utafiti.

### 1.8.9 Hitimisho

Mtafiti amefafanua aina ya data iliyokusanywa pamoja na kuonyesha mbinu zilizotumika kukusanyia na kuchanganulia data hiyo. Pia, ameeleza vifaa vilivyotumika kukusanyia na kuchanganulia data. Aidha, msingi wa kidhana umechorwa. Halikadhalika, ameonyesha jinsi utafiti huu ulivyozingatia maadili pamoja na kueleza sababu zinazoufanya kuaminika na kutegemewa.

Sura imeangazia usuli wa mada na suala la utafiti. Imeangazia pia maswali ya utafiti, malengo ya utafiti,sababu za kuchagua mada, umuhimu wa utafiti, upeo wa utafiti, msingi wa nadharia. Imejadili pia yaliyoandikwa kuhusu mada, mbinu za utafiti, usampulishaji, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa matokeo.

# SURA YA PILI

# DHAMIRA ZILIZOWASILISHWA KUPITIA KWA WAHUSIKA WA KIUME

## 2.0 Utangulizi

Katika sura ya kwanza tumezungumzia utangulizi wa utafiti unaojumuisha usuli wa mada, suala la utafiti,malengo ya utafiti na maswali, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, udurusu na tafiti za awali, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti. Sura hii tumechanganua dhamira mbalimbali zinazojitokeza katika riwaya teule ambazo *ni Hiba ya wivu*, *Kipimo cha Mizani*, *Tumaini* na *Dago wa Munje*. Wahusika ni watendaji katika kazi ya fasihi hivyo tukitaka kuwaelewa ni muhimu kuangalia mambo wanayoyatenda na mitindo ya lugha ambayo waandishi waliyoitumia kuelezea wahusika hao. Wahusika wa kiume ambao ndio walengwa wa utafiti huu, ndio waliobeba maudhui na hulka fulani. Kabla ya kufanya hivyo tumeeleza dhana ya dhamira kwa ujumla na kisha kujadili dhamira zinazopatikana katika kila riwaya iliyoteuliwa.

## 2.1 Dhana ya dhamira na wahusika

Wamitila, (2008), anaeleza kuwa dhamira ni wazo kuu linaloitawala kazi ya kifasihi kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Wazo hili hukuzwa kwa njia zilizo wazi kwa kujibainisha katika kazi nzima uisomapo. Katika kuchanganua dhamira hizo, nadharia ya ujifunzaji wa kijamii na mwanaume mpya zimetumika kuonesha namna mhusika wa kiume anavyochorwa katika kuziwakilisha dhamira husika. Hata hivyo nadharia ya uhalisia imetumika

kama kielelezo cha kuupima uchoraji huo wa mhusika wa kiume kama unaendana na hali halisi kulingana na jamii inayozungumziwa.

## 2.2 Dhamira katika Riwaya za Kipimo cha Mizani, Hiba ya Wivu, Dago wa Munje na Tumaini

Katika riwaya teule zimebainishwa dhamira mbalimbali kulingana na kile alichokilenga mwandishi kukieleza kwa jamii lengwa. Dhamira ziko nyingi ila katika sura hii zimechambuliwa chache ambazo zimeonekana kutawala katika kila riwaya miongoni mwa nyingine nyingi zilizoainishwa katika riwaya teule.

### 2.2.1 Dhana ya Ndoa katika Riwaya Teule

Katika riwaya ya *Kipimo cha Mizani* kumekuwa na ndoa kuu za aina mbili ambayo ni ya Halima na mumewe Amini pamoja na ndoa ya Umari na mkewe Mariyamu. Amini ni mtu wa kujituma sana na pia ana mshauri mzuri ambaye ni mkewe aitwaye Halima. Halima ni mama wa nyumbani aliyefanya kazi zake kwa bidii kuilea familia yake kwa kumtunza mumewe na watoto. Alimwamini sana mumewe na wala hakuwa na wivu naye hata alipochelewa kurudi nyumbani maana aliujua uchapakazi wake. Amini alikuwa mwajiriwa na pia anafanya kazi zake binafsi kwa ajili ya kupata kipato cha ziada. Anapopata pesa anaipangilia hadi izae zaidi. Alipopata mtaji mkubwa akafungua kiwanda chake kilichosimamiwa na mzee Hassan.

> Mfano: Amini alifanya jitihada kubwa mpaka akapata pahala ambapo aliona panamfaa kwa kuanzisha kiwanda chake. Alikodi banda lililokuwa tupu na ambalo mwenyewe alivyokuwa halitumii, alimkodisha kwa bei nafuu. Sasa alikuwa na tatizo la ‘nani wa kumwajiri

> kuangalia kazi ile wakati yeye yuko kazini?' Halima alimshauri, "Unaonaje ukimtafuta mzee Hasani?" (Uk. 35).

Kutokana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya ujifunzaji wa kijamii unaosema kuwa: ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Inaonesha kuwa kutokana na utamaduni wao, majukumu aliyokuwa nayo Amini katika ndoa yake ni sawa kabisa. Alipaswa kuiangaikia familia yake ipate kila hitaji. Kutokana na utambuzi wake pia elimu yake vilevile alipaswa kuwa na maisha mazuri na ndio maana aliangaika kufungua miradi mbalimbali ili kukuza kipato. Huu ni muktadha wa kijamii kuwa tabia za uwajibikaji kwa mwanaume kwa ajili ya familia yake ni sawa kabisa na ni kutimiza wajibu.

Vile vile, ndoa ya Umari ni ndoa ya kutaka kujionyesha ni watu wa hali ya juu ilhali ni watu wa maisha ya kati. Umari hana ushauri mzuri kutoka kwa mkewe Mariyamu. Wamekuwa wakitafuta pesa kwa ajili ya kutumia hasa kwa kufanya sherehe zisizo na ulazima ili mradi wajionyeshe kuwa wana maisha ya hali ya juu.

> Mfano: Umari alipolipwa pesa zake na Amini; walishauriana yeye na mkewe, Mariyamu. Wakaamua kutafuta nyumba nzuri, iliyo mpya, yenye nafasi nzuri, tena iwe ya ghorofa, ijapo ghorofa moja, kama alivyotaka Mariyamu. (Uk. 55).

Mariyamu alinunua vitu vyote vya ndani vipya akiwa na maana kuwa nyumba mpya lazima iwe na vitu vipya na sio vya zamani. Umari alipinga ila mkewe hakukubali na ikawa hivyo. Hata hivyo hiyo haikutosha akaona wafanye sherehe kubwa ya kualika watu.

> Mfano: wakati huo pia ilimjia fikra nyingine. Akasema, “Unajua! Unaonaje tukishaitengeneza nyumba yetu na kuipamba vizuri, tufanya hafla kubwa. Tualike watu, kwa kufungua nyumba yetu hii?” Umari baada ya kupinga kidogo, alikubali. (Uk. 56).

Mariyamu na Umari wamekuwa wakiishi maisha ya kujionyesha sana kuwa hawana shida wakati walikuwa wanaishi nyumba ya kupanga. Maisha yao yalikuwa ya kuoneana sana wivu hasa mmojawapo anapochelewa kurudi nyumbani maana wote walikuwa wakifanya kazi za kuajiriwa. Ndoa hii imekuwa ya mashindano sana na ndio maana baada ya kufariki Amini, Umari aliangaika sana ili aweze kumiliki mali za kaka yake alizozichuma pamoja na familia yake badala ya kuangaika kutafuta za kwao.

Kutokana na nadharia ya uhalisia katika mhimili wa kwanza usemao: uyakinifu; kuelezea mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Umari alizoea maisha ya anasa pamoja na mkewe Mariyamu, walikuwa hawana namna nyingine ya kufanya ili kumiliki mali za Amini zaidi ya kufanya ulaghai walioufanya. Ilibidi kutumia uongo ili wamiliki mali zisizokuwa za kwao. Huu ni utamaduni wa watu wasiopenda kujituma kufanya kazi, hupenda kuishi maisha ya kiwango cha juu ilhali hayaendani na kipato chao.

Katika riwaya ya *Hiba ya Wivu* kuna ndoa za aina mbili. Ndoa ya Farida na mumewe Ihucha ambaye ni mfanya biashara mkubwa wa saa. Farida kabla ya kuolewa na Ihucha alifanya kazi katika kiwanda cha saa ambako walikutana na Ihucha aliyekuwa akija kwa ajili ya biashara ya saa. Baada ya kuoana Ihucha alimwachisha kazi Farida ili wasaidiane katika mauzo.

Farida na Ihucha walipendana sana na kusikilizana ila Farida alikuwa na wivu sana na mumewe hasa alipochelewa kurudi nyumbani, alihisi yuko kwenye mambo ya hovyo kumbe yuko kwenye vikao na wafanya biashara wenzie wakipeana mbinu za kuboresha biashara zao. Ihucha alimwonea sana huruma Farida hasa alipoambiwa na majambazi kuwa wamemteka Farida, walimpa masharti ya kutoa pesa ili wamwachie Farida na alifanya hivyo akihofia mkewe kudhuriwa na wateka nyara. Ray alimdanganya Ihucha naye akafanya kama alivyoelekezwa. Ihucha ni mwanaume aliyemsikiliza mkewe. Huyu ni mwanaume mpya anayeshauriwa katika nadharia ya mwanaume mpya., ni mwanaume anayejua wajibu wake kwa mkewe na kusikiliza ushauri wa mkewe na kumsaidia kazi mbalimbali katika familia. Mwandishi anaeleza:

> "Farida, una hakika kuwa mumeo anakupenda sana?" Ndio tunapendana sana, tena ni mwaka jana tu tumefunga ndoa," machozi yalimdondoka………….. "Bwana Ihucha: Mkeo tumemteka nyara jana usiku. Kwa usalama wa maisha ya mke wako, unatakiwa utoe shilingi elfu hamsini kabla ya saa tano kesho asubuhi. Hizo pesa zifunge vizuri, uzipeleke bonde la Mkwajuni chini ya Mbuyu. (Uk. 19).

Vile vile, kuna ndoa ya Sikujua ambaye ni dereva wa teksi kama alivyo Ray. Sikujua alikuwa amehukumiwa kunyongwa baada ya kumuua rafiki yake aliyeitwa Pondamali Malipesa. Ndoa hii ilikuwa na shida maana Sikujua alipotoka kifungoni kwa msamaha wa Rais alikuta mkewe katoroka. Hata Sikujua alikuwa na mpango wa kuachana naye kwa maana alihisi ndiye alitoboa siri za mambo yake aliyokuwa akiyafanya hadi akakamatwa na kutiwa hatiani. Sikujua alikuwa mtu wa kujirusha na marafiki zake. Alianzisha mahusiano mapya na Fatuma na hakuwa mkweli kwa

Fatuma.Hakutaka ajue kuwa hana pesa na wakati mwingine aliacha kula ili Fatuma ale peke yake asilale njaa. Mwandishi anasema:

> Lakini pesa alizozipata kutokana na teksi ziliishia kulipa deni la mzee Fundisha alilolikopa kuwahonga Pwagu na Pwaguzi. Laiti Fatuma angeijua siri hiyo na ulofa wa Sikujua, angemwambia wakale gengeni kwa mama ntilie halafu waje kumalizia na bia hapo Mtoni hoteli. Lakini Fatuma hakujua, aliamini kwamba mpenzi wake kweli anatumia dawa, hivyo hanywi bia wala hajisikii kula. (Uk. 2).

Katika nadharia ya mwanaume mpya katika mhimili usemao; kuwaona wanawake kama viumbe sawa na wanaume kwa kuwaheshimu na kuwapenda katika kila nyanja wanazokuwepo. Katika riwaya hii, ndoa ya Ihucha inapata itilafu kutokana na hali ya kukosa uaminifu kutokana na wivu. Farida anapendwa na kuthaminiwa na mumewe ila anaamua kumfuata mumewe ila anakosea pale anapojificha ili mumewe asimwone pale hotelini kuwa kamfuata. Uchanya wa matendo ya Ihucha unadhihirishwa na Farida mwenyewe kumkuta mumewe akiwa na wafanyabiashara wenzie. Ihucha anadhihirisha kuwa ni mwanaume mpya anayesisitizwa na nadharia ya mwanaume mpya kwa kumsamehe mkewe na kuendelea kumpenda baada ya kuambiwa ukweli na Farida na maisha yao yakaendelea kama kawaida.

Hoja hii ya msamaha katika ndoa imeelezwa na Ligopola, (2012) amejadili kuhusu nafasi ya mwanamke ambacho ni kipengele kimojawapo cha maudhui katika kazi za fasihi. Ameeleza kuwa waandishi wa kazi za Fasihi hutumia kipengele cha maudhui kueleza mambo mbalimbali yaliyomo katika jamii

kama vile elimu, malezi matabaka na ndoa ambayo nguzo yake kuu ya kuimarika ni msamaha katika familia.

Vile vile, Sikujua anakuwa mwanaume mpya baada ya kutoka jela maana kabla alikuwa na roho ya kikatili kwa kuamua kumuua rafiki yake kwa sababu ya kudhulumiwa pesa. Baada ya kuhukumiwa kunyongwa mkewe alijua kabisa mumewe hatarudi na ndio maana akatoroka. Matendo ya Sikujua yalikuwa hasi na ndio maana aliazimia kuwa angeachana na mkewe mara tu akitoka kifungoni kwa kudhani kuwa mkewe ndiye aliyetoboa siri za uovu wake. Sikujua anakuwa mpya baada ya kuanzisha mahusiano mapya na Fatuma, anakuwa wa kujali na kumthamini mpenzi wake na kuacha kile kidogo alichonacho ale Fatuma. Nadharia ya mwanaume mpya inatuonesha mwanaume aliyebadilika na kuacha ubabe na kuwa wa kumthamini mwanamke na kumjali katika nyanja mbalimbali. Inawataka wanaume kama Sikujua wa kabla ya kufungwa wawe wanaume wapya ambao watawapenda wake zao kwa dhati na kutambua nafasi zao kama wanaume katika familia zao.

Wazo hili linaungwa mkono na wataalamu mbalimbali akiwemo Connell, (1987) ambapo anaeleza kuwa si kila mwanaume mbabe katika jamii anafaidika na ubabe huo bali husukumwa na mifumo ya jamii zao hivyo inapobidi wabadilike ili kuleta furaha katika familia badala ya kuendeleza kutoelewana miongoni mwao na kuleta maumivu.

Katika riwaya ya *Dago wa Munje* kuna ndoa ya baba na mama Dago ambao walitunza familia yao ya watoto watatu kwa kuwalea katika maadili mema. Walifanya kazi zao bila kufuatiliana wala kuoneana wivu. Mama Dago hudamka na kuraukia makuti na kuyauza wakati baba Dago akitafuta kibarua chochote ili kupata pesa ya kuitunza familia yake. Mama Dago anapenda sana kufuatilia habari za mwanae anapokuwa na marafiki zake. Kwa mfano Rashidi aliporaukia kwa akina Dago ili amtaarifu wakafue mtoni pamoja na marafiki zake. Dago hakupenda kabisa na akaonesha kukasirika na kumkatalia Rashidi kwa kumjibu vibaya naye Rashidi akakasirika. Walipoagana akiwa hayuko sawa, mama Dago aliingilia kati kujua kwanini hayuko sawa Rashidi. Hata hivyo hakuujua ukweli. Mwandishi anaeleza:

> "Mambo ya vijana wa siku hizi hata hayaeleweki. Sasa ni nani mkweli?" Mama alishangaa akabaki kufikiria. Aliona pengine kulikuwa na sababu nyingine, ingawa hakuwahi kuwaona vijana hawa wawili wakiteta utoto wao wote. Hata hivyo, hakutaka kumsumbua Dago kwa kumwamsha na kuuliza upande wake wa habari. (Uk. 141).

Wako wanandoa kama akina mama na baba Dago ambao wanakuwa na pilika za kazi zao bila kuwafuatilia watoto wao na kupata ukweli ili waweze kuwasaidia. Kwa mfano mama Dago alithamini sana kazi yake ya kusuka makuti asubuhi ile badala ya kufuatilia ugomvi wa watoto wao pamoja na mwenendo wa tabia kwa ujumla ili kuwasaidia. Hata baba Dago alikuwa mtaani anakimbizana kutafuta vibarua vya kufanya.

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili wa tatu usemao: ujifunzaji unahusu kuchunguza kupata habari kutokana na ule uchunguzi

na kuunda maazimio kuhusu utendakazi wa hiyo tabia. Baba na mama Dago wanakuwa na pilika zao na wanazijali badala ya kuwajali watoto wao na kuwafuatilia maendeleo yao ya shule. Dago anakuwa mtoro wa kudumu na tabia za kuwa mchafu na kutofuatilia masomo ila wazazi wake hawana taarifa. Tabia hizi za wazazi wa Dago zinategemea historia yao pamoja na tamaduni zao za kijamii zilizowakuza. Kwao elimu waliipenda kwa ajili ya watoto wao ila ufuatiliaji hawakuuweza kulingana na pilika zao za kijamii. Nadharia hii inawataka kuweka maazimio ya kazi na kuwa wafuatiliaji wa tabia zinazoibuka nje ya mafundisho ya kijamii ili kujua chanzo na namna ya kuzibadilisha. Dago anakuwa na tabia ambazo wazazi wake hawazijui kabisa.

Hata hivyo katika uhalisia kwa kuegemea katika mhimili usemao: uyakinifu; kuelezea mambo kulingana na hali halisi ya maisha, hili linadhihirishwa. Kutokana na hali ngumu wa maisha waliyokuwa nayo wazazi wake Dago iliwapelekea kuangaikia kutafuta mahitaji ya familia kama chakula na siyo kufuatilia maendeleo ya watoto wao shuleni. Baba yake alikuwa akitafuta vibarua na mama yake alikuwa akiraukia kutafuta makuti ya kusuka.

Hoja hii inafafanuliwa na Mazingwa, (1991) ambapo anaeleza kuwa haya yote yana sababishwa na athari za utandawazi katika jamii zetu na kuwafanya wanajamii kujikita katika mambo mapya na kuacha mambo mengi ya kitamaduni ikiwemo kulea watoto. Anasisitiza zaidi watu

kutoacha kabisa utamaduni wao hasa majukumu ya kifamilia kama vile kulea na kuhudumia familia kwa sababu tu ya utandawazi. Utandawazi uturahisishie kuyatenda yote na siyo kuyaacha ya msingi na kupalilia mmomonyoko wa maadili yetu yaliyotukuza.

Katika riwaya ya *Tumaini* kuna ndoa za aina mbalimbali. Kuna ya Bi Amina na mumewe mzee Masumbuko ambaye alikuwa mlevi na mbabe na aliogopwa na kila mtu kijijini kwao. Bi. Amina alivumilia tabia za mumewe na hakuweza kupinga maamuzi ya mumewe hivyo kila alichokisema mumewe ndicho kinatekelezwa. Ndoa hii kwa Bi. Amina ilikuwa kama utumwa. Hawa ni wazazi wake Tumaini ambao walishikilia mila na desturi zao. Mwandishi naeleza:

> Aidha, alipoingia nyumbani, nyumba nzima iliingia tafrani kwani alipasuka kama radi, huku akiulizia chakula kwa hasira utadhani alishikiwa shokoa katika ulimaji wake ulioishia ulevini………… Kwa upande wa mkewe Amina alikuwa mwanamke kinyamale, mwingi wa subira na uvumilivu. Huenda tabia hii ilitokana na vishindo vya mumewe vilivyomwingiza katika ngome ya unyamavu huku akitii amri za mumewe kwa lazima kama ibada. (Uk. 13).

Amina alitii kila alichoambiwa na mumewe hata kama kinamuumiza. Haya ndiyo maisha ya ndoa ya Amina maana alijikuta anaishi maisha ya ndoa isiyokuwa na uhuru kwa kuhofia ukali wa mumewe mzee Masumbuko. Hata tamaduni za jamii yake zilimfunga mama yake akawa hana uhuru wa kukataa hata alivyoona havifai. Tumaini alilazimishwa kutii baadhi ya mambo kwa

sababu tu na mama yake Tumaini alikuwa akiyatii ingawa Tumaini hakuweza kufanya hivyo.Mwandishi anaeleza:

> Hana budi kutii masharti ya jamii yake, masharti ambayo hata mama yake mzazi hakuwa na uwezo wa kuyapinga. Pengine hayo ndiyo yalimtia mamake hamaki alipokuwa akimshauri? Tumaini alijiuliza huku nyavu za mawazo zikishindana akilini mwake. (Uk. 22).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao; ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamiii.Hii inaonesha kuwa jamii ya Amina ilikuwa na mielekeo ya kumfanya mwanamke kuwa mtii kwa kila jambo linalotoka kwa mumewe hata kama linamuumiza. Majukumu ya kifamilia yalitekelezwa na mumewe kama tamaduni zinavyowaelekeza ingawa ilimpa nafasi ya kutawala maamuzi yote ndani ya familia bila kumpa nafasi mwanamke. Mzee Masumbuko alikuwa mlevi na mbabe kiasi kwamba wanajamii nao walimwogopa katika mahusiano ya kawaida ya kijamii. Hali hii ilipelekea hata watoto wake kumwogopa akiwemo Tumaini. Familia haikuwa na ushirikiano katika maamuzi zaidi ya kutekeleza kinachoamuliwa na mzee Masumbuko. Jamii ndiyo inajenga mchakato wa tabia za mtu anazojifunza kulingana na jinsia yake, inapokuwa ambavyo haikubaliani ndiyo humrejesha katika mstari unaotakiwa. Na hapa ndipo mhimili wa nne unapohusika: vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Hii inaonesha kuwa mtu anapojifunza visivyokubalika katika jamii yake ndipo vishawishi hutumika ili kumrejesha katika yale yanayokubaliwa katika jamii yake.

Hoja hii inafafanuliwa na Renzetti, (2012) kuwa mtu anajifunza mambo mbalimbali ila misingi inayoongoza tabia zake ni ya kijamii, tabia nzuri hutuzwa na kuendelezwa na mbaya hupigwa vita kwa kutoa adhabu ili kuikomesha na hapo ndipo kujifunza kwenyewe.

Vile vile, kuna ndoa ya Halima na mumewe Shabani. Hawa walisikilizana na kufanya kazi kwa kushirikiana na pia kwa kufuata mgawanyo wa kazi. Shabani hakuwa na elimu kubwa ila alipenda sana kusoma vitabu kwa hadithi alipenda sana mwanae Riziki asome shule kinyume na mzee Masumbuko ambaye alithamini tamaduni za kuozesha watoto na kutothamini elimu. Hata Tumaini alipotoroka nyumbani kwao alikimbilia nyumbani kwa mamake mdogo Halima na mumewe Shabani na walimuunga mkono kwa kuzikimbia tamaduni ambazo zingemzuia kusoma. Walimsomesha mpaka chuo kikuu. Kwa kusikilizana waliweza kuwa na maendeleo. Mwandishi anaeleza:

> Hata hivyo, Shabani ni mkulima hodari aliyemiliki mashamba mawili. Aliyahudumia na mkewe, na mavuno ya ziada waliyopata waliyauza ili kumsomesha mtoto wao wa pekee Riziki. (Uk. 11).

Nadharia ya mwanaume mpya katika mhimili wa kwanza usemao: kusaidia wake zao na wanawake wengine katika jamii kujiendeleza kielimu na kikazi. Hii inaoneshwa na Shabani kama mwanaume mpya ambaya anashirikiana naye katika shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi pamoja na kuwasomesha watoto wa kike Riziki na Tumaini hadi elimu za juu. Familia ya Shabani iliachana na tamaduni za kumgandamiza mtoto wa kike na kumfanya kuwa tegemezi kwa mwanaume maisha yote. Hoja hii inaungwa mkono na Morell, (2001) anaeleza kuwa mwanaume mpya si wa kumsaidia

tu mkewe na wanawake wengine katika mambo ya elimu na kazi tu bali awe tayari kufanya kazi za nyumbani kama kuosha vyombo na kulea watoto bila kuogopa kuchekwa na watu waliomzunguka. Kazi zote hizi alizifanya Shabani kwa uwazi kabisa na hakuna aliyeingilia maamuzi yake katika familia yake na ndio maana walikuwa na maendeleo tofauti na familia ya Mzee Masumbuko.

Katika nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao; uyakinifu: kueleza mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Jambo hili linajidhihirisha katika riwaya hii kupitia familia hii ya Shabani na Halima. Hawa walidhihirisha kuwa, kulingana na hali halisi ya maisha, elimu ni jambo la muhimu sana kwa jamii ya sasa. Hali ya masikilizano katika ndoa yao na kuithamini elimu, iliwapelekea kumpokea Tumaini mara alipokimbilia kwao akikwepa kulazimishwa kuolewa.

Kwa hiyo, elimu ni ya msingi sana kwa watoto wa kike na wa kiume na ndio maana mzee Sahabani hakubagua watoto kwa jinsia zao. Tumaini alipokimbilia kwao walimpa msaada wa kumsomesha sasa ndiye amekuwa msaada kwa familia yake akiwemo mdogo wake Idi ambaye alikuwa akiwadharau dada zake.

### 2.2.2 Uchapakazi au Bidii ya Kazi katika Riwaya Teule

Katika riwaya ya *Kipimo cha Mizani*, Amini amechorwa kama mchapa kazi. Katika ofisi aliyokuwa akifanyia kazi pamoja na kazi zake binafsi yaani

kiwandani. Vilevile mzee Hasani naye alikuwa mchapakazi tangu akiwa ameajiriwa na hata alipostaafu kazi.

> Mfano: Amini alimjua Hasani kuwa ni hodari wa kazi. Kabla ya kustaafu, aliwahi kufanya kazi katika moja ya ofisi za serikali. Alikuwa ni tarishi- hupeleka barua katika idara mbalimbali na katika ofisi nyingine zilizo nje. Lakini baada ya kumaliza kazi zake, saa za jioni, alikuwa na biashara zake ndogo ndogo. (Uk. 36).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao; mwanafunzi si mpokezi tulivu wa habari, utambuzi mazingira na tabia vinaathiriana katika upataji wa habari wa mwanafunzi. Hii inaonesha namna ambayo Amini aliitumia elimu yake kumtambulisha kupitia uchapaji kazi wake akiwa kazini. Hata hivyo alikuwa na mahusiano mazuri na wenzie kazini hata katika jamii. Ndio maana hata katika kusimamia kazim zake binafsi za shamba aliwatumia wanajamii wakawa wanamsaidia na wakati mwingine kumhitaji aende kule shamba mara inapobidi ila kazi zake zote walizisimamia wao.

Rajabu alipoacha shule alikaa tu nyumbani bila kazi ya kufanya ila kwa vile mama yake anafahamu vizuri alivyo na bidii ya kazi aliamua kumwombea kwa Amini ili apate kujifunza ufundi. Riziki aliongea na Halima ili amwombee nafasi hiyo kwa Amini. Kwa vile walimfahamu uchapakazi wake walijua Amini hawezi kukataa na kweli alikubaliwa kuwa ataanza kazi ila atakuwa akilipwa kiasi kidogo maana kiwanda ndo kilikuwa kinaanza ingawa Riziki alipendekeza kuwa hata asipolipwa cha msingi ajifunze ufundi. Amini alikataa kuwa hawezi kumtuma kazi bila kumpa chochote.

> Mfano, Amini alisema, “Lakini sikufichi Bi. Riziki, malipo yatakuwa madogo, kwa sababu kama unavyojua,

> ndio kwanza ninaanza kazi.” Bi Riziki alijibu kuwa, “Hayo yasikushughulishe. Hata kama hutompa chochote, sio muhimu.” Haiwezekani. Mimi ninamjua Rajabu ni hodari wa kazi, na yupo tayari kutumia siku zote. Si mvivu hata kidogo. Pengine huenda akajifunza kidogo kidogo pia. (Uk. 40).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kutoonesha udikteta katika familia zao na jamii inayowazunguka. Amini ni mwanaume mpya katika familia yake na jamii kwa ujumla. Alishauriana na mkewe kwa kila jambo alilotaka kulifanya. Alisikilizana na mzee Hasani pamoja na Riziki kuhusu namna ya kumsaidia Rajabu ili kuweza kujitegemea. Nadharia inatusisitiza kuwa wapya katika familia na jamii zetu.

Katika nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao; wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii. Ni kawaida kwa binadamu kusaidiana mara wanapokwama. Hili siyo jambo la jamii moja bali lipo kila jamii tangu enzi na enzi ingawa hutofautiana kutoka jamii moja na nyingine. Amini kumpa Rajabu kibarua pale kiwandani kwake si suala la utu na kuijali familia ya Bi. Riziki ambaye alikuwa akiishi maisha magumu kiuchumi. Vile vile suala la kumfundisha Rajabu ufundi na huku akilipwa ni suala la utu ambalo kila mwana jamii lazima alifurahie. Katika riwaya hii ya *Kipimo cha Mizani* zimeoneshwa sifa nyingi za mhusika wa kiume kwa mfano ni mwenye huruma na utu kama alivyofanya Bakari kuwapokea watoto wa Halima na kuwatafutia makazi ya kudumu kwa Bi. Rehema. Ana bidii ya kazi na kujituma kama vile mzee Hasani, Amini na Bakari mwenyewe. Mbali na hizo sifa nzuri mwanaume pia amechorwa kwa sifa mbaya kama vile uchu wa

mali kama aliokuwa nao Umari kupenda sana pesa na kuishi maisha ya anasa ilhali uwezo wake ni wa kuishi maisha ya kawaida. Kuna roho ya kikatili kama vile Daktari Juma alivyokuwa akimchoma sindano Halima ilhali haumwi ukichaa, hayo yote aliyafanya sababu ya rushwa aliyoipokea kutoka kwa Umari. Haya yote yanafungamana na nadharia ya mwanaume mpya ambayo inamtaka mwanaume kuwa mpya kwa kuishi maisha yanayoleta furaha katika familia yake kwa kumsaidia mkewe kazi pamoja na kuihudumia familia. Nadharia hii inaitaka jamii kubadilika kwa wanaume kuacha matendo ya kishetani yanayoendekeza ubabe dume na kuwaona wanaume kila wanachokifanya kuwa ni sahihi hata kama kinaiumiza familia yake. Nadharia hii inasisitiza usawa wa kijinsia katika jamii ili kuleta maendeleo.

Mawazo haya yanafafanuliwa na Butler, (1990) kuwa binadamu hawako katika utuli bali huweza kubadilika kwa namna yoyote ile ili kuendana na namna jamii inavyowataka wawe. Tabia zisizofaa hurudisha nyuma maendeleo ya familia na hatimaye jamii. Mwanaume mbaya anaweza kuwa mzuri na mke mbaya anaweza kuwa mzuri kitabia. Mabaya huwa yanapimwa na jamii husika ili kuhimiza mabadiliko yanayotakiwa.

Haya mambo yanaendana na uhalisia kwani kuna jamii ambazo zina itikadi mbovu zinazotumiwa kuwanyanyasa baadhi ya wanajamii aidha wanawake au wanaume. Mkondo wa usasa wa nadharia ya uana unaitaka jamii kubadilika ili kuachana na itikadi hizo ambapo kila mwanajamii atakuwa akiwajibika kwa mambo yallizomo katika jamii bila kuigandamiza jinsi yoyote.

Kwa upande mwingine, katika riwaya ya *Hiba ya Wivu*, Ihucha amesawiriwa kuwa na bidii ya kazi sana. Alifanya kazi usiku na mchana. Hata Farida alipopata wivu akihisi mumewe yuko kwenye mambo machafu na kuamua kumfuata usiku sana hadi hotelini, alikuwa kwenye kikao na wafanya biashara wenzie akina Feruzi na mzee Kibwana. Hata hao marafiki wa Ihucha walikuwa wachapakazi sana na walikuwa na matumaini ya kufanikiwa katika biashara zao. Mwandishi anasema:

> "Tena safari hii Bwana mdogo ukishauza ile mali, utaibuka na donge nono! Hapo utamnunulia binti yangu benzi, naye ajisikie kuwa kapata mume, sio lofa!" Tena anavyopenda gari Yule, mbona siku hiyo vitapigwa vigelegele." Alitamka Ihucha huku tabasamu likiwa limeutawala uso wake. (Uk. 3-4).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili usemao: vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Hapa tunaona Mzee Kibwana ambaye ni mkongwe wa biashara ya kuuza saa akitoa motisha kwa Ihucha kama kishawishi cha kumfanya awe na bidi zaidi ya kuuza mzigo wake. Kuna mambo mengi wafanyabiashara hawa walifundishana katika kazi zao ikiwemo kurekebishana mambo yasipoenda sawa na matarajio yao.

Katika nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume. Tunaona Ihucha kama mwanaume mpya maana ilipofika usiku sana kabla hajarudi nyumbani aliomba wafanyabiashara wenzie wamrejeshe kwa gari lao ili awahi nyumbani kwani ulikuwa usiku sana alihisi Farida atakasirika ingawa hakumkuta Farida mara alipofika nyumbani kwake. Ihucha anaonekana kujikosoa kama mwanaume kurudi nyumbani usiku sana wakati muda wa kazi ulishaisha, siyo vizuri kwa familia yake hasa mkewe.

Hii hoja inaungwa mkono na Beynon, (2002) anaposema kuwa mwanaume mpya anapaswa kuwa na mamlaka katika mambo ya kiuana kwa kujitambua nafasi yake na kujikosoa pale asipoenda sawa. Anapaswa kufanya mambo sawa ili asiwachochee wanaharakati wa mtazamo kike kupata ya kuchunguza kuhusiana na mienendo yake.

Katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao; mshikamano. Mwanamke na mwanaume wanapaswa kuwa na mshikamano katika shughuli wazifanyazo kwa maendeleo ya uchumi wa familia yao. Ukikosekana mshikamano ndipo mambo kama haya ya kuanza kuhisiana mambo ya ajabu. Mshikamano unaambatana na ushirikishwaji pamoja na uaminifu. Hata hivyo Farida alifanya maamuzi ya ajabu mara baada ya kumkuta mumewe hotelini akiwa na kikao na wafanyabiashara wenzake. Huu ni uhalisia unaoleta matatizo kwa baadhi ya wanajamii, Farida alifanya maamuzi ya kukimbia kwa teksi ili amuwahi mumewe na mipango haikukamilika sababu ya itilafu ya gari huko njiani. Ihucha alipata mateso ya kutolala usingizi usiku mzima na kuamkia polisi kutoa taarifa ya kupotea kwa mkewe. Uhalisi unakuja pale wanajamii wanapofanya maamuzi bila kujali madhara yake na matokeo yake kusababisha shida upande mwingine.

Kwa upande wake, Baba Dago katika riwaya ya *Dago wa Munje* anafanya kazi kwa bidii ili apate mahitaji ya kuitunza familia yake ikiwemo kuwapa wanae hitaji la muhimu katika maisha yao yaani elimu. Alizidisha bidii ya

kazi na wala hakubagua kazi ili apate pesa za kumlipia Nchimoni aende shule baada ya kufaulu kwenda shule ya upili. Mwandishi anaeleza:

> Baba aliamka asubuhi zaidi ili kujaribu kumaliza vibarua vingi kwa siku moja. Mama naye aliongeza juhudi zake za biashara na kuraukia makuti azidi kupiga kwa wingi, baada ya kuuza vyakula alivyopika sokoni. (Uk. 29).

Nchimoni ambaye ni dada yake Dago, ana bidii ya kazi huko alikoajiriwa Mombasa, anajituma ili awasaidie wazazi wake. Alitamani kuwasahaulisha shida zote walizozipitia katika kuangaika kuihudumia familia. Alikuwa akisaidia hata kununua mahitaji ya shule ya Dago. Alikuwa mchapakazi sana huko Mombasa. Mwandishi anaeleza:

> Hadi leo Nchimoni ni mwalimu katika shule mojawapo ya chekechea mjini Mombasa. Bado anajitahidi kufanya kazi hiyo ili awasaidie wazazi wake na kidogo alichokipata. Yeye hufanya juhudi za kuwatembelea wazazi wake kila anapopata nafasi. Kila alipokuja aliwahimiza wadogo zake watie juhudi masomoni. Aliwasaidia wazazi kwa kuwaletea mchango wake kwa karo za ndugu zake. (Uk. 33).

Katika nadharia ya mwanaume mpya, mhimili usemao: kusaidia wake zao na wanawake wengine katika jamii katika kujiendeleza kielimu na kikazi. Hii imedhihirishwa na baba yake Dago ambaye aliwathamini watoto wake wa kike ambao ni Nchimoni ambaye aliweza kusoma mpaka kiwango cha elimu ya juu. Ingawa mdogo wake alibeba mimba akafukuzwa shule ila baba Dago alimpeleka shule bila ubaguzi. Hata Dago ambaye ni mtoto wa kiume alipelekwa shule kama dada zake ila yeye hakupenda shule. Dada zake walimsisitiza kusoma na kumnunulia vitabu ambavyo hakuvisoma vikaishia kusomwa na marafiki zake Dago.

Vile vile mwalimu Sifa alikuwa na bidii ya kazi sana hasa kwa kufuatilia mienendo na tabia za wanafunzi zinazowaathiri kitaaluma. Alikuwa akimfuatilia na kumwadhibu Dago kwa kutowahi darasani kila siku pamoja na kutofaulu vizuri masomo yake. Mwalimu Sifa alimwita Dago ofisi kwake ili apate kumhoji kwanini anakuwa kama alivyo, anakuwa akikejeliwa na marafiki mara kwa mara ila habadiliki. Mwandishi anaeleza:

> "Dago twende ofisini mwangu". Mwalimu sifa aliposema maneno hayo, yalikuwa kama maliwazo kwa Dago. ……… Suala jingine lililomsumbua mwalimu ni kutojua kwanini Dago hakufanya bidii yoyote darasani. Je, hakuelewa chochote waalimu walipofunza, au hakupenda kusikiza? Mwalimu Sifa leo alitaka kuambiwa majibu ya maswali yake, ndiposa kumwita Dago ofisini mwake. (Uk. 56-57).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili usemao: ujifunzaji unahusu kuchunguza kupata habari kutokana na kuunda maazimio kuhusu utendakazi wa tabia hiyo. Hii inaoneshwa na mwalimu Sifa ambaye ana bidi ya kazi na kuamua kufuatilia chanzo cha tabia za Dago kuchelewa shuleni kila siku na kutofanya vizuri katika masomo. Mwalimu anafanya uchunguzi kwa kuwatumia marafiki zake Dago na baadae kuamua kuwajuza wazazi juu ya mienendo ya Dago. Pamoja na kwamba mtu anajifunza mambo katika jamii yake ila yale yanayoonekana hayafai ndipo huchunguzwa ili kuweza kufahamu chanzo na kuyakomesha.

Wazo hili linaelezwa na Skinner, (1963) kuwa tabia alizonazo binadamu huwa zina sababu ya kisayansi zinazotoka katika jamii yake. Zinapaswa kufanyiwa ufuatiliaji wa kina kama zinafaa ziboreshwe na kuendelezwa kwa vishawishi na kama hazifai zikomeshwe kwa adhabu.

Hata katika nadharia ya uhalisia, mhimili usemao: wahusika waonyeshwe kama kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii. Hii inadhihirishwa na mwalimu Sifa kwa kuwajua wanafunzi darasani pamoja na tabia zao na ndio maana aliweza kumfuatilia Dago mara tu alipobadilika kitabia na kurudi nyuma kimasomo. Katika jamii walimu wanaaminika sana kwa kuwalea vyema wanafunzi ndio maana tangu enzi na enzi mwalimu anatambulika kama mlezi.

Katika riwaya ya *Tumaini*, Shabani alikuwa na bidii ya kazi pamoja na familia yake kwa ujumla na pesa walizozipata katika familia alizitumia kwa mambo ya maendeleo kwa kukubaliana na kupanga pamoja. Mzee Masumbuko pamoja na ubabe na ukorofi wake katika familia, alikuwa mchapa kazi sana. Pesa walizozipata kama familia alizitumia kwa ulevi na kuiacha familia ikiishi maisha magumu sana. Kazi alizifanya kwa bidii bila kuhimizwa na mtu. Mwandishi anaeleza:

> Alipokasirika, midomo hiyo ilicheza kama mtu anayetaka kupasua kicheko muda wowote, huku akipepesa macho. Kutokana na umbo lililoshitadi siha na nguvu, mzee huyu alipoingia shambani, alilima mithili ya trekta. Alikata miti, akafyeka magugu na na kupiga matuta utadhani kapagawa……. Kutokana na ukakamavu wake katika kilimo, shamba lake liliguna kwa wingi wa mavuno. (Uk. 12).

Kutokana na nadharia ya ujifunzaji wa kijamii, mhimili usemao: ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Hii imeoneshwa na familia ya mzee Masumbuko kulea uhasi wa tabia zake za ulevi na kutumia pesa zote peke yake wakati familia nzima imeshiriki kuzitafuta. Waliogopa kumchukulia hatua kwa sababu ni

mwanaume mwenye maamuzi ya mwisho katika familia. Hali hii iliifanya familia yake kuishi maisha ya shida. Tumaini alipoelimika alitambua kabisa kuwa mama yake aliishi maisha ya shida sana kulingana na tabia za baba Tumaini.

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume. Mzee Masumbuko anapaswa kuwa mwanaume mpya kwa kujikosoa haya mabaya anayoyafanya kwa kumiliki kipato chote cha familia kibabe na kutumia pesa zote kwa ulevi na kuiacha familia ikipata shida. Wataalamu wanatueleza kuwa hakuna mwanaume mwenye tabia mbaya za kudumu bali wanaweza kuacha huo ubabe na ushetani na kuwa wanaume wazuri wa kuwasaidia na kuwadhamini wanawake katika familia zao na jamii kwa ujumla. Mfano, Hill, (1977) anaeleza kuwa wahusika huweza kubadilika na kueleza hali halisi iliyomo katika jamii. Walio wazuri huweza kuwa wabaya na wabaya huweza kuwa wazuri. Hii husisitiza kubadilika kwa wahusika kulingana na nyakati pamoja na mahitaji ya jamii.

Hata katika nadharia ya uhalisia inatuelekeza kuwa wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii. Jamii inapaswa kuonyesha mambo kama yalivyo hata yawe mabaya kiasi gani. Uhalisi huu ndio unapelekea mabadiliko. Hata mazuri ya wahusika yaonyeshwe kama yalivyo mfano ushirikiano wa Halima na Shabani, kuthamini elimu kwa mtoto wao pamoja na moyo wao wa kuwasaidia watu wenye matatizo kama

Tumaini aliyetoroka nyumbani kwao akiwa na nia ya kuendelea na masomo yake na siyo kuolewa kama baba yake alivyotaka.

### 2.2.3 Maadili ya Kazi katika Riwaya Teule

Maadili ni mafunzo mema au tabia njema kulingana na mila na desturi za jamii husika. (TUKI 2004). Maadili hutofautiana baina ya jamii moja na nyingine.

Katika riwaya ya *Kipimo cha Mizani*, wahusika wamechorwa kwa namna mbalimbali. Wapo wanaofuata maadili yao ya kazi na wanaokiuka maadili hayo. Juma anakuwa mkiuka maadili ya kazi yake kutoka na kutumia lugha ya ukali awapo ofisini kwake kiasi kwamba wafanyakazi wengi wanaogopa kuingia ofisini kwake. Anakuwa katili sana kwa wagonjwa na kukiuka maadili ya kazi yake baada ya makubaliano fulani. Kwa mfano, Halima alipoletwa hospitali kulikuwa na makubaliano na Umari ya kumchoma sindano ya ukichaa ilhali haumwi ugonjwa wa akili. Lengo ilikuwa kumpumbaza na kumfanya aishi hospitali siku zote na huku nyuma Umari amiliki mali za Halima na wanawe. Haya yalijitokeza Salama ambaye ni muuguzi alipoenda kuuliza Juma kuhusu taarifa za Halima.

> "Salama akasema: Nimekuja kwa ajili ya mgonjwa aliyepo chumba namba 75". "Ana nini?" Akauliza ."Hana neno", alijibu Salama………."Nimetafuta jalada lake kila mahali sijaliona, tumfungulie jalada jingine?" "Na wewe umeshughulishwa na nini? Huna kazi ya kutosha?" akampokea Salama. (Uk. 8-9). " aliamrisha afungwe kamba kwenye kitanda, na pia afungwe mdomo… akamwamrisha ampige sindano –sijui ya nini". (Uk. 14).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: mwanafunzi si mpokezi tulivu wa habari, utambuzi mazingira na tabia vinaathiririana katika upataji wa habari wa mwanafunzi. Juma anaenda kinyume na maadili ya kazi yake na kuamua kumuumiza Halima kwa madawa wakati haumwi ugonjwa wa kichaa. Aliitumia elimu yake na cheo chake cha u ili kuendana na matakwa ya Umari. Lengo lilikuwa ni kuendana na mielekeo ya kijamii kuwa mwanamke mjane hawezi kusimamia mali peke yake ilhali kuna ndugu wa kiume wa marehemu anayeweza kufanya hivyo. Aliwafuata mahakimu ambao alijua watapindisha nyaraka na kuwapa rushwa ili wafanye atakavyo. Jamii inatambua kuwa ni majukumu ya mzazi kumpa mwanae malezi bora ila inapokuja suala la kumiliki mali mwanamke anakosa hiyo nafasi kutokana na kujipendelea kwa mwanaume katika sehemu hiyo ya kumiliki mali kama alivyofanya Umari.

Katika nadharia ya mwanume mpya inayomtaka mwanaume kuwa mpya kwa kumsikiliza na kusaidiana na mwanamke. Juma pamoja na kukosa maadili ya kazi bado ni mwanaume wa kale anayeendekeza mfumo dume, asiyetaka kusikilizana na mwanamke hata kama anakuja na wazo zuri. Juma hakuwa na sababu ya kumsema kwa ukali Salama aliyetaka kujua taarifa za mgonjwa wakati yeye ndiye muuguzi wake.

Hata hivyo Salama na Bi Wakati ni wachapa kazi na wanafuata maadili ya kazi yao ila wanakatishwa tamaa na Juma ambaye alikuwa na majibu makali kwa Salama sababu ya kujihami katika ubaya aliokuwa akiufanya kwa mgonjwa Halima. Salama aliumiza sana kichwa ili amsaidie Halima hadi akaenda kusoma

baadhi ya vitabu kabla ya kumwona Isa. Isa naye alikuwa na roho nzuri na mfuata maadili ya kazi yake hivyo alimtia moyo sana Salama katika jitihada za kumsaidia Halima kwa kumuelekeza hatua za kufuata. Hii ilijitokeza pale Salama alimueleza tatizo la Halima. Alieleza kuwa yeye ni wa hospitali kuu hivyo hawezi kwenda kumhudumia Halima bila kupita kwa Juma ambaye ni wa hospitali alikolazwa Halima na kituo cha Salama cha kazi.

Katika nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kuwaonesha wanawake kama viumbe sawa na wanaume kwa kuwaheshimu na kuwapenda katika kila nyanja wanazokuwepo. Tunaona Isa ni mwanaume wa sasa anayemsikiliza mwanamke na kumpa nafasi ya kujieleza na ndipo anampa maelekezo. Salama alipata maelekezo mazuri kwa Isa na kuelekezwa nini cha kufanya ili kumsaidia mgonjwa

Mwandishi anaeleza kuhusu Salama alivyoelezwa na Juma kuwa:

> "Baada ya kuhangaika na kutanga usiku kucha bila ya kupata usingizi, alikumbuka kuwa anajuana na mmoja – Isa, aliyefanya kazi Hospitali Kuu" (Uk. 15).
>
> "Unaelewa kuwa mimi siwezi kuingilia, wala hata kufanya lolote bila ya kushauriwa na huyo aliyeko hapo?" (Uk. 19).

Katika nadharia ya uhalisia mhimili wa tatu usemao: usadikifu; yale yanayoibuliwa katika jamii yawe yanasadikiwa na wasomi. Katika riwaya hii, Salama alisadiki kuwa lile atakalolisema Isa litakuwa ndilo la kweli maana yeye ndiye msomi wa u. Vile vile Isa aiyasadiki aliyoyasema Salama maana ni msomi wa uuguzi**.** Isa ni mwanaume wa kisasa ambaye anajua wajibu wake kama na taratibu za kazi zake ili asilete madhara upande wowote. Anamtaka Salama

kufuata taratibu katika kumsaidia mgonjwa ili asimtie matatizoni Salama wala juma ambaye ndiye mkuu katika hospitali hiyo. Huu ndio uwajibikaji kama anavyoeleza Gibbe, (1978) kuwa katika dhamira mbalimbali zizungumziwazo katika kazi ya fasihi, kwa wafanyakazi uwajibikaji ni jambo la muhimu katika kipengele cha tathmini katika utendaji kazi.

Mzee Hasani ni mchapakazi na alikuwa na maadili ya kazi yake ya kuuza duka la Amini. Umari alipokuja dukani alitaka kuchukua vitu avitakavyo bila kulipa pesa akidhani ataruhusiwa na mzee Hasani. Umari alimsemea mzee Hasani maneno makali lakini bado alimjibu kwa busara akimwelekeza utaratibu wa kazi yake na namna ya kuchukua vitu dukani. Anasema:

> "Hapo unakosea," alijibu mzee Hasani. "Kweli duka na vitu vilivyomo ni vyake, sijakataa. Lakini mimi ndiye dhamana, na hajanipa ruhusa hiyo ya kutoa vitu ila kwa mnunuzi tu." (Uk. 67).

Katika nadharia ya Ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Huu unaonesha kuwa uasi wa Umari kwa mzee Hasani kulingana na lugha ya dharau na matusi aliyommiminia mzee yule ni kutokana na mahusiano aliyoyajenga Umari kwa wafanyakazi katika familia yake pamoja na kwa kaka yake. Umari alifunzwa mazuri na familia yake na kuwa kijana mzuri ila anakuwa na tabia za ajabu kwa wengine kutokana na hali aliyojijengea juu ya wafanyakazi katika familia yao. Hakuwa mtu wa kuwathamini wafanyakazi hata kidogo. Alipaswa kupewa elimu na jamii ili aweze kubadilisha hiyo dhana ya kutowathamini wafanyakazi na kuwanyanyasa kwa kuona hawana mamlaka yoyote. Hata hivyo uchanya wa mzee Hasani kwa lugha aliyoitumia kwa

Umari inadhihirisha kuwa mzee Hasani amejenga mahusiano mazuri na watu hata kama wanamtendea mabaya. Umari anapaswa kujifunza yaani kupata elimu kutoka kwa mzee Hasani namna anavyoishi na watu. Abrams, (1993) anaeleza wahusika kuwa wanadamu wanaowasilishwa katika kazi za kidarama au usimulizi ambao hufasiriwa na msomaji kuwa wenye  hisia, maadili na sifa bainifu. Anasisitiza suala la maadili katika jamii ili kuleta nidhamu miongoni mwa wanajamii.

Katika riwaya ya *Hiba ya Wivu* Sikujua ambaye alikuwa mwendesha teksi alijua fika maadili ya kazi yao kuwa ni kutokuwa msemaji hovyo kila jambo analokutana nalo katika kazi zao za kubeba abiria. Sikujua alimbeba Ray kwenda bonde la Mkwajuni kuchukua elfu hamsini iliyowekwa na Ihucha ili kumnusuru mkewe Farida aachiwe na wateka nyara. Musa ambaye ni mjomba wake Farida aliongozana na Ihucha wakaenda kumfuatilia dereva wa teksi iliyokodiwa na wateka nyara. Walifuatilia hilo gari wakalipata na dereva aliyekuwa ndani ni Sikujua. Sikujua alipoulizwa na anasema:

> “Ninachoweza kukufahamisha mimi ni kwamba huyo bwana alinikuta hapa hapa kituoni pangu. Akanikodi nimpeleke Bonde la Mkwajuni. Unajua tena kazi yetu, mteja ni mteja tu. Hata hivyo sikuwa na uwezo wa kubuni kuwa hilo ni jambazi. Hivyo nilimchukua hadi huko alikotaka kwenda ambako aliniomba nimsubiri achukue mzigo wake pahala fulani turudi sote mjini. Nilimsubiri, na baada ya muda kidogo alirudi na mfuko ambao sikujua una nini. Nilimchukua hadi Mtaa wa Ohio ambako aliniomba nimwache. (Uk. 65).

Kitendo cha Sikujua kutoa hiyo siri kuwa  alimpelekan Ray mkwajuni kwenda kuchukua mzigo wake ni ukosefu wa maadili ya kazi yake maana mwendesha taksi hapaswi kuwa msema lolote analoulizwa hata kama ni kweli.

Ray alienda kinyume na maadili ya kazi yake kwa kuwa mwongo kuwa gari lake limeharibika na akashindwa kumwahisha nyumbani mteja wake Farida kama alivyohitaji. Ray alikuwa na tamaa ya kimapenzi juu ya Farida. Kila alipoelekezwa na Farida ili ampeleke, Ray aliibua visingizio ili ampeleke nyumbani kwake kwa ajili ya kutimiza lengo lake ingawa halikufanikiwa zaidi ya kumtia hasara Ihucha ya elfu hamsini kwa kujiita mteka nyara. Mwandishi anaeleza:

> Wakati huo Ray alikuwa na mawazo mengi kichwani kuhusu Farida. Msisimko wa penzi lake kwa Farida ambalo lilikwishaingia katika mishipa ya damu yake na moyo wake pasi nay eye Farida kutambua wala Ray kumtamkia, ulimfanya asikie raha kusikia Farida anataka kujua mambo yake. Hakupenda kumtamkia Farida dhamira yake mapema, kwani alihitaji muda wa kupanga aanzeje, aseme nini, atumie mbinu gani. Alikwishatambua ugumu uliokuwepo wa kumpata Farida. (Uk. 27).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao; ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa jamii. Hii inadhihirishwa na Sikujua kuwa alilelewa kama mtoto wa kiume ambaye ni dereva afuataye maadili ya kazi ili aendelee kuaminiwa na kupendwa na wateja wake. Kwa upande wa Ray anaonesha kuwa malezi yake katika jamii aliyasaliti kama dereva wa kiume ambaye anakuwa na uchu wa mapenzi kwa wateja wake badala ya kufanya kazi kimaadili kama impasavyo.

Hata hivyo Ray angeweza kumfikisha mteja wake kwa usalama na akatafuta njia nyingine ya kuwasiliana naye badala ya kumtia hatiani. Hili pia linadhihirishwa na katika nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao;

zitumike sajili ambazo ni za kawaida. Ray alipaswa kutumia njia ya kawaida kueleza hisia zake kwa Farida badala ya uongo alioutumia na mkumtia matatizoni hadi kufikia ulaghai wa kujiita jambazi na kumtapeli Ihucha pesa zake na kumtia hekaheka Sikujua ambaye gari lake lilitumika kupeleka pesa mbuyuni.

Katika nadharia ya mwanaume mpya tunaona kuwa mwanaume mwenye tabia mbaya anaweza kubadilika na kuacha ubaya huo na kuwa mzuri na kufanya mambo yanayokubalika katika jamii. Hii inazungumziwa na Chaterji, (2004) katika utafiti wake anaochunguza mabadiliko katika mfumo wa kuumeni kwa kuzingatia jamii ya Wahindi kule Uhindi. Anaeleza kuwa wanaume wenye matendo mabaya wana uwezekano mkubwa wa kubadilika na kuwa wazuri na kuwa chachu ya madilko kwa jamii kuhusu ugandamizwaji wa wanawake.

Katika riwaya ya *Dago wa Munje*, jengo kubwa la ofisi lililojengwa shuleni kwa msaada wa mfuko wa hazina,ofisi ya mwalimu mkuu ilikuwa jirani sana na ofisi ya walimu wengine. Tendo hili liliwafanya walimu kuwa watii zaidi kwa maana walikuwa wakionwa na mkuu wao namna waingiavyo na kutoka. Walimu walifuata taratibu zote za kazi kama walivyokuwa wakisimamiwa na mkuu wao. Kwa kufanya hivyo walifuata maadili ya kazi yao ya kuwahi kazini na kukaa kwenye kituo cha kazi bila kwenda kulandalanda mitaani muda wa kazi. Mwandishi anaeleza:

> Hata hivyo, walimu wote walifurahia afisi yao mpya, ingawa ilikuwa pua na mdomo mno na ile ya mwalimu mkuu…………..Tabia hii ya unyapara

> haikuwaridhisha wengi lakini, badala ya kuitwa afisini na kusomewa barua kama ilivyosemekana, kila mtu alishika njia zake mapema. (Uk. 18).

Mwalimu Sifa ambaye alikuwa makamu mkuu wa shule alijua maadili ya kazi yake. Aliwafuatilia sana wanafunzi katika mienendo ya kimaadili na kitaaluma. Aliwapa adhabu za kila namna na alipoona hawabadiliki, aliwashirikisha wazazi ili wasaidiane kumfuatilia mwanafunzi aweza kubadilika. Mfano, alimwadhibu sana Dago kwa fimbo na hata kufyeka nyasi ila bado hakubadilika na ndipo akachukua jukumu la kuwajuza wazazi wake. Mwandishi anaeleza:

> "Naam, jana ulifyeka nyasi, leo nitakupiga viboko vitatu mbele ya darasa, na jioni, nitawaelezea wazazi wako juu ya tabia hii. Najua sera ni kwamba wanafunzi wasichapwe. Lakini tangu sera hii ibuniwe utundu na kutojali vimekuwa vingi. Wanafunzi wamedhania kuwa imewapa uhuru wa kutenda watakalo." (Uk. 45).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii, mhimili wa kwanza na wa pili tunaona kuwa maadili ya kazi yanapozingatiwa yanafanya kazi ziwe na ufanisi na fani kuheshimika. Walimu wa Dago hawakutaka kuwa karibu na ofisi ya mwalimu mkuu wao ili wasiwe wanaonana kila saa maana kiutendaji inawanyima raha. Majukumu ya kazi hutegemea utamaduni, historia na elimu pamoja na mielekeo inayotawala. Kiongozi ni mtu wa kuheshimiwa hivyo haifai kukaa mnapishana kila wakati koridoni. Vile vile mahusiano ya binadamu yalivyojengwa ndiyo huleta uasi na uchanya kwa hao wanaohusika. Hii inaweza kuleta athari hasi pengine kufanya jambo kwa bahati mbaya ila likaonwa na mkuu wa kazi, tayari utakuwa umejitia matatizoni.

Kila kazi huwa ina maadili yake ambayo mtu wa fani hiyo hupaswa kuyafuata na kuyadumisha katika kazi zake azifanyazo kila siku maana hujifunza kulingana na muktadha wa fani yake. Hii inajidhihirisha katika riwaya ya *Tumaini* wakati ambapo Tumaini alikuwa akijisomea chini ya mti akisubiri mtihani, alidondokewa na nyoka na baadae akaingia majanini na kukimbia. Tumaini alipiga kelele sana hadi bwenini na kusababisha taharuki kubwa sana shuleni. Mwalimu aliyekuwepo ilibidi kutumia nguvu ya ziada na vitisho ili kumnyamazisha Tumaini. Mwalimu huyu alitumia fani yake aliyoisomea kumnyamazisha Tumaini. Baada ya hapo aliweza kuongozana na Tumaini ili akaone eneo la tukio na kuweza kumshauri Tumaini cha kufanya maana alikuwa na hofu bado wakati anajiandaa kuingia kwenye mtihani. Mwalimu alijitahidi sana na kweli Tumaini akatulia na kuweza kufanya mtihani. Mwandishi anasema:

> Hapo Mwalimu Johnson wa somo la Fizikia alimkabili Tumaini na kutishia kumpiga kofi kali jambo lililomshtua na kumrejesha katika hali ya utulivu. Mwalimu huyo aliamini hiyo ndiyo njia nzuri ya kumfanya aone mambo katika uhalisi, na sio ule wehu aliokuwa nao wakati ule. (Uk. 120).

Kutokana na nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili wa kwanza na wa tatu tunaona kuwa majukumu ya mwalimu katika kazi yake ni kuifanya kiuadilifu. Hata hivyo Tumaini alivyodondokewa na nyoka akisubiria kuingia kwenye mtihani, mwalimu alitumia ushauri nasaha ili kumrudisha katika hali ya kawaida Tumaini ili kuweza kutulia na kufanya mtihani na kweli mwalimu alifanikiwa kuitumia elimu yake kumtuliza Tumaini. Katika mhimili wa tatu pia tunaona mahusiano ya mwalimu na mwanafunzi yalimfanya Tumaini

kutii na kuamini alichoambiwa na mwalimu wake na ndipo kikaweza kumsaidia. Mahusiano ya binadamu yamejengwa kiuana na pia katika elimu inayotolewa kwa wanafunzi hili husisitizwa kuwa mwalimu wa kike au wa kiume wote wana jukumu wa kuyafuata maadili ya kazi yao ili kuwafanya wanafunzi kupata elimu inayotakiwa. Haya ni maarifa ya kifani ambayo mtu hujifunza kulingana na kazi yake.

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili wa tano usemao: kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume. Mwalimu Johnson ambaye alifundisha somo la Fizikia alionekana kujikosoa nafasi yake kama mwanaume na kuanza kumhudumia Tumaini ambaye ni binti vinginevyo angemuacha akiendelea na maangaiko yake. Alihakikisha Tumaini anakuwa sawa hadi kuweza kufanya mtihani. Hili ni suala la kisaikolojia kama linavyoelezwa na Hull (1930) kuwa utulivu wa mtu kujifunza hutokana na vichocheo vya kisaikolojia ndani yake. Tumaini alipotulizwa akawa tayari kisaikolojia kujibu mtihani licha ya mshutuko alioupata.Matendo kama haya hufanywa na walimu wachache hasa wanaojua maadili ya kazi zao na kuishi katika fani zao za kiualimu.

### 2.2.4 Urafiki wa Kweli katika Riwaya Teule

Urafiki ni uswahiba,hali ya kuwa karibu na mtu kwa kuelewana. (Kamusi ya karne ya 21). Katika riwaya ya *Kipimo cha Mizani*, mwandishi amemsawiri mhusika wa kiume kama rafiki wa kweli. Amini alikuwa na rafiki mmoja tu ambaye alimshirikisha kila jambo alilolipanga katika familia yake na hata masuala ya kazi. Selemani ndiye alikuwa rafiki wa Amini aliyetegemewa na

familia nzima ya Amini hasa Halima. Hili linajidhihirisha Amini alipotaka kuacha kazi ili alipwe kiinua mgongo na afungue kiwanda chake ambayo ndiyo ilikuwa ndoto ya maisha yake.

Mfano:

Halima aliona lazima achukue jambo hilo kwa siasa.

> Akasema, "Ninavyoona, kwanza unaonaje, kabla ya kuchukua hatua yoyote, ukamshauri rafiki yako, Selemani? Yeye ana ujuzi mwingi kuhusu mambo ya biashara, na huenda akakupa fikira nzuri, badala ya kujitumbukiza tu katika jambo kama hilo?" (Uk. 28).

Selemani alikubaliana na wazo la Amini kuanzisha kiwanda chake cha seremala na akampa mbinu za kupata wateja maana alikuwa ni rafiki yake Amini na alimtakia sana maendeleo pamoja na familia yake. Huyu ni mwanaume mpya anayesisitizwa na nadharia ya mwanaume mpya, anamsikiliza mkewe na kupata ushauri wa kimaendeleo. Mfano mhimili wa kwanza usemao: kuwaona wanawake kama viumbe sawa na wanaume kwa kuwaheshimu kwa kuwapenda na kuwashirikisha katika kila nyanja wanazokuwepo. Amini hakufanya jambo lolote bila kumwambia mkewe ili naye atoe mawazo kwa maana alijua maendeleo ya familia ni yao wote.

Mfano:

> Selemani alimwambia: "Ninajua kuwa wewe ni hodari wa kazi za uchongaji, na una fikira nzuri za fanicha za kisasa unazotaka kutengeneza, pamoja na vyombo vingine. Lakini usisahau kuwa siku hizi, watu wanafanya biashara kwa matangazo. Lazima uitangaze kazi yako, uonyeshe watu uhodari wako, uwasifie, hapo watavutika, na utapata biashara. (Uk. 46).

Katika nadharia ya mwanaume mpya mhimili wa pili usemao: kukubali majukumu yoyote ya kiuana bila kujali jinsia na bila kujali watu wanaowazunguka. Selemani alitambua kuwa Amini ndiye mhimili wa familia

yake na hivyo anapaswa kuwa na kipato kinachoeleweka. Kutoka na elimu ya kiuana aliyokuwa nayo, alitambua kuwa mwanaume anapofariki anayechukua majukumu ya familia ni mke wa marehemu na ndiyo maana Selemani aliangaika sana kumrudisha Halima katika familia yake baada ya kuhujumiwa mali zake na Umari.

Amini alipofariki bado Selemani aliendelea kuwajibika pamoja na Bi Riziki ili kumfariji Halima baada ya kuondokewa na mumewe. Umari alikuwepo ila hakuweza kuwajibika kwa lolote akionesha kuwa kaumizwa sana na kifo cha kaka yake kumbe akili yote iliwaza namna ya kumiliki mali za marehemu kaka yake.

Mfano:

> Selemani alisimamia yote yaliyolazimu, kwani Umari naye alijitia simanzi na kukaa tutwe bila kushiriki katika shughuli za mazishi. Bi Riziki alishughulikia ya nyumbani na pia kuwaangalia watoto. Halima hakujiweza kwa lolote, na pia alilazimika kukaa eda. (Uk. 80).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Selemani alijifunza kuwa karibu na marafiki ila pia aliweza kufuatilia tabia ya ukaribu wake na Amini inandelea kwa familia yake hata baada ya Amini kufariki. Alikuwa bega kwa bega kufuatilia haki ya Halima na wanae. Hii ni hatua nzuri katika nadharia hii kama ifafanuliwavyo na Julian, (2017) amabapo anaeleza kuwa mazingira ya mtu katika kujifunza huwa na mchango mkubwa

katika kubadili tabia ambayo huweza kubadili asili ya mwitikio na vishawishi vya ujifunzaji ambavyo huleta mitazamo tofauti.

Katika nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao; zitumike sajili ambazo ni za kawaida. Hii ni kweli katika muktadha wa msiba wa mtu wa karibu anayegusa watu wengi huhitaji msaada wa marafiki walio waaminifu maana huwa kuna hali ya kutoukubali msiba ule. Selemani na Bi Riziki walimsaidia sana Halima kwa kuwajali watoto wake pamoja na mali zake hasa katika kipindi chote cha msiba.

Katika riwaya ya *Hiba ya Wivu*, Feruzi alikuwa rafiki wa kweli wa Ihucha katika biashara na katika mambo mbalimbali ya kijamii. Ihucha alipotoka kwenye mkutano wa biashara, akafika nyumbani hakumkuta Farida, mtu wa kwanza kumfahamisha alikuwa Feruzi na baadae Musa ambaye ni mjomba wake Farida. Feruzi alikuwa mshauri mkuu wa Ihucha katika mambo mbalimbali. Alipoambiwa na wateka nyara kuwa napeleke elfu hamsini katika bonde la Mkwajuni elfu hamsini alimshirikisha Feruzi, akampatia gari atakayoitumia katika mizunguko ya kwenda benki kuchukua pesa za kuwapelekea wateka nyara.

Mwandishi anaeleza:

> Baada ya kufikiri kwa dakika tano hivi, alimpigia simu Feruzi, Meneja Masoko wa kiwanda cha saa……………. “Loh, pole sana. La muhimu ni kumuokoa huyo binti kwanza. Lakini angalia sana usalama wako. Ningekushauri utafute ulinzi, usiende peke yako kupeleka hizo pesa.”……… Ni sawa Bastola ninayo……….. Mimi ningekuwa radhi kabisa

> kuandamana nawe, lakini kesho saa mbili nina kikao cha Bodi ya Wakurugenzi ya Kiwanda….. Ninachoweza kukusaidia mimi ni gari, kama utalihitaji”. (Uk. 24-25).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao : mwanafunzi si mpokezi tulivu wa habari, utambuzi mazingira na tabia zinaathiriana katika upatajiwa habari wa mwanafunzi. Mhimili huu unadhihirisha kuwa kiuana watu wanaopatana na kuelewana husaidiana. Ihucha alimshirikisha mambo ya kimaendeleo Feruzi maana ndiye alikuwa akishauriana naye. Alifahamu kuwa Feruzi ana elimu ya kiuana hivyo angeweza kumsaidia katika matatizo yaliyompata mkewe Farida. Wahusika hawa walikuwa marafiki waliosaidiana kwa kila hali waliyoipitia. Pamoja na kwamba Ihucha alijifunza namna ya kukabiliana na mambo mbalimbali katika familia yake, bado la kutekwa nyara mkewe Farida lilimuwia gumu ikabidi aanze kutafuta habari mbalimbali kujua mkewe alipo na kufanya maamuzi. Inapotokea hivi mmojawapo hupata shida kisaikolojia. Hoja hii inaelezwa na Tannen, (1990) kuwa mahusiano baina ya wanawake na wanaume husababishwa na matatizo ya kisaikolojia, ikiwemo upendo usiokuwa wa kweli, pamoja na athari za ukosefu wa uwiano wa usawa katika mambo ya kisiasa na ya kiuchumi.

Hata hivyo katika nadharia ya uhalisia katika mhimili unaoeleza kuwa; utumikaji wa sajili za kawaida. Haya yanajidhihirisha pale ambapo Feruzi alimsaidia gari Ihucha atakalolitumia katika mizunguko yote ya kufauatilia wateka nyara, kwenda polisi na kufanya utafiti ili Farida apatikane. Kulingana na muktadha huu, rafiki kumsaidia mwenzie aliyepatwa matatizo ni jambo la kawaida katika kuonesha hali ya kujali katika matatizo hayo yaliyompata.

Katika riwaya ya *Dago wa Munje*, Dago alikuwa na marafiki zake ambao ni Juma na Rashidi. Walipenda sana kumfuatilia katika mienendo yake pamoja na tabia mbalimbali ambazo zilimfanya Dago aonekane ni wa tofauti shuleni ni mtoto wa ajabu. Walijitahidi sana kuwa karibu naye ili wambadilishe kitabia akawa anawakwepa ila hawakukata tamaa. Mwandishi anaeleza:

> Rashidi alisema, "Dago, sisi ni marafiki, lakini wewe mwenyewe wajiletea matatizo shuleni, kwa kutofanya kazi za shule. Hata tunapokuita tusaidiane nyumbani kwetu, wewe hukataa. Mara ngapi tumekuambia jambo la kufanya unapolala? Wewe hutusikizi!" (Uk. 89).

Juma na Rashidi waliendelea kumkazania Dago mpaka wakafanikiwa kwenda naye mtoni ambako walimfanyia mizaha na kejeli sana hadi wakamchania shati lake la shule. Dago alikasirika sana na kuibuka ugomvi baina yake na Abdalla. Dago alipigana kwa bidii mpaka akamshinda Abdalla hadi wote wakastaajabu. Dago alitangazwa mshindi na kuimbiwa sana kwa mashangilio. Ushindi huo ulimbadilisha Dago akawa mtoto mzuri anayefanya bidii ya kazi za nyumbani na za shule. Mwandishi anaeleza:

> Alipolala usiku ule wa Jumamosi, mawazo yake yalikuwa ni ya kufanya bidii shuleni. Ushindi wa mtoni angetaka kuupata shuleni pia. Kwani akili zake zilitofautianaje na zile za vijana wenzake? Alikata shauri kuwatia aibu waliomcheka darasani. (Uk. 189).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: ujifunzaji unahusu kuchunguza kupata habari kutokana na ule uchunguzi na kuunda maazimio kuhusu utendakazi wa tabia hiyo. Hii inaonesha namna ambavyo marafiki zake Dago walivyokuwa na mwamko wa kiuana kwa namna walivyojifunza katika familia zao. Hawakupendezwa kabisa na tabia za kijana mwenzao kuwa mchafu, kuchelewa darasani, kukojoa kitandani na kutofanya bidii ya

masomo. Walijisikia vibaya sana na ndio maana walimuasa kubadilika ili aache kuwatia aibu. Rashidi na Juma walipenda sana maendeleo ya rafiki yao Dago.

Mishi ni rafiki wa dada yake Dago, alimfuatilia sana Dago awapo shuleni na kumtetea mara anaposongwa na marafiki pamoja na wanafunzi wenzie. Rashidi na Juma walimkazania sana Dago kwa kumsema kila mara, jambo ambalo Dago alilichukia na kuona ametiwa kifungoni. Walimsema sana kuhusu uchafu wa nguo za shule pamoja na kukojoa kitandani. Mishi aliingilia kati baada ya kumkuta Dago akiwa na marafiki zake ila hana raha kabisa na alitaka kujua yaliyomsibu. Baada ya kujua wanamsema kwa ajili ya uchafu ndo akaamua kumtoa hapo walipokuwa na kuongozana naye. Mwandishi anaeleza:

> "Uchafu ni wake, nyinyi mwamtaka nini?" Aliuliza Mishi. "Mwacheni nendeni zenu mkacheze kwingine. Dago twende zetu." Kwa kutii, alimfuata malaika aliyemuokoa, ingawa masikioni aliendelea kuyasikia maneno aliyorushiwa na walioachwa. (Uk. 55).

Mishi alikuwa rafiki yake wa kweli wa Swafiya. Aliposikia kuwa amepata mimba aliumia sana. Alitafakari mengi kichwani mwake kuhusu maisha ya Swafiya na Yule aliyempa mimba kama ataweza kumsaidia kwa maisha yake ya sasa na baada ya kujifungua. Alijiuliza kwanini rafiki yake kamficha. Alijawa na fikra nyingi juu ya rafiki yake huyu aliyekatisha maisha yake ya kitaaluma wakati alikuwa na maendeleo mazuri sana shuleni. Mwandishi anasema:

> Habari mimba ya Swafiya zilipomfikia Mishi, alighadhabika na alijiuliza mara nyingi,"Jambo hili lilitukia lini na mimi nilikuwa wapi? Mbona Swafiya hakuniambia kuwa alihadaika kwa ulaghai wa vijana kiasi cha kupatiwa mimba?"…...Mawazo haya yalimsumbua Mishi akilini, hasa kwa sababu rafiki yake hakutaka kumweleza waziwazi hadithi yote. "Kwanini kanificha Swafiya na sisi huelezana siri zetu?" Mishi aliendelea kujisaili kila alipolifikiria jambo hilo. (Uk. 35-36).

Nadharia ya mwanaume mpya inatueleza kuwa mwanaume aliyempa mimba Swafiya hata kama alikatiza ndoto zake za kitaaluma angeweza kubadilika na kuwa mwanaume mpya mwenye tabia nzuri katika jamii ila wazazi wake Swafiya hawakutaka hata kumuona na kusema kuwa ni mtu wa kuja hivyo hafai kumuoa mtoto wao. Kwa hili waliendelea kumkosesha haki Swafiya ya kupata nafasi ya kulea ujauzito na mtoto baada ya kuzaliwa akiwa na mwenzie aliyempa ujauzito.

Nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao; zitumike sajili ambazo ni za kawaida. Hii inajidhihirisha katika matendo yaliyooneshwa katika riwaya hii. Swafiya kubeba mimba akiwa sekondari na wazazi wake walishamlipia ada tena wanayoipata kwa kuangaika ni jambo linalowaumiza wazazi. Baba yake Swafiya alihuzunika sana maana aliyajua maendeleo mazuri ya kitaaluma ya binti yake pamoja na bidii katika shughuli mbalimbali. Hata hivyo maji yakimwagika hayazoleki, Swafiya alifukuzwa shule baada ya kugundulika mjamzito na hivyo kuwatia aibu wazazi wake. Kosa lilifanywa na kijana wa kiume na wa kike ila anayeonekana kutia aibu ni wa kike. Hii inafafanuliwa na Senkoro, (1982) katika kuchunguza sura ya malaya katika fasihi ya Kiafrika na riwaya za Kezilahabi, anaeleza kuwa mwanamke na mwanaume

wote wananyanyasika ila kwa mwanamke ni zaidi na taswira ya mwanamke inakuwa mbaya zaidi hasa anapopata ujauzito kabla ya ndoa wakati anayempa ujauzito ni mwanaume.

Katika riwaya ya *Tumaini*, Sifa amesawiriwa kuwa rafiki wa kweli wa Tumaini. Alikuwa akimwandikia barua nzuri za kumtia moyo na kumshauri kutia bidii katika masomo. Jambo lilimfanya Tumaini kuendelea kumwamini na kuwa karibu naye. Alifurahi sana maana alimwona Sifa kuwa ni mvulana wa tofauti na wavulana wengine ambao hupenda kuwasumbua wasichana kwa mambo ya mapenzi na kuwanyima nafasi ya kuonesha msimamo wao katika hayo mapenzi. Mwandishi anaeleza:

> Tumaini alifurahishwa sana na barua hii. Kwa mara nyingine, barua hii haikughasi nafsi yake, bali ilimwongezea matumaini. Kinyume na wavulana wengi aliowafahamu, Tumaini alimheshimu Sifa ambaye nyaraka alizomwandikia hazikuwa na uchokozi wowote au hila za kutaka mapenzi kwake. Alitambua kwamba barua zake hizo hazikuwa na lengo baya. Kwahiyo wakati huu, aliijibu barua ya Sifa. (Uk. 117).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili wa usemao; ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Inadhihirisha kuwa marafiki wanaopendana hushauriana ili waweze kufanikiwa katika mambo mbalimbali. Tumaini alipata elimu ya kiuana na kudhania kuwa msichana na mvulana wakiwa marafiki lazima mahusiano ya mapenzi yatajitokeza. Hata hivyo Sifa ni kijana wa tofauti ambaye hakutaka uharibifu kwa njia ya mapenzi bali alimshauri sana Tumaini kuwa na bidii katika masomo na pia kumshauri masomo atakayoendelea nayo chuo kikuu.

Kiukweli Tumaini alifurahi mara baada ya kugundua kuwa Sifa si kijana mwaribifu kupitia mapenzi bali anapenda na kuthamini masomo. Sifa na Tumaini walithamini sana maendeleo na ndiyo maana walikuwa na bidii katika masomo hadi kufikia ndoto zao. Vile vile katika uhalisia, mhimili usemao; itumie sajili ambazo ni za kawaida napo tunaona kuwa katika kujenga ukaribu katika jamii lazima kutumia mitindo na taratibu za kawaida zilizomo katika jamii. Hata Sifa alipoenda kutembea kwa akina Tumaini alitumia lugha ya kawaida ya kumtambulisha kuwa ni mwanafunzi mwenzie ambaye alikuja kumjulia hali na kumshauri masuala ya kimasomo na ndipo alipokelewa vizuri na kupewa ushirikiano.

### 2.2.5 Ukosefu wa Haki katika Riwaya Teule

Katika riwaya ya *Kipimo cha Mizani* mtunzi ameonesha kuwa nchi za Afrika Mashariki zimejaa watu wengi ambao hawakutendewa haki. Katika nchi yenye ukatili, kula rushwa, uonevu, utapeli, dhuluma na kila aina ya uovu, maadili yanakuwa ni kitu adimu sana. Haya yanadhihirishwa na mwandishi pale ambapo Umari anafanya njama mahakamani ili yeye awe msimamizi wa mali za marehemu kaka yake, akae na watoto ilhali mama yao yuko hai. Lengo lilikuwa kumdhulumu haki yake na wanae. Vile vile Umari anafanya mpango na  Juma ili Halima akae hospitali maisha yake yote. Halima anatendewa uovu wa kila aina na  Juma pamoja na askari polisi kwa kudhani ni mwenda wazimu kumbe ni fitina na uongo alioutengeneza Umari ili afanikiwe azima yake ya kumiliki mali za marehemu Amini badala ya mkewe na wanae.

Mfano:

> Juma, mara baada ya muuguzi kuiweka chini simu, aliinyanyua na kupiga nyumbani kwa Umari. Alipoitikia, alimwarifu yale yaliyotokea. Umari alishtuka, akauliza, " Vipi ameweza kutoka? Lazima mumtafute haraka! Umewaarifu polisi? Tena akipatikana lazima apewe adabu kali, ili asijaribu kukimbia tena!"……….. Umari aliingiwa na wasiwasi, akiwaza Halima amekusudia nini? Pengine atakuja pale kwake na kutaka kulipa kisasi? (Uk. 141).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kutoonesha udikteta katika familia zao na jamii zinazowazunguka. Daktari Juma alionyesha ubabe katika kumjibu Salama pamoja na wafanyakazi walioonekana kufuatilia matibabu ya Halima. Hii ilikuwa ni kutetea malipo manono aliyopewa na Umari pamoja na ahadi ya kununuliwa gari la kutembelea endapo atafanya kama walivyokubaliana. Nadharia hii inaonesha kuwa hakuna ubabe unaodumu kwa mtu hivyo Daktari Juma alipaswa kubadilika na kuwa mwanaume mpya anayeshirikiana na wafanyakazi wenzie kwa kutumia lugha nzuri katika kuwahudumia wagonjwa. Hii ilidhihirika baada ya Halima kuhamishwa hospitali hiyo pamoja na Salama. Daktari Juma aliendelea kuwa mwanaume mpya kwa kuwa na lugha nzuri na kushirikiana kwa kila namna kuhakikisha wagonjwa wanapata huduma nzuri wawapo hospitalini.

Katika nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao: usadikifu: yale yanayoibuliwa katika jamii yawe yanasadikiwa na wasomi. Umari alitumia uhalisia wa mambo ya kijamii kuwa mwanamke akiwa kichaa hawezi kukaa na watoto na kufanya mambo timamu ya kusimamia kiwanda na maduka ya marehemu mume wake. Mambo haya ya uongo yalisadikiwa mahakamani na

kumruhusu kukaa na watoto kihalali kumbe zilikuwa njama za kujimilikisha mali zisizokuwa za kwake. Hata wasomi wa mahakamani walikubaliana naye kuwa ana nia njema ya kuwaandalia watoto wa marehemu maisha yao ya baadae kumbe ni ulaghai.

Katika nchi yenye sifa kama hizi wakati mwingine hata kuua watu wengine huhalalishwa hutegemea mtendaji ni nani na anamtendea nani. Wananchi kwa ujumla walikuwa na kiu ya haki. Umari kuchukua mali za kaka yake bila aibu, anaenda dukani na kiwandani kukagua nyaraka za pesa pamoja na hati za nyumba kama vile ni mali yake. Hii ilijidhihirisha Umari alipoenda dukani alikokuwa akiuza mzee Hasani akauliza makaratasi alioambiwa hakuna hakuamini kabisa mpaka aingia kupekua makabatini.

Mwandishi anaeleza:

> Umari hakumsadiki. Akamtaka afungue kabati dogolililokuwa pale pembeni. Hasani hakuweza kukataa, ingawa alifanya hivyo kwa shingo upande. Umari alihakikisha kuwa hamkuwa na karatasi zozote mle ndani. Akamuuliza kuhusu pesa zilizopatikana. Hasani alimweleza hesabu zake. Tena Umari alisema, “Basi hizi nitachukua.” (Uk. 87).
>
> Alipotoka hapo Umari, alikwenda kule kiwandani. Aliwakuta wafanyakazi wanaendelea na kazi zao kama desturi, wakisubiri amri yoyote itakayotoka kwa mke wa marehemu Amini. Umari aliingia na kuwaambia anataka kuangalia hesabu zote za pale. Mkuu wa pale alisema, “Sisi hatujui lolote kuhusu hesabu hapa. Marehemu alikuwa akiangalia hesabu zote mwenyewe, na pia akiagizia kila kinachohitajika” Umari aliangalia kila upande, lakini hakuona kitu, akaondoka. (Uk. 88).

Hata hivyo Ali, Uledi na Baraka walidhulumiwa haki ya kukaa na mama yao na mama yao alidhulumiwa haki ya kukaa na watoto wake wakati wana

umri mdogo unaowalazimu kutaka kukaa na mama yao. Halima alipotoroka hospitali cha kwanza aliwaza kuwaona watoto wake ndipo aende kwa Bi. Riziki.

> Aliona kuwa huko hataweza kupata msaada, lakini alijua kuwa wakati ni muhimu, na Bi. Riziki huenda akawa hayupowakati ule; au hata akiwepo, huenda akahitaji maelezo marefu. Akaamua kwenda kuwaona wanawe kwanza. (Uk. 148).

Halima alipofanikiwa kufika nyumbani kwa Umari aliweza kuingia ndani baada ya purkshani kubwa pale mlangoni na dada wa kazi. Aliweza kuwaona wanae ambao walifurahi sana baada ya kumwona mama yao. Aliwatoa nje aondoke nao ila dada wa kazi alipiga simu polisi kama alivyokuwa ameelekezwa na Umari na Mariyamu hapo awali. Polisi walimchukua Halima baada ya ugomvi mkubwa na watoto wakarejeshwa ndani. Mariyamu aliporudi ndani akaanza kuwaongelesha watoto vibaya kuwa kwanini wanamfuata mama yao ambaye ni mwendawazimu. Ali alikataa kuwa siyo mwendawazimu bali Mariyamu ni mwongo. Mariyamu alikasirika sana na kumpiga Ali kibao kikali. Hapo ndipo Umari aliingilia kati na kusema kweli kuwa umri ule watoto ni lazima wamtake mama yao.

Mfano:

> Tena alimvuta Mariyamu upande, akamwambia, “Usisahau. Hao ni watoto wadogo. Lazima watamtaka mama yao” (Uk.152-153).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume. Umari alikuwa na kazi nzuri pamoja na mkewe Maryamu hivyo walikuwa na kipato kizuri tu ambacho kinawatosheleza na familia yao. Nadharia hii inamtaka Umari kuwa mwnaume mpya kwa

kujikosoa matendo yake anayoyafanya kwa Halima na wanae ambao ni familia ya kaka yake. Aache utegemezi wa mali za marehemu na kuanza kutumia za kwake na familia yake. Kama mwanaume ajitambue nafasi yake katika familia yake pamoja na namna ya kuwasaidia watoto wa marehemu kaka yake badala ya kudhulumu walivyoachiwa.

Vilevile, katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao mshikamano: hapa tunaona mshikamano kati ya msichana wa kazi wa Umari, Umari mwenyewe pamoja na polisi wanafanikiwa kumrudisha Halima hospitali wakati alitumia mbinu za hali ya juu kutoroka hospitalini ili arudi kuwaona watoto wake. Hata hivyo Mariyamu na mumewe waliujua ukweli kuwa ni lazima watoto wadogo wale wanapaswa kukaa na mama yao hata kama uchu wa mali uliwatuma kumfanyia unyama ule. Hii inafafanuliwa na Miruka, (1994) kuwa matendo ya wahusika huweza kutofautiana baina ya mhusika mmoja na mwingine. Wahusika huwa wanatenda matendo tofauti ambayo hujidhihirisha katika dhamira. Dhamira zinazoigusa jamii unyanyasaji, unafiki na dhuluma. Haya ndiyo aliyofanyiwa Halima na shemeji yake Umari.

Katika riwaya ya *Hiba ya Wivu*, Ihucha alipokuta Farida hayupo nyumbani alichanganyikiwa sana. Alijaa hofu, aliwataarifu marafiki na ndugu wa karibu kama mjomba Musa ila hakuwapa taarifa wazazi wake Farida yaani Mzee Kimambo mpaka alipoona taarifa gazetini. Ihucha hakumtendea haki kabisa mzee Kimambo na alimlaumu sana. Mzee Kimambo alikosewa haki ya kupewa taarifa za mwanae kupotea. Mwandishi anaeleza:

> "Mwanangu! Imekuwaje mambo kama haya yanatokea hamtupi habari mpaka tunayaona kwenye magazeti? Au sio Farida mtoto wetu tuliyemwona kwenye gazeti anatangazwa kuwa kapotea?" Ilikuwa sauti kali yam zee Kimambo, baba yake Farida. "Samahani sana mzee." Ihucha alijikaza kisabuni akaongea, "Tuliona tukiwapeni habari kabla ya kufanya uchunguzi kwanza, tutawapeni wasiwasi. Mpaka sasa kuna dalili ya mafanikio ya kumpata." (Uk. 38).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Hii inaoesha kuwa IhIcha alijifunza kuwa mzazi akipewa taarifa zozote mbaya juu ya mwanae lazima zitamshtua hivyo alianza kufanya utafiti wa kujua nFarida alipo ndipo ikishindikana kumpata awajuze wazazi wake. Kwa bahati mbaya taarifa ikawafikia kupitia gazeti na ndio maana iliwashtua sana. Ihucha alipima madhara ya kuwajuza kuwa Farida amepotea kabla ya kufanya jitihada za kumtafuta ndiposa akaona amtafute kwanza. Haya ni maarifa aliyojifunza katika jamii yake iliyomkuza.

Katika nadharia ya uhalisia kwenye mhimili usemao usadikifu: kueleza mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Ihucha aliogopa kumwambia mzee Kimambo kuhusu kutoweka kwa Farida nyumbani. Kwa hakika alikosewa haki hiyo ila ni kutokana na hali halisi kama mzazi Ihucha alidhani akimwambia mzee huyo ambaye ni mzazi wa Farida, itawajengea hofu kubwa sana huko kijijini walipokuwa. Hata hivyo ulitakiwa mshikamano mkubwa kati ya familia ya Ihucha na mzee Kimambo kushirikiana mpaka Farida apatikane badala ya kuanza kulaumiana.

Katika riwaya ya *Dago wa Munje*, Swafiya alikosa haki yake ya kupata elimu ya msingi ilhali alikuwa na maendeleo mazuri ya kitaaluma. Hii ni kutokana na tatizo la kujihusisha na mapenzi akiwa mwanafunzi na hatimaye kubeba mimba na alipobainika alifukuzwa shule. Hata baba Dago na mama Dago walikosa haki ya kuona binti yao Swafiya akihitimu na kufaidika na matunda ya elimu ya mtoto wa ilhali walijinyima sana kumsomesha. Kitendo hiki kiliwaumiza walimu maana walimpenda kwa bidii yake ya masomo na hata marafiki zake pamoja na wazazi wake waliokuwa na maisha duni ila walijitahidi sana kumsomesha. Mwandishi anaeleza:

> Swafiya alifukuzwa shule tu baada ya kujulikana ni mjamzito. Aibu waliyopata wazazi haikuwasumbua. Uchungu wao zaidi ulikuwa ni kukatizwa kwa matumaini yao kuhusu maisha ya baadaye ya mtoto wao. Ah! Hawakujaliwa kwa upande wa wasichana. Swafiya alipelekwa kwa nyanya yake wa ukeni Tiei akalelee mimba yake huko. (Uk. 42-43).

Nadharia ya mwanaume mpya katika mhimili usemao: kusaidia wake zao na wanawake wengine katika jamii katika kujiendeleza kielimu na kikazi. Baba Dago licha ya kwamba alikuwa na maisha duni. Aliangaika kutafuta vibarua ili watoto wake wa kike waweze kusoma, aliwapa mahitaji ya msingi bila kujali kuwa ni watoto wa kike kama jamii ilivyowachukulia. Hata Dago ambaye ni wa kume naye alipelekwa shule ingawa yeye hakupenda masomo. Kobia, (2004) anaeleza kuwa kuwa ukombozi wa mwanamke uhusishe jamii nzima mwanaume akiwepo. Mwanamke akikombolewa ni jamii nzima imekombolewa. Ukombozi ufanyike kwa kumpa elimu itakayomfanya awafundishe watoto wake wa kike kwa wa kiume wajue tamaduni zinazomgandamiza mwanamke.

Katika nadharia ya uhalisia mhimili wa tatu na wa nne, inaonyesha kuwa jamii nzima wakiwemo wasomi wanasadiki kuwa mwanafunzi anapopata ujauzito hawezi kuendelea na masomo na hivyo hufukuzwa shule. Jambo hili humnyima haki yake ya msingi mwanafunzi wa kike maana anapofukuzwa shuleni hurudi nyumbani kusubiria kujifungua. Jambo hili huwafanya wanafunzi wengi wa kike kukata tamaa ya kuendelea na elimu hasa baada ya kuanza majukumu ya kulea mtoto. Hata hivyo mhimili wa nne unaonyesha kuwa mambo yasiyofaa katika jamii yanapaswa kupigwa na kubadilishwa kutokana na mshikamano wa jamii nzima kwa ujumla. Mabadiliko yoyote katika jamii yanahitaji mshikamano ili kufanikiwa na kufikia malengo. Kobia, (k.h.j) anaeleza kuwa njia ya kumuelimisha mwanamke itamwezesha kupambana na tamaduni zinazomgandamiza na kumfanya akose haki ya kusoma mara apatapo ujauzito ilhali mtoto wa kiume aliyempa ujauzito anaendelea kusoma.

Katika riwaya ya *Tumaini*, Tumaini alikoseshwa haki nyingi na baba yake ikiwemo kusikilizwa na wazazi wake juu ya maamuzi yake ya kuendelea na masomo ya sekondari badala ya kuolewa. Hakusikilizwa hata kidogo hivyo akaamua kutoroka na kwenda kwa mama yake mdogo Halima ili akasomeshwe huko maana wale walikuwa wanathamini elimu. Alikoshwa haki yake ya kupendwa na kuhudumiwa na wazazi wake katika kuisaka elimu. Mwandishi anaeleza:

> Ma Mdogo wake Bi. Halima, hakuchoka kumpa moyo na kumhimiza kusoma kwa bidii. Yeye pia alichangia katika kukamilisha masomo yake. Mapenzi ya wazazi

> aliyakosa kwao nyumbani, aliyapata kwa wafadhili hawa ambao walimchukua Tumaini sawa na binti yao Riziki. (Uk. 122).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Mzee Maumbuko alijifunza katika jamii yake kuwa mtoto wa kike hapaswi kusikilizwa hata kama ana haki. Baba ndiye muamuzi wa kila kitu katika maisha ya mtoto wa kike. Alitumia pombe kama kishawishi cha kuyatimiza haya ila bado Tumaini alipata njia nyingine ya kujikwamua katika mtego huo wa baba yake kutaka kumuozesha ili asiendelee na shule.

Katika nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao; usadikifu: yale yanayoibuliwa katika jamii yawe yanasadikiwa na wasomi. Hii inaonesha kuwa Tumaini hakupewa nafasi ya kujieleza kwa wazazi wake ili wajue kwanini hakukubaliana na mila na desturi zilizoonekana kutaka kumvurugia ndoto zake za kuifikia elimu ya juu na badala yake akawa analetewa watu wa kumfanyia hiyo mila. Hata walipogundua kuwa hataki kabisa, bado waliendelea na mipango ya kutaka kumfanyia hicho asichokitaka. Hali hii ilimpelekea Tumaini kutoroka nyumbani kwao ili akimbilie atakapopata msaada wa kuifikia ndoto yake ya kusoma.

Vile vile, Tumaini alikoseshwa haki kwa wazazi wake ya kupongezwa afanyapo vizuri kitaaluma, tofauti na alivyokuwa akifanya mzee Majaliwa kwa kumnunulia mwanae Sifa zawadi ya baiskeli sababu ya kufanya vizuri katika masomo yake. Mwandishi anaeleza:

> Alianza kuwahusudu akina Sifa na Yohana, ambao hawakuwahi kukumbwa na matatizo kama yake. Walikuwa hodari katika masomo na kila mara wazazi wao waliwahimiza kusoma zaidi. Alikumbuka jinsi Sifa alivyonunuliwa baiskeli na babake, Mzee Majaliwa kwa sababu ya juhudi zake masomoni. Alianza kujisikitikia alipofikiri kuwa licha ya yeye kufaulu vyema katika masomo, halikumpitikia wazo hata siku moja Mzee Masumbuko kumtunukia bintiye zawadi yoyote. (Uk. 21-22).

Hata hivyo mwalimu wa Tumaini alimkosesha haki ya kujichagulia masomo ayapendayo. Mwalimu Majaaliwa hakutaka kabisa wajaze masomo ya sayansi wakati ndilo chaguo la Tumaini ambaye alikuwa na ndoto za kusomea u. Mwandishi anasema:

> “Heh! Tumaini, sijakujua wewe kama mwanafunzi mbishi. Leo umeonyesha ukaidi mkubwa,” mwalimu alitamka kwa hasira na kumsisitiza ajaze masomo mengine bali si yale ya sayansi. (Uk. 116).

Nadharia ya mwanaume mpya inamtaka mwalimu Majaaliwa kuwa mwanaume mpya kwa kumpa uhuru mtoto wa kike kuchagua masomo ayapendayo na kuacha dhana ya kuwa watoto wa kike hawawezi masomo ya sayansi ambayo inaibuliwa na nadharia ya ujifunzaji wa kijamii juu ya watoto wa kike katika taaluma. Hii inafafanuliwa na Gruser, (1992) anaposema kuwa tabia za binadamu hutokana na binadamu kumuambukiza mwingine katika utendaji wake ndani ya familia au jamii kwa ujumla. Mtu huangalia, huiga na kutenda. Kutokana na hali ya mazoea ndipo hujenga tabia.

Nadharia ya uhalisia inaonesha kuwa kutokana na chuki waliyokuwa nayo wazazi wake Tumaini kwa kutokubaliana na mila na desturi walizotaka kumfanyia, bado waliendelea kutomwonesha upendo wa kumpongeza hata

alipofanya vizuri masomoni ingawa jambo hili halikumfanya Tumaini kurudi nyuma kimasomo. Mhimili wa nne unaonesha kuwa mambo yasiyofaa katika jamii ya akina Tumaini pamoja na nyinginezo, yanafaa yaondolewe kwa mshikamano. Jamii ishikamane ili kuyapinga na kuleta mabadiliko yatakayoifanya jamii kupiga hatua chanya.

### 2.2.6 Umuhimu wa Elimu katika Riwaya Teule

Elimu ni maarifa anayoyapata mtu juu ya jambo fulani. (Kamusi ya karne ya 21). Elimu ni muhimu sana maishani. Katika nchi nyingi za Kiafrika mwandishi wa Riwaya ya *Kipimo cha Mizani* anaonyesha kuwa elimu iliyopewa kipaumbele ni ile ya darasani. Suala hili limejidhihirisha pale Bakari alipoletwa kwa Bi. Rehema kufanya kazi za ndani, Bi. Rehema alimuuliza kama amemaliza shule na ndipo alijibu kuwa ameishia darasa la nne. Yule mama alichukua jukumu la kumnunulia vifaa vya shule akamsomesha mpaka akapata shahada yake. Baada ya hapo akaanza kufanya biashara.

Mfano:

> Lakini Rehema alimwambia: “Basi ikiwa kweli unataka kuishi hapa na sisi, lazima uende shule”.
>
> Bakari alishangaa, “Shule! Lakini mimi…”
>
> “Hapana cha lakini. Hilo ndilo sharti langu. Unaona watoto wote hapa wanakwenda shule. Unasemaje?” Bakari alikubali ingawa kwa shingo upande. Rehema hakupoteza wakati. Alimtafutia shule, akamnunulia sare zilizohitajika. Akampeleka mwenyewe kwenda kumwandikisha. (Uk.163).

Hata hivyo Bi. Riziki aliumia sana kuona Rajabu anaacha shule. Alimshirikisha Halima na ndipo wakaona ni vyema kumtafutia kazi kwa kiwandani kwa Amini ambaye alikuwa na shahada yake ya mambo ya ufundi. Mwandishi anasema:

> “Ndio maana ninamwona anakawia kutoka asubuhi.” “Huwa anasubiri ampeleke Ali shule kwanza.” Halima alisita tena akauliza, “Vipi Rajabu? Siku hizi haendi shule?” “Ah, amejitoa mwenyewe. Nimekwisha sema naye lakini hataki kwenda! Sijui nimfanye nini!” (Uk. 38).

Kutokana na nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili usemao; ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Hii inaonesha kuwa Bi Riziki alielewa kuwa mtoto wa kiume namna anavyolelewa anapaswa kuwa na kipato kwa ajili ya kuitunza familia yake. Hii ni elimu ya kiuana katika jamii ambayo mtu hujifunza katika familia au jamii yake kwa ujumla. Baada ya kuona Rajabu kaacha shule na hana kazi yupo tu, ilimlazimu Bi. Riziki kumtafutia kazi kiwandani kwa Amini ili aweza kupata kipato na kujifunza ufundi. Wandera, (2002) anaeleza kuwa elimu katika masuala ya uana ni jambo linalotakiwa kutiliwa mkazo na watafiti wa fasihi maana watafiti wengi masuala ya kijinsia wamekuwa wakijikita katika fasihi ya upande mmoja yaani fani na maudhui yanayoashiria mwanamke.

Elimu ni jambo muhimu sana katika maisha ya binadamu. Katika riwaya ya *Hiba ya Wivu*, Feruzi na Ihucha walikuwa na elimu ya biashara. Biashara yao ilienda vizuri kwa vile walikuwa na elimu ya biashara na masoko. Kila mara walikutana kwa ajili kuwekana sawa na kupeana mbinu mpya.

Farida aliishi kwa mjomba wake Musa ambako alilelewa vizuri na kupewa elimu iliyomwezesha kupata ajira kiwandani ambako aliweza kufahamiana na Ihucha na hatimaye kuoana. Mwandishi anaeleza:

> Mama Farida na Bwana Kimambo hawakupinga ombi la Musa. Walimruhusu amchukue Farida, mtoto wao wan ne, kwa sharti kwamba Musa atamtunza vema na kumsomesha mpwa wake……… Farida alitunza vema, akasomeshwa na hatimaye akahitimu masomo ya sekondari. Baada ya mafunzo chuoni, aliajiriwa na kiwanda cha saa kama Afisa Mipango msaidizi. (Uk. 8).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii usemao: ujifunzaji unahusu kuchunguza kupata habari kutokana na ule uchunguzi na kuunda maazimio kuhusu utendakazi wa tabia hiyo. Hapa Ihucha na Feruzi walishirikiana kwa vile ni wanaume waliokuwa na elimu ya biashara na masoko na ndio maana walifika mbali kibiashara. Hata hivyo Feruzi alijenga mahusiano ya karibu na Farida hadi kuoana kwa sababu ya mahusiano ya kibiashara. Ihucha alimwachisha kazi Farida katika kiwanda cha saa ili amsaidie katika masoko. Hii ni kwa sababu Farida ni mwanamke aliyekuwa na elimu hiyo na alitii maana alielewa kuwa nguzo kuu katika mahusiano yao kijamii ni utii.

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kuwaona wanawake kama viumbe sawa na wanaume kwa kuwaheshimu na kuwapenda katika nyanja wanazokuwepo. Ihucha alimpenda sana Farida na kutambua utendaji kazi wake. Hata baada ya kumwoa alimuachisha kazi ili wasaidiane katika kubuni na kuendeleza biashara yao wenyewe ya uuzaji saa. Ihucha ni mwanaume

mpya anayemthamini mkewe na kumtegemea kama kiumbe sawa na mwanaume.

Inaelezwa na Butler, (1990) anasema kuwa masuala ya kiuana hayako katika mwelekeo mmoja bali huweza kubadilika kutokana na uhitaji pamoja na malengo ambayo hupelekea utendaji wa mara kwa mara.

Katika Riwaya ya *Dago wa Munje*, Mama Dago na baba Dago kwa kujua umuhimu wa elimu waliangaika kwa kila njia ili wawapatie watoto wao mahitaji ya shule ili waweze kusoma. Mama Dago aliamka mapema kila siku kwa ajili ya kumwandalia Dago chochote cha kuweka tumbani kabla hajaenda shule. Alimpikia uji na wakati mwingine viazi au maandazi ili ale kabla ya kuondoka. Wazazi wengi walithamini umuhimu wa watoto kwenda shule badala ya kukaa mtaani wanacheza tu. Mwandishi anasema:

> Kila mzazi alijaribu kumpeleka mwanawe shule; watoto wakae nyumbani kufanya nini na kisomo ndicho kinacholeta maisha bora ya baadaye? (Uk.7-8).

Hata hivyo siku ya Ijumaa ndiyo siku ambayo wazazi wa Dago, pamoja na kwamba hawakusoma walipenda watoto wao wawe na elimu. Hiyo siku walimkagua yote aliyoyasoma wiki nzima, jambo lililompelekea Dago kuichukia siku ya Ijumaa kwa sababu hakuwa na bidii ya masomo. Walimhimiza sana kutia bidii sana ili aweze kufaulu. Mwandishi anaeleza:

> Dago hakuipenda siku ya Ijumaa hata kidogo. …………. Tena, hii ndiyo siku ambayo wazazi wake walimtaka awaonyeshe kazi alizozifanya shule kipindi cha juma zima. Walitaka kuiona bidii ya mtoto wao shuleni ili wazidi kumhimiza. (Uk. 86).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao; ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Hii inadhihirisha namna Dago hakutilia umuhimu wa elimu kwa vile yeye ni mtoto wa kiume. Alikuwa akifanya uzembe kwa sababu yeye ni mtoto wa kiume peke yake. Baada ya dadake kufukuzwa shule, wazazi walimsisitiza sana kutia bidii masomoni ili awafute machozi ya ada waliyoipoteza kumlipia Swafiya na baadae akafukuzwa shule. Matokeo ya Dago kutopenda shule na kutohudhuria darasani kwa wakati yalimpelekea kutofaulu mitihani.

Katika riwaya ya *Tumaini*, Tumaini alipambana sana kuisaka elimu licha ya vipingamizi vya kitamaduni alivyokumbana navyo kutoka kwa baba yake ambaye alimtaka aolewe ili atolewe mahari. Baba yake Tumaini hakuona umuhimu wa elimu kwa mtoto wa kike. Tumaini alipomaliza darasa la saba alikosa matumaini kabisa ya kusonga mbele kielimu kutokana na msimamo wa baba yake. Mwandishi anasema:

> Hata hivyo, hakuna na matumaini ya kuyabadilisha mawazo ya baba yake kuhusu kuendelea na masomo ya darasa la nane. Matumaini yake yalizidi kufifia babake alipoanza kufanya mipango ya kumpasha tohara. Papo hapo Tumaini alifahamu kuwa huo ndio uliokuwa mwanzo wa mwisho wake katika masomo. (Uk. 14).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii kwenye mhimili usemao: mwanafunzi si mpokezi tulivu wa habari, utambuzi mazingira na tabia vinaathiriana katika upataji wa habari wa mwanafunzi. Tumaini alilelewa kimaadili kama mtoto wa kike ili aweze kuwajibika katika jamii na kujitambua. Malezi haya ya kiuana yalimsaidia sana Tumaini kuweza kujipigania kuitafuta haki yake ya elimu aliyoikoseshwa na mzee Masumbuko

na vile vile kuweza kuishi popote. Hata alipokimbilia kwa Halima na Shabani, walimpenda sana kwa tabia yake ya kujituma. Walimu wake pia walimpenda kwa uwajibikaji wake kimasomo. Jambo alilokuwa akilipenda alitia bidii sana. Kwa mfano, mwalimu wake alimkatalia kusoma masomo ya sayansi ila Tumaini alionesha kuyapenda na akaweka bidii sana na kuyafaulu vizuri hadi mwalimu wake akafurahi na kujisikia vibaya kwanini awali alimkataza kusoma masomo hayo. Brown,(1990) anathibitisha wazo la Campbel pale anapoeleza kuwa ushujaa uko wa aina nyingi ikiwemo kupambania jambo walilodhani hautaweza kulifanya na ukafanikiwa hadi kuwashangaza. Mfano, kusafiri safari ya mbali ukafika, kusoma masomo magumu na ukafaulu vizuri, huu nao ni ushujaa.

Tumaini alipambana katika masomo ya sayansi akafanya vizuri mno kinyume na matarajio ya walimu wake ambao walimshauri awali kuacha masomo ya sayansi. Alifaulu vizuri hadi akapewa tuzo. Mwandishi anaeleza:

> Mwisho wa muhula, Tumaini aliwastaajabisha zaidi walimu wake kwa kupata tuzo za juu zaidi katika masomo yote, hususan masomo ya sayansi…... Matokeo ya Tumaini yalimfurahisha mwalimu mkuu ambaye alipeperushia mbali shaka yoyote aliyokuwa nayo juu yake. (Uk. 117).

Nadharia ya mwanaume mpya inamtaka mwalimu wa Tumaini kubadilika na kuwa mwanaume mpya wa kutowadharau watoto wa kike kuwa hawawezi masomo ya sayansi. Tumaini aliwaonesha kuwa mtoto wa kike anaweza kufanya vizuri masomo ya sayansi kama ilivyo kwa mtoto wa kiume bali kinachotakiwa ni bidi katika masomo hayo kama ilivyo kwa masomo mengine.

Nadharia ya uhalisia inaakisi hili katika kusisitiza mshikamano. Katika suala la elimu walimu na wanafunzi hushikamana ili kuweza kupata matokeo mazuri ya kitaaluma katika shule zao. Tumaini alishikamana na wanafunzi wenzie pamoja na walimu ndipo akafanya vizuri kitaaluma. Wandera, (1989) anaeleza kuwa masuala ya kijinsia ni jambo la msingi katika maisha ya binadamu hivyo yafaa jamii kushikamana ili kudumisha yanayosisitizwa na watafiti pamoja na wataalamu wa uwanda huo.

### 2.2.7 Malezi katika Riwaya Teule

Wazazi wana jukumu kubwa katika malezi ya watoto wao kwa sababu watoto wanahitaji kujengewa msingi imara katika maisha yao ya baadaye. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kipimo cha Mizani*, Amini na mkewe Halima waliwalea watoto wao Ally, Uledi na Baraka katika malezi mazuri kiasi kwamba walipohamia kwa Umari baada ya Amini kufariki waliweza kumudu kufanya kazi walizopangiwa na Mariyamu.

Umari na mkewe Mariyamu hawakuwalea watoto wao vizuri. Kila kazi walifanyiwa na dada wa kazi mpaka kuwapiga mswaki kinywani mwao hawakuweza kabisa.

> Ikawa ndiyo ada ya kila siku. Kila alipotoka asubuhi, Mariyamu kuwapeleka wanawe shule na kwenda kazini, aliwaamsha Ali na ndugu zake, akawapa orodha ya kazi anazotaka wazifanye kabla ya yeye kurudi. Na kila aliporudi, alitaka maelezo kwa mtumishi yan vitendo vyote vya watoto hao. Mara nyingi walipatikana wana kosa fulani, na adhabu yao ilikuwa kulazwa na njaa. (Uk. 106-107).

Hata hivyo Mariyamu aliwazuia Ali na wadogo zake kwenda shule ili wabaki nyumbani kufanya kazi za nyumbani wakisaidiana na mtumishi. Vilevile, aliona uvivu kuwaandaa watoto wake pamoja na watoto wa Halima kwa pamoja kila asubuhi, akaona ni bora wa Halima waache shule.

Mwandishi anaeleza:

> Mariyamu aliona ni taabu kubwa kuwatayarisha watoto wote asubuhi kwa kwenda shule; kwa hivyo aliwazuia wale watatu wa Halima, akiwaambia,” Nyinyi msiende shule. Na mnakwenda kufanya nini? Si bora mkajizoesha kufanya kazi za mikono, kama baba yenu?” (Uk. 105).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Maryamu alijifunza kuwabagua watoto wa wenzake na kuwadekeza wa kwake jambo ambalo lilikuwa faida kwa Ali na wadogo zake ambao aliona kama anawanyanyasa kumbe ilikuwa ni njia ya kuwafunza kujitegemea mapema hata walipofukuzwa hapo nyumbani kwa Umari waliweza kufanya kazi kwa Bi Rehema ilhali wana umri mdogo. Malezi ndiyo huonesha matokeo baadae kitabia.

Katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao; wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii. Mariyamu alionekana kuwa mvivu kimalezi na ndiyo maana majukumu mengi ya kulea alimwachia msichana wa kazi. Ndiyo maana watoto wake hawakujua kazi. Halima wanae aliwalea mwenyewe na kuwafundisha uwajibikaji na ndio maana hawakusumbuka hata walipoambiwa kufanya kazi fulani wakiwa kwa Umari. Umari na mkewe walikuwa na roho ya kibaguzi katika malezi ya watoto na

ndiyo maana watoto wa Halima waliachishwa shule na Mariyamu kwa sababu aliona uvivu wa kuwaandaa watoto wote asubuhi kwenda shuleni. Hata umari alipoambiwa kuwa wameachishwa shule naye hakuchukua hatua.

Malezi ni jambo la msingi sana katika uhai wa watoto. Katika riwaya ya *Hiba ya Wivu*, Farida alilelewa vizuri na mjomba wake na ndio maana alikuwa na uoga wa kukubaliana na mipango yote aliyoipanga Ray. Hata hivyo Ray alilelewa katika mazingira ya uhuru sana kulingana na kazi alizokuwa akizifanya, alikuwa akiishi peke yake na wala hana mke. Aliangaika kutafuta pesa ila pia alikuwa na matumizi makubwa hasa kwa tamaa za mapenzi. Malezi ndiyo yanayopelekea tabia za mtu awapo mtu mzima. Ray anamshawishi Farida amwache mumewe ili amwoe ila anagonga mwamba. Mwandishi anasema:

> “Nakupenda kwa penzi la mke na mume. Penzi la dhati, penzi la huba. Sio penzi la kaka na dada, au la mchaga kwa mchaga. Nataka uwe mke wangu wa ndoa Farida”. Baada ya kusema hayo Ray alikuwa alihema, kama mtu aliyeutua mzigo……………. Farida alidakia, “Kuniambia yepi zaidi? Kwamba unanipenda! Nasikitika kuwa umechelewa, samahani sana. Mimi niliishapendwa na niliishapenda, nikafunga ndoa. Sitapenda tena kwa mara ya pili hiyo ni ndoto.” (Uk. 73-74).

Nadharia ya mwanaume mpya m mhimili usemao : kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume. Ray alijifunza kuwa mwanaume anachomwambia mwanamke lazima amkubalie na ndio maana alikuwa na matumaini makubwa kuwa atampata Farida kutoka wa Ihucha. Hata hivyo Ray alijifunza ubaguzi wa kikabila na hivyo alijua Farida atamkubali kwa vile ni mchaka mwenzie na kumuacha Ihucha amabye ni Mnyaturu. Nadharia hii

inamwonesha Ray kuwa mwanaume mpya kwa kujikosoa yale aliyoyafanya na kumpa uhuru Farida kuamua. Alitekeleza Farida alichosema kwa mfano kumrejeshea zile elfu hamsini zilizotoka kwa Ihucha ndipo Farida mwenyewe akubaliane na mipango ya Ray au la ya kumkubali kimapenzi.

Katika nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao; wahusika waonyeshwe kama walivyo. Hii inaonyesha kuwa maisha ya Ray yalikuwa ya kiujanja kulingana na alivyolelewa. Tabia yake ilikuwa tofauti na ya Farida ambaye alilelewa katika maadili ya dini na pia hakuzoea uongo. Ndiyo maana uongo na njama zote walizozipanga na Ray zilishindikana na hatimaye kukamatwa na mumewe Ihucha kuwa ni mwongo na hatimaye akatubu na kusema kweli kuhusu mchakato mzima wa kutekwa kwake nyara.

Malezi ndio msingi wa familia. Kila mzazi anapaswa kumlea mwanae kwa kufuata maadili mema ili aweze kuendana na mienendo ya jamii anamoishi. Katika riwaya ya *Dago wa Munje*, wazazi wa Dago hawakumfuatilia kitabia na ndio maana alikuwa na tabia mbaya za kutopenda kusoma pamoja na kuwa mchafu asiyependa kufua nguo zake wala kuoga. Ilifikia wakati akawa sugu kabisa kwa adhabu alizokuwa akipewa shuleni bila kubadilika kitabia. Mwandishi anaeleza:

> Dago hakuogopa adhabu yoyote. Alikuwa amezoea kupewa adhabu, kwa sababu alikuwa akichelewa shule mara nyingi, ingawa mama yake hakuyajua haya. (Uk. 15).

Hata hivyo Charo ambaye alimpa mimba Swafiya, alikuwa hafahamiki vizuri pale Munje maana alikuwa ni mtu wa kurandaranda tu hivyo hakueleweka kama alikuwa ana kazi ya kuweza kumtunza Sawafiya na mwanae baada ya kujifungua. Mwandishi anaeleza:

> Kwanza, Charo hakuwa na kazi na hajawahi kuajiriwa tangu amalize kidato cha nne mwaka uliokuwa umepita. Hakufuzu vizuri lakina hakujali. Charo alikuwa mfano mzuri wa wale vijana waliorandaranda mitaani wakitegemea pesa za wazazi wao. (Uk. 41).

Dago alidekezwa sana na wazazi wake na ndio maana hawakumfuatilia sana kitabia, akawa mvivu na mchafu. Aliona wazazi wake wanampenda sana na ndio maana akawa hatii bidii masomoni. Kazi ya kulea wanafunzi ni ya wazazi kwa kushirikiana na walimu wanaomfundisha. Kudeka kulimfanya Dago awe na tabia zisizopendeza hadi kuwa anafuatiliwa na marafiki zake wa shuleni ambao walimfuatilia hadi nyumbani. Mwandishi anaeleza:

> Jinsi walivyovunjwa moyo na Swafiya, walijaribu sana kumsukuma Dago. Katika msukumo huu pengine wazazi walimdekeza mno mvulana huyu wa pekee pale nyumbani, akajiona dume, la kufanyiwa na waliopo! Na mara kwa mara mawazo ya kumrudisha Swafiya shule baada ya kujifungua yaliwajia. (Uk. 86).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: ujifunzaji unahusu kuchunguza kupata habari kutokana na ule uchunguzi na kuunda maazimio kuhusu utendakazi wa tabia hiyo. Hapa tunamwona Dago akiakisi malezi aliyolelewa kama mtoto wa kiume maana jamii yao ilimwonesha kuwa hapaswi kulazimishwa asichokipenda na matokeo yake kuibuka na tabia za ajabu katika familia na jamii kwa ujumla za kuwa mtoro shuleni, mchafu na kikojozi.

Nadharia ya mwanaume mpya inaonesha kuwa Dago anapaswa kubadilika na kuwa mwanaume mpya maana hakuna tabia zinazodumu kwa mtu isipokuwa ni kukubali mabadiliko ya kutoka kwenye uhasi na kuingia kwenye uchanya kama ilivyoelezwa na (Butler, 1990).

Katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao; wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii, tunaona kuwa Dago amechorwa kama alivyo kulingana jamii ya sasa. Mtoto anapodekezwa akikua anafanya vitu vya kuwaumiza wazazi wake ila wanashindwa kuvisahihisha maana wanakuwa wameishachelewa. Kihistoria watoto wa kiume walithaminiwa na kuonyeshwa kuwa hawapaswi kuwajibika sana katika masuala ya usafi kama walivyo watoto wa kike. Suala hili ni tofauti katika jamii ya sasa maana elimu ya afya inatolewa kwa watoto wa kike na wa kiume ili wote wajue umuhimu wa usafi na elimu bora. Dago alikuwa sugu kwa adhabu alizokuwa akipewa shuleni kila siku kutokana na uzembe darasani pamoja na kuchelewa shuleni kila siku.

Katika riwaya ya *Tumaini* kuna malezi ya namna tofauti ambapo vijana walikuwa na tabia za ajabu kutokana na malezi waliyolelewa. Idi ambaye ni mdogo wake Tumaini aliwadharau sana dada zake na kuwaona kama watumishi tu pale nyumbani. Hii dhana alijengewa na baba yake, mzee Masumbuko ambaye naye alikuwa na tabia hiyo. Mzee Masumbuko alimwendekeza sana Idi kwa sababu ni mtoto wa kiume. Mwandishi anaeleza:

> Kila mara alimkabili na kumkumbusha babake kuwa lugha aliyotumia dhidi yao ilikuwa inamwathiri vibaya kaka yake mdogo. Babake alimkemea na kumkanya kutoingilia malezi ya Idi kwani yeye ni mtoto wa kiume, si wa kike. (Uk. 14).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii tunaona katika mhimili usemao: ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Mzee Masumbuko alikuwa mtu wa kudharau jinsi ya kike na ndiyo maana akamuambukiza mwanae Idi kimalezi naye akawa anawadharau dada zake na kuwaona pale nyumbani siyo kwao isipokuwa yeye. Dhana hii ilimaanisha kuwa watoto wa kike ni kwa ajili ya kuolewa hivyo wa kiume ndiye mwenye mji. Elimu ya kiuana waliipata katika familia hii baada ya Tumaini kuendelea kimasomo na kuwa na kipato kizuri ndiye akawa msaada kwa familia yake. Idi pamoja na kuthaminiwa kuwa ni mtoto wa faida kwa vile ni wa kiume, naye alisaidiwa na dada yake aliyekuwa akimwona kama mfanyakazi pale nyumbani. Mzee Masumbuko naye alikuja kupata elimu hiyo baada ya kuanza kuasaidiwa na binti yake, kinyume na alivyotarajia.

Majuto ambaye alijiona mwamba alifukuzwa shule kila mara kutokana na malezi mabaya ya wazazi wake. Ilifikia wakati shule ikamshinda kabisa na wazazi wake hawakuona kama ni tatizo lao la malezi kwani walimtetea sana. Alifikia wakati wa kuwarushia mawe walimu wake mara walipomkanya kutokana na tabia zake mbaya.

Mwandishi anasema:

> Mara kadhaa Majuto alifukuzwa shule kwa sababu ya utovu wa nidhamu lakini Bwana Andrea alimtetea mwanawe huku akitumia cheo chake, na Majuto alikubaliwa fursa nyingine. Wakati mwingine, Majuto kwa kushirikiana na mwenziwe Kijungwe, walivunja afisi ya mwalimu mkuu na kuiba madaftari ambayo walimwuzia Bwana Karim. (Uk. 20).

Nadharia ya mwanaume mpya katika mhimili usemao: kukubali majukumu yoyote ya kiuana bila kujali jinsia na bila kujali watu waliowazunguka. Mzee Masumbuko, Idi na Majuto pamoja na babake Majuto wote wanaweza kubadilika na kuwa wapya kwa kuacha ubaya wa kubagua kazi kijinsia na kufanya kazi yoyote katika familia na jamii kwa ujumla ili kuleta heshima na maendeleo kwa jinsia zote bila kubaguana na kudharauliana.

Nadharia ya uhalisia inaliakisi hili kwa kuelekeza kuwa wahusika waonyeshwe kama walivyo. Majuto alikuwa na kiburi sana, hii ilitokana na wazazi wake kuona wana uwezo wa kifedha wakadhani pesa ni kila kitu. Mtoto wao alipofukuzwa shule wao waliona hajatendewa haki. Wazazi wenye uwezo kiuchumi wanawalea watoto wao katika malezi mabaya yanayowafanya washindwe kukubalika katika baadhi ya maeneo ya kijamii ikiwemo shuleni.

### 2.2.8 Migogoro katika Riwaya Teule

Migogoro ni hali ya ukinzani katika pande mbili au ni hali ya kutoelewana baina ya kundi na kundi au mtu na mtu. Mgogoro unaweza kuwa nafsini mwa mtu ambapo anakuwa na ukinzani wa kifikra. (Kamusi ya karne ya 21) Jamii yoyote ile haikosi migogoro. Katika jamii za Kiafrika migogoro mingi

huibuka katika jamii kutokana na sababu mbalimbali. Katika riwaya ya *Kipimo cha Mizani* imo migogoro ya aina nyingi ukiwemo mgogoro wa kijamii, kiuchumi na wa nafsi. Mgogoro wa kijamii umetawala sana katika riwaya hii maana yanaibuka masuala ya kitamaduni ambapo Umari anaona ana haki ya kukaa na watoto wa marehemu kaka yake ambaye ni Amini. Mzee Hasani na Bi. Riziki wote wanashangaa utaratibu huo na kumsisitiza Halima ambaye ni mama wa watoto hao asikubali. Hata hivyo Umari bado anaona ana haki ya kufuatilia mirathi ya marehemu kaka yake pamoja na kusimamia mali zote jambo ambalo linapingwa vikali na Halima pamoja na Selemani ambaye ni rafiki mkubwa wa Amini na mshauri wake.

Umari aliwachukua watoto wa Halima wakiwa shuleni bila mama yao kujua ila dereva anakataa kabisa wasichukuliwe na Umari, kunaibuka mzozo mpaka Umari anafanikiwa kuwachukua. Mwandishi anaeleza:

> "Vipi bwana? Hawa watoto mimi ndiye ninayewachukua kila siku. Wewe nani? Na unawapeleka wapi?" Umari alimjibu kwa ukali, "Mimi ni baba yao mdogo. Waulize wenyewe watakwambia. Nitawachukua nyumbani. Na wewe chukua bahasha hii, umpelekee mama yao." (Uk. 94).

Halima alipopokea barua kuwa mahakama imeamua watoto wakae kwa Umari hakukubaliana nayo maana alijua kabisa hizi ni njama za Umari maana watoto hawawezi kukaa na baba mdogo wakati mama mzazi yuko hai na watoto bado ni wadogo. Halima aliamua kuwafuata wanae kwa Umari ambapo kuliibuka ugomvi mkubwa maana Umari hakutaka kabisa watoto warudi kwa mama yao Halima. Mwandishi anaeleza:

> Mzozano ulikuwa wa kweli. Halima alikuwa mkali. Hakusikia wala kujali lolote. Alikuwa kama chui anayelinda watoto wake. Alipoona Umari anamjibu kwa bezo na dharau na stihizai, hakuweza kuzuia hamaki zake. Alimrukia na kumkamata shati. Hamaki zake zilifoka wakati ule bila ya kizuizi. Umari alisimama mbele yake akimzuia asiingie ndani. Halima alianza kumpiga Umari makofi na akamchania shati lake. (Uk. 96).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao; mwanafunzi si mpokezi tulivu wa habari, utambuzi mazingira na tabia vinaathiriana katika upataji wa habari wa mwanafunzi. Hii imedhihirishwa na Halima kuwa alielewa kabisa kuwa ana haki ya kukaa na wanae na ndiyo maana alipambana na Umari ili asimdhulumu haki yake ya msingi ya kukaa na watoto wake. Halima hakujali kuwa Umari ni mwanaume bali alipigania haki yake. Hali ya maendeleo katika jamii inaletwa na wanawake na wanaume. Amini alishirikiana na mkewe katika shughuli mbalimbali na hivyo baada ya Amini kufariki Halima angesimama mwenyewe katika shughuli zake za kimaendeleo ila alikatishwa na njama za Umari.

Vile vile, kuna mgogoro wa kiuchumi ambao uliibuliwa na Umari kutaka kujimilikisha mali na kufuja pesa wakati anaishi kwenye nyumba ya kupanga. Yeye na mkewe Mariyamu wanapenda kuishi maisha ya hali ya juu wakati uwezo huo hawana. Baada ya kukosa pesa na kuona hali ya uchumi inakuwa ngumu ndipo Umari anaanza kutafuta namna ya kupata sehemu ya shamba alilorithishwa na baba yake ili aliuze. Kunakuwa na sintofahamu baina yake na kaka yake Amini baada ya kumshauri kutotumia pesa vibaya na

kumwambia awe anatunza kwa ajili ya maisha ya baadae pamoja na familia yake kwa ujumla. Mwandishi anasema:

> “Lakini hufikirii ya mbele. Wewe unataka kuchezea pesa tu. Sasa zikimalizika, utafanya nini?”“Haijakuhusu. Mimi ninataka sehemu yangu. Wewe uza, au nunua sehemu yangu, kama unavyotaka! Lakini mimi nipate haki yangu tu. Sasa hapo kuna ubaya gani?” (Uk. 28).

Umari aliendelea kumshambulia kaka yake kwa maneno. Umari alishapewa pesa kwa ajili ya shamba na alipoitumia ikaisha akarudi kwa Amini akitaka auze duka ili ampe sehemu yake. Amini alikataa na kuendelea kumshauri ila mdogo wake akawa hataki kuelewa maana shida yake ni pesa tu kwani hali ya kiuchumi ilimuwia ngumu sana pamoja na kwamba yeye na mkewe walipenda maisha ya kifahari. Mwandishi anaeleza:

> “Lakini mimi sehemu yangu ninataka kuuza. Basi angalia mwenyewe. Ikiwa unataka, unaweza kununua sehemu yangu. Kama, hutaki, basi tutafute mtu atie bei, tupate kuuza!”…………………….. Pesa zote nilizokuwa nazo ndizo nilitoa kumlipa kwa ile sehemu yake, ili nyumba ibaki. Leo tena anataka tuuze duka. Pesa zile zote amezifanyia nini?” (Uk. 30).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao : kutoonesha udikteta katika familia zao na jamii inayowazunguka. Umari anaweza kuwa mwanaume mpya kwa kuacha tabia zote mbaya za kupenda kuuza vitu na kutumia pesa hovyo. Kupenda kuvuna ambako hajapanda mfano kutaka kumiliki mali za marehemu kaka yake kikiwemo kiwanda na duka pamoja na nyumba ya marehemu kaka yake na kuwaacha wanae wakilelewa na watu baki mfano Bi Rehema wakati yeye mdogo wake marehemu yuko. Anakuwa kama anafurahia kifo cha kaka yake ili familia yake iishi kwa mateso ayasabishayo Umari mwenyewe na mkewe Maryamu. Akiacha tabia hizo mbaya na kuwa

na nzuri hapo ataacha udikteta na kumwona Halima kuwa anaweza kutunza wanae pamoja na mali zake na marehemu mumewe.

Halima alikuwa na  mgogoro wa nafsi baada ya kupata barua ya Umari kuwa watoto wake mahakama imeamua wakae kwa Umari. Halima alipata mshtuko sana baada ya kupokea barua kutoka kwa dereva, akaifungua na kuisoma. Mikono ilimtetemeka sana na moyo kumdunda. Bi. Riziki naye alijaa hofu akisubiri Halima amwambie kuna nini katika ile barua. Wote walijaa hofu bila kujua kilichomo katika barua na nini wafanye ili kumsaidia Halima akae sawa. Mwandishi anaeleza:

> Halima alitikisa kichwa, tena akajitupa juu ya kiti. Akafumba macho na kuvuta pumzi, ili kujaribu kuutuliza moyo wake uliomwenda mbio…………. Alipomaliza, alipiga kelele, akasema, “La, haiwezekani. Sikubali. Hii sio haki. Wanataka kuninyang’anya wanangu!” (Uk. 95).

Umari naye alipata mgogoro wa nafsi mara aliporejea nyumbani na kukuta Mariyamu kawafukuza watoto wa Halima kuwa wamfuate mama yao ilhali watoto ni wadogo na hawajui mama yao alipo. Mariyamu alionesha kabisa kuwa hahitaji watoto wale warudi kukaa kwake. Alimwambia Umari kuwa hakuhitaji kuwatafuta na hata Umari akiwatafuta awatafutie pa kwenda na sio kuwarejesha pale nyumbani. Mariyamu alisema kuwa endapo atawarejesha mle ndani, atachukua watoto wake aondoke mle ndani amwache Umari na watoto wa Halima. Umari alipata wakati mgumu maana hataki kumhudhi mkewe na vilevile anawaonea huruma wale watoto wadogo maana hawana pa kukaa. Umari alibaki tu ndani akinung’unika moyoni bila kuwa na uamuzi wa nini afanye. Mwandishi anaeleza:

> Nimewafukuza! Na wamfuate huyo mama yao!" Mariyamu alijibu. Umari alishangaa, tena akasema, "Umefanya vibaya sana. Unasahau kama hao ni watoto wadogo bado, na lazima watamtaka mama yao?"………. Umari ingawa alihisi vibaya, lakini hakuwa na hamu kubwa sana ya kutoka nje, kuangaika majiani kuwatafuta. Alishusha pumzi na kusema, "Baada ya muda, lazima watarejea wenyewe" (Uk. 174).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao; vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Hapa Umari alifunzwa na familia yake namna ya kuwa na upendo kwa jamii nzima ikiwemo familia yake na ya ndugu zake. Kitendo cha kukuta akina Ali wamefukuzwa na Maryamu kilimshtua sana na kumpa mawazo maana wale watoto ni wadogo, baba yao kafariki na mama yao kafanyiwa njama na Umari ili aishi hospitali. Vishawishi vya mali vilimfanya aondoe utu ila bado haukuondoka wote na ndio maana alikosa raha kutokana na watoto kufukuzwa nyumbani wakiwa hawana pa kuishi.

Katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao; uyakinifu: kuelezea mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Hii inaonekana katika familia ya Umari, Mariyamu aliwafukuza watoto wa Halima wakati anajua ni wadogo sana na amewataka kumfuata mama yao wakati aliko hawawezi kwenda. Umari alipojua aliumia sana moyoni ingawa hakuwa na maamuzi kwani mkewe angekuja juu sana.

Katika riwaya ya *Hiba ya Wivu* kuna migogoro mbalimbali ambayo imezungumziwa na mwandishi. Mgogoro wa kijamii ndio ambao umetawala

kwa sehemu kubwa katika riwaya hii. Farida anakuwa na tabia ya kutomwamini mume wake hasa anapochelewa kurudi nyumbani anapokuwa katika shughuli za biashara. Farida anaamua kutoka nyumbani usiku kumfuata mumewe huko hotelini anakofanyia vikao na wafanya biashara wenzie. Hata hivyo mgogoro huu unakuzwa na Ray ambaye anakuwa na tamaa juu ya Farida na kumpeleka nyumbani kwake na kukaa naye siku mbili na siku ya tatu ndipo anamruhusu kurudi nyumbani baada ya kufanya njama za kumlipisha pesa Ihucha.

Mgogoro huu unaibua mafarakano na kuleta mtafaruku katika familia ya Ihucha maana Ihucha hakumwamini kabisa mdogo wake Aisha ambaye alibaki ndani na Farida wakati Ihucha alipoenda kazini. Aisha alimweleza kaka yake kwa masikitiko kuwa naye anaumia kwa Ihucha kutomwamini kuhusu kupotea kwa Farida. Mwandishi anaeleza:

> "Kaka Ihucha, kwanza, mimi nasikitika sana kwa jinsi unavyonihisi kuwa mimi nakuficha lolte kuhusu kupotea kwa wifi. Hata mimi roho inaniuma sana kwa kutokujua lililolomfika Farida. Kutokana na hasira zako kwangu ambazo kwakweli hazinistahil, nashindwa hata kukuuliza nujue umefikia wapi katika kumtafuta. Pili, ningekushauri sana ujaribu kula chochote. Tangu jana usiku hujala kitu," aliongea Kinyaturu. (Uk.16).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao : ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Hii inadhihirishwa na mhusika Farida ambaye alipata elimu ya kiuana kuwa si kila mwanaume anapochelewa kurudi nyumbani anakuwa katika mambo mabaya. Kuondoka kwake Farida akimfuata mumewe na bila kumuaga wifi

yake Aisha, kunapeleka Aisha kutoaminika kwa kaka yake Ihucha hasa alipofika nyumbani na kumkosa mkewe. Tabia ya kuondoka kwa Farida nyumbani usiku bila taarifa kwa aliye naye ndani wala mumewe ndiyo ilileta matokeo mabaya ya kuwatia hasara za kutangaza magazetini na kuwapa misukosuko wazazi pamoja na ndugu wengine wakiwemo marafiki. Taswira za kimaendeleo zinajidhihirisha kwa wahusika wanaoweza kufanya maamuzi bila kuwaathiri wengine. Farida anaonesha wivu wa hali ya juu unaompelekea kufanya maamuzi ambayo yangeweza kuhatarisha maisha yake, hii ni dalili kuwa alikosa elimu ya kiuana.

Vile vile kuna mgogoro wa kiuchumi ambao unaibuka pale dereva wa teksi Bwana Chaurembo anapopata pesa kutoka kwa Ihucha kuwa yeye ndo kampata Farida kama tangazo la gazetini lilivyoeleza kuwa atakayempata Farida atapewa zawadi nono. Farida alikodi teksi ya Bwana Chaurembo na kupelekwa nyumbani kwa mumewe. Aliumia sana kuona jamaa huyo anapewa ujira bila kuufanyia kazi. Mwandishi anaeleza:

> "Mimi ni Bwana Chaurembo. Nimempata huyo binti. Nimemtoa Ilala Sharifu Shamba mpaka hapa kwa teksi yangu. Yeye kaomba nimshushe mbali kidogo na hapa kwake labda hakupenda majirani wamwone akishuka kwenye gari.……. Hivyo nadai zawadi yangu kama ulivyoahidi."…….. "Tulia Farida, usihamaki," alitamka Ihucha taratibu.….. Wewe alikukodi tu, na hela yako kaisha kulipa. Yaliyompata ni makubwa, usitake kumsumbua bure." (Uk. 54).

Mgogoro wa nafsi pia umetawala katika riwaya hii. Ihucha alipata wakati mgumu alipofika nyumbani akamkosa mkewe nyumbani. Hakujua Farida kaenda wapi na nini kimemkumba usiku huo. Ihucha hakulala kabisa mpaka

asubuhi alipoamua kwenda polisi na kutangaza gazetini. Vile vile hata Farida akiwa kwa Ray alishindwa kulala kabisa, akawa anawaza juu ya mumewe Ihucha. Farida aliwaza na kulia usiku kucha na macho yakavimba na kuwa mekundu. Ray pia alipata mgogoro wa nafsi mara baada ya kupigiwa simu na Ihucha kuwa anataka kwenda Ilala Sharifu Shamba nyumbani kwa Ray ili wapate kuzungumza. Alisema anapafahamu hahitaji kuelekezwa. Ray alipata wakati mgumu sana maana hakujua ni kwa vipi Ihucha amepajua nyumbani kwake na anataka waongee nini. Ndipo Ray aliamua wakutane siku hiyo hiyo na si kesho yake kama Ihucha alivyoomba. Vile vile Ray alizidi kupata wakati mgumu akilini mwake alipomwona Ihucha anafika nyumbani kwake akiwa na Farida. Alijua kuwa mipango yake yote imefahamika. Mwandishi anaeleza:

> "Mimi ni Ihucha. Nimekupigia saa hizi kwa sababu nasikia mchana una biashara ya teksi. Nina shida na wewe kidogo, nataka tukutane………… Mimi ni mumewe Farida aliyekuwa amepotea." ….Simu ya Ihucha ilimdhihirishia Ray kuwa Farida ndiye aliyedondosha mkufu huo, na kwamba amekwishatoa siri. Kama sio hivyo, kwanini Ihucha ampigie simu? Kamjuajuaje? Kaifahamuje nyumba yake? Kwa upande mwingine, alibashiri kwamba kama Farida hakutoa siri, basi Ihucha kamtambua katika uchunguzi wake baada ya kumwona siku ile alipokuwa akichukua pesa bondeni. (Uk. 101).

Nadharia ya ujifunzaji mhimili usemao: vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Ihucha licha ya kwamba alikuwa amekunywa pombe, kitendo cha kumkosa mkewe usiku ule nyumbani pombe zote ziliisha maana alijifunza kuwa mkewe anapaswa kuwa ndani usiku huo, kitendo cha kutokuwepo kilimpa hofu kubwa. Vile vile Ray alidhani akiongea na Ihucha siku ile ile kidogo itampunguzia hofu ya kubainika kuwa alimtaka Farida kimapenzi ila haikusaidia hata kidogo.

Katika nadharia ya uhalisia kwenye mhimili usemao; uyakinifu: kueleza mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Hali iliyompata Ray baada ya kumwona Ihucha nyumbani kwake akiwa na Farida ni udhihirisho tosha kuwa binadamu ni kawaida yake kufanya mambo mabaya ila yanapobainika humpa wakati mgumu sana. Hata njama alizozitumia Farida kuandika kikaratasi ambacho alikifikisha kwa Ray kiujanja ili aweze kuinusulu ndoa yake. Hakika huu ndio uhalisi wa msemo wa majuto ni mjukuu. Hali aliyokuwa nayo Farida pamoja na Ray baada ya kubainika kuwa kila walichokifanya ulikuwa ni uongo, kiuhalisia iliwalazimu kutubu ili waweze kujinusulu.

Katika riwaya ya *Dago wa Munje* kuna mgogoro wa nafsi, kiuchumi na wa nafsi ambayo imejidhirisha kupitia matendo ya wahusika. Mgogoro wa kijamii. Huu ndio umetawala kwa kiasi kikubwa katika riwaya hii. Jamii ya Munje ilikuwa na mambo mbalimbali ya kijamii ikiwemo mila na desturi. Walithaminiwa sana watoto wa kiume kuwa ndio wapelekwe shule ili waje kusaidia familia wakiwa na maana kuwa watoto wa kike wataolewa na kwenda kwingine nje ya familia yao. Haya yalijidhirisha baada ya Swafiya kupata mimba akiwa shuleni. Wazazi wake walijuta sana kumpeleka shule. Mwandishi anaeleza:

> "Kulea msichana kweli ni vigumu. Kumsomesha japo ni maendeleo huleta matatizo. Haya hasinaliyapata mwanangu kama ningesikia ya nyanya yake. Niliambiwa lakini sikusikia. Mhm, kidonda kibichi ndicho kinachotoneshwa. Masomo humuondoa haya msichana."(Uk. 38).

Familia ilimtegemea Dago kwa maana ndiye anabaki kwenye mji dada zake wanapoolewa. Hata hivyo jamii iliona kuwa kumsomesha mtoto wa kiume ni faida zaidi kuliko mtoto wa kike. Mwandishi anaeleza:

> Si ajabu basi, kwamba kila mtu nyumbani mwao alimtegemea Dago kuuleta mwanga uliohitajika sana nyumbani humo. Wazazi wake Dago walikuwa wakitaka mtoto wao apate elimu ya kutosha. kwa sababu Dago alikuwa mtoto wao wa pekee aliyebakia shule, na wa kiume atakayeushikilia mji wasichana wanapokwenda kwa waume zao, walijaribu juu chini kumpatia kila kitu walichoona ni faida kwake. (Uk. 43).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao; ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Hii inadhihirisha kuwa wazazi wa Dago walimwona kuwa yeye ndiye tegemeo la familia yao maana alikuwa wa kiume peke yake. Hii ilitokana na kuwa wazazi hawa ndiyo elimu ya kiuana waliyokuwa nayo. Kumwonesha Dago kuwa yeye ndiye nguzo ya familia kulimpelekea kuwa na tabia zisizopendeza maana hakutia bidii masomoni akawa anaanguka katika mitihani yake. Hili lilikuwa tatizo la jamii nzima ambapo waliwashangaa sana baba na mama Dago kwa kuwasomesha watoto wa kike. Kutoka na taswira hiyo, ndio maana jamii ya Munje ilikuwa nyuma kimaendeleo kutokana na msimamo huu juu ya elimu ya kiuana.

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume. Hii inaonesha kuwa Dago na baba yake pamoja na wanaume wengine katika jamii ya Munje wanaweza kubadilika na kuwa wazuri kitabia kwa kuachana na hizo mbaya za kuwabagua watoto wa kike

kielimu na kuwaona ni vimbe sawa na wanaume katika sehemu mbalimbali katika jamii.

Mgogoro wa kiuchumi nao ulijidhihirisha kwa namna ya tofauti. Kijiji cha Munje kilijaa watu masikini wasio na uwezo wa kujenga nyumba nzuri. Nyumba zote zilikuwa ni za hali ya chini kiasi kwamba watu walikuwa hawawazi kufanya mabadiliko kwani hawana namna nzuri ya kujikwamua. Baba na mama Dago walishindwa kumpeleka Nchimoni shule ya sekondari kwa maana hawakuwa na pesa za kulipia ingawa alifaulu vizuri masomo yake na kupangiwa shule. Jambo hili liliwaumiza sana kama familia ingawa Nchimoni aliridhika tu kukaa nyumbani wakati wazazi wake wakitafuta namna ya kumsaidia. Baba yake Dago alimwambia mwalimu mkuu wa Munje bwana Beja kuwa Nchimoni hataweza kwenda sekondari sababu ya ukosefu wa ada hivyo aende mwingine mwenye uwezo wa kulipa ada. Mwalimu alimtafutia Nchimoni chuo cha ualimu wa chekechea na akaenda masomoni. Mwandishi anaeleza:

> Babake Nchimoni alikuwa keshamwelezea mwalimu huyo kuwa mwanawe hangeweza kuhudhuria shule aliyopewa, kwa hivyo nafasi yake ingepewa mwanafunzi mwingine aliyekuwa na uwezo wa karo. Baada ya kuelezwa matatizo ya karo za shule ya upili, na fikra za Nchimoni, mkuu wa shule alijawa na huzuni. (Uk. 33).

Nadharia na mwanaume mpya mhimili usemao: kusaidia wake zao na wanawake wengine katika jamii katika kujiendeleza kielimu na kikazi. Baba Dago alijieleza kwa mwalimu kuwa anapenda kumsomesha Nchimoni ila hana pesa za ada na ndipo alipata msaada wa kumpeleka kwenye chuo. Mwalimu wa Nchimoni na baba Dago ni wanaume waoya maana

wanamsaidia mtoto wa kike kupata elimu na babadae Nchimoni alipata kazi na kuwa msaada kwa familia yake. Mgogoro huu ulitatuliwa na mwalimu wa Nchimoni kwa njia hiyo vinginevyo baba Dago angeendelea kuishi kwa kukosa raha mkila amwonapo mwanae nyumbani.

Mgogoro wa nafsi umeelezwa kwa namna mbalimbali. Dago alipata wakati mgumu alipokojolea nguo za shule zikalowa kabisa wakati ndizo anapaswa kuzivaa shuleni. Alipoamshwa na mama yake alipata wakati mgumu sana. Aliweza kujiandaa kwenda shule. Aliwaza sana kuzinyoosha kwa kutumia pasi ya mkaa ila akahisi mama yake atagundua kuwa kakojoa kitandani na ndipo aliwaza kwenda kunywea uji wake karibu na meko ili azivae nikiwa mbichi zikakaukia pale mekoni anywapo uji wake. Mwandishi anaeleza:

> "Na hizi ndizo nguo nitakazovaa kwenda shuleni" Moyo ulimdunda kwa hamaki iliyochanganyika na hisia za uchungu moyoni. "Watu watasemaje leo nikifika shule?" Dago alifikiria akiwa bado anapindukapinduka kitandani. Punde si punde alitoka akiwa ameshika fuko wa vitabu mikononi mwake. Alifululilza moja kwa moja hadi jikoni…………… Fikra za Dago zilikuwa kuketi karibu na moto, ili nguo zake zipate kukauka. (Uk. 10-13).

Mama Dago alipata mawazo sana, Swafiya alipopata mimba akiwa anasoma. Alijiuliza maswali mengi paipokuwa na majibu. Aliumia sana moyoni bila kujua cha kufanya. Huyu mama alibaki kukumbuka yale yote aliyoambiwa na mama yake kabla ya kuwapeleka watoto wa kike shule ingawa hayakuwa suluhu la tatizo lililoikumba familia yake baada ya Swafiya kufukuzwa shule. Mwandishi anaeleza:

> "Mwanangu, ni jambo gani kubwa ulilolikosa nyumbani ukawa unalitafuta nje?" Hakutarajia kupata jibu la swali

> lake, kwani alijisemea hayo pasi ya bintiye kuwepo pale. (Uk. 39).

Vile vile mama Dago alipata mgogoro wa nafsi waliposhindwa kumlipia karo Nchimoni. Alijiuliza maswali mengi bila kuwa na majibu. Mfano:

> Mara kwa mara alijipata akizungumza na nafsi yake; "Ya Rabi Maulana, liegeshe dau langu nisije nikadidimia."
> Haikufahamika wazi ikiwa ikiwa dau hili ni yule mwanawe, ama ikiwa ni hali ya maisha iliyowakumba kama familia. (Uk. 87).

Vile vile Dago alipata mgogoro wa nafsi alipochaniwa shati lake akiwa mtoni. Alienda na marafiki zake ambao walimpitia nyumbani kwao kwa lengo la kwenda kufua nguo zao na kuoga. Walipofika mtoni walianza kumtania na kumkebehi sana Dago, jambo ambalo hakulipenda. Alizomewa sana mpaka akakasirika na ndipo walimzonga na kumsukuma huku na kule hadi wakachana shati lake la shule. Dago aliwaza sana juu ya lile shati lake na ni nini kitatokea atakapomwambia mama yake kuwa shati lake limechanika. Aliwaza sana na kukosa raha na kwa hasira akaanza kugombana na Abdalla ambaye aliendelea kumkebehi wakati wengine walipoona amekasirika waliacha kumtania na kumkebehi. Mwandishi anaeleza:

> Hakuwa chimbuko la mgogoro huu. Alipomaliza kusema, alivuta kifua juu; alivuta pumzi kwa nguvu na mithili ya Mohammed Ali, bingwa maarufu wa ndondi ulimwenguni, alikunja ngumi kwa umakinifu na kuwakabili wenzake……… Siyo kwamba alikuwa na hakika angewashinda bali alikuwa amekata shauri kunusurisha hadhi yake. Liwalo na liwe. "Mwanamume anayejisikia na aje hapa." Dago aliwaambia wenzake maneno haya…Potelea mbali viendavyo na maji ni vingi! (Uk. 179-180).

Nadharia ya ujifunzaji wa jamii mhimili usemao : vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Kishawishi cha Dago

kuchaniwa shati lake kilimpa nguvu za kuweza kupigana na akaweza kumshinda na Abdalla ambaye alionekana ni mwenye nguvu. Kishawishi hicho kilimpa nguvu za kupigana ila hakikumwezesha kupenda shule wala kuwa msafi na kuacha kukojoa kitandani. Hata hivyo kwa mujibu wa nadharia ya mwanaume mpya, Dago anaweza kuachana na tabi azote mbaya na kuwa mwanaume mpya anayefanya matendo mazuri yanayopendwa na familia pamoja na jamii kwa ujumla.

Katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao; uyakinifu: kuelezea mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Hii inaonyeshwa kuwa jambo lolote ambalo mtu hushindwa kupata suluhu humpelekea kuwa na mawazo mengi. Hili linadhihirishwa na mama Dago aliokuwa akiangaika na mumewe ila bado hawakupata ada ya mtoto wao Nchimoni ambaye alifaulu kuendelea na masomo. Hawakujua la kufanya. Hali halisi ya maisha waliyokuwa nayo iliwapelekea kutofikia malengo hayo. Wakiwa katika mawazo ya kumtafutia maisha mbadala Nchimoni Swafiya akabeba mimba shuleni, jambo ambalo liliwapa wakati mgumu pia. Hali ya maisha waliyokuwa nayo ilizidi kuwaacha pagumu kulingana na masahibu yanayoiandama familia yao isiyokuwa na uwezo kiuchumi. Hili linaelezwa na Isiaho, (2001) ambapo anasema kuwa mwanamke asiposhirikishwa katika masuala kadhaa katika familia au jamii kwa ujumla, hana budi kuwajibika katika kuhakikisha mambo yanakaa sawa kwa jitihada zake.

Katika riwaya ya *Tumaini* kuna migogoro katika makundi makuu matatu, wa kijamii, nafsi na kiuchumi. Mgogoro wa kijamii unatokea Bi Amina alipomweleza Tumaini habari za tohara naye akakataa. Tuma alikataa kabisa na mama yake akakasirika sana. Tuma alimweleza kuwa mambo ya tohara kwa wasichana ni ya kizamani ila Bi Amina hakukubali kwani alithamini sana mila zao na desturi kwa mtoto wa kike. Mama yake alikasirika sana na kumtolea maneno makali sana hadi Tuma akaomba msamaha ila bado mamake alipoona hakubaliani naye alimpiga Tuma kofi la shavuni hadi akaona nyota. Mwandishi anaeleza:

> Tuma alimwambia mama yeke: "Ikiwa unayotaka kunieleza yanahusu tohara, mama-sahau kabisa maana nilisema kitambo kuwa mila kama hiyo ni ya kizamani………….. "Tuma, sina wakati wa kukubembeleza hapa. Mimi najaribu kukueleza ya muhimu, wewe unanivunjia heshima! Mtoto huna adabu we! Hata sijui huko shuleni mnafunzwa nini hata unijibu hivyo. Hebu keti!" (Uk. 16-17).

Hata hivyo Mzee Masumbuko, aliozesha mtoto wake Mashaka kwa mzee na kumfanya aishi maisha magumu. Hili ni tatizo kwa Mashaka na familia kwa ujumla maana hawezi kuishi maisha ya raha na hawezi kuifurahia ndoa yake. Mwandishi anaeleza:

> Mzee Masumbuko alipokea mahari ya Mashaka, akamwoza kwa lazima kwa Mzee Lusimbo, kama mke wa tatu. Ndoa hiyo ilimsababishia Mashaka madhara makubwa ya kimwili na kiakili pia. Mzee huyo alikuwa na umri mkubwa sawa na babake Mashaka. (Uk. 122-123).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao:ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Wahusika kama mzee Masumbuko wanathamini sana pesa bila kujali

mahusiano ya kijamii. Kwa mfano, Tumaini kukataa kuolewa na kutaka kuendelea na shule, kwa mzee Msumbuko lilikuwa kosa kubwa sana. Mzee huyu pamoja na familia yake walipata elimu ya kiuana ya kiubaguzi wa jinsia hivyo wanapaswa wajue elimu si kwa mtoto wa kiume tu. Mzee Masumbuko kumwozesha mwanae kwa mzee sana kuliko umri wa mwanae tena bila ridhaa ya binti ni kwa sababu ya tamaa ya pesa. Ndoa hii haikuwa furaha hata kidogo kwa Mashaka bali ni suala la utii wa binti yake na kuogopa kuenda kinyume na tamaduni zao. Baba ndiye alimuamulia mtoto wa kike aolewe lini na nani. Kwa mujibu wa andharia ya mwanaume mpya, mzee Masumbuka anapaswa kuwa mwanaume mpya kwa kuachana na hizo mila gandamizi kwa mtoto wa kike na kumwona kama kiumbe sawa na mwanaume ili kuwepo na usawa wa mgawanyo wa kimajukumu badala ya kuendeleza ubaguzi unamgandamiza mtoto wa kike kuendelea kuwa chini ya mwanaume. Hoja hii ya mogoro wa kijamii inafafanuliwa na Senkoro, (1976) ambapo anaeleza kuwa ujio wa wageni katika Afrika Mashariki uliathiri utamaduni wetu na kuzifanya jamii kujikita katika mambo ya kigeni na kusababisha migogoro katika jamii maana kulikuwa hakuna kuheshimiana tena, kusaidiana na kuthaminiana kama ilivyokuwa desturi yetu kabla ya ujio wa wageni.

Mgogoro wa pili katika riwaya ya *Tumaini* ni mgogoro wa nafsi. Katika mgogoro wa nafsi tunamwona Tumaini akijawa na mawazo kuhusu maisha yake kama angefanyiwa tohara. Alikuwa akichangia sana mjadala shuleni kupinga namna tohara kwa wanawake ilivyo na madhara, nafsi yake ikawa inawaza sana namna mama yake na baba yake  pamoja na ndugu wengine

walivyokuwa wakimkazania kufanyiwa tohara. Hata hivyo aliwaza sana na kugundua kuwa mama yake alikuwa akimdanganya ili akubali kwenda tohara kuwa babake angempeleka shule baada ya tohara jambo ambalo alikuwa kweli. Aliwaza sana maisha ya baada ya tohara yangekuwaje na akaumia sana.

Vilevile, Tumaini aliumizwa sana na maneno ya Bi. Amina kumlazimisha sana tohara hadi akaanza kulia kwa uchungu. Mwandishi anaeleza:

> Tumaini alinyanyuka taratibu pale alipokaa akaful;uliza hadi chumbani mwake. Humo ndani, aliketi kitandani huku mawazo mengi yakimzonga. Mara alishtukia machozi ya moto yakibubujika na kufanya michirizi mashavuni mwake……… Tumaini aliwaza na kuwazua kuhusu hatua ambayo angechukua ili kujiopoa. (Uk. 18-19).

Mgogoro mwingine ni ule wa Kiuchumi. Katika mgogoro huu mwandishi anamsawiri mdogo wake Tumaini, Rehema aliishi maisha ya shida sana maana mumewe alikuwa hawezi kumtunza kutokana na kuwa na kipato kidogo. Hata alipougua mumewe alikosa pesa ya kumpeleka hospitali hadi ndugu zake Rehema akiwemo Tumaini pamoja na wazazi ndio watoe msaada wa kumpeleka hospitali. Maisha yao yalikuwa ya taabu sana maana hata nyumba waliyokuwa wanaishi ilikuwa ya hadhi ya chini sana. Mwandishi anaeleza:

> Mumewe hakuweza kumlisha vizuri kwa maana chakula kilikuwa cha shida kutokana na pato lake dogo.Tumaini alihofia usalama wa dadake, na alifahamu kuwa hata baada ya kujifungua, mumewe Rehema angelipata taabu ya kuwatunza mkewe na mtoto wao mchanga. (Uk. 123).

Hata hivyo Mzee Okwemba naye aliishi maisha magumu sana. Kula yake na matumizi ya kila siku yalitegemea uchuuzi wa samaki alioufanya. Alikuwa akiangaika sana ili kupata matumizi yake ya kila siku. Kwa umri wake alipaswa kuwa ana namna ya kuishi tofauti na hiyo kazi ya uchuuzi wa samaki aliyoifanya kwani alishakuwa mzee. Hali ngumu ya kiuchumi aliyokuwa nayo ilimlazimu kufanya kazi hiyo ili kupata mahitaji ya kila siku. Mwandishi anaeleza:

> Mzee Okwemba aliyasitiri maisha yake kwa kuchuuza samaki. Shaibu huyu alikuwa akitembea mwendo mrefu kwenye mabwawa ya maji ambako shughuli za uvuvi ziliendelea. Huko, alijinunulia samaki na kuwachuuza mtaani humo. (Uk. 3).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii inaonesha kuwa jamii inafunzwa kuhusu mwanaume kujitegemea daima hata kama afya yake siyo nzuri bado jamii inamwona anaweza kwa vile ni mwanaume. Mzee Okwemba alipaswa kupata msaada wa kiuchumi ila aliendelea kukaa peke yake kutokana na mtazamo wa kijamii. Aliishi kwa shida sana ila jamii haikujali kwa maana ni mwanaume.

Nadharia ya uhalisia inatueleza kuwa kuwe na uyakinifu: kueleza mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Katika ulimwengu tulio nao sasa, suala la kumchagulia msichana au mvulana mchumba ni kumtia matatizoni. Mashaka kuolewa na mzee Lusimbo tena bila ridhaa yake kwa sasa wakati huu halina nafasi. Vilevile familia kuishi hali ya umasikini ni jambo ambalo si geni katika jamii. Mfano, Rehema aliolewa ila bado mumewe hakuweza kumtunza kwani alikuwa na kipato kidogo. Mzee Okwemba kukosa watu wa kumpa msaada akawa anajitegemea kwa kuchuuza samaki, ni mambo ambayo yapo katika

jamii zetu, tunapambana nayo kwa namna tofauti kama yalivyoibuliwa na mwandishi wa riwaya hii. Jamii zinapambana kwa namna mbalimbali ili kuitatua migogoro ya kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.

Kwa hiyo, katika riwaya nne ambapo mbili ni za waandshi wanawake wa Kenya na wawili wa Tanzania, zinadhihirisha kuwa wanaume katika jamii wanatenda mambo mbalimbali yaliyomo katika jamii aidha kutokana na tabia zao binafsi au mifumo iliyomo katika jamii husika. Kuna mambo ambayo yanaonekana kufaa katika jamii zetu, waandishi wameyaibua ili jamii iweze kuyaendeleza kulingana na ulimwengu halisi. Mambo yasiyofaa ambayo yanatendwa na wahusika wa kiume, wanapaswa kubadilika na kuwa wapya kwa namna walivyofundishwa na jamii zao. Jamii ndiyo inamkuza mtu na kumbadilisha kulingana na mienendo ya kijamii.

### 2.3 Hitimisho

Dhamira zimewasilishwa na wahusika wa kiume kwa namna wanavyojidhihirisha katika jamii husika zilizoandikiwa na waandishi wanawake wa Kenya na Tanzania. Kama ilivyoonekana katika riwaya teule, wahusika wa kiume kuna mambo wanayoyafanya si kwa matakwa yao bali ni mfumo wa jamii iliyowakuza. Hata waandishi wanawake wamewachora wahusika wa kiume kwa namna walivyowachora sababu ya mifumo iliyowakuza waandishi hao. Mambo wayafanyayo wahusika wa kiume yanaendana na ulimwengu halisi kulingana na mabadiliko yaliyopo. Kwa matendo yanayotendwa na wahusika wa kiume na hayafai katika jamii,

wanaume wanapaswa kubadilika na kuwa wapya kwa kuwathamini wanawake na kuwasidia kama wanavyofanya kwa wanaume wenzao. Kuna mahali waandishi wametofautiana ila kwa sehemu kubwa wanafanana maana jamii nyingi za Kenya na Tanzania zinafanana kwa kiasi kikubwa.

# SURA YA TATU

# TASWIRA ZINAZOTUMIWA KUWASAWIRI WAHUSIKA WA KIUME KATIKA RIWAYA TEULE

## 3.0 Utangulizi

Katika sura ya pili tumejadili dhamira mbalimbali zinazowasilishwa na wahusika wa kiume katika riwaya teule. Kwenye sura hii tumejadili taswira zinazotumiwa na wahusika wa kiume katika riwaya teule. Kwanza tumefafanua maana mbalimbali za wahusika kwa namna wanavyoelezwa na wanazuoni mbalimbali wa fasihi kwa namna tofauti. Njogu na Chimerah, (1999) wanafafanua kuwa mhusika ni kiumbe apatikanaye katika kazi za fasihi na anafanana na binadamu kwa kiasi fulani. Wahusika vile vile, ni viumbe watumiwao na mwandishi katika kusuka matukio na visa ndani ya kazi yake. Wahusika hawa wanaweza kuwa watu na viumbe hai vingine kama miti na wanyama na visivyo hai kama vile mawe. Wahusika hao hutenda kama watendavyo binadamu kwani huwakilisha matukio yanayoendelea katika jamii waishimo binadamu. Wahusika hutumiwa na mtunzi katika kuwasilisha mawazo yake katika hadhira lengwa. Wahusika hubeba maudhui ya kazi hiyo kama anavyowachora mtunzi. Taswira ni picha inayobainishwa na mhusika katika matendo ayafanyayo katika kazi ya fasihi. (Wamitila, 2008).

Wahusika ndiyo nguzo kuu katika maudhui kwani ndio hubeba dhamira zilizomo ndani ya kazi ya fasihi. Msokile, (1993) anaeleza kuwa wahusika ni vitu, kama wanyama au watu katika kazi ya fasihi kutegemeana na mtunzi

alivyoisana kazi hiyo. Pia mimea, mashetani na mizimwi yanaweza kutumiwa kama wahusika katika kazi ya fasihi. Mtunzi wa kazi huwa huru kutumia aina ya wahusika aipendayo kutegemeana na ujumbe aliolenga kuifikishia jamii.

Wamitila, (2008) anafafanua kuwa wahusika ndio watendaji wa matukio na matendo yanayotumika kuziendeleza dhamira ambazo ni sehemu maudhui ya kazi hiyo ya fasihi. Wahusika katika kazi ya fasihi hutumika kubainisha tabia, fikra, matendo ya kijamii, mienendo yao pamoja na mabadiliko ya kijamii kulingana na wakati pamoja na mazingira waliyomo wahusika hao. Jamii huweza kuonekana nzuri au mbaya kutoka na tabia pamoja na mienendo ya wahusika waliovaa uhusika wa nyanja mbalimbali.

Kazi ya fasihi huundwa na wahusika ambao hupewa sifa mbalimbali kulingana na lengo la mtunzi ambalo huwasilishwa kwa kupitia taswira zinazowasilishwa kupitia wahusika hao.

Wahusika tumewaangazia kwa kutumia nadharia ya ujifunzaji wa kijamii, nadharia ya mwanaume mpya na ya uhalisia ili kuakisi mambo ya kiuana na chanzo chake, yanayojidhihirisha katika riwaya teule zilizoandikwa na wanawake kama yanaendana na hali halisi iliyopo katika ulimwengu wa leo kulingana na waandishi wanawake walivyolenga kuwasawiri wahusika wa kiume katika kazi zao. Hivyo ni muhimu kufanya ulinganishi wa kazi husika kulingana na namna walivyobainisha taswira ya mwanaume kulingana na matendo yao pamoja na yale yazungumzwayo na wahusika hao.

### 3.1 Taswira ya Mwanaume katika Riwaya ya *Kipimo Cha Mizani*

Kazi yoyote ya fasihi inapoandikwa, mtunzi huwa ana kitu alichokilenga. Lengo la mtunzi linaweza kuwa zaidi ya kile anachokifikiria au kukitafuta msomaji wa kazi hiyo ya fasihi. Kwa hiyo, mhakiki wa kazi ya fasihi anaweza kuibua masuala mbalimbali katika kazi hiyo. Katika uchambuzi wa kazi hii amemchora mhusika wa kiume kama kiumbe dhaifu japo udhaifu ni wa kiubunifu si kwamba ndiyo hali ambayo mwanaume huzaliwa nayo.

Hii inadhihirishwa na Umari ambaye anapangiwa kila kitu na mkewe Mariyamu kuanzia hadhi ya nyumba wanayokaa na pia suala la kumiliki mali. Mariyamu ndiye mwamuzi wa mwisho kabisa katika kila jambo bali Umari anafanya utekelezaji. Kwa mfano, Amini alipofariki Mariyamu alimshinikiza Umari aende mahakamani na amtafute wakili ili amtetee Umari amiliki mali zote za Halima na wanawe, alimchochea maneno mengi na Umari akayasikiliza na kuyafuata hadi kumpokonya Halima wanae. Mwandishi anaeleza:

> "Hayo ndiyo niliyotaka kukuuliza," alisema Mariyamu. "Watoto sasa bado wadogo, lazima wewe sasa ndiye utakayekuwa dhamana wa watoto wale, kama baba yao mdodo. Lakini fikiri! Halima akitoka eda atakuwa na haki ya kuolewa na mume mwingine. Ikiwa utamwachia kila kitu mikononi mwake, anaweza akampa mtu mwingine ile mali ya marehemu. Na wewe utabaki na dhamana ya kuwaangalia watoto wake. Hapo si wewe, si watoto! Mtaondokea patupu!" (Uk. 82).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii muhimili usemao: ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Inaonesha kuwa Umari hakuwa na maamuzi katika

familia yake bali aliamuriwa na mkewe katika kutekeleza majukumu yake. Elimu aliyokuwa nayo Umari na namna alivyokuwa akisaidiana na kaka yake Amini enzi za uhai wake, hakupaswa kumfanyia yale aliyoyafanya kwa mke wa marehemu kaka yake ambaye ni Halima. Kupokonywa watoto kwa nguvu na kuishi hospitali kama kichaa ni mbinu waliyoitumia ila haikuonyesha utu hata kidogo. Tamaa ya mali ya kumsikiliza mkewe Mariyamu, Umari anatenda unyama kwa Halima pamoja na watoto wa kaka yake. Jamii haikumwelewa kabisa Umari na ndio maana mzee Hasani, Selemani na Bi Riziki waliangaika sana kuiokoa familia ya marehemu Amini.

Hata hivyo Maryamu alivyokuwa akimshinikiza Umari kufanya unyama huo kwa Halima jamii nzima ilimshangaa kwa maana mwanamke hapaswi kuwa hivyo. Hoja hii inaelezwa na Wolf, (1995) kuwa wanawake wamefunzwa katika hali za kuwafanya wawe na umakini kuliko wanaume na wanapozembea kufanya hivyo watakuwa wamekengeuka maadili yao na kujikita katika hisia ngeni kwa maana akili zao zimeumbwa kwa kuwafanya wawe na hali ya kuwajali walio karibu nao.

Pili mwanaume alichorwa kama mtu ambaye mkorofi na mshari. Haya yanadhihirishwa na Umari kwa shemeji yake Halima. Hata hivyo Umari tabia hii alikuwa nayo kwa Halima ila kwa Mariyamu ambaye ni mkewe alikuwa hafurukuti. Tabia hii ya ushari aliionesha kwa Halima tangu enzi za uhai wa Amini. Hii inaakisi usemi usemao kuwa tabia ya mtu ni ngozi. Umari

aliendeleza ushari huo hata baada ya Amini kufariki na ndio maana aliweza kufanikiwa kumpokonya Halima wanae na kumpeleka Halima hospitali kwa kusingizia kuwa ni mgonjwa. Halima tangu enzi za uhai wa mumewe alionesha kumvumilia sana Umari ushari wake ila ilipozidi alimwambia Amini. Mwandishi anaeleza:

> Halima alijua kuwa Umari hampendi na hata wakati mwingine ile heshima ya kishemeji hawezi kumpa, bali husema naye kwa ufupi tu na kwa ukali. Halima alistahamili hayo, kwani hakupenda kugombana naye, wala hakupenda kuleta ugomvi baina ya Amini na ndugu yake, lakini baadhi ya wakati, ujeuri wake ulikuwa humkasirisha sana, hata humuelezea Amini. (Uk. 42).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kuwaona wanawake kama viumbe sawa na wanaume kwa kuwaheshimu na kuwapenda katika nyanja wanazokuwepo. Umari anaweza kuacha ukorofi na kuwa mwanaume mpya kwa kumwona Halima kama mwanamke anayeweza kuwalea wanae na kusimamia mali kama vile alipokuwepo Amini. Kazi hiyo alikuwa akiifanya mara nyingi Amini alipokuwa anabanwa na kazi za kwenye ajira yake hivyo alikuwa na uwezo wa kuzimudu. Mwanaume mpya anaachana na uovu na kuwa mzuri kwa kumthamini mwanamke na kutomuingilia ili kumdhulumu mali zake. Hoja hii inaelezwa na Cancian, (1987) anapofafanua kuwa ili kuwa na maendeleo ya kiuana ni muhimu kuwa na mabadiliko yanayoambatana na upendo. Hii hupelekea kuthaminiana katika jamii zetu.

Katika muhimili wa nadharia ya uhalisia usemao: uayakinifu; kuelezea mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Ukweli ni kwamba Halima aliujua kabisa kuwa baada ya Amini kufariki, Umari hawezi kutoa ushirikiabno mzuri kwa

Halima ilhali anajua kaka yake kafariki. Umari alionyesha ukorofi kwa kudai mali walizoziacha wazazi wao. Alikuwa akimkera sana Amini hadi akaamua kumpa haki yake. Hii ilitokana na hali halisi ya malezi kwa Umari tangu akiwa mdogo kwa maana alikuwa ni wa kupenda mteremko. Hata alipokuwa akimfanyia unyama Halima, baadhi wa wanajamii waliona yuko sahihi na wengine waliona anakosea. Kwa wale waliotawaliwa na mfumo dume, waliona kuwa mwanamke akifiwa na mume hawezi kufanya maamuzi juu ya mali za marehemu bila ndugu wa mume kuingilia kati japo wapo wanaoona anafaa kujisimamia ili kuepusha usumbufu kama aliouleta Umari kwa familia ya Halima.

Zipo jamii ambazo bado zimejikita msimamo wa kuwaona watoto wa kiume kuwa hawafanyi makosa na kwa muda wote wafanyayo yanapaswa kuheshimiwa na jamii kwa ujumla. Hata hivyo, jamii nyingi hazitilii maanani dhana hiyo na kumuacha mtoto wa kiume akiwa na ujeuri kwa ndugu zake wa jinsi nyingine. Connell, (2005) anafafanua kuwa mifumo hii ni ya kibabe ambayo huonesha kuwa mwanaume anachofanya ni sawa. Dhana hii inaangazia uhusiano wa nguvu, mamlaka na kihimaya baina ya wanaume na wanawake na jinsi wanaume wanavyotumia uwezo huo ili kuwatawala, kuwadhulumu na kuwanyanyasa wanawake.

Tatu, mwanaume anachukuliwa kama mdanganyifu na mwenye kuringa. Taswira hii imedhihirishwa na Umari katika sherehe yao ya kuhamia nyumba mpya. Alimwonesha kaka yake kuwa yeye anabadili nyumba na

kukaa nyumba ya gorofa ambayo ni ya kiwango cha juu ili jamii imtambue kuwa anajipenda pamoja na familia yake. Ili kuyatimiza haya alikopa pesa hazikutosha na akaamua kwenda kwa kaka yake Amini ili amwazime kiasi kilichopelea. Amini alipokosa pesa hizo ilileta mzozo sana maana alitaka shamba liuzwe ili apate pesa kwa ajili ya jambo hilo la kujiringisha kwa watu kuwa yeye na familia yake ni wa kiwango cha juu. Vile vile Umari alipanga uongo kwa wakili wake mahakamani ili apate kibali cha kukaa na watoto wa kaka yake ili aweze kumiliki mali zote za marehemu. Baada ya kupata kibali hicho aliwavizia watoto shuleni na kuwachukua. Halima alipoenda nyumbani kwa Umari ili awachukue wanae. Umari alipiga simu polisi na kuwadanganya kuwa amevamiwa na kichaa nyumbani kwake. Mwandishi anaeleza:

> Polisi walimchukua na kumtia garini. Mmoja alimwuliza Umari: “Je, unamjua?” Umari alijibu, “Ninamjua vizuri. Alikuwa mke wa marehemu ndugu yangu. Sasa amepotea akili, kama mnavyomwona.” Tena polisi walimtaka Umari afike kituo cha Polisi ili kuandikisha maneno yake. Halima alilia, lakini hakuweza kushindana na wale waliomkamata. Yule dereva aliduwaa, hakuwa na la kusema wala la kufanya. (Uk. 97).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: ujifunzaji unahusu kuchunguza kupata habari kutokana na ule uchunguzi na kuunda maazimio kuhusu utendakazi wa tabia hiyo. Hii inaonyesha kuwa jambo linalotendeka katika jamii linalenga kuleta maendeleo ya namna fulani katika masuala ya kiuana. Umari alipenda aonekane ni mwanaume wa kiwango cha juu ila kutokana na uwezo wake kuwa wa kati, alijikuta anadumbukia katika kumuumiza shemeji yake na watoto wa marehemu

kaka yake. Hayo kujionyesha yaliyofanywa na Umari yameainishwa na Butler kuwa kuna uanaume wa kujipenda. Yaani mwanaume anataka aonekane anavaa vizuri, anaishi pazuri ili kuutambulisha uanaume wake (West, 1987).

Mwanaume alichukuliwa kama mtu mwenye tamaa. Kwa mfano, Umari alikuwa na kazi yake pamoja na mali zake ila baada ya kaka yake Amini kufariki akatamani kumiliki mali zake zote kuanzia duka, kiwanda na nyumba ya kuishi. Alianza kwenda dukani na kumkuta mzee Hassani na kumtaka ampe pesa pamoja na nyaraka kama hati ya nyumba na kiwanda. Umari alijipa dhamana ya kumiliki kila kitu cha marehemu na ndio maana aliweza kwenda dukani kuchukua pesa kwa mzee Hassani na kutafuta nyaraka ambazo hazikupatikana pale dukani. Mwandishi anaeleza:

> Umari alikwenda kule dukani. Akamkuta mzee Hasani anaendelea na kazi yake kama desturi. Akamwambia, "Ninataka kuangalia karatasi zote zilizopo hapa dukani. Bila shaka marehemu alikuwa anaweka hesabu zake hapa!" Hasani alimjibu, huku akitikisa kichwa," La, hakuwa akiweka chochote hapa Umari hakumsadiki. Akamwuliza kuhusu pesa zilizopatikana. Hasani alimweleza hesabu zake. Tena Umari akasema, "Basi hizi nitachukua." Hasani alimwambia: "Ninavyoona ni kuwa hizi pesa ingefaa apelekewe mkewe, na hivyo ndivyo nilivyoazimia, itakapofika mwisho wa mwezi. Maana mwenyewwe, marehemu alikuwa akitia hesabu zake wakati huo."
> "Hayakuhusu wewe. Mimi sasa ndiye dhamana wa kila kitu. Utafuata hayo ninayokwambia." (Uk. 87).

Nadharia ya mwanaume mpya muhimili usemao: kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume. Umari alizoea kudeka kwa kaka yake Amini kwa kuomba pesa pale anapopungukiwa, sasa kaka yake hayupo hivyo hana

budi kubadilika na kuwa mwanaume mpya anayeweza kuisimamia familia yake kulingana na kipato alichonacho halali badala ya kuwa mdhulumaji. Mwanaume anaweza kuwa muwajibikaji na akajitegemea kiuchumi na katika Nyanja nyinginezo. Crous, (2005) anaeleza haya katika utafiti wake kuhusu masuala ya wanaume yalivyowasilishwa katika simulizi bunifu za waandishi teule huko Afrika Kusini ambapo anaeleza kuwa wanaume wamekuwa na mionekano tofauti na ile iliyotegemewa na wanajamii. Wanajikosoa na kuwa na sura tofauti katika kazi hizo.

Katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao: wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii. Umari alikuwa mkorofi na mwenye tamaa tangu mapema. Anaonekana alivyopenda mambo makubwa bila kuyatolea jasho. Jamii inaonesha kuwa watu kama Umari wapo katika jamii zetu na wanarudisha nyuma maendeleo ya wenzao. Halima angekaa na familia yake na kusimamia miradi yake, wanae wasingekuwa wa kutangatanga kuomba msaada katika majumba ya watu kwani familia yao ingekuwa na maendeleo mazuri. Miescher, (2003) anaeleza kuwa mwanaume huwa anajionyesha matendo yake ya kibabe kuwa ndivyo mwanaume anavyotakiwa kuwa. Kadri anavyoendelea kukua na kuchangamana ndipo huweza kuwa vinginevyo ila uasili wake haupotei.

Mwanaume amechorwa kama mtu mwenye bidii na mchapakazi. Hii imedhihirishwa na Amini pamoja na mzee Hasani. Amini alipofungua duka lake na mkewe waliwaza wa kuwasaidia kuuza duka lao hadi wakamkumbuka

mzee Hasani kuwa ni chapakazi na anajituma sana katika kazi. Amini alikuwa akifanya kazi serikalini lakini bado alikuwa na juhudi za kufungua kiwanda chake ili akuze kipato chake. Alikuwa akihudumia shamba lake kwa kuwasimamia vibarua waliomsaidia na kuwalipa kadri ya kazi walizozifanya. Aliwajibika sana kwa ajili ya familia yake. Mwandishi anaeleza:

> Wakati huu, Amini alikuwa na kazi nyingi sana hata hakuwa na nafasi ya kukaa sana nyumbani na kupumzika, au kuzungumza, au kucheza na wanawe kama zamani. Alikuwa akirejea mchana wakati wa chakula, na baada ya kula na kupumzika muda mfupi tu, alitoka tena kuendelea na kazi zake… Duka alimwachia mzee Hasani, ambaye aliliendesha kwa uaminifu na Amini hakupata kumsaili kwa hili wala lile. Alimpitia tu kila mara kumsikiliza kuhusu mahitajio na hesabu, na bidhaa gani zinazohitajika. (Uk. 63).

Katika nadharia ya ujifunzaji mhimili usemao; mwanafunzi si mpokezi tulivu wa habari, utambuzi mazingira na tabia vinaathiriana katikam upataji wa habari wa mwanafunzi.Amini na Mzee Hasani walijifunza kuwa mwanaume lazima afanye kazi kwa bidi na wakawa ni wachapakazi sana na wana bidii ya maendeleo. Amini akiwa bado kwenye ajira bado alifanya biashara yake na kilimo. Mzee Hasani alipendwa sana kazini kwake alipokuwa bado kaajiriwa kutokana na uchapakazi wake. Uchapaji kazi huo ndio ulimfanya Amini amtafute na kumkabidhi aliendeshe kwani alimjua bidii yake. Hii ni kutokana na malezi waliyopewa ya kuwaandaa kujitegemea kama watoto wa kiume ambao watakuja kuwa baba wa familia na majukumu. Hii inaakisi usemao kuwa mwanaume ndiye kichwa cha familia. Hii ni pamoja na kuweza kuihudumia familia yake kwa mahitaji mbalimbali. Wanasaikolojia wanaeleza kuwa mtu mzungumzaji anapaswa awe mtendaji mzuri pia. Skinner, (1947)

anaposema kuwa tabia za maneno zidhihirishwe kwenye matendo ya wazungumzaji.

Mwanaume amechukuliwa kama mwenye upendo, mkweli na muwazi. Hii imedhirishwa na Amini alipofuatwa na Bi. Riziki kumwombea mwanae kazi kiwandani. Amini alijua udhaifu wa Rajabu lakini alikubali kumpa kazi maana alijua akikaa tu nyumbani atakuwa mzigo kwa mama yake. Amini alimbeba kwenye baiskeli na kumpeleka kiwandani kwa maana alijua ni mbali Rajabu akitembea kwa mguu atachoka sana. Alifika wakati akamnunulia Rajabu baiskeli yake ambayo aliitumia kwenda kazini. Amini pia alikuwa muwazi wakati Rajabu anaanza kazi, alimwambia Bi. Riziki kuwa malipo yatakuwa baadae maana kiwanda ndo kwanza kinaanza na hakijaanza kuazlisha na kuingiza kipato. Kwa furaha Bi. Riziki alilipokea na kusema kuwa hata asipolipwa ili mradi ajifunze kazi. Mwandishi anaeleza:

> Mama yake alimwambia afuate yale anayoambiwa tu kwa sasa hivi, na hiyo kazi ataijua kidogokidogo. Riziki alifanya jitihada ya kuonana na Amini siku ile na kumshukuru, akimwambia, “Umeniondoshea wasiwasi mkubwa, maana sasa nitajua Rajabu yuko wapi wakati wote. Na pia atakuwa ameshughulika, ataepukana na ule ubilisi wa vijana wengine.”(Uk. 39-40).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Amini alijifunza kuwasaidia watu wote bila kujali uwezo wao pale anapopata nafasi. Mwanaume anafunzwa kuwa mtu wa msaada katika mambo mbalimbali katika jamii. Hii inakuwa tabia ya Amini na anaionyesha kwa Rajabu na

Mzee Hasani ambao anawasaidia katika mambo ya kujipatia kipato kwa ajili ya familia zao.

Katika nadharia ya uhalisia isemayo; mshikamano. Amini alishikamana na jamii yake kwa maana alikuwa na upendo. Ni vigumu kushikamana na mtu usiyempenda. Amini alimsaidia Rajabu kupata kibarua kiwandani kwake maana alimjua udhaifu wake. Alimpenda sana mama Riziki hivyo alitaka kumsaidia mwanae ili asiwe mzigo kwa mama yake. Flood, (1990) anaeleza kuwa tunaishi katika jamii ya mfumo dume ila wapo wanaume ambao wamejifunza kukaa vizuri na watu wote katika jamii bila kujali jinsia zao.

Mwanaume amechukuliwa kama katili na asiye na huruma. Hii imedhihirishwa na Juma ambaye alipewa hongo na Umari ili amuweke Halima chumba cha vichaa na akae huko siku zote kuwa ni kichaa ili asirudi nyumbani kumsumbua Umari na familia yake kuwataka wanae na mali zake zote ambazo Umari anazifaidi. Juma aliitwa na Umari nyumbani kwake na kumuahidi zawadi nono ya gari aina ya Mercedes, BMW modeli mpya ili amweke Halima hospitalini muda wote. Mwandishi anaeleza:

> Hapo Umari alimwambia Juma kuwa anahitaji msaada wake. “Msaada mdogo tu! ” ……………Nataka umuweke yule mwanamke ndani, mpaka nitakapokwambia. Tena pasiwepo maelezo au maandishi yoyote juu ya kadhia yake. Wala jina langu lisitokeze.”….. Utapata zawadi yako. Unaonaje gari jipya?”… Juma alicheka akasema: “Hapo umenipata.” Juma aliona kuwa hapatokuwa na taabu yoyote kwake kutekeleza yale aliyoyataka Umari; na yeye atajipatia faida ndani yake. Akakubali. (Uk. 102).

Kutokana na zawadi hiyo nono ndiyo maana Juma alipambana sana na Salama alipokuwa akimtetea Halima asichomwe dawa ya wagonjwa wa kichaa. Hii ilimletea ugomvi mkubwa sana Salama na Juma hadi akashtakiwa mpaka akahamishwa kituo cha kazi. Salama alipomfuata kumweleza kuwa Halima hana ghasia hapaswi kufungwa kivile maana anaumizwa bila sababu. alikuwa mkali kwa Salama na kumjibu vibaya. Mwandishi anaeleza:

> Salama alimwambia, "! Huyu mgonjwa si mtu wa ghasia, na wewe unajua. Ina haja gani ya kumfunga kama hivi?" "Alitoroka, na tukimwachaia lazima atajaribu tena," alijibu na huku akiangalia ile namna alivyofungwa. "Sasa," aliendelea, "Ninataka utayarishe sindano. Apigwe sindano hiyo kila siku mara mbili, ilia pate kulala na kutulia." "Lakini …." "Sikiliza," alisema na huku akimwangalia Salama kwa hasira. "Nani mwenye amri hapa, wewe au mimi?" "Wewe, bila shaka, lakini sio uamrishe kufanyika kosa na mimi nikubali," alijibu Salama, akiwa hamaki zimempanda. (Uk. 177).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Hii inadhihirisha kuwa Juma alikuwa akijua anachokifanya na ndiyo maana alipoulizwa na Salama alimjibu vibaya kwa kuona anaingilia kazi yake na pia anajifanya kujua sana kazi ya ilhali yeye ni muuguzi. Hata hivyo Juma alikuwa mchapakazi kama mtoto wa kiume kwa maana alikuwa kazini muda mwingi kulitumikia taifa lake kwa fani yake. Hii ilitokana na malezi yake kama mtoto wa kiume ili akikua aweze kujitegemea. Tamaa ya rushwa ndiyo iliingiza doa katika kazi yake baada ya kuahidiwa gari na Umari mara atakapofanikisha kumkalisha Halima hospitalini ili mipango ya dhuluma ya Umari iweze kwenda sawa.

Salama pia alikuwa na malezi ya kiuana na ndiyo maana alipambana kwa kila hali kuhakikisha Halima kama mgonjwa anapata huduma stahiki. Uwajibikaji wake kazini ulimletea matatizo na migogoro isiyo na ukomo na Juma kwa maana hakukubali kufanyiwa uonevu na Juma wakati alikuwa sahihi katika kumfuatilia mgonjwa. Juma ambaye ni mwanaume aliona ana haki ya kumwonea Salama kwa vile ni muuguzi wa kike ambaye hawezi kuwa na sauti ila ilikuwa kinyume chake. Salama alienda kushitaki mpaka ikabidi ahamishwe sehemu hiyo ya kazi kwani waliona hawawezi kufanya kazi pamoja wakati tayari kuna mgogoro baina yao.

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kuwaona wanawake kama viumbe sawa na wanaume kwa kuwaheshimu na kuwapenda katika kila nyanja wanazokuwepo. Juma anapaswa kubadilika na kuwa mwanaume mpya ambaye anamthamini mwanamke na kuona kuwa ana uwezo sawa na mwanaume. Kwa mfano Daktari Isa ni mwanaume mpya ambaye alisikilizana na Salama na kushauriana kuhusu namna ya kumtibu Halima ilhali Dr Juma alijibu kwa ujeuri na hakutaka kutoa ushirikiano kwa Salama ambaye ndiye muuguzi wa Halima. Bird, (1996) anaeleza kuwa mwanaume anaweza kubadilika na kuwa vyovyote vile kitabia. Mfano anaweza kuwa wa kujitegemea kiuchumi, mwonekano mzuri, mwenye hasira au wa kutumia nguvu miongoni mwa wanajamii.

Vilevile, mwanaume amechorwa kama mwenye kujitoa, upendo wa dhati na mwenye hali kuwajali wenzake. Haya yemedhihirishwa na Bakari

alipowapokea Ali na wadogo zake mara baada ya kufukuzwa kutoka kwa baba yao mdogo hasa manyanyaso yalipozidi. Hata hivyo Mariyamu hakuwapenda kabisa bali alipenda mali za wazazi wao hawa watoto. Bakari aliwapokea akawaogesha na kuwahudumia pale dukani kwake. Baada ya kutafakari na kuzungumza nao kwa muda aliona awatafutie pa kukaa maana yeye hawezi kuishi nao dukani. Siku hiyo alifunga duka lake akaenda kumtafuta Rehema ambaye alikuwa na roho ya kuwasaidia wenye shida maana ndiye aliyemsaidia Bakari na kumsomesha. Kabla ya kumpata mzee Hasani aliwaombea kwa Rehema na akawapokea vizuri na kuwasaidia na ndipo jitihada za kumtafuta Mzee Hasani zikaendelea.

Baada ya kuwapokea akina Ali, Rehema pia alitamani kuongea na Mzee Hasani ili ajue kuhusu wazazi wa watoto hao wako wapi na walikumbwa na nini hadi watoto wanaishi kwa msaada wa wanajamii. Bakari aliahidi kumtafuta mzee Hasani na kweli alifanya hivyo na akampeleka kwa Bi. Rehema walipokuwa akina Bakari. Hata Amini enzi ya uhai wake alikuwa na upendo sana kwa familia yake na kuwajali katika nyanja zote. Inaumiza sana baada ya kufariki wanae wanaanza kutangatanga hadi kuangukia mikononi mwa Bakari aliyewatafutia makazi kwa Bi Rehema.

Mwandishi anaeleza:

> Jioni ile, Bakari alimkuta mzee Hasani pale barazani kwake. Alimkaribisha, wakakaa na kuzungumza. Bakari alimwelezea yote yaliyojiri. Mzee Hasani alistaajabu. Aliitikia na kutikisa kichwa kwa huzuni, maana alihisi maneno yamempotea. Bakari alimwambia, “Nimeona bora nije kukuchukua, ikiwa utaweza, nikakuonyeshe walipo. Utapata kupajua. Tena Ali siku nzote ana hamu

> ya kukuona. Pia utapata kuzungumza na kujuana na Bi Rehema, ambaye ni mzee wangu. Mtaelewana, kwani yeye ni mtu mwema sana. Tena utaondokewa na wasiwasi kuhusu Ali na ndugu zake.” (Uk. 169).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: ujifunzaji unahusu kuchunguza kupata habari kutokana na ule uchunguzi na kuunda maazimio kuhusu utendakazi wa tabia hiyo. Bakari alijifunza kukaa na watu vizuri kama yeye alivyokaa vizuri na Bi. Rehema hadi akamsomesha mpaka elimu ya juu ya chuo kikuu. Alijifunza utii na ukweli kwa wakubwa kama mtoto wa kiume. Ndivyo alivyofanya kwa akina Ali mara alipowapokea. Baada ya kuona hataweza kuwapa msaada wanaouhitaji aliamua kumwomba Bi. Rehema ili awasaidie. Ali na wadogo zake walikaa kwa Bi. Rehema baada ya kujiridhisha kuwa hawana wazazi kwa wakati huo wa kuwalea. Aliwalea vizuri na kuwapa mafunzo yote kama mzazi hadi mama yao alipopatikana kutoka hospitalini baada ya muda mrefu.

Katika nadharia uhalisia mhimili usemao: itumie sajili ambazo ni za kawaida. Rehema alitumia utaratibu wa kawaida katika mahusianao ya binadamu ya kutaka kujua historia ya maisha ya watoto anaowapokea ili apate pa kuanzia kuwasaidia badala ya kuwaweka ndani tu. Bakari aliyewaleta anafahamiana na Rehema ila haikuwa kielelzo cha kutosha kuwapa msaada wanaostahili kupata kutoka kwa Rehema. Kwa umri ule watoto wanapaswa wakae na wazazi wao ili kupata malezi hilo lilimshangaza Rehema na kutaka kujua kilichowapata wazazi wao. Malezi ni jambo la msingi sana linalopelekea tabia

mbalimbali.malezi ndiyo humkuza mtoto kisaikolojia na kumfunza mambo ya kiulimwengu (Rotter, 1954).

Mwanaume katika riwaya hii pia amechorwa mwenye kujituma, kumakinikia mambo kwa upendo wa dhati na mwaminifu kwa watu wanaomzunguka. Mzee Hasani amedhihirisha hili pale alipofika kwa Rehema akazungumza na Bi. Rehema kwa kirefu ila alipoletewa akina Ali na wadogo zake alipata uchungu sana maana alikaa sana na hao watoto miaka akiwa anauza dukani kwa Amini. Aliwapenda watoto wale nao walimpenda sana. Sasa baada ya kuchukuliwa na Umari kwa nguvu akawa hajui walipo na wala mama yao. Bi Rehema alimhakikishia mzee Hasani kuwa atakaa na watoto wale kwa upendo na kuwasaidia ingawa alipenda kupata habari za mama yao ili ajue kama yuko hai au kafariki. Baada ya maongezi yao kumalizika Mzee Hasani alimkabidhi kitabu cha benki ambacho alikichukua kule dukani ili iwe mali ya watoto badala ya kumilikiwa na Umari pamoja na familia yake.

Hasani aliahidi kuwa atakuwa akienda kwa Bi. Rehema kuwasalimia watoto na kuwaonyesha upendo, alienda na Bi. Rehema kwa Bi. Riziki ili awape habari za Halima ingawa naye hakujua mahali alipo Halima. Mwandishi anaeleza:

> Rehema alimwita Bakari na kumwambia akawalete watoto. Mzee Hasani alinyanyuka na kuwakumbatia kwa furaha, huku akifuta machozi. Tena aliwahakikishia kuwa atakuwa anakuja kila mara kuwaangalia………………. Alitoa kile kitabu katika mfuko wa koti, akamkabidhi Rehema, akamwambia, “Hii ndio amana ya baba yao. Nilikichukua nilipoondoka kule dukani.

> Nimeona ni haki ya wanawe. Ikiwa nimekosa, Mungu Atanisamehe." (Uk.170-171).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Mzee Hasani alikuwa na historia ya uchapaji kazi. Alipokuwa ameajiriwa alikuwa akitambulika kwa uchapaji kazi wake. Katika kuwapokea watoto wa Halima yaani Ali na wadogo zake, kiutamaduni lazima apate maelezo ya mtu mzima. Kwa vile mama yao alikuwa hospitali ilibidi Bakari amtafute mzee Hasani ambaye alikuwa na majukumu ya dukani kwa Halima hivyo aliwajua vizuri wale watoto nao walimpenda sana. Mielekeo ya kijamii ni kuwa mtu mzima anaeleza ukweli hivyo maelezo ya mzee Hasani yaliaminiwa na Rehema ndipo akawapokea watoto kwa mpango wa kuwatunza na kuwasomesha mpaka mama yao atakapopatikana.

Mzee Hasani amekuwa kielelezo katika masuala ya kiuana na ndio maana alitoa ushirikiano kwa Bi. Rehema kuhusu malezi ya watoto wa Halima. Wapo ambao wanafanya kinyume na haya ayafanyayo mzee Hasani na hivyo wanatakiwa kubadilika na kuwa wanaume wapya. Kwa mfano, Umari alivyotoa rushwa kwa mwanasheria ili aruhusiwe kisheria kukaa na watoto wa kaka yake huku lengo lake likiwa kumiliki mali za marehemu kaka yake. Vile vile alitoa rushwa kwa Juma ili amkalishe Halima hospitali kwa kisingizio cha kuumwa akili.

Mzee Hasani ni mwanaume mpya maana alikuwa akifanya kazi kwa uaminifu na pia kila alipoenda aliwajibika ipasavyo na kujenga uaminifu na ndio maana hata maelezo yake yaliaminiwa na Bi Rehema ndipo akaanza kukaa na Ali na wadogo zake. Nadharia ya mwanaume mpya inamtaka mwanaume kumthamini mkewe, kushirikiana naye, kuwajibika na kutambua wajibu wake katika familia na jamii kwa ujumla.

Mwanaume pia amechorwa kama mshauri mzuri na wa kuaminika. Hii imedhihirisha na Selemani kwani aliaminiwa sana kwa ajili ya kuwashauri mambo ya maendeleo. Amini alipotaka kuacha kazi ili afanye biashara yake ndipo Selemani alimshauri kuwa asiache kazi kabla biashara haijasimama maana itampa shida kumudu kuihudumia familia.Selemani anamshauri mambo mengi hasa ya kujiimarisha kiuchumi pamoja na familia yake. Mwandishi anaeleza:

> "Ninajua kuwa una hamu ya kufanya hivyo. Lakini umefikiri utaishi vipi? Kiwanda chako bado kichanga. Hakijafanya kazi vizuri kiasi ya kukuwezesha kuendesha maisha. Tena lazima ukumbuke kuwa utahitaji pesa ili kutia bidhaa katika duka na kumwajiri mtu wa kazi. Muhimu ni maisha yako ya kila siku…" (Uk. 47).

Nadharia ya ujifunzaji mhimili usemao: mwanafunzi si mpokezi tulivu wa habari, utambuzi mazingira na tabia vinaathiriana katika upataji habari wa mwanafunzi. Amini alipata ushauri kutoka kwa Selemani maana tunajifunza kuuliza ili tupate kushauriwa. Pamoja na ushari wote bado alikaa na mkewe kufanya maboresho ya ushauri kabla ya kutenda. Amini ni mwanaume mpya aliyesikilizana na mkewe katika utendaji wa mambo ya kazi na ya kifamilia.

Katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao: uyakinifu yaani kueleza mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Kiuhalisia Amini alifanya jambo zuri sana la kuwa na rafiki wa kumshauri katika mambo ya maendeleo hasa uwekezaji. Selemani alikuwa na utaalamu wa uchumi na mzoefu wa uwekezaji hivyo alimpa mawazo mazuri sana Amini. Hali halisi inaonesha kuwa ukifanya jambo bila kujipanga unapata matatizo. Selemani alikuwa mwaminifu kwa familia nzima ya Amini hata baada ya Amini kufariki bado aliendelea kuwashauri familia yake mambo kadha wa kadha kabla Halima hajatoweshwa na Umari kumficha hospitalini bila marafiki wa familia ile kujua. Selemani angejua Halima alipo asingeacha kupambana kumtoa ili aje kukaa na wanae. Alitoa ushauri mzuri kwa Amini ili asiache kazi kabla ya miradi kuimarika maana atayumba kiuchumi na kuitesa familia yake. Amini alisikiliza ushauri wa Selemani na ndiyo maana alifanya mambo kwa weledi zaidi hadi kifo kilipompata. Mambo tunayoyatenda katika familia zetu na jamii yafaa tutumie akili ili tusiangamie. Chomsky, (1959) anaeleza kuhusu dhana ya Skinner ya tabia ya mazungumzo katika lugha.

### 3.2 Taswira ya Mwanaume katika Riwaya ya *Dago Wa Munje*

Ryanga amewachora wahusika wa kiume kwa taswira mbalimbali kulingana na lengo lake. Kwanza amemchora mhusika wa kiume kama mvivu, mchafu na asiyependa kusoma. Hii imedhihirishwa na Dago ambaye alikuwa akiwatia aibu marafiki zake kwa kuchelewa kuja shule na akifika anakuwa mchafu sana. Marafiki zake walikuwa wakimshauri sana kufanya bidii darasani ila

akawa bado hajitumi. Hii ilidhihirika pale Dago alipowasili darasani kwa kuchelewa akakuta mwalimu anaita majina darasani. Mwandishi anaeleza:

> "Hakuna siku anayowasili shuleni kabla ya kengele kupigwa," Juma alimning'onezaea mwenzake. "Na nguo zake waziona zilivyo!" Rashidi aliongeza, akiashiria jinsi zilivyokunjanakunjana…….. "Na mswaki pia pengine hajapiga, mchafu yule!" Juma alinong'oneza maneno haya huku akimfanyia Dago ishara ya kuonyesha kinywa hatari! (Uk. 24).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kutokuonesha udikteta katika familia zao na jamii inayowazunguka. Dago anapaswa kubadilika na kuwa mwanaume mpya kwa kutokuwa na ujeuri na mbabe katika familia yake na kwa walimu pamoja na wanafunzi wenzake wanaomfuatilia ili awe kijana mpya anayependa kusoma na kufaulu. Dago anapaswa kuwa msikivu darasani na kuanza kujisomea na ndipo tabia nyingine zitakuwa zikibadilika hatu kwa hatua na kuwa mwanaume mpya. Ubadilikaji wa tabia ni hatua kwa hatua na hatimaye kuwa mpya kabisa. Skinner, (1963) anaeleza kkuwa ubadilikaji wa tabia ni sayansi inayoenda hatua kwa hatua na kuhitaji ufuatiliaji kwa kila hatua mpaka kufikia sehemu lengwa.

Nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao: uyakini; kueleza mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Hii inaonesha kuwa mwanaume anapokuwa na tabia za ajabu, wanaume wenzie au kama ni mwanamke basi wanawake wenzie huona aibu. Dago alioneka mchafu siku zote na wala hapendi kusoma. Jambo hili liliwapa wakati mgumu marafiki zake mara waanzapo kumsema Dago darasani. Huu ni ukweli katika jamii tuliyonayo

maana kila mwanajamii hujipa na nafasi ya kufuatilia mwenendo wa mwanajamii mwenzie.

Mhusika wa kiume amesawiriwa kama kikojozi na mwenye tabia za kuishangaza jamii kulingana na umri. Dago ni kijana mkubwa wa kujitambua ila anayoyafanya yanashangaza sana jamii. Kwa mfano anakojoa kitandani ila anakuwa na ujanja wa kujificha ili mama yake asijue kama amekojoa kitandani. Mwandishi anaeleza:

> Alipoamka leo asubuhi alijikuta taabani katika shida nyingine. Nguo zake alizozilalia jana usiku zilikuwa zimetota. Hazikutota kwa kunyeshewa na mvua tu, zilitota kwa mikojo. (Uk. 5).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao; kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume. Dago alipaswa kubadilika kwa kujua kuwa ayafanyayo siyo mazuri na yanawahudhi wazazi wake kwa kuwapa simanzi na kuwasikitisha mno. Hii ni kutokana na umri alionao Dago. Baada ya kuyajua hayo ndipo atafanya kila njia ili abadilike na kuwa mwanaume mpya asiyekuwa na tabia mbaya za kukojoa kitandani na kuwa mchafu muda wote.

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili usemao: ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Jamii inafundisha watoto wa kiume kuwa karibu na wenzao na kuwafuatilia mara wawaonapo wakiwa na tabia mbaya za kuidhalilisha jinsia ya kiume. Hii inaelezwa kuwa katika riwaya hii, Dago kama mhusika wa kiume alikuwa anatia aibu kukojoa kitandani wakati ni mkubwa. Kila rafiki yake aliyekuwa

karibu naye hasa wanaume walishangazwa na tabia zake za kukojolea nguo na kutopenda kufua na kuoga. Hii iliwafanya vijana wa kiume wamuone kuwa kijana wa ajabu sana anayewaaibisha na asiyejitambua kulingana na umri wake. Anapaswa kupambana ili kujinasua katika tabia hizo mbaya na ndiyo itakuwa tiba yake. Rotter, (1954) anaeleza kuwa, kijana yeyote yule awe wa kike au wa kiume kujisimamia na kujipambania ndiyo silaha yake ya kumuokoa katika majanga anayokumbana nayo maana marafiki hubadilika wakati wowote.

Mwandishi amemchora mhusika wa kiume kuwa ni mtu asiyejiamini. Hii imedhihirishwa na Dago ambapo mara zote alivyokuwa akiitwa na marafiki zake ili kuchangamana nao katika kufanya mambo mbalimbali yatakayompelekea kubadilika kitabia ili aendane na marafiki zake waliompenda kwa dhati. Walijitahidi sana kuwa karibu naye ili kumbadilisha ingawa alikuwa mgumu sana kuwaitikia wamwambiayo na akiwa anawapiga machenga kila wakati. Mwandishi anaeleza:

> Hadi sasa macho ya Dago yalikuwa yakiangalia chini, bado hakuweza kuyainu. Hakujiamini katika hali yake, kukubali kushirikiana nao katika wito wao wa kwenda matembezi pamoja Jumamosi. (Uk. 88-89).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kukosoa nafsi zao na mazoea yao kama wanaume. Dago anapaswa kubadilika kwa kujikosoa yale hayafanyayo na hasa kuwa mbali na marafiki zake ambao wana nia ya kumbadilisha. Lengo la marafiki ni kuwa karibu naye ili wamwambukize tabia nzuri ambazo zinafaa kuwa nazo mwanaume ili awe mpya

asiyedharauliwa kwa uchafu wake na utoro shuleni. Asiwe wa kuchekwa na wanafunzi wenzake na badala yake awe mwanafunzi mpenda shule kama wenzie.

Nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao: wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii. Inaonesha kuwa Dago alikosa ujasiri kila mara aitwapo na marafiki zake kwa maana ilikuwa desturi yao kumuita kumkanya kulingana na tabia zake za kukojoa kitandani, kuchelewa darasani, kutofanya vizuri katika masomo na kuja shule akiwa mchafu. Kiuhalisia, kila binadamu huwa anakuwa na tabia ya kutojiamini mara kutanapo na mtu anayejua tabia yake. Kijamii, mtu mwenye tabia zisizopendeza hurekebishwa na wanajamii wenyewe. Kila Dago alipoitwa alijua tayari anaenda kuelezwa tabia zake hizo zisizopendeza katika jamii.

Mhusika wa kiume amechorwa pia kama msemakweli na mpenda urafiki na wenzake. Hii imedhihirishwa na marafiki zake Dago ambavyo wamekuwa wakimshauri kila mara na kuwa karibu naye ili kumbadilisha kitabia. Rashidi na Juma wamekuwa wakimwambia ukweli Dago wakitaka awe sawa na wenzake kitabia na kimasomo. Suala la uchafu na kutopenda kusoma na kuchelewa kuja shuleni walikuwa wakimweleza waziwazi wakitarajia rafiki yao abadilike ili asiwe anasemwa semwa na kila mtu shuleni na mtaani kulingana na mwonekano wake. Walimweleza ukweli na hawakutaka kumcheka maana walijua akiona nao wanamcheka atakata tamaa na kuona hana tena mtetezi pale shuleni na mtaani. Dago hakuwasikiliza kwa ushauri

wampao ila wao waliendelea kumkazania na kumfuatilia katika nyendo zake. Mwandishi anaeleza:

> Rashidi alisema, "Dago, sisi ni marafiki, lakini wewe mwenyewe wajiletea matatizo shuleni, kwa kutofanya kazi za shule. Hata tunapouita tusaidiane nyumbani kwetu wewe hukataa. Mara ngapi tumekuambia jambo la kufanya unapolala? Wewe hutusikizi!" Dago aligeuka na kuwakabili, "Marafiki kama nyinyi siwataki. Niondokeeni." (Uk. 89).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Rashidi na Juma walifunzwa kuwa wakweli kwa wanaume wenzao ili kuweza kuleta mabadiliko kwa mwanaume mwenzao. Hilo walilisimamia kwa Dago kwa mujibu wa familia zao na jamii kwa ujumla ingawa halikuzaa matunda yote kwa Dago japo ilimsaidia kwa kiasi kikubwa kuwajua marafiki zake wa kweli.

Nadharia ya uhalisia mhimili usemao: itumie sajili ambazo ni za kawaida. Inaonesha kuwa marafiki zake Dago walikuwa wasema kweli kwake hawakuwa na unafiki kabisa. Kila jambo lililoonekana halipendezi, walimwambia kwa kutumia taratibu za kawaida za mazungumzo ya marafiki na kushauriana. Rashidi na Juma ndio vielelezo vya marafiki wa Dago ambao ni wasemakweli waliomtaka Dago kubadilika ili jamii isiwe inamshangaa. Hii inaonesha kuwa ubadilikaji wa tabia ni suala la kijamii pia. Pfohl, (1994) anaeleza kuwa tabia ajifunzazo mwanadamu ndizo humkuza. Kujitoa kwa ajili ya wenzao na kusaidiana kurekebisha tabia zisizofaa ni jukumu la wanajamii kwa ujumla.

Mwandishi amemchora mhusika wa kiume kama anayethaminiwa kuliko wa kike na vile huwa na mwitikio wa kupambana kuleta usawa wa kijinsia. Hii inadhihirishwa na baba Dago. Mama Dago huamka asubuhi kwenda kufanya biashara yake ya kuuza maandazi na kalimati. Humtengea mumewe chai ili anywe ila pia mwanaume anapokuwa akihitaji kunywa chai na mkewe hayupo, huchukua mwenyewe na kunywa. Hii ni tofauti na wanaume wengine ambao wake zao wakiwa hawapo nyumbani wao hugoma kula kwa vile wake zao hawajawaandalia. Vilevile mama Dago amedhihirisha suala la upendeleo kwa watoto wa kiume kwa kufuatilia mila jamii yao inaonekana kuwa watoto wavulana huthaminiwa zaidi kuliko wasichana. Watoto wa kiume wanakuwa hawawajibiki kama wa kike na hivyo kutokuwa na usawa wa kijinsia. Mwandishi anaeleza:

> “Ni nani alisema wasichana si watoto? Aliyemzaa mvulana ndiye aliyemzaa msichana.” Alijiruhusu kudadisi mila za jamii zinazoipitisha mbele thamani ya watoto wavulana. “Lau kama mwanangu wa kiume angejibidisha kama dada zake. Mafanikio yetu yangekuwa makubwa si haba!” Ijapokuwa aliwathamini watoto wake sawa, hangeepuka kuhisi uchungu kuhusu matatizo anayoyapata kutokana na tabia ya Dago. (Uk. 112-113).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamiii mhimili usemao: ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Jamii ndiyo humfundisha mtoto wa jinsia yoyote namna ya kuwa hivyo Dago anavyoshindwa kujitengea chakula hadi apewe na mama yake ndivyo anavyofunzwa hata akiwa mkubwa atayaendeleza hayo. Hii inaonesh kuwa katika jamii kuna familia zinazowathamini watoto wa kiume kuliko wa kike. Hili limo katika familia ya akina Dago ambapo mama Dago pamoja na

majukumu ya kibiashara aliyokuwa nayo ni lazima anapoamka aanze kumwandalia mumewe chakula na Dago pia. Dago alikuwa na umri wa kumsaidia mama yake ila alidekezwa kwa vile ni mtoto wa kiume. Ili jamii iweze kuendelea inapaswa kuwafundisha watoto wa kike na wa kiume kuwajibika ili kuweza kuleta maendeleo. Rashidi na Juma walifanya kazi zote za nyumbani kwa kuwasaidia wazazi wao na dada zao. Familia hizi zilikuwa na elimu ya kiuana ya kuwafanya watoto wa jinsi zote kuwajibika ili waweze kujitegemea huko mbeleni na kupata mafanikio kulingana na bidii zao. Hii inaoneshwa na familia za mfumo wa kuumeni kama anavyoeleza Miescher, (2003) kuwa familia za mifumo dume huonesha matendo yanayotendwa na wanaume na namna wanavyopaswa kutenda kwa jamii yao.

Katika nadharia ya mwanaume mpya inaonesha kuwa baba Dago ni mwanaume mpya maana mkewe akiwa hayupo nyumbani anajipakulia chakula. Hata hivyo Dago anaweza kuwa mwanaume mpya kwa kuziacha hizo tabia mbaya na kuanza kuwathamini wanawake na kuwasaidia katika majukumu bila kujali jinsia.

Mwanaume amechorwa kama mpenda maendeleo bila kujali jinsia. Hii imedhihirishwa na mzee Majanda ambaye anapenda kuhimiza bidii kwa maana naye ni mtu wa bidii. Hakuwa na bidii kwa jamaa pekee bali hata kwa wanae bila kuwabagua kijinsia, aliwasomesha wanae wa kike na wa kiume ingawa uwezo wake ulikuwa mdogo ambapo aliumia sana alipokosa ada ya kumlipia Nchimoni kwenda shule ya upili. Aliwalea wanae kwa upendo sana

na ndiyo maana Nchimoni alivyoona karo imekosekana aliamua kutafuta kazi ili apate pesa amsomeshe Dago ingawa hakupenda shule. Jambo hili la Dago kutopenda shule lilimuumiza sana mzee Mjanda. Mwandishi anaeleza:

> Mzee Mjanda alijulikana pale kijijini kuwa mtu wa bidii. Juhudi zake hazikuwa za kufidia jamaa yake peke, bali, ingawa hakuwa na mali, aliweza kusaidia yeyote aliyekuja kwake kupata suluhu ya tatizo lake. Ingawa hakupata kisomo alipata hamu ya kuwasomesha watoto wake wote, wa kike na wa kiume, nafasi na karo ilipopatikana. (Uk. 115).

Nadharia ya mwanaume mpya katika mhimili usemao: kuwasaidia wake zao na wanawake wengine katika jamii katika kujiendeleza kielimu na kikazi. Hii imedhirishwa na mzee Majanda kwa wanae bila ubaguzi. Hii imeelezwa na Songoyi, (2005) anapofafanua kuwa kuna jamii ambazo huwapa kila jinsia nafasi sawa katika uwanda wa elimu na uongozi japo kuna mahali ambapo ubaguzi hujidhihirisha hasa katika ngazi ya familia.

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili usemao: vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Familia inavyofunzwa ndivyo inavyokuwa. Inaonesha kuwa familia zilizo na elimu ya kiuana zinajenga misingi ya usawa kwa watoto wa jinsi zote bila ubaguzi. Baba yake Nchimoni aliwasomesha watoto wake wa kike na wa kiume, hata alipokosa ada ya Nchimoni aliumia sana. Nchimoni alijituma kufanya kazi ili aisaidie familia yake kama mtoto wa kike. Alipopata pesa alimsomesha mdogo wake Dago kwa maana alijua baba yao hana pesa. Dago alinunuliwa vitabu vyote na mahitaji ya shule ingawa hakuipenda shule.

Mwandishi amemchora mhusika wa kiume kama kigeugeu, mnafiki na jasiri kwa namna ya tofauti. Hii imedhihirishwa na Juma na Rashidi ambao ni marafiki zake Dago. Hawa walimshawishi sana waende mtoni kucheza, alipokubali wakafika huko, waliungana na wengine akina Abdalla kumsema na kumwimba Dago kuwa ni kikojozi. Dago alikosa mtetezi hakika na ndipo baada ya kuchaniwa shati ilibidi kujipigania mwenyewe. Ugomvi mkubwa uliibuka kati ya Dago na Abdalla baada ya Dago kuzomewa sana na kupandwa hasira. Dago alipoibuka mshindi ndipo walianza kumshangilia akina Juma na Rashidi wakati mwanzo ndo walikuwa wakimzomea na kumsema vibaya kuwa ananuka mikojo. Hii inaonesha kuwa wahusika hawa wa kiume wamechorwa kama vigeugeu maana kwa kumpeleka Dago mtoni kama rafiki yao, hakutegemea kama wangemgeuka. Walimsonga walimsonga na kumchania nguo zake jambo lililomtia hasira sana Dago. Mwandishi anaeleza:

> "Mlinitaka nije mtoni ili mnipasulie nguo zangu? Mlianza kunicheka tangu zamani na mimi sikuwajali, nilinyamaza tu. Mmeendelea kunitafuta kwa mambo yasiyo na maana. Mnaniimba nyimbo na kunifumbia mafumbo ya nini name niko hapa nanyi?" (Uk. 178).

Nadharia ya mwanume mpya mhimili usemao: kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume. Hii inadhihirisha kuwa hakuna tabia inayodumu bali ni kukubali mabadiliko ya kukutoa kwenye uhasi kwenda kwenye uchanya. Rashid na Juma pamoja na Abdalla wanaweza kubadilika na kuacha ukigeugeu, kushabikia na kupenda ugomvi na kuwa wanaume wapya. Hii inasisitizwa na Omari, (2009) anapochunguza tabia zinazofanywa na wanawake katika muziki wa kufoka foka kuwa yale mabaya yanaweza

kubadilishwa yakawa mazuri ya kuiboresha tasnia ya muziki sehemu ya kufoka foka na kuwa ya kuvutia zaidi.

Nadharia ya uhalisia, mhimili usemao: uyakinifu; kuelezea mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Inaonesha kuwa marafiki wa Dago walitaka kumbadilisha kitabia. Walimbembeleza sana ili aende kucheza mtoni wakiwa na lengo la kwenda kumbadilisha kitabia. Walikuwa wazomeaji kama wengine. Jambo hili lilimuumiza sana Dago maana aliwaona wanafiki sana kwa kumzomea. Baada ya ugomvi wake na Abdalla na kuwa mshindi ndipo walianza kumshangilia na kumwona rafiki.

Mhusika wa kiume pia amechorwa kama mgomvi na mwenye hasira. Hii imedhihirishwa na Dago baada ya kukasirishwa sana na marafiki zake kule mtoni ambapo walimwimbia nyimbo za kumkashifu kutoka na kukojoa kitandani na kutopenda shule na kuwa mchafu kwa ujumla. Walimzomea sana hadi wakamchania shati lake. Hapo alikasirika sana na kuwa mbogo. Abdalla ambaye alijifanya pingwa kati ya marafiki zake wote waliokuwa mtoni akaendelea kumzomea na Dago akawa na mori wa kupigana naye. Walipigana sana hadi Dago akamzidi nguvu Abdalla, jambo ambalo liliwashangaza wote walioshuhudia maana walitegemea kuwa Dago ni mdhaifu hivyo atapigwa. Baada ya Dago kumpiga Abdalla aliimbiwa wimbo kuwa yeye ndiye shujaa mpya wa Munje. Hii ni baada ya Rashidi kuwaachanisha maana aliona Abdalla kaishiwa nguvu kabisa. Wote walimshangilia sana Dago maana hata

Rashidi alipata kazi kweli kuwaachanisha ili kumaliza mapigano yale. Mwandishi anaeleza:

> "Mshindi wetu wa leo bila shaka ni Dago!" Kila mtu alimshangilia na kusifu ushupavu wake.walimstajaabia jinsi watu wangemstajaabia kijana Daudi alipomwua Goliathi. Unayedhani siye ndiye. Abdalla kwa upande wake aliachwa pekee kujikukutakukuta nyasi na mchanga; alikuwa amesahauliwa, na yawezekana hata yeye binafsi hakutaka kukumbukwa kwa wakati ule wa jadhba kubwa, baada ya kushushwa hadhi na Dago aliyekuwa akimdharau kwa muda mrefu. Wote waliungana na shangwe zikamwendea shujaa Dago. (Uk. 186).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kutoonesha udikteta katika familia zao na jamii inayowazunguka. Tabia za ugomvi kwa watoto wa kiume huwa zinaweza kukoma endapo wao watakubali kubadilika kwa kujua madhara yake kwa familia na jamii kwa ujumla. Dago na Abdalala wanasisitizwa kubadilika na kuwa wanaume wapya wasioutumia ubabe na kushabikia ugomvi kama njia ya kumaliza tofauti zao. Hata akina Rashidi na Juma pamoja na kundi la wenzao lote linaweza kubadilika na kuacha kushabikia wenzao kugombana. Hapo ndipo wanakuwa wanaume wapya kwa kuachana na mabaya na kuyashika mazuri. Inafafanuliwa na Philip, (2009) katika kuhamasisha mabadiliko ya tabia ambazo ni mbaya na kuziendeleza nzuri katika jamii.

Nadharia ya uhalisia kamtika mhimili usemao: itumie sajili ambazo ni za kawaida, tunaona Dago akiwa na hasira sana baada ya kuchaniwa nguo zake huko mtoni baada ya kuzomewa. Katika hali ya kawaida hakuna binadamu anayependa kudhalilishwa mbele za watu. Dago alijawa hasira sana na jazba

baada ya kudhalilishwa na marafiki zake wote kwa kumzomea na akabaki bila mtetezi. Abdalla aliyejitosa kuendelea kumzomea baada ya wenzie kunyamaza ndiye aliyepigwa na Dago hadi akaishiwa nguvu. Dago kiuhalisia alijua kabisa kwao hali ya kiuchumi ni ngumu, akawaeleleza kwa kutumia lugha ya kawaida kuwa kwanini wameamua kumfanyia vile ila wao waliona kama mchezo.hata hivyo kiuana mtoto wa kiume jamii inamuandaa kujipambania na kuipambania familia yake. Kimani, (2003) anaeleza kuwa jamii nyingi za nchi zinaendelea zimekuwa nyuma kwa kuzaa watoto wengi wakitafuta watoto wa kiume. Imani yao kwa watoto wa kiume ni kuwa wao ndio walinzi wa mji, walindaji wa mali na walindaji wa watoto wa kike.

### 3.3 Taswira ya Mwanaume katika Riwaya ya *Hiba ya Wivu*

Zainabu Mwanga amewachora wahusika wa kiume kwa namna tofauti tofauti. Kwanza amechorwa kama mwenye upendo wa dhati. Hii imedhihirishwa na Ihucha ambaye ni mume wa Farida anaonyesha upendo wa dhati kwa mkewe. Anaijali familia yake na kuihudumia kwa namna mbalimbali. Ihucha anapata wakati mgumu baada ya kurudi nyumbani usiku bila kumkuta mkewe nyumbani. Mwandishi anaeleza:

> Ihucha aliendelea na mawazo ya kila namna. Alijiuliza maswali, akajijibu mwenyewe; alipanga akapangua; ili mradi mambo kichwani hayakumwendea vizuri. Alivurugikiwa hasa. Hakulala mpaka saa kumi na nusu ndipo usingizi ulimpitia. (Uk. 13).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii, mhimili usemao: ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Hapa tunaona Ihucha ambaye ni mwanaume katika familia,

alimpenda sana mkewe na kuijali familia yake. Haya ndiyo majukumu ya mwanaume katika jamii, utamaduni pia humwelekeza mwanaume kufanya hivyo maana ndivyo alivyofunza katika familia ili amtunze mkewe kwani asipofanya hivyo kiuana anakuwa hajawajibika kama mkuu wa kaya. Mielekeo ya jamii pia inaonesha kuwa mwanaume ndiye mtawala wa familia hivyo anapaswa kuyakabili majukumu ya kuitunza familia na kumpenda mkewe. Katika nadharia ya mwanaume mpya inatueleza kuwa mwanaume anapaswa kujitambua nafasi yake katika familia na katika jamii. Anapaswa kusimama kwenye nafasi yake kama mwanaume huku akishirikiana na mkewe katika kazi mbalimbali za familia ili kuleta maendeleo.

Kiuhalisia mwanaume akikwepa majukumu hayo, jamii inayoendekeza mfumodume huona ni kawaida na wala haimshangai na kumuona wa ajabu au hovyo. Zipo familia ambao zina wanaume wa namna hiyo na mwanamke akilalamika jamii inamshangaa kwani kufanya hivyo ndiko kuuendekeza ubabedume. Jamii inamuangalia mwanaume kama kichwa cha familia katika mambo ya maamuzi ila familia ikiyumba na kuanza kuombaomba anayelalamikiwa ni mwanaume kwa kutotimiza wajibu wake wa kutoa maamuzi ya nini kifanyike kwenye familia yake ili kujinasua katika hali ngumu inayowakabili. Katika jamii za namna hii mwanamke anakuwa hana nafasi ya kufanya lolote yeye anakuwa kama mtoto wa kupewa maelekezo nini afanye. Anayeleza haya Connell, (1995) kuwa mwanaume anapomiliki kila kitu katika familia akiwemo mkewe huo ndio uanaume. Hayo ndiyo yanakuwa maisha ya kawaida katika jamii zenye mfumodume.

Mwanaume pia amchorwa kama mwenye hali ya kujali matatizo ya wenzao. Ray aliharibikiwa na teksi yake wakati akimkimbiza Farida nyumbani ili amuwahi mume wake kabla hajafika nyumbani ili isifahamike kama alitoka kwenda kumfuata. Kwa bahati mbaya gari liliharibika na kushindwa kufikia malengo. Farida alivyokuwa akisikitika na kuumia kwa kutofanikiwa kuwahi nyumbani kwake kabla ya mumewe, Ray naye aliumia sana bila kujua kinachomuumiza Farida wakati ni gari lililoharibika. Ray aliumia sana baada ya Farida kumtaka ampeleke Mwenge usiku huo na kutotaka kwenda Kinondoni tena. Alitafakari sana Ray bila majibu ndipo akaamua amuulize Farida ili ajue kilichomsibu pengine angeweza kumsaidia kwa namna fulani. Mwandishi anaeleza:

> Dreva wa teksi aligeuza uso akamtazama Farida. Alijiuliza tatizo gani kubwa lililomsibu kiumbe huyo wa kike hata aamue kwenda Mwenge usiku ule wa manane? Na huko Kinondoni alikokuwa anakimbilia kwenda kabla ya lile gari kuna nini? Alitamani sana kujua, na ndipo alipoamua kumuuliza.
>
> “Inavyoelekea, una tatizo kubwa sana dada. Ni vibaya ukinieleza tatizo lako? Huenda nikakusaidia kwa kukupa ushauri.” Alitabasamu baada ya kuuliza. (Uk. 9).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii inaonesha kuwa mwanaume anafunzwa mambo mbalimbali anapokuja duniani. Ray alifunzwa kumthamini mwanamke na kumpenda na ndiyo maana alifanya hivyo kwa Farida alipopata matatizo. Hata hivyo nadharia ya mwanaume mpya inatuelekeza kuwa Ray ni mwanaume mpya anayemjali na kumsikiliza mwanamke na ndio maana hata alipokuwa nyumbani kwa Ray huko Sharifu Shamba hakuweza kumgusa wala kumfanyia chochote licha ya kumtaka kimapenzi.

Katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao: uyakinifu; kuelezea mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Katika halisi ya maisha binadamu huoneana huruma nmwenzake apatapo matatizo. Ray alimwonea huruma sana Farida alivyosikitika na kukosa amani mara baada ya gari kuharibika akajua lengo la kumuwahi Ihucha nyumbani halitafanikiwa. Ray alitaka ajue kilichomsibu ili ampe ushauri ingawa Farida hakutoa ushirikiano bali alijaa hasira na kumtolea maneno ya ukali Ray. Ilibidi Ray awe mpole ili safari iendelee.

Mwandishi amemchora mhusika wa kiume kama mtu anayejali wenzake na kujitoa. Feruzi ambaye ni rafiki wa Ihucha na mfanyabiashara mwenzie, aliumizwa sana na suala la Farida kupotea. Alimpa moyo sana Ihucha kuwa mkewe atakuwa salama. Hata baada ya watekanyara kumpigia simu Ihucha kuwa apeleke elfu 50 ndipo wamwachie mkewe, Feruzi alitoa gari lake na kumpa Ihucha ili aende nalo bonde la mkwajuni kupeleka hizo pesa na alimtia moyo sana kuwa hawatamdhuru kwani wana shida ya pesa tu. Mwandishi anaeleza:

> Baada ya kufika ofisini kwake, alimkabidhi Ihucha gari. Gari hilo lilikuwa ni mali ya Feruzi mwenyewe, halikuwa la kiwanda.
>
> “Kwaheri bwana, tutaonana nikirudi salam!” Usitie hofu, Ihucha. Wewe ni mwanaume. Nina imani shida yao ni pesa tu, hawatakudhuru. Utarudi salama, Inshallah.” “Amina.” Aliwasha gari moto akaelekea Benki. Alimkuta Musa tayari keshafika, kasimama nje ya jingo la Benki anamsubiri. (Uk. 30).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Feruzi anamtia moyo sana na anaonyesha utu kwa kumjali Ihucha kwa namna ya

tofauti. Mahusiano ya kiuana kati ya Feruzi na Ihucha ilikuwa ni katika biashara yao ya saa. Alimtia moyo sana Ihucha kuwa hatadhurika huko chini ya mbuyu. Feruzi alikuwa amebanwa na kazi ila alimpatia gari la kwenda nalo uko bondeni la mkwajuni. Hili limetoa elimu kwa jamii kuhusu masuala ya kiuana katika kusaidiana mara tupatapo matatizo. Mwanaume anajifunza kumsaidia mwanaume mwenzie au mwanamke ni kuweza kujenga mahusiano mazuri. Hii inafafanuliwa na Parsons, (1957) anapoeleza umuhimu wa mafunzo ya kiuana ili wanawake na wanaume wajue namna ya kuwa tofauti na namna ya kuzithamini tamaduni zao hasa mgawanyo wa majukumu.

Mwanaume pia amechorwa kama mwenye uchu wa wanawake. Hii imedhihirishwa na Ray baada ya kumsaidia Farida kumpa malazi, asubuhi yake akaanza kumtamani kimapenzi. Pamoja na Farida kuonyesha kuwa mawazo yake yote yako kwa mumewe, licha ya ujinga alioufanya kwa kusukumwa na wivu hatimaye kujitia matatizoni na kumuangaisha mumewe bila kulala wala kufanya kazi kwa siku zote alizokuwa akumuwaza na kumtafuta mkewe. Ray alimwita Farida dada maana walitokea wote Moshi ila bado alimtamani kimapenzi. Alitamani aachane na Ihucha ili awe mke wake. Mwandishi anaeleza:

> Mwishowe nije kushikwa wizi, wizi ambao huitwa ugoni. Sitaki! Japo Farida namtaka. Namtaka sana, tena sio awe rafiki tu, bali namtaka awe mke wangu. Kaolewa ndio, lakini hata mie pia ni mwanaume, naweza kuoa. Kati ya wasichana wote niliowahi kuwaona, mtoto huyu wa kwetu kanimaliza. Nimempenda, nimeishachagua, nitamwoa. Ni mzuri,.anajua kupenda. Penye nia pana njia. Uwezo ninao,na sababu ninayo. (Uk. 29).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kusaidia wake zao na wanawake wengine katika jamii katika kujiendeleza kielimu na kikazi. Ray alitakiwa kumsaidia Farida bila kutegemea malipo ya mapenzi. Lengo la Farida ilikuwa ni kusaidiwa ili ajinasue katika ujinga wa wivu alioufanya na siyo kumsaliti mumewe. Ray alipaswa kumnasua katika huo mtego ili ndoa yake iwe salama na si vinginevyo. Ray anapaswa kubadilika na kuwa mwanaume mpya aache kuendekeza tamaa za mwili za kumwona kila mwanamke na kuhisi ni halali yake kufanya naye mapenzi.

Katika nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao: wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii. Ray alionesha uchu wa wanawake kwa kumtaka Farida kimapenzi baada ya kumpa malazi nyumbani kwake. Alitamani Farida amwache Ihucha aje kuolewa kwake kwa maana ni mchaga mwenzie. Katika muktadha wa kihistoria, watu wanapokutana na kujenga ukaribu huanzisha undugu zaidi ya ule wa watu wa tumbo moja. Katika mahusiano ya kijamii, Farida angefanya kituko cha ajabu kumwacha mumewe na kuolewa kwa Ray ilhali yeye ndiye aliyefanya upuuzi wa kumfuata mumewe akihisi yuko kwenye mambo machafu. Kutokana na hilo aliona bora arudi kwa mume wake kwa kumdanganya Ray kuwa ataenda kumwacha. Hata hivyo kwa hoja hii Farida alijiponza mwenyewe kutokana na ujinga alioufanya na kumwingiza Ray mtegoni. Mbilinyi, (1991) anaeleza kuwa mwanamke anagandamizwa sana na kukosa haki nyingi ambazo nyingine hujikosesha mwenyewe.

Mhusika wa kiume mwandishi pia amemchora kama mchapakazi na mtafutaji kwa bidii. Hii imeoneshwa na Ihucha pamoja na marafiki zake akina Feruzi ambao walitumia muda mwingi kuweka mikakati ya kazi zao za kibiashara namna ya kuziimarisha. Hata Ray alikuwa akiendesha teksi usiku kucha ili kujipatia kipato na vile vile alifanya biashara ya magendo na ndizo zilimpa mwanga wa maisha. Ndiyo maana Farida alijisikia vibaya sana alipomfuata mumewe akidhani yuko kwenye mambo ya kipuuzi kumbe yuko kwenye kikao cha biashara na wenzake. Mwandishi anaeleza:

> “Masikini mie! Kumbe kweli alikuwa katika mazungumzo ya biashara na wenzake. Bwana Feruzi na mzee Kibwana nawafahamu sana, ni Maafisa niliokuwa nafanya nao kazi katika kiwanda cha saa. Ni watu muhimu sana katika kuendeleza biashara ya Ihucha. (Uk. 5).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: ujifunzaji unahusu kuchunguza kupata habari kutokana na ule uchunguzi na kuunda maazimio kuhusu utendakazi wa tabia hiyo. Jamii inaamini kuwa mwanaume anapaswa kuwa mchapakazi ili aweze kuitunza familia yake na kufanya mambo mbalimbali ya kimaendeleo. Jamii inategemea iyaone hayo maana ndivyo inavyowafunza. Ihucha pamoja marafiki zake akina Feruzi walifanya kazi muda mwingi ili kujipatia kipato. Ihucha aliridhika Frida akae ndani ila yeye aendelee kufanya kazi muda mwingi na kuitunza familia kwa ujumla.

Ray naye alikuwa mchapakazi sana na hata aliweza kumwacha Farida ndani akaenda kufanya kazi. Dhamira ya uwajibikaji imejidhirishwa na Ihucha na marafiki zake pamoja na Ray kama wanaume waoonesha uwajibikaji. Sherman na Wood, (1982) wamechunguza kuhusu mwanamume na jinsi jamii

inavyomtegemea kuwa aweze kujiendeleza katika majukumu yake. Wanaendelea kusema kuwa ni muhimu mwanamume kutirniza majukumu yake yote aliyotengewa na familia pamoja na jamii kwa ujumla.

Mwanaume pia amechorwa kama katili na muuaji. Hii imedhihirishwa na Sikujua ambaye alimuua rafiki yake na akahukumiwa kunyongwa ila baadae alikuja kutoka kwa msamaha wa Rais. Baada ya Sikujua kutoka kifungoni alianza mahusiano na Fatuma kwani kwani mkewe alitoroka Sikujua alipokuwa kifungoni. Mwandishi anaeleza:

> Jaji Utakunywa alimhukumu adhabu ya kifo baada ya kupatikana na hatia ya kumuua rafiki yake Pondamali Malipesa. Lakini mkuu wan chi alibatilisha adhabu hiyo na kuifanya iwe kifungo cha maisha badala ya kunyonywa.……. Rais alitoa msamaha kwa wafungwa wote waliokaa jela si chini ya miaka mine, na ambao walionyesha nidhamu. Sikujua alikuwa mmojawapo kati ya wale waliosamehewa. (Uk. 1).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume. Sikujua alizoea kujiamulia mambo bila kujali madhara yake. Nadharia hii inamtaka kuwa mwanaume mpya kuachana na huo ukatili wa kutoa roho za watu na kuwa mwanaume mpya anayewathamini wenzake na kuwaonea huruma.

Nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao: usadikifu; yale yanayoibuliwa katika jamii yawe yanasadikiwa na wasomi. Kiuhalisia mhalifu huadhibiwa hivyo Sikujua kama mhusika wa kiume alifanya uhalifu wa kuua na ndipo alihukumiwa kufungwa jela. Wasomi wanasadiki kuwa mtu akitoka gerezani

anakuwa ameshika adabu na kubadilika kuwa mtu mzuri. Sikujua baada ya kutoka kifungoni akawa mtu mzuri na akawa na mipango ya kutaka kuoa. Jamii inasadiki kuwa gereza ni chuo cha mafunzo, mtu akitoka huko anakuwa amaeiva kimaadili.

Kwa kupitia uandishi wa Zainabu Mwanga kamchora mhusika wa kiume kama mwenye nidhamu ya hali ya juu. Hii inadhihirishwa na Sikujua. Pamoja na kwamba alimuua rafiki yake na kuhukumiwa jela kunyongwa hadi kufa ila alipokuwa jela alibadilika sana kitabia na kuwa na nidhamu. Kupitia Sikujua inaonekana kuwa mhusika wa kiume anajutia makosa yake aliyoyatenda baada ya kuponea kwenye tundu la sindano kunyongwa hadi kufa. Sikujua alihukumiwa kifo ila adhabu yake inabadilishwa na Rais na kuwa kifungo cha maisha ila baada ya kuwa na nidhamu ya hali ya juu anasamehewa kifungo. Hapo alijutia makosa yake na kumshukuru Mungu kwa muujiza huo na kuapa kutokurudia kosa hilo la mauaji. Mwandishi anaeleza:

> Alipotata taarifa ya msamaha alinyanyua mikono juu akamshukuru Mungu. Sikujua alistahili kusamehewa kwakweli maana nidhamu yake huko jela ilikuwa ya hali ya juu. Aliapa kutokuua tena maishani. (Uk. 1-2).

Nadharia ya mwanaume mpya inadhihirishwa hapa kuwa hakuna tabia zinazodumu, mtu hubadilika na kuwa vinginevyo. Tunamwona Sikujua gerezani na baada ya kutoka anavyobadilika na kuwa mwanaume mpya mwenye utu na mapenzi kwa watu. Anaporejea uraiani bado jamii inampokea na kushirikiana naye. Binadamu huweza kubadilika kitabia (Butler, 1990).

Nadharia ya ujifunzaji katika mhimili usemao: ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Sikujua alilelewa katika malezi mazuri kama mtoto wa kiume ila baada ya kujichanganya na marafiki akawa na tabia za ajabu hadi akawa muuaji. Yeye alipewa malezi mazuri ila akawa anabadilika na kuleta taswira mbaya ya mauaji katika familia yake. Hata hivyo tabia za binadamu zinabadilika kulingana na mazingira hivyo Sikujua alipokaa gerezani alibadilika na kuwa na tabia nzuri sana. Hukumu yake ilikuwa ya kunyongwa hadi kufa ila tabia yake na mwenendo mzuri gerezani ulipelekea kusamehewa na Rais na kumfanya awe huru na kurudi nyumbani akiwa mwanaume mwenye tabia nzuri baada ya kurudi katika jamii yake iliyomkuza. Kila mtu alimshangaa Sikujua kwa namna alivyobadilika na kuwa na tabia nzuri tofauti na alivyokuwa kabla ya kifungo. Nadharia hii ya ujifunzaji wa kijamii ndiyo inaeleza uchanya na uhasi wa mwanaume.

Nadharia ya mwanaume mpya inamtaka mwanaume kuwa mpya kwa kuwa na matendo chanya ya kuwajibika katika familia yake na jamii kwa ujumla ili kuleta maendeleo badala ya kuendekeza ubabe dume unaozorotesha maendeleo. Kwa mfano Sikujua alipofungwa alipoteza muda gerezani kwa kosa la kuua na akakuta wenzie katika jamii walishasonga mbele kimaendeleo.

Mhusika wa kiume amechorwa kama mwenye moyo wa kujitoa na kuwasaidia wenzake. Hii imeoneshwa na Ray mara baada ya kuona Farida sasa yuko

matatizoni kwa kutolala nyumbani kwa mumewe kwa siku 2, ilibidi wakae chini kubuni njia ya uongo ya kumrudisha Farida kwa mumewe bila kujali madhara yatakayotokea. Ray alijitoa kwa moyo kumsaidia Farida ili arudi kwa mumewe ingawa njia waliyoitumia ilikuwa ni ya hatari sana kwa Ray ila hakujali yote hayo cha msingi afanikiwe kumrudisha Farida kwa Ihucha. Ray aliamua kujiita mteka nyara ili aweze kupata njia ya kufanikisha lengo lao na Farida. Mwandishi anaeleza:

> Baada ya Ihucha kujitambulisha, Ray aliendelea, "Mimi ni mteka nyara wapenzi wa watu wenye pesa kama wewe. Mkeo Farida tunaye, tumemchukua jana usiku wewe ulipokwenda kuzurura au kutafuta pesa, sijui. Kwa usalama wa mkeo, unatakiwa utoe shilingi elfu hamsini. Kesho kabla ya saa tano asubuhi tuzikute pesa hizo zikiwa zimefungwa vizuri katika mfuko na kuchimbiwa chini ya ule Mbuyu ulioko bonde la mkwajuni, kule mbali kabisa na mji. Ukishazichimbia pesa hizo, ondoka upesi usionekane hapo karibu. La sivyo utayapoteza maisha yako na mkeo. Ukitimiza haya, siku hiyohiyo mkeo atarudi nyumbani salama. (Uk. 23).

Nadharia ya ujifunzaji mhimili usemao: vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Hii inaonesha kuwa Ray alifunzwa kuwa na tabia ya utu na kujali shida za watu wengine wakiwemo wanawake. Ray alijali shida zilizompata Farida na kushiriki kuzitatua ili arudi kwa mumewe. Hata hivyo ni Ray kwa sehemu hii ni mwanaume mpya aliyemthamini mwanamke katika magumu aliyokuwa akiyapitia.

Katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao: mshikamano tunaona kuwa jambo linalolenga kuleta matokeo chanya ni lazima kuwa na ushirikiano. Ray alishirikiana na Farida kupanga namna ya kumrejesha Farida kwa mumewe.

Kwa mshikamano wa mawazo yao walifanikiwa baada ya Ray kujiita mteka nyara na kumnyoa nywele Farida. Farida alirudi nyumbani kwa mumewe ikawa furaha sana kwa familia ingawa baadae alijichanganya mpaka wakamshtukia. Hakuweza kueleza vizuri mkasa mzima wa kutekwa. Angeendeleza mshikamano wa mawazo yake na Ray waliyoyapanga ya Ray asingeshtukiwa. Kwa vile Ihucha alimpenda kwa dhati mkewe, alimsamehe maisha ya ndoa yakaendelea baada ya kukiri kosa alilolifanya. Ihucha pia alijieleza kuwa alihisiwa kuwa maeneno mabaya usiku wakati alikuwa katika shughuli za utafutaji kama lilivyo jukumu lake. Lauer, (1982) anaeleza kuhusu majukumu ya kiuana ikiwemo mwanaume kutimiza wajibu wake katika kuitunza familia. Suala la msingi ni kuongeza kipato ili kumudu kuitunza familia.

Mwanaume pia amechorwa kama mwaminifu. Hii imedhihirishwa na Ray baada ya kupokea elfu hamsini kutoka kwa Ihucha ambaye ni mume wa Farida, walikubaliana kuwa hizo pesa Ray azirejeshe kwa Farida ili zikawasaidie na mumewe katika maisha yao. Ray baada ya kuzipata hizo pesa na Farida akarudi kwa mumewe kama ilivyokuwa kiu yake kuu, Ray ndiye anamfuatilia Farida ili afuate zile pesa azirejeshe kwa mumewe kama walivyokuwa wamekubaliana. Farida anaonekana hana haraka ila Ray ndiye anamfuatilia kwenda kuzichukua pesa zao. Mwandishi anaeleza:

> "Hizo pesa utanirudishia siku hiyo hiyo ninayoondoka au lini? Aliuliza kwa sauti ya upole kidogo ili asimuudhi Ray ambaye alionyesha nia ya kumsaidia. (Uk. 20).
>
> Wewe tafuta muda kesho njoo kama tulivyokubaliana, nikupe na zile pesa uanze kutafuta namna ya

> kumrudishia, atulie. Utakuja saa ngapi? Nikipata nafasi ya kutoka nitakuja. Muda siwezi kukuambia. La muhimu, niskute mtu." "Nitakusubiri." (Uk. 67).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili usemao: ujifunzaji unahusu kuchunguza kupata habari kutokana na ule uchunguzi na kuunda maazimio kuhusu utendakazi wa tabia hiyo. Ray kama mwanaume ilikuwa jambo la kushangaza kwa namna alivyoonesha uaminifu kwa Farida. Alijifunza kuwa mstaarabu, kujitoa mhanga, mwaminifu na kuthamini shida ya mwenzie awapo matatizoni. Alitamani kumuoa Farida ila haikuwezekana na Farida hakuwa mkweli kwa Ray kwani yeye alitaka arudi kwa mumewe. Hata hivyo Ray alionesha roho ya uaminifu sana kwa kumfuatilia Farida ili akarejeshe pesa za mumewe bila kujali kuwa Ray alijiweka matatani maisha yake kwa kujiita mteka nyara na kuchukia zile pesa kwa kutumia teksi inayofahamika mjini. Ray amedhihirisha kuwa ni mwanaume aliyepata malezi ya kiuana katika jamii kuwa mwanaume anapaswa kuwa na ujasiri anayefanya lolote bila kuhofia yatakayokuja mbeleni. Mwanaume anapaswa kukabiliana na mambo ya hatari bila woga kama alivyofanya Ray wakati akichukua hizo pesa kutoka chini ya mbuyu kwenye bonde la mkwajuni. Pamoja na yote hayo bado alizitoa pesa hizo zirudi kwa Ihucha bila kujali madhila aliyoyapata kuzipata na hakutaka hata ujira kidogo kwa kufanikisha zoezi hilo.

Mbali na kuwa mwaminifu, mwanaume pia amaechorwa kama mtu asiyekuwa na tamaa. Hii imedhihirishwa na mzee Maulidi pale Mtoni Hoteli ambapo aliokota mkufu wa Farida wa thamani kubwa ila aliutunza na kutoa tangazo gazetini ili aliyeupoteza aende kuuchukua. Kwenye suala la mkufu huo pia

Mzee Maulidi na mzee Majengo ambaye ni mwendesha teksi wamekuwa wasema kweli kwa kile walichokiona kuwa ni kweli Farida alikuja pale hotelini usiku wa jumatano maana mkufu uliokotwa asubuhi sana Alhamisi wakati wa kufagia. Farida alipouona mkufu wake alishukuru sana na akaahidi kutoa zawadi. Baada ya kuambiwa ukweli kuwa Farida alikuwa pale na mkufu ukatambuliwa na Farida kuwa ni wa kwake, Ihucha alifurahi sana akaahidi kumpa zawadi mzee Maulidi ila mzee Majengo alimpa shilingi mia moja kama shukrani. Mwandishi anaeleza:

> "Asante sana baba! Nashukuru kwa moyo wako mzuri. Mungu akuzidishie imani. Zawadi yako nzuri sana nitakuletea kesho maana saa hizi usiku umeingia." "Amina mama! Niko hapa kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi sa tisa mchana. Siku mbili hizi nimechelewa kuondoka kwa sababu ya tangazo hili. Nilikuwa nasubiri nimwone mwenye mali."
>
> Ihucha pia alitoa shukrani zake kwa mzee Maulidi na kutoa ahadi ya zawadi, lakini alipotaka kuondoka, mzee Mulidi akamshika mkono, akamwambia ana kitu anataka kumwambia. (Uk. 94).

Nadharia ya mwanaume mpya inatuonesha kuwa mzee Mulidi na Ihucha wote ni wanaume wapya ambao wanamthamini mwanamke na kumwona kama kiumbe sawa na mwanaume. Mzee Maulidi hapati tamaa baada ya kuona Farida ameutambua mkufu wake na ulikuwa wa thamani. Anakubali kupewa chochote alichojisikia Ihucha kumpa kama shukrani. Anakuwa mwanume mpya asiye na tamaa wala roho mbaya na anakuwa mwaminifu kwa kazi yake. Symon, (1999) alitafiti kuhusu wanaume nchini Uingereza na kuona kuwa katika miaka ya 1988-1995 wanaume walibadilika sana na tafiti zao nyingi zilianza kufanywa kipindi hiki. Hii inaonyesha kuwa wanaume huweza kubadilika kitabia.

Nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao: itumie sajili ambazo ni za kawaida. Hii inadhihirishwa na mzee Maulidi ambaye hakuwa na tamaa. Alieleza mkasa ulivyokuwa kwa Ihucha kwa kutumia maelezo ya kisa kizima hadi akaokota mkufu asubuhi wakati akifagia. Alieleza kwa kutumia lugha ya kawaida tu kulingana na kisa chenyewe. Kweli Ihucha aliamini kuwa ni kweli mkewe alikuja pale hotelini. Farida alifurahi sana kwa kuona yule mzee Maulidi alieleza ukweli wote bila kuingia tamaa ya kuuza ule mkufu wa dhahabu maana ulikuwa wa pesa nyingi. Walichukua mkufu ule bila kumpa chochote na Farida akaahidi kumletea zawadi maana kainusuru ndoa yake. Mzee Maulidi hakuwa na tamaa na ndiyo maana alitangaza gazetini ili mwenye mkufu aende kuuchukua. Nkonge, (2006) ametafiti kuhusu masuala mbalimbali yanayowakumba vijana akaainisha mambo mengi ikiwemo tamaa ya pesa ambayo huwafanya kupenda vitu vya thamani tofauti na watu wazima. Tamaa hii huwapelekea kuingia katika njia mbaya kama wizi,dhuluma na mapenzi katika umri mdogo. Vijana wakikomboka kutoka hapo jamii itasaidika sana.

Mhusika wa kiume pia amechorwa kama mpenda starehe na mlevi. Hii imedhihirishwa na Ray ambaye aliishi maisha ya kutumbua hasa na kunywa pombe sana. Alipenda kunywa pombe na kujiburudisha kwa wanawake. Alimtamani sana Farida na kutaka amwache Ihucha ili aje kuolewa naye. Alijiriski maisha yake kwa kutunga uongo ili amrejeshe Farida kwa Ihucha kwa kutegemea atakuja kuwa mkewe baadae. Aliamini kuwa hilo litawezekana kwa maana ana uwezo wa kifedha na pia maaskari ni rafiki zake

ambavyo asingeweza kudhuliwa na Ihucha. Ray alikuwa akifanya biashara ya teksi na nyinginezo za magendo ila alizitumia pia kwa starehe. Mwandishi anaeleza:

> Raymond alikuwa kijana mpenda starehe sana, na alijua namna ya kuzitafuta pesa. Ulanguzi na magendo ndivyo vilikuwa mwanga wake wa maisha. (Uk. 18).
>
> Ray alimwangalia kupitia dirishani, akabaki hapo mpaka Farida alipopotea ndipo akajitupa kitandani……….. Ili kupata mbinu zingine zaidi za kufanikisha ndoto yake iwe kweli, aliiendea friji akachukua bia akaanza kunywa chupa baada ya chupa, huku anawaza. (Uk. 79).

Nadharia ya ujifunzaji katika mhimili usemao: ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyka katika muktadha wa kijamii. Wanaume jamii haiwashangai wanapokuwa wapenda starehe kwa kunywa pombe na kupenda wanawake ila inakuwa kinyume chake kwa upande wa mwanamke. Kihistoria jamii imejiaminisha kupitia mafunzo yake kwa jamii kuwa mwanaume yuko huru kufanya apendacho tofauti na mwanamke. Ray alikuwa mpenda starehe sana kwa kulewa pombe na kupenda wanawake ila haikuwa ajabu kwa kijana wa kiume. Utamaduni unaonesha kwa baadhi ya jamii mwanaume kuwa na wanawake wengi ni sawa tu. Mielekeo inayotawala ni kuwa, dereva ili aweze kufanya kazi yake vizuri anapaswa kunywa pombe, jambo ambalo huwafanya vijana wengi kuwa walevi na kuishia kupata ajali kutokana na hali hiyo. Hii inafafanuliwa na Connell, (1995) kuwa tabia za vijana mojawapo ni kujiingiza katika ulevi na mahusiano ya mapenzi.

Mhusika wa kiume amechorwa kama mdadisi, mwenye tamaa na mpelelezi. Hii imeoneshwa na Ihucha ambaye anafanya biashara ya saa. Mkewe Farida

baada ya kutekwa, majambazi walimpigia simu Ihucha kuwa awapatie elfu hamsini ili wamwachie mkewe. Wakati wa kuchukua zile pesa zilizowekwa bondeni na Ihucha, Ray alikodi teksi ya Sikujua na kwenda kuzichukua hizo pesa. Baada ya mambo haya kugundulika kuwa Farida hakutekwa nyara bali ulikuwa ujanja ujanja wa Ray ili kumwezesha Farida kurudi kwa mumewe. Farida alipofika nyumbani kila alichomweleza mumewe Ihucha kilimpa wasiwasi mpaka akaamua afuatilie teksi iliyokodiwa na Ray kwenda kuchukua zile pesa ili awahoji kuhusu hao majambazi waliomteka mkewe. Hata suala la mkufu kupatikana pale Mtoni Hoteli ilibidi afanye udadisi na ufuatiliaji ndipo akaujua ukweli. Suala la tamaa limedhihirishwa na Bwana Chaurembo ambaye ni dereva wa teksi aliyeingiwa tamaa ili afike kwa Ihucha akadai elfu tatu ya kumpata Farida kama ilivyoandikwa kwenye gazeti kumbe yeye hakumpata bali alikodiwa na Farida ili amlete nyumbani kwake. Mwandishi anaeleza:

> "Nimekupata, nataka kukupeleka kwa mumeo nikadai zawadi yangu." Unanipeleka kwani mimi sasa nakwenda wapi, si nyumbani kwangu?"…….. "Hukunipata nimekukodi." "Mengi ya nini? Kama kweli unakwenda kwako twende tutaongea huko tukishafika." Dreava huyo aliingiwa na tamaa ya elfu tatu za bure, akaamua kujaribu bahati yake. Ndio kufa kufaana huko kunakosemwa na Waswahili. Mwenzako aumie, wewe upate. (Uk. 52).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kutoonesha udikteta katika familia zao na jamii inayowazunguka. Chaurembo anapaswa kubadilika na kuwa mwanume mpya maana alikuwa mkali sana kwa Farida baada ya kuona hataki alipwe ujira wa kumpata Farida kama ilivyotangazwa gazetini. Hilo lilizua zogo sana ndipo Ihucha akaamua kumpa kiasi kidogo cha pesa ili

aondoke. Hata hivyo Ihucha alikuwa na furaha ya kupatikana kwa Farida asingeweza kuendelea kupishana na Chaurembo aliyekuwa na tamaa ya pesa wakati yeye alikodiwa tu.

Nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao: wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii. Hii inadhirishwa na Ihucha ambaye anapata wasiwasi kuhusu suala la kutekwa kwa mkewe Farida. Kutoka na hofu aliamua afanye upelelezi ili kuujua ukweli. Anadadisi kwa kupitia madereva pamoja na wafanyakazi wengine wa mtoni hoteli ndipo anaujua ukweli. Katika hali halisi binadamu hawakosi tamaa na ndiyo maana Chaurembo aliingiwa tamaa licha ya kuwa alishalipwa pesa zake za usafiri na Farida, bado aliitaka elfu tatu ya Ihucha kuwa kampata mkewe kama ilivyotangazwa gazetini. Kihistoria, jamii inatambua kuwa madereva wengi ni wadanganyifu kutokana na kutaka kulipwa pesa nyingi kwa safari fupi au kutaka kupata malipo ya ziada bila kufanya kazi ya ziada. Ihucha alibishana na Chaurembo bila mafanikio ila kwa kuepusha zogo nyumbani kwake usiku na furaha ya kurudi mkewe nyumbani akiwa salama, alimpa pesa kidogo ili aondoke na akaipokea. Hivyo Chaurembo na madereva teksi wenye tamaa wanapaswa kuwa wanaume wapya na inawezekana kwa mujibu wa Bird (2014) anapoeleza kuwa tabia huwa zinabadilika kulingana na nyakati zinazoambatana na umri pamoja na utayari wa mhusika.

Kwa upande wa upelelezi Ihucha alimtafuta dereva aliyekodiwa na Ray kwenda kuchukua pesa bondeni ili awasaidie kumpata huyo mteka nyara.

Ihucha alifanikiwa kumpata dereva huyo na wakamhoji ingawa hawakufanikiwa kumpata bali walikuja kufanikiwa kupitia Farida mwenyewe kusema ukweli baada ya kuona hana namna. Ihucha aliangaika sana kwa ajili ya kujua huyo aliyechukua pesa zake ni nani na anakaa wapi na alikuwa na nia gani kumteka nyara mkewe kama ambavyo mwandishi anaeleza kuwa:

> "Hivyo bwana, sisi tunataka utueleze unahusika vipi na hilo jambazi. Tumekujia kwa amani, hatutaki ghasia za kuleta polisi. Nafikiri tutafanya ubinaadamu utueleze ukweli." "Asante bwana kwa maelezo yako. Ninachoweza kukufahamisha mimi ni kwamba huyo bwana alinikuta hapahapa kituoni pangu.…….. Hivyo ndugu, mimi sihusiki naye kamwe. (Uk. 65).

Nadharia ya ujifunzaji mhimili usemao: ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Ihucha alijifunza kuwa kama mwanaume hapaswi kukubali mambo kirahisi bila kufanya ufuatiliaji. Hata hivyo ni jukumu la mwanaume kumlinda mkewe na kuhakikisha usalama wake. Hivyo Ihucha alikuwa na haki ya kufanya ufuatiliaji wa kina ili ajue aliyemteka nyara mkewe na nia yake ya kufanya hivyo. Mwanaume ana majukumu mengi likiwemo la kuitunza familia na kuilinda (Sherman na Wood, 1982).

Katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao: usadikifu; yale yanayoibuliwa katika jamii yawe yanasadikiwa na wasomi. Hii inajidhirisha kupitia Ihucha alipompata dereva wa teksi iliyotumiwa na Ray kwenda kuchukua pesa chini ya mbuyu. Maelezo ya dereva yalikuwa ni ya kusadikika kuwa si kila anayekukodi umjue jina na kujua anakaa wapi bali anakulipa chako baada ya kazi mnaachana. Yaliyoibuliwa yaliaminiwa na watu mbalimbali akiwemo

Ihucha na ndio maana aliachana na huyo dereva ila alikuja kupata ukweli kutoka kwa Farida mwenyewe hadi akampeleka kwa Ray ndipo wakayamaliza.

Mwandishi amemchora mhusika wa kiume kama mwenye ushauri mzuri kwa rafiki zake. Hii imedhihirishwa na Feruzi ambavyo alikuwa akimpa tahadhari sana Ihucha kuhusiana na biashara yao ya saa maana maaskari walikuwa wakiitolea macho. Alimpa tahadhari sana ili asije akaangamia kibiashara. Feruzi ni rafiki yake mkubwa wa Ihucha maana hata katika mambo yake mengi ya kifamilia alikuwa akimshauri sana. Mwandishi anaeleza:

> Wakati Ihucha na Feruzi wanaagana pale Motel Agip mnamo saa nane hivi, Feruzi alimpa tahadhari mteja wake. "Uchunge sana bwana mzigo huo. Maaskari siku hizi wako macho kweli tusije tukapatikana. Ukishikwa wewe basi na mimi nitamwaga unga maana hizo saa zinajulikana ni za kiwandani kwetu." (Uk. 80).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao; vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Tunaona kuwa jamii inawalea vijana wa kiume kuwa wakweli na wanaopendana. Inaaminika kuwa mwanaume anapenda mafanikio ya mwanaume mwenzie tofauti na wanawake. Hii ni kutokana na malezi walelewayo watoto wa kiume kwa kuwaandaa kuwa na roho kama hiyo. Kwa maana hiyo ndipo Feruzi alikuwa akimtahadharisha Ihucha katika biashara yake ya saa ili asikamatwe na maaskari.

Mhusika wa kiume vile vile amechorwa kama muungwana. Hii imedhihirishwa na Ihucha alipopata uhakika kuwa Ray ndiye aliyemhifadhi Farida kwa siku mbili na wakakubaliana njia ya utekaji nyara ili kumsaidia Farida kurudi kwa mumewe. Ihucha alifurahi sana na akaamua kumpa zawadi Ray na akasema asipoipokea itampa wasiwasi sana kuwa kuna jambo lilikuwa linaendelea kati yake na Farida. Huu ni uungwana maana kwa hekaheka alizozipata Ihucha baada ya kupotea mkewe kwa siku mbili, hata kama ilikuwa ni kwa wema asingediriki kumpa zawadi. Mwandishi anaeleza:

> "Bwana Ray! Kama yote uliyosema ni ya kweli-kwamba ulijitolea kumsaidia mke wangu kwa kuwa ni dada ya rafiki yako, utanithibitishia hayo kwaa kupokea hizi pesa. Usipozipokea pesa hizi nitashindwa kukuamini kwa sababu nitahisi kuwa una nia ya kupata ujira au shukurani za namna nyingine toka kwa Farida……. Kumbuka huu sio ujira, ni shukurani. Tafadhali pokea hizi pesa, unitoe wasi wasi wangu." (Uk. 107).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: mwanafunzi si mpokezi tulivunwa habari, utambuzi mazingira na tabia vinaathiriana katika upataji wa habari wa mwanafunzi. Kupitia mhimili huu, Ray alionesha uungwana wa hali ya juu maana mwanaume anapogundua mtu aliyelala na mkewe kwa muda kadhaa, lazima kuwepo na uadui wa hali ya juu. Ihucha alipata elimu ya kiuana na anaonesha ni mpenda maendeleo kwa maana anajua kuwa kuna wakati mwanaume anaweza kulala na mwanamke kwake kama njia ya kumsaidia na wala pasiwepo na mahusiano ya kimapenzi. Taswira za kimaendeleo zinadhihirishwa na Ihucha kwa kumpa Ray zawadi kwa kumtunza Farida kwa siku mbili na akafika kwa Ihucha akiwa salama. Hii

inaonyesha kuwa Ihucha ni mwanaume mpya anayejipenda na asiyelipa visasi kwa mambo ambayo yameishapata muafaka (Messner, 1990).

Mwandishi pia amemchora mhusika wa kiume kama mwenye mapenzi ya kweli kwa mkewe. Ihucha anampenda sana mke wake Farida na ndiyo maana alipopotea Ihucha alipata mawazo sana na akashindwa kula wala kulala usingizi. Baada ya kuujua ukweli na kuiridhisha nafsi yake alirudi nyumbani na mkewe Farida na wakaombana msamaha kwa yaliyotokea na maisha yakaendelea kwa upendo na ndoa ikawa yenye furaha na amani. Mwandishi anaeleza:

> “Farida mke wangu, unajua nakupenda sana. Nimekusamehe kwa kuwa nafahamu umefanya yote haya kwa sababu ya kunipenda.” “Asante kwa kunikunipenda. Asante kwa kunisamehe.” Farida alijibu kwa sauti ya chini. (Uk. 109).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemaoa: kukubali majukumu yoyote ya kiuana bila kujali jinsia wala watu waliowazunguka. Ihucha alimpenda mkewe na walirudi nyumbani kuishi vizuri kama vile hakuna kilichotokea na wala kujali jamii itasema nini kuhusu maamuzi ya Ihucha kumsamehe Farida. Huyu ni mwanaume mpya anayefanya mabadiliko chanya kwa mkewe bila uoga na kujisimamia kwa alitendalo.

Nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao; wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii. Kihistoria mwanaume huwa anakuwa na jukumu la kumtunza mkewe na akipotea jamii inamdai mwanaume kwa maana ndiye aliyakabidhiwa kumlinda na kumtunza. Farida

alipopotea, Ihucha alishindwa kulala na akakosa hamu ya kula akawa mkali kwa dada yake ili ajue mkewe alipo. Ihucha ana upendo wa kweli kwa mkewe ila pia kuna msukumo wa kijamii kuwa lazima wazazi wa Farida watamdai Ihucha mtoto wao. Kutoka na hayo yote, Ihucha aliangaika kwa kila njia kuhakikisha Farida anapatikana. Alipopigiwa na wateka nyara, alikubali masharti yao ilimradi Farida apatikane akiwa mzima. Hili ilikuwa ni katika utekelezaji wa majukumu ya mwanaume kama wasemavyo Sherman na Wood, (1982) kuhusu majukumu ya mwanaume ambayo hutofautiana baina ya jamii moja na nyingine.

### 3.4 Taswira ya Mwanaume katika Riwaya ya *Tumaini*

Clara Momanyi ametumia wahusika wa kiume katika riwaya yake ya Tumaini ingawa mhusika mkuu ni mwanamke ambaye ni Tumaini. Amewachora wahusika wa kiume kwa namna mbalimbali. Kwanza kabisa, mhusika wa kiume amechorwa kama mwenye tamaa na mbabe. Hii imedhihirishwa na mzee Masumbuko ambaye alikuwa na tamaa ya kumuozesha mwanae tena kwa ubabe kabisa kwa maana aliona kuwa pesa za mahari ni kitu cha msingi kwake kuliko binti yake kuendelea na masomo. Alifanya mipango ya kumwozesha bila ridhaa yake Tumaini na wala mkewe hakuwa na la kusema juu ya hili maana mumewe alikuwa mkali sana. Alikuwa na tamaa ya kupata pesa za mahari haraka. Mwandishi anaeleza:

> Mzee Masumbuko aliamini kuwa kumwoza bintiye ugenini kungemwepushia mambo mengi. Alitaka kutekeleza mipango ya kumwoza Tumaini baada ya yeye kukamilisha darasa la nane. Hii ni kwa sababu hata kama

> angalifaulu mtihani wake, karo ya shule ingekuwa kisingizio bora cha kumwoza Tumaini. (Uk. 52).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili: vishawishi vinapimakatika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Jamii inamfunza mtu namna ya kuwa katika jamii yake kulingana na tamaduni zao. Inaonyesha kuwa katika riwaya hii mzee Masumbuko alikuwa na tamaa ya kupata pesa kupitia kumwozesha mwanae Tumaini kwa nguvu. Alikuwa mbabe sana na wala mkewe hakumsikiliza. Baada ya kumlazimisha Tumaini kufanya tohara ili aolewe. Kiutamaduni mwanaume anapewa mamlaka katika familia na ndiyo maana mzee Masumbuko hakumsikiliza mkewe pamoja na ndugu zake katika maamuzi. Mielekeo ya jamii inayotawala ni kuwa wanaume ni wababe hasa wafanyavyo mambo yasiyokubalika katika jamii au familia. Katika mfumo wa kuumeni hili huonekana siyo kosa. Mfano Connell, (1987) anafafanua mamlaka za kijinsia kuwa mwanaume anapaswa kuonesha uanaume wake kwa kuwa na mamlaka katika familia yake. Yeye ndiye muamuzi wa mwisho.

Mwandishi amemchora pia mhusika wa kiume kama mtu mwenye kuthamini jinsi ya kike. Shabani mumewe Halima alimpenda sana binti yake Riziki na kumpatia elimu tofauti na wanaume wengine ambao waliothamini jinsi ya kiume na kuwaacha wa kike. Wazazi wa Riziki hawakukubaliana kabisa na ndoa za utotoni na kuwatakatiza masomo mabinti na kuwaoza kwa waume wasiowajua na kuwasababishia matatizo mengi katika familia zao. Mwandishi anaeleza:

> Wasichana wadogo waliozwa kwa waume wasiowajua na mipango yote ilitekelezwa na wazazi. Wale waliobahatika

> kum tumaliza elimu ya msingi na kujiunga na shule za upili walikuwa wachache mno. Riziki alikuwa mmojawapo wa waliobahatika. Hii ni kwa sababu wazazi wake waliuona umuhimu wa kumuelimisha mtoto wa kike. Shabani na mkewe Halima walikuwa mstari wa mbele kupinga ndoa hizo za lazima. (Uk. 15).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili usemao: ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Shabani alifunzwa namna ya kumjali mkewe pamoja na familia yake kwa ujumla bila kuwabagua. Inaoneshwa kupitia Shabani baba yake Riziki ambaye anatumia nguvu yake kubwa kumsomesha mwanae wa kike Riziki kwa kumsisitiza kufanya vizuri katika masomo. Riziki alijitahidi sana kimasomo kulingana na alivyokuwa akisisitizwa na baba yake. Shabani alikuwa na elimu ya kiuana na ndiyo maana aliwathamini sana watoto wa kike tofauti na mzee Masumbuko ambaye aliwaona kama chanzo cha mapato kupitia mahari mara waolewapo.

Vilevile Shabani alikuwa na moyo wa kumsomesha Tumaini mara alipokimbilia kwao ili asitahiriwe na kuozeshwa badala ya kuendelea na masomo. Shabani na Halima walimtia moyo kuwa asiwe na wasiwasi wao wanajua matatizo ya baba yake na ndio maana anataka kuwaozesha wanae kwa lazima ili apate pesa ya mahari. Tumaini alikata tamaa sana ila Shabani na Halima walimtia moyo kuwa atasoma mpaka atakapotaka yeye. Tumaini alipomaliza mitihani yake alifurahi sana na kuwashukuru kwa kumfikisha hapo. Mwandishi anaeleza:

> Majuma mawili yalikuwa yamepita baada ya Tumaini kurejea nyumbani kutoka shuleni. Alikuwa na wingi wa

> furaha na matumaini kwani aliweza kuukamilisha mtihani wa kitaifa salama salimini. Aidha, alimshukuru Ba Mdogo wake kwa sababu ni kupitia kwa ukarimu wake wa kugharamia masomo yake ndipo akaweza kusoma bila shida. Ma Mdogo wake Bi. Halima hakuchoka kumpa moyo na kumhimiza kusoma kwa bidii. (Uk. 122).

Nadharia ya mwanaume mpya katika mhimili usemao; kusaidia wake zao na wanawake wengine katika jamii kujiendeleza kielimu na kikazi. Shabani ni mwanaume mpya ambaye aliachana na tabia za kuwagandamiza wanawake wasisome bali wawe tu wa kuolewa na kukaa ndani. Inaonyesha kuwa Shabani alikuwa na mahusiano mazuri na watoto wa kike na ndio maana hawakumwogopa kama ilivyokuwa kwa wazai wengine kama mzee Masumbuko ambaye hakuwa na uhusiano mzuri na watoto wake wa kike. Upya wa Shabani kwa kuwa karibu nao uliwafanya watoto wa kike wamsikilize na kufauata anayowashauri na ndio maana walifanikiwa kimasomo. Tumaini alipita miji mingi ila akakimbilia kwa Sahabani kwa maana alijua kuna msaada. Shabani alipenda maendeleo ya watoto bila kubagua jinsi kama ilivyo kwa wanaume wengine. Hii inaelezwa na Hill, (1977) anaposema kuwa uhuru wa wahusika huwafanya waweze kueleza uhalisia wa mambo yanayopatikana katika mazingira halisi wanayoishi.

Mhusika wa kiume vilevile mwandishi amemchora kama mtu asiyeshaurika. Hii imedhihirishwa na Mzee Masumbuko pale Tumaini alipokimbilia kwa Shabani. Tumaini wakati akihojiwa na Halima ili kujua kilichomsibu hadi akatorokea kwao, Halima alionesha kuwa anajua kilichotokea maana alikwishaongea na mzee Masumbuko bali hakukubaliana naye na kubaki na

msimamo wa kuwa anataka kumtahiri Tumaini na kumwozesha ili apate mahari. Aliposhauriwa aliishia kuwatukana washauri na kuwaona wanavunja miiko ya kijamii. Mzee Masumbuko alishikilia msimamo wake wa kumwozesha Tumaini baada ya tohara na ndicho kisababishi cha huyo binti kutorokea kwa Shabani na Bi Halima. Mwandishi anaeleza:

> "Mwanangu, hutaki kuniambia lakini nimeelewa. Nilijua mimi tangu pale mwanzo kuwa mambo yatakuwa haya. Mzee Masumbuko nilimketisha mimi. Nikampa pwi na pwiriri. Nililovuna kwake ni matusi na kuambiwa ninavunja miiko." (Uk. 8).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kutoonesha udikteta katika familia zao na jamii inayowazunguka. Mzee Masumbuko alikuwa dikteta kwa mkewe na wanae pamoja na wanajamii kwa ujumla na ndio mana aalikuwa hashauriki. Nadharia hii inamtaka kubadilika na kuwa mwanaume mpya asiyeshikilia misimamo ya kumgandamiza mtoto wa kike. Kwa kuacha udikteta atakuwa karibu na familia na jamii kwa ujumla ili kushirikiana katika mambo mbalimbali katika familia kwa ajili ya kuleta maendeleo. Mnenuka, (2011) anaeleza kuwa umuhimu wa mtu huonekana pale anapokuwa na mabadiliko ya kitabia na ndiyo humwezesha mtu kujitambua kuwa anastahili kuheshimu na kuheshimiwa.

Nadharia ya uhalisia mhimili usemao; mshikamano. Hii inadhihirisha kuwa mtoto anapokuwa na mzazi mkorofi kama mzee Masumbuko, jamii inapaswa kushikamana ili kupinga tabia hizo. Mzee Masumbuko alikuwa hashauriki hata kidogo kuhusu watoto wake. Alichoamua alitaka kiwe hichohicho, hata mkewe hakumsikiliza wala marafiki zake. Shabani na mkewe walishikamana

kumsaidia Tumaini na walimweleza kuwa wanazijua tabia za baba yake hivyo walimtia moyo na kumhakikishia kuwa watampa kila aina ya hitaji la shule ili aweze kusoma na kufikia ndoto zake. Mshikamano ni jambo linaloleta mafanikio kwa kuunganisha nguvu ya pamoja. Halima na Shabani walishikamana kumsomesha Tumaini na Riziki na Tumaini walishikamana katika masomo hatimaye wote wakafanikiwa.

Mhusika wa kiume amechorwa pia kama mchapakazi. Shabani alikuwa mchapakazi hasa kwani alikuwa mkulima hodari na mpenda kusoma hadithi. Alifanya kazi zake kwa bidii na baada ya kazi za shamba alitulia kwa kupumzika huku akisoma hadithi zenye mafunzo mbalimbali. Hii ilimtia moyo Riziki kuongeza bidii katika masomo kulingana na uchapaji kazi wa wazazi wake hasa mzee Shabani. Aliona mzazi anavyopenda kusoma hadithi na akawa akipata hamasa kubwa. Mwandishi anaeleza:

> Hata hivyo, Shabani ni mkulima hodari aliyemiliki mashamba mawili. Aliyahudumia na mkewe, na mavuno ya ziada waliyopata waliyauza ili kumsomesha mtoto wao wa pekee Riziki. Ijapokuwa Shabani hakuenda mbali kwa mambo ya elimu, alipenda kusoma vitabu mbalimbali hasa vya Kiswahili. (Uk. 11).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Shabani alifunzwa kuwa mwanaume anapaswa kuwa mchapakazi ili kumudu majukumu yake kwenye familia kama mwanaume. Hii inatueleza kuwa jamii inaamini kuwa mwanaume lazima awe mchapakazi kwa ajili ya kuitunza familia yake kwa kuwapa mahitaji ya kila siku. Kiutamaduni mwanaume

anapotoka kazini hufika nyumbani na kupumzika akitegemea kuhudumiwa na mkewe chakula na mambo kadhaa ya hapo nyumbani. Shabani wakati akisubiri huduma za nyumbani ndipo alisoma vitabu. Mielekeo inayosmbazwa na wanaume wenzake mara wamkutapo nyumbani ni kwamba ametawaliwa na mwanamke na ndiyo maana haendi kunywa pombe wala kuchangamana na wanaume wenzie. Shabani baada ya kazi zake alizozifanya kwa bidii alirudi kupanga kazi za kesho na kupata muda wa kupumzika. Mtu mwenye elimu ya kiuana hawezi kupelekeshwa na mielekeo inayosambazwa katika jamii na kumwaribia mipangilio yake na familia yake. Kwa msimamo huo ndio maana Shabani na mkewe waliweza kufanikiwa mipango yao.

Huyu ndiye mwanaume mpya kwa mujibu wa nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kukubali majukumu yoyote ya kiuana bila kujali jinsia na bila kujali watu waliomzunguka. Yote yaliyosemwa kwa Shabani na wanajamii hakujali. Hii inafafanuliwa na Whitehead, (2001) kuwa mwanaume mpya anakuwa na msimamo wa mambo hayatendayo kwa maana ni mazuri kwake, familia na jamii yake.

Mwandishi amemchora mhusika wa kiume kama mwenye malezi mabaya na wa kutetea maovu ya mtoto wa kiume. Hii imedhihirishwa na Bwana Andrea ambaye alikuwa akimtetea mwanae Majuto shuleni kwa maovu aliyokuwa akiyafanya. Ilifikia wakati Mjuto akaonekana ni mwanafunzi aliyeshindikana maana alikuwa hawaheshimu walimu wake hata kidogo. Majuto alifanya makosa makubwa sana ya kumfukuzisha shule moja kwa moja ila bado

hakufukuzwa jumla na ilipelekea mwalimu Mwadime kuhisiwa kuwa alipokea mlungula kwa baba yake alikuwa na cheo kikubwa. Majuto alipokuwa akiadhibiwa shuleni hakukubaliana kabisa na adhabu kiasi cha kusumbua darasa kwa kurusha mawe darasani kwa kupitia dirishani. Mwandishi anaeleza:

> Mara kadha Majuto alifukuzwa shule kwa sababu ya utovu wa nidhamu lakini Bwana Andrea alimtetea mwanawe huku akitumia cheo chake, na Mjuto alikubaliwa fursa nyingine. Wakati mmoja Majuto akishirikiana na mweziwe Kijungwe, walivunja afisi ya mwalimu mkuu na kuiba madaftari ambayo walimwuzia Bwana Karim. (Uk. 20).

Nadharia ya uhalisia mhimili usemao: uyakinifu; kuelezea mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Hii inatueleza kuwa jamii ina matukio kulingana na hali halisi iliyopo. Kutokana na watu kutofautiana kimapato na ndio maana kunakuwa na matajiri na masikini. Wenye pesa yaani matajiri mara nyingi huwa na malezi mabaya na pia hutumia pesa zao kununua haki. Bwana Andrea alimtetea mwanae sana mara afanyapo fujo shuleni. Majuto alikuwa akifanya fujo za kupiga mawe juu ya paa mara alipoadhibiwa kwa kosa fulani. Ilipofikia Majuto anapaswa arejeshwe nyumbani kwa sababu ya kushindikana kitabia, mzazi wake alitoa rushwa na Majuto kuendelea na masomo. Hili ni suala la kawaida kwa watoto wa matajiri kuwa wasumbufu shuleni na pia wazazi wao kutokubaliana na adhabu wapewazo watoto wao. Suala hili hupelekea wwalimu kufanya kazi kwa mazingira magumu kutokana na kutoridhishwa na mienendo ya watoto hao wa matajiri. Wakati mwingine walimu huogopa kutoa adhabu kubwa kwa watoto wa matajiri wakihofia kufanyiwa mambo mabaya na matajiri hao. Haya ndiyo matokeo ya matabaka

katika jamii. Hili pia ni suala la kisaikolojia ambalo linahitaji mabadiliko ya hatua kwa hatua. Anafafanua Renzetti, (2012) kuwa tabia zinapaswa kudhibitiwa katika hatua za makuzi maana ni suala la kisaikolojia vinginevyo atashindwa kuendana na mambo mengi katika jamii.

Mhusika wa kiume amechorwa kama mtu wa kuwadharau wanawake na kuwaona hawana maana yoyote katika jamii kwa kuwafananisha na bidhaa zinazosubiri kununuliwa. Tabia hii anayo mzee Masumbuko ambayo alimrandisha mwanae wa kiume Idi akaanza kuwadharau dada zake na kutumia lugha ya dharau kwao kwa vile yeye ni mtoto wa kiume. Tabia hii ilimkera sana Tumaini akawa anakuwa mkali ingawa Idi hakubadilika maana alikuwa akipewa jeuri na baba yake. Mzee Masumbuko pia alikuwa hashauriki kabisa kuhusu malezi ya wanae na aliposhauriwa na mkewe pamoja na wanae aliwajibu kuwa nazi haishindani na jiwe. Mwandishi anaeleza:

> Pacha hao walifuatiwa na mtoto wa kiume aliyeitwa Idi. Huyu alimranda sana babake, sio kwa sura tu bali hata kwa tabia. Alikuwa mwingi wa hamaki na ukaidi. Kutokana na vitimbi vya babake, kijana huyu mdogo aliwaona dada zake kama watumishi pale nyumbani. Alithibitisha haya kutokana na kauli kalikali alizoelekeza kwa dada zake, kama vile kuwaambia wao ni kama bidhaa za uwekezaji tu pale nyumbani. Walisubiri tu kuolewa ili wazazi wapate pesa za kumsomeshea. (Uk. 14).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili usemao: ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Idi alifunzwa na baba yake kuhusu kutowathamini wanawake. Hapa tunaona

kuwa mtoto humleavyo ndivyo akuavyo. Idi alikuwa na dharau kwa wanawake kwa sababu alilelewa hivyo na mzee Masumbuko aliyekuwa akiwadharau watoto wake wa kike. Mwanae wa kiume alimdekeza sana na hakutaka afanye kazi. Watoto wa kike ndio waliokuwa wakifanya kazi zote. Idi aliwaona dada zake kama bidhaa. Tabia hiyo ya Idi ilisababisha mgogoro baina yao. Tumaini alimsema sana ila Idi hakubadilika. Hata hivyo mzee Masumbuko alijua kabisa kuwa hayo ayafanyayo ni mabaya ila aliendelea kumfundisha Idi na kutoonesha kuwa huo ni udhaifu kwake. Hili linaelezwa na Winerman, (2005) kuwa, wanaume wanapokumbwa na shida, huwa ni vigumu kutambulisha hisia zao kwani huwa hawataki kabisa kuonekana kuwa ni wanyonge. Dalili za kuathirika kwao kiakili huwa zinakuja kutambulika kwa shida mno hasa na wapendwa wao wa karibu. Dalili za atahri zao hujidhihirisha kupitia kukosa usingizi, kuwa na hasira na hali ya kukata tamaa katika shughuli zao za kimaisha na kuishia kuchanganyikiwa.

Wengi wao huanza kujitenga na watu. Wao huona vigumu kudumisha mahusiano na watu wengine au hata kuwasiliana nao. Aidha, huwa hawana hamu ya mapenzi kwa wake.

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kuwaona wanawake kama viumbe sawa na wanaume kwa kuwaheshimu na kuwapenda katika kila nyanja wanazokuwepo. Mzee Masumbuko na Idi wanapaswa kubadilika na kuwa wanaume wapya kwa kuwathamini wanawake katika jamii kwa ujumla na kuwaona wanawake ni sawa na wanaume. Hii inasisitizwa na Carole,

(1986) anapozungumzia usawa wa waandishi wa kazi za fasihi. Anaelza kuwa waandishi wote ni sawa,hakuna mwandishi wa kike wala wa kiume bali wote ni waandishi wa kazi za fasihi.

Mwandishi amemchora mhusika wa kiume kama mlevi. Haya yanaelezwa na Bi Halima mara baada ya kumpokea Tumaini nyumbani kwake alipotoroka kukimbia tohara na kuozeshwa kabla ya kumaliza masomo. Mzee Masumbuko alitaka mwanae Tumaini akaolewe baada ya tohara ili aweze kupata pesa ya mahari. Mzee huyu alikuwa mlevi sana asiyeshaurika juu ya maamuzi yake. Hata mke wake Amina alikuwa hamsikilizi wala kukubaliana na mawazo ya mkewe juu ya Tumaini na wadogo zake kuhusu masula ya elimu. Tabia hii ya mzee Masumbuko ndiyo ilipelekea Tumaini kufanya maamuzi ya kutorokea kwa mzee Shabani na Bi Halima ili wamsomeshe. Mwandishi anaeleza:

> Bi Halima aliyafahamu vyema makusudio ya mzee Masumbuko kwani alikuwa mroho sana wa pesa. Tayari alijua kiasi cha mahari ambacho angepata baada ya kumwoza Tumaini. Alifahamu pia jinsi mzee huyo alivyofisidi mapato yake ulevini. Lakini hakutaka kuyatamka hadharani mambo haya mbele ya watoto wale. (Uk. 24).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume. Mzee Masumbuko kila mtu alimtambua kama mlevi mwenye tamaa ya kuwaozesha wanae katika umri mdogo. Nadharia hii inamtaka kujikosoa ili abadilike na kuwa mwanaume mpya anayethamini maendeleo ya binti zake kieleimu na pia kuacha sifa mbaya ya ulevi.

Nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao: usadikifu; yale yanayoibuliwa katika jamii yawe yanasadikiwa na wasomi. Inaeleza kuwa mambo yaliyooneshwa na mzee Masumbuko kwa sababu ya ulevi wa kupindukia, yalimfanya awe na tabia za ajabu. Tumaini aliamua kutorokea kwa Shabani na Bi. Halima ili waweze kumsaidia kimasomo kumgaramia maana baba yake hakuthamini elimu kwa mtoto wa kike zaidi ya kumtaka aolewe ili apate pesa za mahari. Yale aliyoayasema Tumaini kuhusu baba yake yalisadikiwa na Shabani na mamake mdogo Bi. Halima kwani walimjua sana mzee Masumbuko na tabia zake za ulevi na tamaa ya pesa. Wasomi wanasadiki kuwa katika jamii wapo walevi na matendo yao yanashangaza jamii hasa kuwakatisha watoto wa kike ili wakatahiriwe tayari kwa kuolewa. Mambo haya yanaweza kubadilika kulingana na nyakati (Bird, 2014).

Mhusika wa kiume amechorwa pia kama chanzo cha matatizo ya watoto wake wa kike. Wadogo zake Tumaini hawakuendelea na shule, matokeo yake wakaozeshwa kwa wanaume wasiowataka na kuishi maisha ya shida. Haya yamedhihirishwa na mzee Masumbuko kwa kuwaoza Mashaka na Rehema katika umri mdogo badala ya kuendelea na masomo. Tumaini alilazimika kuwa anampelekea Rehema vyakula pamoja na huduma mbalimbali akiwa kwa mumewe kwani mumewe alikuwa na kipato kidogo kisichomwezesha kumpatia mahitaji muhimu kama chakula mkewe. Kutokana na ulaji duni Rehema aliishiwa damu akiwa mjamzito na kulazimika kumwongezea damu. Rehema aliishi na mumewe Shauri kwa maisha ya dhiki sana maana hata pesa ya kukodi gari kumpeleka zahanati Rehema alipoumwa na uchungu

hawakuwa nayo. Mzee Masumbuko kwa kupenda pesa ya mahari wanae walidumbukia katika maisha ya shida kwa kuolewa katika umri mdogo. Mwandishi anaeleza:

> Agahabu, Tumaini aliwaza juu ya dada zake, jinsi walivyokosa elimu kwa sababu ya tamaa ya baba yake. Mzee Masumbuko alipokea mahari ya Mashaka, akamwoza kwa lazima kwa mzee Lusimbo, kama mke wa tatu. Ndoa hiyo ilimsababishia Mashaka madhara makubwa ya kimwili na kiakili pia. Mzee huyo alikuwa na umri mkubwa sawa na babake Mashaka. Kwahiyo, wakawa hawasikilizani kabisa. Yale yaliyomfurahisha Mashaka, mumewe aliyaona ni ya kitoto tu. (Uk. 122-123).

Nadharia ya mwaanaume mpya mhimili usemao: kutoonesha udikteta katika familia zao na jamii inayowazunguka. Udikteta wa mzee Masumbuko ndio uliwadumbukiza wanae matatizoni kwa kuolewa katika familia duni wakiwa wadogo. Nadharia hii inamtaka mzee Masumbuko kubadilika kwa kuachana na udikteta na kuwa mwanaume mpya anayewahurumia watoto wake wa kike na kuwawezesha kupata maendeleo kitaaluma.

Nadharia ya uhalisia mhimili usemao; uyakinifu; kuelezea mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Hapa tunaona mzee Masumbuko akiwasababishia wanae wa kike matatizo kutokana na tamaa zake za pesa ya mahari. Hii ni kutokana na hali halisi ya ulevi aliokuwa akiuendekeza. Ni jambo yakini kwa watu wenye tamaa kufanya mambo ya ajabu yasiyokubaliwa katika jamii mfano kumwozesha Rehema kwa mzee Lusimbo ambapo alikuwa na wanawake wengine. Hii imelezwa na Mavisi, (2007) kuwa katika jamii za mfumo wa kuumeni, ndoa zilipangwa na wazazi. Mapenzi hayakuthaminiwa

kabisa wala kupewa nafasi kama kigezo kinachuhusika katika uchaguzi wa wachumba. Msichana aliposwa na kuozwa kwa mwanaume aIiyechaguIiwa na wazazi.

Mwandishi amemchora mhusika wa kiume kama mtii na mpenda masomo. Sifa na Yohana walikuwa watii sana shuleni na walikuwa na bidii ya shule kwani walifundishwa hivyo na wazazi wao tangu wakiwa wadogo. Wazazi wao waliwapa motisha sana na kuwapongeza walipofanya vizuri katika masomo ili kuwafanya wawe na bidii zaidi katika masomo. Sifa alinunuliwa baiskeli na baba yake mara alipofaulu mtihani. Mwandishi anaeleza:

> Walikuwa hodari katika masomo na kila mara wazazi wao waliwahimiza kusoma Zaidi. Alikumbuka jinsi Sifa alivyonunuliwa baiskeli na babake, Mzee Majaliwa kwa sababu ya juhudi zake masomoni. (Uk. 21-22).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili usemao: mwanafunzi si mpokezi tulivu wa habari, utambuzi mazingira na tabia vinaathiriana katika upataji wa habari wa mwanafunzi. Sifa na Yona wamefunzwa kuwa mwanaume anapaswa kuwa na bidi katika kila jambo analotakiwa kulifanya ikiwemo masomo. Mafanikio ni wajibu kwa mwanaume. Ndio maana walikuwa wapambana ji sana na kuwashauri wenzao akiwemo Tumaini juu ya masomo ya kuyasoma ili waweze kufanikiwa. Hii inaeleza kuwa malezi ya watoto ndiyo yanawafanya wawe na tabia fulani wawapo wakubwa. Sifa na Yohana ni vielelezo vya watoto wa kiume wenye tabia nzuri walipokuwa masomoni. Wazazi wao waliwaandaa kuwa watoto wa kiume wenye bidii ili waweze kufanikiwa. Hii ni tofauti na mzee Masumbuko alivyomlea Idi.

Malezi mazuri hujidhirisha katika tabia za watoto wawapo wakubwa. Hii inasisitizwa na wataalamu wa saikolojia kuwa mtoto anavyolelewa ndivyo unavyopata majibu katika matendo yake. Bandura, (1963) anaposema kuwa ujifunzaji wa kijamii huanza utotoni na ndiyo huwa dira ya maendeleo kwani tunajifunza ili kupiga hatua ya kimaendeleo.

Mhusika wa kiume amechorwa kama mwenye busara. Hii imedhihirishwa na Sifa alipotaka kwenda kumchumbia Tumaini. Alimpenda sana Tumaini ila hakutaka kumgusia kabisa masuala ya mapenzi bali walikuwa wakihimizana kusoma kwa bidii. Walisaidiana kimasomo walipokutana na kuelekezana fani za ubobezi kimasomo. Sifa baada ya shule ndipo alianza kumtafuta Tumaini kumbe hakuwa kwa wazazi wake bali kwa Bi Halima na Mzee Shabani ambao walimsomesha hadi elimu ya juu. Sifa alipofika nyumbani kwa Mzee Shabani, walimpenda sana kwa busara aliyoitumia kujitambulisha maana hawakuwahi kumwona kabla. Baada ya utambulisho wa waliridhika naye na ndiyo maana wakamwita Tumaini kutoka ndani aje kumkaribisha mgeni wake. Waliongea mengi sana na mahusiano yakaanza baada ya makubaliano. Mwandishi anaeleza:

> “Tuma, huyu mwenzio amekuja kukuona. Sikujua kwamba Mzee Majaliwa ana mtoto aliyesoma nawe. Leo ndio kijana huyu amenifahamisha,” alisema Shabani na kumwachia Tumaini kiti ili azungumze na mwenziwe. (Uk. 134).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili usemao; uujifunzaji unahusu kuchunguza kupata habari kutokana na ule uchunguzi na kuunda maazimio kuhusu utendakazi wa tabia hiyo. Sifa alifunzwa namna ya kuwa na subi Hii

inaonesha kuwa Sifa alionekana kijana mwenye busara katika jamii hasa alipofika nyumbani kwa Shabani akiwa na lengo la kuongea na Tumaini kuhusu uchumba wao. Sifa kama kijana wa kiume hakuonesha hisia za mapenzi kwa Tumaini ambaye ni msichana katika kipindi cha masomo yao. Alikuja kumweleza hasa mara baada ya kumaliza masomo yao. Hii ni dhana chanya na taswira ya busara katika jamii. Shabani na Bi Halima walipomwona Sifa, hawakusita kumruhusu kuongea na Tumaini kwa busara aliyoionyesha kwao. Elimu ya uana aliyoipata Sifa ilimfanya awe kijana mwenye busara. Grusec, (1992) anafafanua kuwa makuzi ya binadamu kisaikolojia hudhuhirisha tabia zake kutokana na yale aliyojifunza katika familia na jamii kwa ujumla.

Vile katika nadharia ya uhalisia inaonekana kuwa wahusika waonyeshe kama walivyo katika muktadha kihistoria na kijamii. Hii ni kupitia tabia za vijana kama Sifa na Yohana. Hawa walikuwa na busara kutokana historia ya familia zao kwa namna walivyolelewa. Uhalisia unaonesha kuwa mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Sifa alionesha tabia njema sehemu mbalimbali alizopita hasa kuwa na bidii shuleni na kupenda kufikia malengo kwa sababu ya malezi aliyolelewa.

**3.5 Hitimisho**

Waandishi wametumia taswira mbalimbali kuwasawiri wahusika wa kiume ambapo imedhihirika kuwa wanazo taswira kama ubabe, ujeuri, ulevi, unyanyasaji wa wanawake,kutopenda elimu kwa watoto wa kiume pamoja na

taswira nyinginezo. Wahusika wa kiume katika riwaya zote nne wameonesha taswira hasi na chanya ambavyo zimo katika jamii nyingi za Kiafrika na kwingineko kwa lengo la kuzitaka jamii kubadilika na kwa zile chanya kuziendeleza ili jamii iweze kuwa na maendeleo zaidi.

Utafiti huu ni tathmini ya juhudi zinazofanywa na baadhi ya waandishi wa kike wa za Kiswahili na kuzibaisha taswira ya wahusika wa kiume katika kazi za kifasihi. Aidha, ni kigezo cha kutathmini mchango wa waandishi wa kike kutumia sanaa ya uandishi kujitambulisha na kugeuza hali yao katika jamii kama ilivyoelezwa katika tafiti tangulizi kuwa waandishi wa kike walikuwa hawapewi kipaumbele katika uandishi wao na wala kazi zao hazikuthaminiwa kama zilizoandikwa na waandishi wanaume. Sasa hali inabadilika maana waandishi wanawake wanazidi kushika kasi katika uandishi.

Vile vile, kazi za waandishi wa kike zinasomwa kila mahali hadi kwenye mitaala ya ngazi mbalimbali za elimu. Isitoshe, hii imekuwa ni nafasi nzuri ya mtafiti kufanya utafiti na kuyatoa mawazo na mapendekezo kwa wasomi na watafiti wengine kama inavyomwajibikia mtafiti yeyote. Mihimili ya nadharia ya mwanaume mpya,ujifunzaji wa kijamii na uhalisia imedadavua taswira zinazowasilishwa na wahusika wa kiume katika riwaya teule.

# SURA YA NNE

# MITAZAMO INAYOIBULIWA NA WAHUSIKA WA KIUME KATIKA RIWAYA TEULE

## 4.0 Utangulizi

Sura ya tatu imeeleza taswira zinazotumiwa kuwasawiri wahusika wa kiume katika riwaya teule. Taswira hizo ni hasi na chanya ambazo zimetofautiana baina ya mwandishi mmoja na mwingine kulingana na lengo la mtunzi. Katika sura hii tumejadili mitazamo inayoibuliwa na wahusika wa kiume. Mitazamo hiyo huibuliwa na wahusika kutokana na matendo yao kwa namna walivyochorwa na mwandishi. Wahusika ni viumbe wa sanaa ambao hutumiwa katika kazi ya fasihi kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kulingana na msanii alivyowasawiri na kuwatumia wahusika hao kama njia ya kuuwasilishia ujumbe lengwa kwa wasomaji ama watazamaji wake. Wahusika huweza kuwa wanyama, binadamu, mazimwi na majitu, wahusika vitu kama mawe, miti nk. Kwa upande mwingine, mtazamo ni hali ya mwandishi kuyaona mambo yanayotendeka na yanavyotendeka katika jamii husika ambapo inaweza kuwa vibaya au vizuri.

Katika kuzitazama kazi za fasihi wasanii huwa na mitazamo ya aina mbili ambayo ni; Mtazamo wa kidhanifu/kidini ambao huuchukulia ulimwengu kama kitu kinachobadilika kulingana na matakwa ya Mungu. Msanii wa mtazamo huu, huuwasilisha kupitia namna anavyotunga kazi zake. Mtazamo wa pili ni ule wa kiyakinifu ambao unautazama ulimwengu au mazingira yanayomzunguka binadamu kisayansi. Msanii wa aina hii huona ulimwengu

ni kitu kinachobadilika kufuatana na masuala ya kihistoria. Mtazamo wa aina hii humfanya msanii kuutazama ulimwengu kama kitu cha kweli na kilicho katika uhalisi wa mambo yaliyopo (Wamitila, 2008). Uhusika ni namna msanii anavyosawiri wahusika na kuwapa sura fulani itakayowawezesha kubeba dhamira, migogoro, ujumbe na kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira**.**

### 4.1 Mtazamo katika *Kipimo Cha Mizani*

Katika muktadha wa kidhanifu mhusika wa kiume anajiona kuwa kimaendeleo kama anavyodhihirika katika riwaya ya *Kipimo cha Mizani* iliyoandikwa na Zainabu Burhani Usawiri wa wahusika kimaendeleo; Mwandishi wa riwaya hii amewasawiri wahusika kadhaa wa kiume kuwa wanajichukulia kama wachapakazi na watunzaji wazuri wa familia, wanaotumia muda wao mwingi na akili zao zote kufanya kazi kwa bidii kuhakikisha wanainuka kiuchumi na familia zao zinapata mahitaji yote muhimu kwa wakati.

Katika riwaya hii, tunamuona Amini ambaye mwanzo alikuwa akifanya kazi ya kuajiriwa anaweza kufanya kazi kwa bidii na kutunza kiasi cha mshahara aliokuwa anaupata mpaka alipoona amepata mtaji wa kutosha kufungua kiwanda akaacha kazi na kufungua kiwanda chake mwenyewe. Baada ya kufungua kuwanda hicho anaendelea kufanya kazi kwa bidii na familia yake inazidi kufanikiwa kimaisha na kufungua duka kubwa, kununua gari, kununua mashamba na kupeleka watoto shuleni. Amini alikuwa mchapakazi na

aliyejali sana familia yake kwani mpaka siku mauti inamkuta alitoka kuwachukua watoto shuleni akawarudisha nyumbani na kuondoka kwenda shambani yote hayo ikiwa kuhakikisha anaandaa mazingira bora kwa familia yake ya sasa na baadae.

Hata jamii nzima ilimtambua Amini kwa msaada wake katika jamii. Kwa mfano, alitoa msaada wa baisikeli kwa Rajabu ili kumrahisishia maisha. Mwandishi anaeleza:

> Siku ile, baada ya kurejea kazini, Amini alifululiza moja kwa moja mpaka dukani, akanunuaa baisikeli na kuiangalia kuwa ina vifaa vyote vinavyohitajika. Akaichukua moja kwa moja mpaka nyumbani kwa kwa Bi Riziki. Rajabu hakuweza kusadiki, Amini alipomwuliza ikiwa ataweza kuiendesha. Alisema,” Ninajua kuendesha baiskeli. Ninaweza kuiendesha vizuri.” (Uk. 41).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao; ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya tabia hiyo. Hii inajidhihirisha katika hoja hii kwa maana Amini alilazimika kumsaidia Rajabu ili aweze kujitegemea kwa maana mielekeo ya jamii yao, ni lazima kijana wa kiume akifikia balehe aanze kujitegemea na kuisaidia familia yake.

Tunawaona watu kama Amini pia katika jamii zetu leo ambao wanafanya kazi kwa hali na mali kuhakikisha wanasonga mbele kimaisha wao na familia zao wengine hufanikiwa kufikia malengo yao lakini wengine hushindwa kama Amini kutokana na sababu au vikwazo mbalimbali. Amini alipambana kwa

kila njia hadi akafungua kiwanda. Alisikiliza sana ushauri katika kukamilisha mipango yake ya kufungua kiwanda. Kwa mfano:

> Amini alifanya jitihada kubwa mpaka akapata pahala ambapo aliona panamfaa kwa kuanzisha kiwanda chake. Alikodi banda lililokuwa tupu na ambalo mwenyewe alivyokuwa halitumii, alimkodisha kwa bei nafuu. Sasa alikuwa na tatizo la nani wa kumwajiri kuangalia kazi ile wakati yeye yupo kazini? Halima alimshauri,"unaonaje ukimtafuta mzee Hasani?"………………. "Nitakwenda kumtafuta, nimsikilize. Nitafurahi sana akikubali, maana sitokuwa na wahaka nikijua yupo pale kwenye kiwanda." (Uk. 35).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kusaidia wake zao na wanawake wengine katika jamii kujiendeleza kielimu na kikazi. Amini alimthamini sana mke wake na kumshirikisha kila jambo alilotaka kufanya. Alimsaidia kufanya kazi za nyumbani hasa ulezi wa watoto. Ndio maana waliweza kupata maendeleo kwa haraka sababu ya kusaidiana katika mamuzi na mambo mengine katika familia. Jacobus, (1986) anaeleza kuwa uchangamani wa kazi za wanawake na wanaume umeondoa utengano na dharau na kuleta kuthaminiana katika ngazi ya familia na jamii kwa ujumla. Imeweza kumulika wale wanaonyanyaswa na kutengwa na jamii ili kufanya mabadiliko na kuleta maendeleo.

Katika nadharia ya uhalisia, mhimili usemao; uyakinifu: kuelezea mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Amini alikuwa mpambanaji sana ila hali halisi ya mazingira ya kazi pamoja na ndugu yake Umari alimwingilia sana katika mipango yake na kumvuruga kiasi cha kumcheleweshа na kumkwamisha kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, Umari aliamini kuwa katika

shida zake hakuna wa kumsaidia zaidi ya kaka yake Amini. Umari alikuwa wa kuomba omba msaada hasa alipokuwa akiishiwa pesa, kimbilio lilikuwa ni kwa kaka yake akiamini kuwa hawezi kumnyima. Umari maisha ya kuomba kwake ilikuwa ni kawaida maana matumizi yake yalikuwa makubwa kuliko kipato chake. Mfano, Umari alimwambia Amini:

> "Sikiliza Amini, nimekuja maana ninahitaji msaada kidogo. Msaada wa namna gani?" Aliuliza Amini ingawa akili yake ilikwishamhadharisha kuwa lazima ni wa kifedha. "Ah, ninahitaji pesa kidogo. Nimeona labda utaweza kunisaidia, au hata kunikopesha." (Uk. 43).

Utegemezi na kutojiamini kwa baadhi ya wanajamii kama Umari kunawafanya wasipige hatua kimaendeleo na badala yake wanaishi kwa unyonge katika yale wanayoyapanga kuwakwamua. Hii inaelezwa na Herman, (2007) anapofafanua dhana ya matabaka kuwa inatengeneza watu wasiojiamini kwa tabaka linaloonekana ni la juu na kuishi kwa kuwa wategemezi.

Kuangaza madhila ya wanyonge na kutetea maslahi yao; pia katika riwaya hii tunaona wahusika wa kiume wakitazamwa kama wenye huruma na upendo wenye moyo wa kujitoa kwa hali na mali kuwasaidia watu wengine wakati mwingine hata wasiokuwa ndugu zao au watu wao wa karibu. Mfano kijana Bakari alivyowasaidia watoto wa Amini na Halima tangu siku ya kwanza alipomuona Ali akirandaranda peke yake mitaani alimchukua katika pikipiki yake na kuacha duka lake akaanza kuzunguka naye kumtafuta mzee Hassani japo jitihada hizo hazikuzaa matunda katika siku ya kwanza.

Bakari huyu huyu ndiye aliyewachukua Ali na ndugu zake baada ya kufukuzwa kwa Umari akaanza kuishi na watoto hao mpaka alipoona ni vema kuwapeleka kwa mama aliyemlea ili wakaweze kupata huduma bora zaidi wakati huohuo aliendelea kumtafuta mzee Hassani hadi akampata. Walishirikiana na mzee Hassani na Bi. Rehema kuwalea watoto hawa na kuwasomesha huku wakiendelea kumtafuta mama yao mpaka walipofanikiwa kumpata. Bakari na mzee Hassani ni waungwana ambao wanafaa kuwa mfano wa kuigwa katika jamii zetu kwani wameonesha upendo wa dhati kwa watoto hawa bila kujali watanufaika nini kupitia watoto hawa siku zijazo hali ambayo ni tofauti katika jamii za siku hizi watu wamekuwa wakithamini zaidi maslahi binafsi bila kujali utu jambo ambalo sii sahihi.

Bakari alifanya maamuzi magumu kulingana wa wakati mgumu waliokuwa nao akiana Ali na wadogo zake kwa kukaa nao kwake katika chumba chake kwa maana hakuwa na namna maana Maryamu aliwafukuza.Hivi ndivyo mwandishi anavyowatazama wahusika wa kiume kama wenye upendo na huruma kwa watoto wadogo akina Ali na wadogo zake. Hata hivyo Ali alionyesha kujitambua mapema sana katika umri mdogo wa miaka 9 ambapo alijua yeye ndo wa kupambana ili aweze kuwatoa wadogo zake kwa Maryamu ambapo waliishi kwa kunyanyasika. Mwandishi anaeleza:

> Ali, ambaye ndiye aliyekuwa mkubwa, alianza kuelewa kidogo hali yao ilivyo, kwani sasa alikwishafikia miaka tisa. Kwake hali ilikuwa tofauti. Yeye alikuwa na hofu na wasiwasi, kwani hakujua anakwenda wapi. Alimfikiria mzee Hasani na Bi. Riziki, hakuwajua walipo, wala hakujua njia ya kuendea kwao..……….. Alikumbuka pale aliposimama karibu na barabara, na yule rafiki,

> Bakari, aliyemsaidia siku ile na kumpakia juu ya pikipiki. Sasa alipata nguvu kidogo,akaona atajaribu kwenda pale dukani. Aliwaambia ndugu zake, “Kazanani.” (Uk. 155).

Hii inaakisi nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili usemao; ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya tabia hiyo. Ali alifunzwa na wazai wake namna ya kuwajibika katika kazi mbalimbali na ndio maana alimudu kufanya kazi ngumu. Hata Bakari alifunzwa kuwa mkarimu kwa wahitaji na ndio maana aliweza kufanya kila jitihada za kuwasaidia Ali na wadogo zake walipofika dukani kwake. Halima na Amini waliwalea watoto wao wa kiume katika misingi ya kuanza kujitegema mapema na ndio maana Ali aliweza kufanya kazi za ndani bila kujali umri wake. Pamoja na kwamba Ali hakuwa na uhakika kama atapakumbuka anakoelekea ila alijipa ujasiri mpaka akafika kwa Bakari ambako alipata msaada. Malezi ni jambo jema linalowapa mafunzo watoto ambayo hujidhihirisha wawapo wakubwa. Miller, (2011) anaeleza katika nadharia za maendeleo ya kisaikolojia kuwa binadamu anavyolelewa matokeo yake huonekana kadri anavyokua.

Kutokana na madhila yaliyokuwepo juu ya Halima, alitia huruma na watu wengi waliguswa na kutoweka kwake na kuwaacha wanae kwa muda mrefu wakilelewa na watu wengine ilhali baba yao kafariki. Sefu alikuwa mmojawapo na walioguswa na kujiona ana uwezo wa kufanya uchunguzi na kujua Halima alipo ili waende kumwona. Sefu alijiona msemakweli na mwenye moyo kwa maana hiyo kazi ya uchunguzi aliifanya bila msukumo

wowote isipokuwa upendo wake na huruma aliyokuwa nayo juu ya Halima na wanawe. Mwandishi anaeleza:

> alitoa ruhusa kwa yule mchunguzi aende akaonane naye, ofisini saa za asubuhi. Sefu alikuwa kila siku huenda pale kusikiliza habari zozote, na alifurahi alipopata maagizo yale kutokana na Salama, alikwenda kuonana na kama alivyotakiwa. alimtaka amwelezee kwanini alimtafuta mgonjwa yule, na alitumwa na nani. Sefu alieleza upande wake, na alisema pia kuwa watu hao walikuwa wakimtafuta siku nyingi bibi huyo, lakini hawakumjua yuko wapi. "Ninafikiri wakijua tu, watataka kuja kumtembelea, ikiwa mtawapa ruhusa." alifikiri, tena akasema, "Sasa hivi umekwishapata ulilolijia. Umejua kuwa huyo mtu unayemtafuta yupo hapa. Ama kuhusu ziara! Hayo tutayafikiria baadaye, labda wakija watu hao kutaka ruhusa wenyewe.." (Uk. 212).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Sefu alifunzwa kuwa mchapakazi na mtu wa kujitoa na kuwa msaada kwa wenye shida. Anajitoa kuhakikisha Halima anajulikana alipo na anafanya kwa moyo.

Katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao; usadikifu; yale yanayoibuliwa katika jamii yenyewe yanasadikiwa na wasomi. Katika hoja hii, Sefu aliaminiwa na familia ya akina Bi Riziki na Selemani kwa utafiti alioufanya ili kujua Halima alipo maana alipotea muda mrefu wakawa wanahisi pengine alishakufa kwa maana asingekaa miaka bila kuja kuwaona wanae. Sefu aliporejesha majibu ya uchunguzi wake waliyaamini na kwenda huko hospitali wakaonana na Halima. Watu huwa na hofu binadamu mwenzao anapopotea na wasijue alipo. Mlacha na Madumulla, (1991) wanaeleza kuwa, riwaya ya Kiswahili, imepiga hatua na kuwa na maendeleo katika kuwasawiri

wahusika mbalimbali. Wahusika hao wanaweza kuwa wa kike au wa kiume pamoja na viumbe wengine wenye uhai na wasiokuwa na uhai ili kufikisha ujumbe alioulenga mtunzi kwa hadhira.

Katika madhila aliyokuwa nayo mzee Hasani baada ya kukosewa adabu na Umari, ilikuwa vigumu kuihimili ile hali isipokuwa Amini alijiona kuwa ana uwezo wa kumtia moyo mzee Hasani na kumfanya ajisikie vizuri na kuiona ni hali ya kawaida kwa kumdharau Umari na tabia zake za ajabu kwa kupenda kufuja mali za wenzake na kuonyesha dharau kwa watu waliomzidi umri. Umari alimsemea vibaya mzee Hasani alipomgomea kuchukua vitu dukani kama alivyotaka Umari. Mwandishi anaeleza:

> Alipokuja Amini siku ile, alimkuta mzee Hasani bado ameinamia kitabu chake. Aliposema naye, Amini alielewa kwa sauti yake, kuwa amekereka. Akamwuliza: “Je, vipi leo mzee Hasani, huyu kijana amekukera nini?” “La si yeye. Ni yule ndugu yako!” Mzee Hasani kwa hasira yake, hata hakutaka kulitaja jina lake. “Umari?” aliuliza Amini. “Kwani alikuja hapa?” Alikuja. Tena alitaka kuchukua vitu, lakini sikumuacha kuchukua, sio kwa sababu yoyote ila alisema na mimi kwa ujeuri tu.” “Ah, mzee Hasani. Wewe unamjua Umari tokea zamani. Mchukulie tu.” “Lakini hakuwa hivi kabla!” “Watu huenda na kubadilika,”alijibu Amini. “Lakini usikasirike bure. Una haki na wewe ya kumtolea ukali na kumrudi, sawasawa na mzee wake.” (Uk. 68-69).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao; mwanafunzi si mpokezi tulivu wa habari, utambuzi mazingira na tabia vinaathiriana katika upataji wa habari wa mwanafunzi. Mzee Hasani alifunzwa kuishi na watu wa tabia zote mbaya na nzuri kuweza kukabiliana nao. Umari alikuwa mkorofi tangu enzi za uhai wa wazazi wake na ndio maana baada ya kuwa mkubwa akawa

hawezi kumheshimu kaka yake Amini pamoja na watu wa umri wa kumzaa kama mzee Hasani. Matendo ya Umari ukubwani yanaakisi methali isemayo; mtoto umleavyo ndivyo akuavyo. Schaik, (2011) anaeleza kuwa ujifunzaji katika jamii lazima ufanyiwe tathmini za kitamaduni maana mtu anavyolelewa ndivyo anavyotakiwa kukua kwa maana makuzi yanahusisha ukuaji wa akili.

Usawiri wa binadamu kiyakinifu; Pia tumewaona wahusika ambao wanapenda maisha ya anasa bila kufanya kazi kwa bidii kitu kinachowasababishia kuuza na kutumia vibaya mali zao kisha kuwa na tamaa ya kuchukua vitu visivyo vyao. Hii inasababisha uonevu pale muhusika anapotetea haki yake isichukuliwe na huyu anayedhulumu kutokana na uwezo aliokuwa nao ama wa kifedha ama kielimu anatumia mabavu kuhakikisha anafanikiwa kudhulumu mali ile. Mfano mzuri ni muhusika Umari aliyependa maisha ya anasa yeye na familia yake bila kutia bidii kufanya kazi. Walikuwa wakiuza mali za urithi na kutumia kipato chao kwa anasa kupanga nyumba za kifahari, kununua magari ya kifahari n.k bila kujali maisha yao ya baadae. Umari alimtolea kaka yake Amini maneno makali akitaka wauze mali yao yaani shamba ili apate pesa. Hii ni baada ya kufuja mali zote alizokuwa nazo. Mwandishi anaeleza:

> Ingawa alijaribu kumfahamisha Umari hayo, lakini yeye jawabu lake lilikuwa, "Sasa umekuwa mwenye mali. Una duka na bidhaa. Huwezi kutufikiria sisi wengine tusiokuwa na kitu." Maneno hayo yalimkera pia Amini, kwani kwanza yalikuwa si kweli. Umari alikuwa na kazi na mshahara wa kumtosha. Pia mkewenanafanya kazi.

> Hawakuwa wahitaji hata kidogo, ila kwa sababu ya israfu yao tu. (Uk. 69-70).

Tumeona namna Umari alivyonyanyasa na kumuonea Halima kwa kumnyang'anya wanae, duka, nyumba na kiwanda na kama haitoshi akamsingizia wenda wazimu Halima akachukuliwa na kupelekwa hosipitali ya vichaa huku nyuma Umari anakodi mawakili ili kumuandika yeye ndiye mmiliki halali wa mali za kaka yake. Hii ilitokana na uchu wa mali ya kaka yake aliokuwa nao Umari. Alifanya njama za kuimiliki mali na akafanikiwa baada ya kumnyanyasa shemeji yake Halima. Mwandishi anaeleza:

> Umari alizipokea karatasi, akaziangalia. Tena alitoka kwenda kufanya miswada ya karatasi zile. Sasa Umari alijiona ana nguvu. Amekwishapata kila kitu. Ile mali ya Amini – aliyokuwa akiitamani – sasa itakuwa mikononi mwake. Kwa wakati ule uliopita, mara tu baada ya kifo cha Amini, Umari alihuzunika sana, na hasa alijiwa na imani, akafikiria kuwa ni juu yake kuwaangalia watoto wa ndugu yake. (Uk. 93).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume. Umari anapaswa kubadilika na kuwa mwanaume mpya kwa kuacha tabia mbaya za kutowaheshimu wakubwa, roho ya tamaa, dhuluma na kuwa na tabia nzuri.

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao; ujifunzaji unahusu kuchunguza kupata habari kutokana na ule uchunguzi na kuunda maazimio kuhusu utendakazi wa tabia hiyo. Matendo hasi yaliyofanywa na Umari kwa Halima yalijikita katika mielekeo ya kijamii kuwa mwenye jukumu la kuitunza familia ni mwanaume. Ndio maana Umari alitumia nafasi ya uasi wa mtazamo huu kukamilisha malengo yake ya kujimilikisha mali ya kaka yake

ilhali mkewe na wa watoto wa marehemu wapo.Hata hivyo wakati Umari alipoanza njama hizo za kumpokonya Halima mali zake, aliona ni bora amnyang'anye watoto wake kwanza ndipo michakato mingine iendelee. Kwa vile isingekuwa rahisi kukubaliwa na Halima kuwachukua wanawe, alienda shuleni huko ili awawahi kabla dereva anayewafuata hajawachukua. Umari alionesha ukali usiokuwa na sababu kwa dereva yule mara alipomuuliza kuwa kwanini anawachukua watoto ilhali naye katumwa kuwachukua. Dereva alimuuliza Umari ili apate uhakika kama kweli yeye ni baba mdogo wa watoto wale na kwanini waende wawili kuwachukua watoto wale kwa wakati mmoja. Mwandishi anaeleza:

> Yule mwenye gari aliwaona. Akatoka mbio kumfuatia, akamwambia, "Vipi bwana? Hawa watoto mimi ndiye ninayewachukua kila siku. Wewe nani? Na unawapeleka wapi?" Umari alimjibu kwa ukali, "Mimi ni baba yao mdogo. Waulize wenyewe watakwambia. Nitawachukua nyumbani. Na wewe chukua bahasha hii, umpelekee mama yao." Dereva alimuuliza Ali: "Kweli, huyu ni baba mdogo kwenu?" Ali aliitikia. Dereva yule alirudi matao ya chini. Akanyamaza na kupokea ile bahasha aliyopewa. Akasimama akiwaangalia mpaka walipoondoka. Alihifadhi nambari ya gari, akaona isije baadae ikahitajiwa. Tena alitia moto gari yake na kuondoka. (Uk. 94).

Nadharia mpya katika mhimili usemao: kutoonesha udikteta katika familia zao na jamii inayowazunguka. Umari anapaswa kubadilika kuwa mwanaume mpya asiyetumia ubabe kuwadhulumu watu hasa mjane na wanae.

Kiuhalisia mhusika huyu amewakilisha kundi kubwa la jamii yetu leo, watu wanapenda sana kuishi maisha ya starehe yenye ufahari na gharama kubwa bila kufanya kazi kwa bidii. Hii ndio sababu kumekuwa na dhuluma na maovu

mengi ya kutisha katika jamii na chanzo kikubwa ni tamaa hivyo ni vema watu wafanye kazi kwa bidii na kuridhika na vipato vyao ili kuepusha hayo. Nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao; mshikamano unatusisitiza kushikamana katika kuziondoa tabia kama za Umari katika jamii ili kuweze kuwa na maendeleo ambayo kila mtu anayapata kwa jasho lake. Mtu yeyote anapopitia changamoto ndipo anapata njia ya kuzitatua kwa kushikamana na wenzake. Mboya, (1996) anaeleza kuwa mwanamke anapitia changamoto nyingi zinazosababishwa na mwanaume na anapendekeza njia za kujitatua nyingi ikiwemo njia ya mshikamano na kukubali mabadiliko.

Usawiri wa matukio kihistoria; Katika riwaya hii pia tumewaona wahusika wa kiume wakiendeleza uonevu na unyanyasaji kwa wanawake, wakimuona mwanamke kama mtu dhaifu asiyekuwa na haki yoyote kama inavyoonekana tangu zamani katika jamii zetu. Hii inapelekea baadhi ya wanawake katika jamii kudhulumiwa haki zao za msingi. Mfano; Juma ambaye alikuwa akiamuru Halima achomwe sindano na kufungwa kamba mikono na miguu kutokana na rushwa aliyopewa na Umari huku anafahamu fika kwamba Halima hakuwa mgonjwa wa wazimu.

Kupitia riwaya hii mwandishi anawatazama wafanya kazi mbalimbali, wanaokubali kukiuka miiko na taratibu zinazowaongoza katika kazi zao na kutenda mambo ambayo ni kinyume na taaluma zao ili kujipatia maslahi binafsi bila kujali matatizo au maumivu wanayoyasababisha kwa wale wanaowatendea. Mwandishi anawataka watu kama hawa kubadilika na kufata

kaida zinazoongoza taaluma zao na pia kujali utu na sio kitu. Kwa mfano Juma anakuwa mkali kazini kwa Salama pamoja na wafanyakazi wengine kwa ajili ya kutetea uovu wake wa kuwaonea na kuwanyanyasa wagonjwa wanawake kama alivyofanya kwa Halima. Mwandishi anaeleza:

> Baada ya muda, alinyanyua uso alioukunja, na kumwangalia. Akamuuliza, "Ehe! Kuna nini?" Salama alikohoa ili aweze kutoa sauti ambayo ghafula ilimpotea, akasema: "Nimekuja kwasababu ya yule mgonjwa aliyemo chumba nambari 75." "Ana nini?" akauliza . "Hana neon", alijibu Salama. Tena alimeza mate na kuendelea, "Nimetafuta jalada lake lakini sijaliona."Na wewe unashughulishwa na nini? Huna kazi ya kutosha?" akampokea Salama.…………….. "Sikiliza! Mimi ndiye hapa, sio wewe! Nitakapohitajia jalada la mgonjwa nitakuarifu." "Usipoteze wakati wangu. Endelea na kazi yako." (Uk. 8-9).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kuwaona wanawake kama viumbe sawa na wanaume kwa kuwaheshimu na kuwapenda katika kila nyanja wanazokuwepo. Juma na Umari wanapaswa kubadilika na kuwa wanaume wapya kwa kuwathamini wanawake kuwa wanaweza kufanya jambo lolote kama mwanaume. Umari anapaswa kuwa mwanaume mpya kuacha ugandamizaji wa haki kwa kutumia rushwa na Juma kuacha kupokea rushwa na kufuata maadili ya kazi yake. Wanatumia ubaya wao kuziminya haki za Halima na wanae. Muleka, (2000) anaeleza kuwa katika jamii nyingi, mwanamke anachorwa kama wa kukaa jikoni na kutawaliwa na mwanaume. Anaeleza kuwa ugandamizwaji anaoupata mwanamke katika jamii unafanywa na mwanaume hivyo mwanaume anapaswa kubadilika na kuacha hayo yanayoleta utabaka.

Katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao; itumie sajili ambazo ni za kawaida. Ni kweli kuwa watu wasiotenda haki na kukosa utu hawawezi kufuata taratibu zinazotakiwa. Ni lazima wataishi katika jamii kwa kuonea wenzao na kuwaumiza ilimradi wafikie malengo yao. Katika kuondoa tabia kama hizi ni muhimu kutumia taratibu za kawaida ili kuwabadilisha bila kuleta madhara katika kazi wala kwa wafanyakazi wengine.

Hata hivyo mwanaume anakuwa mwenye maamuzi bila kumshirikisha mkewe. Mwanaume anajiona kuwa yeye anapaswa kufanya maamuzi kwanza halafu mwanamke anapewa tu taarifa. Kwa mfano, Amini anapanga kuacha kazi na kuacha mipango ya nini atafanya bila kumshirikisha Halima. Halima aliambiwa baadae hakukubaliana naye na ndipo alimshauri kumshirikisha rafiki yake Selemani ambaye alimshauri kuwa ajipange kwanza kuimarisha hiyo biashara ya kiwanda na ndipo aache kazi. Hata hivyo suala la wanaume kutowashirikisha wanawake ni la kihistoria katika jamii nyingi za Kiafrika. Mwandishi anaeleza:

> Baada ya kula kimya kwa muda, Amini ghafula alisema; "Unajua! Nimefikiria kuacha kazi." Halima alishtuka akauliza, "Kwanini? Na umeamua ghafula tu?" "La si ghafula. Nilikuwa ninayafikiria siku nyingi. Ninaona huko kazini mambo hayaendi vizuri. Kwakweli, mimi na huyo mkubwa wangu hatusikilizani vizuri." (Uk. 27).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume. Amini alibadilika baada ya kumwambia mkewe mipango yake ya kutaka kuacha kazi. Halima alishtuka sana na hakukubaliana naye. Amini alikubaliana na ushauri wa Halima na kuweka mipango sawa

ndipo akaacha kazi. Amini ni mwanaume mpya aliyeacha udikteta wa maamuzi.

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao; ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Amini alifunzwa kushirikiana na watu wote bila kubagua jinsia. Alipoenda kinyume na ndipo alijirekebisha na kufanya maamuzi kutokana na ushauri wa Halima. Jamii inahitaji mabadiliko katika masuala ya kiuana. Amini anayetenda haya ya kutomshirikisha mkewe ni mtu anayejua kuijali familia yake kwa kuipa mahitaji ya kila siku ila analegea katika masuala ya kiuana. Anapaswa kuithamini nafasi ya mkewe katika yale ayafanyayo maana ni kwa faida ya familia nzima. Mtunzi wa kazi hii amesawiri dhamira hizi na wahusika hawa kwa lengo la kuipa elimu jamii kuhusu masuala ya kiuana yatakayopelekea kuleta usawa miongoni mwa wanajamii bila kubagua jinsi zao. Mohammed, (2006) anaeleza kuwa riwaya ya Shaban Robert, Siku ya Watenzi wote imejadili mambo mengi yalizomo katika jamii na kufafanua kuwa mambo mengi yanayoleta migogoro katika jamii ni namna jamii inavyowatazama wanaume. Inafikia wakati jamii inawatazama kama watu wasioshindwa jambo. Suala hili huwafanya baadhi ya wanaume kuishi bila raha wakihofia kuchekwa na kudharauliwa watakaposhindwa jambo lolote. Hayo ndo mambo yanayopaswa kubadilishwa ili kuleta maendeleo.

## 4.2 Mtazamo Katika Riwaya ya *Hiba ya Wivu*

Katika riwaya hii pia tunaona mtazamo wa kidhanifu na kiyakinifu unaodhihirishwa na wahusika wa kiume. Katika mtazamo wa kidhanifu usawiri wa wahusika kimaendeleo ambapo wahusika kama Ihucha na marafiki zake walikuwa wachapakazi kwa kufanya biashara ya saa. Ray naye alifanya biashara ya kuendesha teksi ili kujipatia kipato cha kuendeshea maisha. Katika kutafuta maendeleo ya kazi ustaarabu unadhihirishwa na wahusika wa kiume. Kwa mfano, dereva wa teksi alionekana mwenye kujali na alitumia lugha ya Hekima kumjuza Farida kuwa gari limepata tatizo ingawa Farida alikuwa mkali. Hata hivyo dereva aliendelea kujiuliza kwanini tena Farida hakutaka kuelekea Kinondoni alikokuwa akienda kabla ya gari kuharibika. Mwandishi anaeleza:

> "Nasikitika sana dada. Gari langu ndio limeshakorofisha! Itanichukua muda kulishughulikia ili liweze kutembea tena. Ningekushauri utafute mbinu nyingine kwani hapa tulipo hatuko mbali na Mtaa wa Swahili." Alieleza dreva huyo kwa sauti ya amsikitiko japo hakujua kilichokuwa kinamkimbiza dada yule. (Uk. 6).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao; ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Wanaume wanafunzwa kuwa wachapakazi na kuzihudumia familia zao. Mwanaume anapooa anapaswa kumlinda mkewe na familia nzima. Ihucha alifundishwa kumpenda mkewe kwa dhati. Yeye kama mwanaume ampende mkewe na kumjali. Jamii inaamini kuwa mwanaume akimpenda sana mkewe na kumjali hawezi kumsaliti kimapenzi. Malezi haya ndiyo yalimsukuma Ihucha kutoa pesa alizoambiwa na wateka nyara ili aweze

kumwokoa mkewe licha ya kwamba elfu hamsini ilikuwa pesa nyingi kipindi hicho. Farida alilewa upendo wa mumewe ndio maana alikuwa na wivu kupita kiasi hadi ukamtia matatani hadi akaangukia mikononi mwa Ray na kuleta msukosuko mkubwa kwa mumewe na familia yake kwa ujumla. Mbatiah, (1998) anaeleza kuhusu dhamira ya malezi ya watoto katika jamii kuwa ndiyo dira yao katika utu uzima. Kwahiyo Ihucha, Farida na Ray walivyo, ni muakiso wa malezi waliyoyapata.

Vilevile katika masuala ya kimaendeleo, mwanaume anaonekana kuwa mpole katika maeneo fulani ili asipoteze pesa nyingi. Hii inadhihirishwa na Ihucha akimbembeleza mteka nyara ampunguzie kiasi cha pesa isiwe elfu hamsini bali pungufu ingawa mteka nyara alikataa ikabidi tu Ihucha azitoe ili kuokoa uhai wa mkewe. Ihucha anakuwa msikivu anaposhauriwa na Feruzi kuhusu kwenda na ulinzi apelekapo pesa bonde la mkwajuni ili kuhakikisha usalama wake maana zile pesa anazipeleka kwa amri ya wateka nyara. Mwandishi anaeleza:

> “Loh! Pole sana. La muhimu ni kumwokoa huyo binti kwanza. Lakini angalia sana usalama wqako. Ningekushauri utafute ulinzi, usiende peke yako kupeleka hizo pesa.” “Ni sawa Bastola ninayo, na unavyonishauri, inabidi niwe na mtu au watu wa kufuatana nawe wawe kama walinzi. Lakini sasa hao watu gani watakaokubali watakaokubali kuwa walinzi wangu? Polisi sithubutu kuwaambia, kwani nikifuatana nao inaweza kuzuka vita pindi majambazi hayo yatakapotambua kuwa nimetoa ripoto Polisi.” (Uk. 24-25).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Ihucha alifunzwa

kumpenda mkewe na kumjali na ndio maana anatii wateka nyara wakisemacho ili mkewe asidhurike.

Katika nadharia ya uhalisia kwenye mhimili usemao; uyakinifu; kuelezea mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Ihucha alitoa elfu hamsini kwa wateka nyara na si kwamba haikuwa na kazi. Alienda kuichukua benki ili awahi muda alioambiwa na wateka nyara ili kumwachia mkewe Farida. Ukweli ni kuwa Ihucha aliumizwa zaidi na kutoweka kwa mkewe na ndio maana aliona elfu hamsini si kitu kwa maana hakujua mkewe katekwa vipi wakati alimuacha nyumbani akiwa na wifi yake aitwaye Aisha. Ugumu wa upatikanaji pesa ndio ulimfanya Ihucha aamini kuwa ni kweli wateka nyara watamwachia mkewe wakipata kitita cha pesa walizozihitaji. Hata hivyo Ihucha alikuwa na imani kuwa mkewe atakuwa salama. Hii ni tabia inayotokana na kumbukumbu zinazojengwa kisaikolojia. Burgess, (1966) anasema kuwa mambo yatuzungukayo katika ubongo yanaundwa na saikolojia ya mambo yanayotuzunguka katika jamii zetu. Kwahiyo, hali iliyompata Ihucha kutomkuta mkewe nyumbani inamfanya atazamwe kuwa ni mpole na mwenye kujali kwa maana aliathirika kisaikolojia kutokana na imani aliyokuwa nayo kwa mkewe.

Vile vile, kidhanifu katika hoja ya kuangaza madhila ya wanyonge na maslahi yao, tunaona kuwa wahusika wa kiume wanatakiana mema katika mambo yanayowakabili. Ihucha alikuwa akiangaika sana katika biashara yake baada ya kutetereka ila mzee Kibwana anamhakikishia kuwa anaenda kufanikiwa

katika biashara yake anayoendelea kuifanya ya kuuza saa. Mwandishi anaeleza:

> Mzee Kibwana ambaye alionekana mkongwe wa mambo ya biashara za saa, alivuta suruali yake juu ili ikae vema pahala pake halafu akamwangalia Ihucha na kusema: "Tena safari hii Bwana mdogo ukishauza ile mali,utaibuka na donge nono! Hapo utamnunulia binti yangu benzi, naye ajisikie kuwa kapata mume, sio lofa!" (Uk. 3-4).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili usemao; ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeoa ya hiyo tabia. Wanaume wanafunzwa kuwatia moyo wenzao ili wasikate tamaa katika utafutaji wao. Mzee Kibwana anampa moyo Ihucha kuwa atafanikiwa katika biashara yake kwa maana anajua asipofanikiwa na kuwa na mali nyingi pamoja na pesa za kutosha, atadhaurilwa na mkewe. Majukumu waliyonayo wanaume katika jamii ni pamoja na kuwatunza wake zao kwa kuwapa mahitaji mbalimbali. Kulingana na mielekeo iliyopo, mwanaume anaheshimika katika familia na jamii kwa ujumla anapokuwa na mali pamoja na pesa nyingi zitakazomtambulisha kila anapokuwa.

Katika kipengele hiki cha kidhanifu Ihucha alionesha mapenzi ya kweli kwa mkewe katika madhila ya utafutaji. Alionesha kuwa licha ya kuwa na uhitaji wa pesa, anapaswa kuwa karibu na mkewe Farida ambaye walikuwa wameoana hivi karibuni. Ihucha alitafuta maslahi yake na familia yake ila bado alihitaji kuonesha mapenzi kwa mkewe. Mwandishi anaeleza:

> Alikuwa katika hali ya furaha, glasi ya bia mkononi, mguu mmoja juu ya mwingine, hana wasiwasi. Pamoja na kuwa katika hali hiyo, hakukosa kumkumbuka mkewe nyumbani. Alitamani sana kurudi

> nyumbani mapema iwezekanavyo akakae na mke wake mpenzi ambaye walioana mwaka mmoja tu uliopita. (Uk. 1).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii, mhimili usemao: ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia.Kiuana, uchanya na uhasi wa mhusika unategemea jinsi mahusiano ya binadamu yamejengwa kiuana na elimu ya baadae ya wanaohusika. Huu ni mhimili mmojawapo wa nadharia ya uana ambao unajidhihirisha katika hoja hii kwa maana hii hali aliyoipata Ihucha ilitegemea mahusiano mazuri aliyokuwa na mkewe. Ihucha anakatiza starehe zake ili aende kuwa karibu na mkewe. Uchanya wa mahusiano yao uliwafanya wazidi kupendana na kumfanya kila mmoja awe na hamu ya kuwa na mwenzie muda wote. Ihucha na mkewe wanahitaji kubadilika maana katika maisha kuna mambo kuuwa tofauti na matarajio. Mke na mume wanapendana ila si muda wote wanaweza kuwa pamoja kwa maana kuna dharura kama aliyoipata Ihucha kwenda kuhudhuria kikao cha biashara. Kuna masuala ya kazi na mambo mengine ya kijamii yanayowatenganisha kwa muda hivyo jambo la msingi ni mawasiliano pamoja na uvumilivu ili kuyafanya mahusiano yaendelee kustawi. Mambo yanapokuwa tofauti ni lazima kubadilika na kujipa matumaini. Wegesa, (1996) anaeleza kuhusu ukandamizwaji wa wanawake katika jamii kuwa ni jambo linaloweza kubadilika. Jambo lolote linapobadilika kinyuma na matarajio ya jamii, ni muhimu kutoa elimu na kuipa jamii matumaini ili waweze kuyapokea mabadiliko hayo maishani.

Katika mtazamo wa kiyakinifu, tunaona kuwa wahusika wa kiume wanajidhihirisha kwa namna mbalimbali kulingana na matendo yao halisi. Hii

inadhihirishwa na Ihucha kwa kukosa umakini mara alipofika nyumbani kwake. Aligonga mlango kwa muda mrefu bila kufunguliwa haraka na mkewe kama ilivyo kawaida yake. Ihucha aliendelea kugonga hadi dadake aitwaye Aisha akaja kufungua mlango akidhani wifi yake kapitiwa na usingizi. Bila kuwa makini, mlango ulipofunguliwa, Ihucha akamkumbatia Aisha na kumpa mabusu motomoto akijua ni mkewe aliyemfungulia mlango. Mwandishi anaeleza:

> Aisha alipofungua mlango tu, Bwana Ihucha, kuchanganya na ile nishai ya bia aliyokunywa na hamu ya kuwa na mkewe, akamvamia Aisha, dada yake, na kumbusu huku maneno ya mahaba yakimtoka. Aisha aliruka, akajitoa mikononi mwa Ihucha kwa nguvu huku anapiga kelele. "Kelele! Mimi sikujua kama ni wewe. Samahani sana." (Uk. 11).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: mwanafunzi si mpokezi tulivu wa habari, utambuzi mazingira na tabia vinaathiriana katika upataji habari wa mwanafunzi. Ihucha alifunzwa namna ya kumpokea mkewe mara anapomkaribisha ndani. Hata hivyo ilikuwa njia ya kumbembeleza mkewe kwa vile alichelewa sana kutoka kazini na alikuja amelewa pombe. Ihucha pamoja na kufunzwa hivyo alikosa umakini wa kujua aliyemfungulia mlango ni nani. Nadharia ya mwanaume mpya inamtaka Ihucha kubadilika na kuwa mwanaume mpya kwa kuwa makini na kuonyesha heshima kwa mkewe pamoja na dada yake.

Katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao; wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii. Kihistoria na kijamii mtu akishakunywa pombe huwa anakosa umakini katika baadhi ya mambo na

hujikuta nafanya jambo ambalo huja kumpa wakati mgumu baadae pombe zikimwisha. Aisha ni binti mdogo mwenye umbo dogo wala hafanani au kulingana na Farida hivyo hakukuwa na sababu yoyote ya kumkumbatia na kumpiga mabusu akidhani ni mkewe. Baada ya Ihucha kugundua amekosea bado alizidi kuwa mkali licha ya kwamba alisema samahani. Katika muktadha wa ulevi, mtu anaweza kufanya jambo lolote bila kujali. Zacharia, (2001) anaeleza katika utafiti wake kuhusu mwanamke aliyetengwa katika kiwango cha dini na kiuchumi kuwa binadamu yeyote anahitaji umakini katika jambo lolote alifanyalo katika muktadha wowote ili kulinda maadili ya kijamii.

Kiyakini mwanaume pia anaonekana mpenda starehe. Sikujua licha ya kuwa alimuua rafiki yake aitwaye Pondamali Malipesa. Sikujua alifungwa na alipomaliza kifungo, hata kabla hajazoeleka mtaani akaanza kutumbua na wanawake hasa Fatuma. Wako wanaume ambao wanakuwa na tabia zisizokubalika katika jamii kama ilivyokuwa kwa Sikujua ila bado wanapotoka kifungoni kwa msamaha wa Rais wanajiona ni watu wa matanuzi na kupenda starehe badala ya kutumia kidogo walichonacho kwa kujijenga na kujiimarisha kwa maana walipoteza muda mwingi kutumikia kifungo. Mwandishi anaeleza:

> Jamaa huyu ni mwezi mmoja tu sasa tangu atoke jela baada ya kutumikia kifungo cha miaka mitano. Jaji Utakunywa alimhukumu adhabu ya kifo baada ya kupatikana na hatia ya kumuua rafiki yake Pondamali Malipesa.…......... Rais alitoa msamaha kwa wafungwa wote waliokaa jela si chini ya miaka mine, na ambao walionyesha nidhamu……… Tangu atoke jela, Sikujua hakuwa na pesa za kutosha. Akiba ndogo aliyokuwa nayo Benki ndiyo aliamua kuitumia kwa chakula

> na kujiburudisha kwa maarifa kama alivyokuwa anafanya hapo Mtoni Hoteli akiwa na Fatuma. (Uk. 1-2).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii, mhimili usemao; vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Sikujua alifunzwa kuwa mwanaume anapaswa kujihami na kutafuta pesa kwa ajili ya familia kwa kuihudumia. Sikujua ni mwaanaume hivyo kulingana na malezi ya kiuana kuwa mwanaume anapaswa kumgharimia mwanamke mara wanapokutana, hili ndilo lilimfanya Sikujua kutumbua akiwa Fatuma, badala ya kutumia akiba aliyokuwa nayo kujijenga kiuchumi kwa maana alikuwa kifungoni kwa miaka. Pesa aliyoitoa benki alipaswa kuizalisha ili imsaidie kwa mambo ya maana na sio kukaa hotelini na kuitumia bila kujua ikiisha ataishije. Sikujua ni mwanaume anayepaswa kubadilika na kuwa mwanaume mpya anayejua kubajeti kwa ajili ya matumizi ya baadae.

Kiyakinifu pia katika matukio ya kihistoria, mwanaume anajiona yuko juu ya mwanamke katika kila jambo na ndio maana anakuwa na uwezo wa kujiamulia apendalo bila kumshirikisha mwanamke au mwanamke akifanya jambo basi mwanaume huona hajatendewa haki. Kwa mfano, Ray alijiona ana mamlaka juu ya mwili wa Farida kumgusa na kufanya apendacho. Farida hakukubaliana naye hata kama kampa hifadhi nyumbani mwake bado Farida alikuwa na msimamo juu ya mwili wake na kutokukubali kuisaliti ndoa yake kwa maana alikuwa na mapenzi ya dhati kwa mume na kumwonea wivu sana. Mwandishi anaeleza:

> “Hallo Darling, bado unasononeka tu?” Ray alijitapa kwa lugha ya kizungu kwa uchangamfu huku anamshika Farida begani. “Tafadhali usiniudhi Ray!” Aliuondoa

> mkono wa Ray mabegani huku anamaka. “Ungejua niliyonayo rohoni usingethubutu kufanya utani wowote.” “Lakini wewe mwanakwetu una nini tena? Ufumbuzi umeishapatikana. Bado tu unalalama!……….. Kweli nakuhudhi mimi, mtu ninayekuokoa usiachwe na mume wako?” Alikuwa ameudhika kidogo ingawa macho yake hayakuacha kutabasamu. (Uk. 22).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kuwaona wanawake kama viumbe sawa na wanaume kwa kuwaheshimu na kuwapenda katika nyanja wanazokuwepo. Ray aliona kuwa kwa vile Farida yuko nyumbani kwake hivyo ni lazima atamkubalia ombi la kuanzisha mahusiano ya kimapenzi. Ray hakujali kuwa Farida yuko katika matatizo bali akawa anamwambia juu ya kumtaka kimapenzi. Ray anapaswa kubadilika na kuachana na tamaa za mwili na kuendekeza mapenzi bila kujali shida zinazomkabili mtu. Mapenzi ni suala la kisaikolojia hivyo huwa linahitaji utulivu wa kiakili. Uddin, (2007) anaeleza kuwa jambo analofanya mtu binafsi linahitaji utulivu wa kiakili ili kumfanya mtu huyo aweze kuthaminiwa pia kijamii.

Kistoria pia wanaume hupenda kuoneakana wana uwezo mzuri kiuchumi wa kumiliki mali mbali mbali dhidi ya wanawake. Huwa wanatumia mali zao kuwaonyesha wanawake kuwa wao wana uwezo wa kupambana na kutafuta mali na kuzimiliki kuliko wanawake na ndio maana kihistoria wamekuwa wakiwatawala wanawake kwa kila sekta wakiona kuwa ni haki yao kufanya hivyo kwa sababu kila kitu ndani ya nyumba wamekitafuta wenyewe. Hili limedhihirishwa na Ray alipoulizwa na Farida kama ile nyumba waliyolala ni ya kwake mwenyewe au kapanga. Pia Farida alitaka kujua kama lile gari analotumia ni lake au kalinunua. Katika kumhakikishia Farida kuwa mali ni

zake, Ray alijibu kwa kujiamini sana.Aliongea mambo mengi hata ambayo hakuulizwa. Mwandishi anaeleza:

> “Hapana, sikupanga. Nyumba hii ni mali yangu. Teksi ni mali yangu. Sina mke, sina mchumba. Baba na mama wako Moshi, wanajiweza; hawahitaji msaada wangu. Nimejijenga, nimejengeka. Niko mbioni kununua benzi sasa, na ninaitwa kizito hivyo kama huna habari! Wewe unanidharau hapa,unafikiri mimi ni mkweche kama ulivyoiita teksi yangu siku ile ilipoharibika njiani. We ngoja tu, iko siku utaamini kuwa Ray ni ‘Ray’ kweli, kama utakuwa bado uko mji huu.” (Uk. 27).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii, mhimili usemao; ujifunzaji unahusu kuchunguza kupata habari kutokana na ule uchunguzi na kuunda maazimio kuhusu utendakazi wa tabia hiyo. Ray alifunzwa kama mwanaume kuwa ni lazima kupambana kwa kufanya kazi ili aweze kuwa na mali zake mwenyewe jambo ambalo litamfanya aheshimike katika jamii. Hilo ndilo lilimfanya ajihami na kumtaka Farida kimapenzi. Ray alikuwa na dhamira ya kuanzisha mahusiano ya kimapenzi na Farida na zaidi alienda mbali kwa kumtaka amuache Ihucha ili aolewe na Ray. Alijipa uhuru kumshika Farida akidhani hatamkatalia kwa maana kikawaida walishakubaliana kuanzisha mahusiano hayo ya mapenzi bila kujua kuwa Farida alikuwa akitafuta mbinu za kurudi kwa mumewe. Ray alijitapa kwa Farida kuwa yuko vizuri kiuchumi ikiwa ni mbinu zinazotumiwa na wanaume wengi kuwashawishi wanawake. Kwa vile Farida ana elimu ya kiuana alijua lazima Ray atakubaliana na hoja zote za Farida akiamini kuwa akishafika kwa Ihucha atafanya kila njia kuachana na Ihucha kuja kuolewa na Ray kwa vile ni mchaga mwenzie na Ihucha ni mnyaturu. Jamii imo katika matabaka na mojawapo likiwa la ukabila hivyo unakiwa ukombozi. Mlacha na Madumulla, (1991) wanasisitiza dhana ya

ukombozi katika mambo yanayozikwamisha jamii nyingi kuendelea ikiwemo ubaguzi wa kikabila.

Kiuhalisia jamii inatakiwa kuwa na mshikamano katika kuondoka matabaka ya kiuana pamoja na ugandamizaji bila kuacha nyuma ukabila. Jamii inaposhikamana mabadiliko chanya yatapatikana kwa urahisi kwa kuielimisha jamii kwa ujumla ili kuwe na mabadiliko hasa katika masuala ya kiuana.

### 4.3 Mtazamo Katika Riwaya ya *Tumaini*

Katika mtazamo wa kidhanifu katika riwaya hii, wanaume wanapambana katika kutafuta maendeleo ila wakati mwingine wanajikwamisha wenyewe. Kwa mfano, Majuto alitoka familia yenye uwezo na alisaidiwa kila kitu ili aweze kuwa na maendeleo mazuri kitaaluma kwa manufaa yake ya baadae ila alijikwamisha mwenyewe kitaaluma kutokana na tabia yake ya ujeuri pamoja utukutu uliopitiliza. Kutokana na tabia zake mbaya shuleni, alijikwamisha katika maendeleo yake kitaaluma. Wengi walitamani kupata msaada kutoka kwa wazazi wao ili wawapatie kila aina ya mahitaji ya shule ila hawakuwa na bahati hiyo ila Majuto mwenye nafasi hiyo aliichezea. Tabia mbaya za Majuto zilipelekea kufukuzwa shule. Mwandishi anaeleza:

> Vishindo vya Majuto viliposhitadi, mwalimu alitoa amri darasa lote litoke nje kumfukuza ili limkamate na kumleta mbele yake. Majuto alipoona umati wa wanafunzi ukimwandama, alitimua mbio mithili ya swara…………………… Barua kali kutoka kwa mwalimu mkuu ilimwonya kutokaribia majengo ya shule. Wakati huu hata mlungula wa chifu haukufua dafu. Tumaini aliamini kuwa Majuto hangerudi shule muhula ujao, na huo pengine ndio ulikuwa mwisho wa masomo yake. (Uk. 21).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili usemao; ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Majuto alifunzwa kwa kudekezwa na kubembelezwa mno kama mtoto wa kiume.Inaonesha kuwa Majuto alivyolelewa ndivyo alivyokua. Baba yake alikuwa akamkania mwanae alipoelezwa makosa yake ayafanyayo akiwa shule. Babake alimdekeza sana mtoto wa kiume na kumwachia uhuru sana. Babake alifikia wakati anatoa mlungula ili mwanae aendelee kubaki shule ila tabia zake zilipokithiri walimu wakashindwa kumvumilia ikabidi wamfukuze shule. Malezi ya mtoto wa kiume Majuto hayakuwa mazuri na ndio maana alijiona ana mamlaka ya kuwavurugia darasa wenzake walipokuwa wakifundishwa na mwalimu darasani. Tabia za wanafunzi darasa la akina Majuto zilionesha matabaka ya watoto wanaotoka familia masikini na zenu uwezo jambo ambalo si zuri kimalezi. Sengo, (1987) anaeleza kuwa matabaka yanaleza misingi ya kubaguana kidini, kielimi,kiuchumi,kijinsia, kikabila na kuchelewesha maendeleo.

Katika maendeleo, wanaume pia wanajiona wachapakazi na wasio waoga usiku kama Tumaini alivyokuwa akiogopa kutembea usiku mara alipotoroka nyumbani kwao. Vijana wa kiume wanajibidisha sana kwa kudamkia shughuli zao za kubeba mizigo usiku sana hadi walimshtua Tumaini alipokuwa amejificha kichakani akisubiri kupambazuke. Vijana hao walifanya kazi bila hofu yoyote kwa maana walipigania maendeleo yao na familia zao. Vijana hao walikuwa wakirauka kuchota maji na kujaza madebe yao huku wakizunguka mtaani na kuuza. Mwandishi anaeleza:

> Alizidi kutumbua macho, huku moyo ukimwenda mbio. Hapo alimwona mzegazega akipita mbio huku amebeba madebe shinda. Nyuma yake, alifauatiwa na kijana mnene mwenye misuli, aliyesukuma rukwama lililosheheni madebe shinda vile vile. Wote walikuwa mbioni utadhani maji yatakauka kisimani walikokuwa wakielekea. Kwa kawaida vijana hao huyajaza madebe maji kasha wakayatembeza mitaani huku wakinadi "Haya maji, haya maji!" kwa wale waliokuwa wazembe wa kuteka maji kisimani. (Uk. 6).

Nadharia ya uwajibikaji wa kijamii mhimili usemao: vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Vijana wa kiume wanafunzwa kuwa wachapakazi na kutokuwa waoga nyakati zote za mchana na usiku ili waweze kufanikiwa. Mafunzo haya huwajengea ujasiri wa kuwa watafutaji bila kubagua kazi kikubwa ni kujipatia kipato halali.

Nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao; wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii. Vijana wanaonyeshwa kama walivyo kiutendaji. Wanaamka asubuhi sana ili wawahi kuchota maji kwa ajili ya kuuza. Wanapata riziki kupitia maji wanyoyauza kwa kutembeza majumbani. Wakati wakivuta mikokoteni yao ndipo walimshtua Tumaini pale kichakani alipokuwa amejificha na akakimbia mbio kwenda pembeni. Mwandishi anawaonyesha vijana wa kiume kama wachapakazi. Jamii inawachukulia vijana wa kiume kama wachapakazi na watafutaji wa riziki kwa ajili ya kutunza familia zao. Sengo, (2009) anaeleza kuwa malezi ni jambo la msingi sana katika makuzi ya binadamu. Mawazo ya maendeleo ni saikolojia ambayo mtu huipata kutoka kwenye malezi ya wazazi na jamii kwa ujumla.

Katika kuangaza madhila ya wanyonge na haki zao kama kipengele cha udhanifu tunaona kuwa Tumaini alipitia wakati mgumu sana ambapo baba yake alitaka kumkatiza masomo kwa kumfanyia tohara na kumwozesha kwa mwanaume katika umri mdogo. Wanaume wanaonekana wenye kushadadia ndoa za utotoni na mila zilizopitwa na wakati kama tohara. Kwa mfano, Idi alitumwa na Mzee Masumbuko akamtafute Tumaini kwa Mzee Shabani ili aje kuolewa baada ya kutahiriwa. Idi alimtisha sana Tumaini licha ya kuwa Idi ni mdogo wake Tumaini ila alijihami kwa vile ni mtoto wa kiume. Idi alimtisha sana Tumaini ili atii yale aliyotumwa na baba yake na kwenda kuolewa kama ilivyokuwa imeamriwa na Mzee Masumbuko. Mwandishi anaeleza:

> "Heh! Tuma leo utapambana na kikoto. Wewe waogopa ku…" alitamka Idi, lakini Tumaini alimkatiza, "Usss! Nyamaza we! Laity ungalijua lililo moyoni mwangu, hungalitamka hayo. Mimi siogopi tohara wala kikoto bali nahofia maisha yangu ya mbeleni." "Yapi hayo, si utaolewa tu," Idi alimjibu kwa dharau. Tumaini aliinuka ghafla kutaka kumpiga Idi lakini Riziki alimzuia. "Idi, tafadhali rudi nyumbani usitutie kero zaidi. Unadhani wasichana jukumu lao ni kuolewa tu hawana jingine la muhimu maishani? Kamwambie babako asubiri wageni leo jioni, kwahivyo asitoke. Na iwapo ananuia kuja hapa, avunje hiyo safari ili awasubiri hao wageni," alisema Bi. Halima. (Uk. 29).

Katika madhila ya Tumaini kulazimishwa tohara na ndoa za utotoni pamoja na kumuachisha shule, Mzee Masumbuko alikuwa mkali sana hasa baada ya kumtuma Idi akarudi bila Tumaini. Hapo alidhani Idi kadharauliwa kwa vile ni mdogo na ndipo alimtuma mama yake Tumaini akidhani atakuja naye. Mzee Maumbuko alikuwa mkorofi na mgomvi ila baada ya Bi. Amina kurudi bila Tumaini aligombezwa sana kwa sababu Mzee Masumbuko alishapiga mahesabu ya kupokea pesa za mahari mara Tumaini atakapoolewa. Baba

Tumaini alikuwa mkali sana hadi akamrushia ufito Bi. Amina kumpiga nao mara alipoona hajaongozana na Tumaini. Mzee Masumbuko alimsemesha mkewe kwa ukali sana huku midomo ikimchezacheza kwa hasira. Mwandishi anaeleza:

> Mkewe alimsalimia lakini badala ya kuitikia salamu hizo, Masumbuko alisimama ghafla na kumnyooshea ule ufito huku akitamka kwa hamaki, “Yuko wapi? Yu wapi huyo mwanao mchuro uliyeenda kumtafuta enh? Nijibu harama ama…” Kabla mkewe hajamjibu, Masumbuko alimrushia ule ufito kwa nguvu zake zote. Ufito ulifyatuka kama mshale, ukayoyomea kwa Bi. Amina ambaye alichutama ghafla na kuupisha. Ufito uliupiga dhoruba kali mpapai uliokuwa umepandwa hapo uani ukakatika vipande viwili. (Uk. 36).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili usemao; ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Wanaume wanafunzwa kuwa ni lazima watakachokisema wanawake wawatii bila kujali umri kama wa Idi kwa Tumaini. Jamii nyingi zinaongozwa mielekeo inayomfanya mwanamke kuwa mtii kwa mwanaume kwa kila jambo bila kujali umri. Mzee Masumbuko alimtuma Idi akidhani Tumaini atamtii kwa vile ni wa kiume bila kujua kuwa Tumaini ameenda shule na ameishapata elimu ya kiuana ambayo inamwongoza kupigania haki zake za msingi kama mtoto wa kike. Jamii inategemea kuwa chochote anachofanya mwanaume hata kama ni kibaya, mwanamke anapaswa kutii. Tamaduni hizi zinazoumiza jinsi moja dhidi ya nyingine zilimpa kiburi mzee Masumbuko kumfokea mke wake na kumrushia ufito kwa sababu alitumwa akamchukue Tumaini na akaja bila kuongozana naye. Jamii inahitaji mabadiliko kuachana na haya mambo mabaya ya kutowathamini wanawake na kuwa na wanaume wapya wanaothamini na kuwapa nafasi wanawake katika maamuzi. Haya yanapswa

yaanzie kwenye malezi. Sengo (keshatajwa) anasisitiza suala la malezi kwa watoto kuwa chanzo cha kuleta mabadiliko katika mambo mengi yafanywayo katika jamii.

Mtazamo wa kiyakinifu katika riwaya hii,mwandishi anaonesha wahusika wa kiume wanavyofanya uharibifu kwa watoto wa kike kwa kuwalaghai na kuwapa zawadi za hapa na pale ili kuwarubuni kujiingiza katika mahusiano ya kimapenzi kabla ya umri wao. Hii imedhihirishwa na Chifu Andrea ambaye alikuwa mtoa zawadi kwa wasichana ili kuwashawishi. Mwandishi anaeleza:

> Majuma mawili yalipita bila matatizo yoyote katika jumba la Chifu Andrea. Tumaini aliendelea kutumika lakini katika siku za hivi karibuni, alianza kuustaajabia ukarimu wa Chifu Andrea. Chifu alianza kumtunukia zawadi, mara leo amletee gora la kanga, kesho amnunulie mafuta mazuri. Siku moja asubuhi alipokuwa akifagia banda la kuku, alimwona chifu akimjia huku kabeba mfuko wa karatasi mkononi. Baada ya kumsabahi Tumaini kwa kicheko na wingi wa bashasha, alimpa mfuko huo akimwambia ni zawadi yake………… Tumaini aliipata sauti yake na kumuuliza chifu huyo alifanya nini hata astahili zawadi ile. Chifu alichekacheka na kumwambia ni kutokana na bidii yake kazini iliyomfurahisha na kuamua kumzawadia mfuko huo. Tumaini aliupokea, shingo upande. Moyoni aliwaza lazima lipo jambo kwani si kawaida mtumishi kupewa zawadi mara kwa mara na tajiri wake hivyo. (Uk. 85-86).

Nadharia ya ujifunzaji katika mhimili usemao; mwanafunzi si mpokezi tulivu wa habari, utambuzi mazingira na tabia vinaathiriana katika upataji wa habari wa mwanafunzi. Hii inadhihirishwa na Chifu Andrea ambaye ni msomi na ana uwezo mzuri kiuchumi ndiye anayeongoza kuwarubuni watoto wa kike ili kuwaingiza katika mahusiano ya mapenzi katika umri mdogo. Dhamira yake kwa Tumaini haikufanikiwa kwa maana alikuwa na malengo na mwamko wa kufika mbali kimaendeleo kupitia elimu hivyo kujiingiza katika mapenzi

katika umri mdogo kungemwaribia ndoto zake. Katika nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao; itumie sajili ambazo ni za kawaida. Hii pia imedhihirishwa na Chifu Andrea katika kupambana kuwadaka watoto wa kike katika mtego wa mapenzi. Alitumia mbinu za kawaida kama zawadi za viatu, nguo, kuwasifia kuwa wanafanya kazi vizuri ili kuweza kuwashawishi ingawa kwa Tumaini aligonga mwamba. Malezi ya watoto ndiyo huwapa msingi wa kujikomboa pindi wapitiapo nyakati ngumu. Wamitila, (2002) anaeleza kuwa makuzi ya mtoto yana mchango mkubwa sana katika kumjenga kisaikolojia ambayo ndiyo humuongoza katika maisha yake ya siku zote.

Vile kiyakinifu, wanaume wakikataliwa na wanawake huamua kuwalipiza kwa kuwatenda mabaya kama kuwakomoa. Chifu Andrea alitarajia kila mwanamke anayemtaka kimapenzi lazima amkubalie. Baada ya kukataliwa na Tumaini, alimfanyia alimfanyia unyama na matendo ya kuumiza ikiwemo kutoa jina lake katika orodha ya wafadhiliwa masomo. Tumaini alikuwa na sifa za kufadhiliwa na jina lake lilipitishwa pamoja na wengine watakaofadhiliwa masomo yao. Cha ajabu Chifu Andrea alilitoa jina lake kama kumkomoa na kupeleka majina ya wafadhiliwa wengine. Ilipodhihirika kuwa ni Chifu aliyelitoa jina lake, hakika aliaibika sana. Hii ni baada ya Tumaini kupata taarifa na kujitoa muanga kuingia katika jopo la wapitisha majina na kujieleza. Wanaume wanajiona kuwa wao ni watenda haki hivyo hawapaswi kukataliwa kwa lolote wanalomwambia mwanamke. Hapa ndo ilipodhihirika kuwa zile zawadi Chifu alizitoa kwa Tumaini ili amkubali kimapenzi na ndiyo maana aliamua kumfanyia hivi ilhali anajua kuwa

Tumaini anatoka familia isiyokuwa na uwezo kiuchumi katika kuhimili gharama za masomo yake. Mwandishi anaeleza:

> Tumaini alipomaliza kutoa kisa chake,alimpa D.O kile cheti cha majibu yake ambacho kilikuwa bado kina unyevunyevu. D.O alijitahidi kusoma maandishi yaliyokuwa humo ambayo hayangesomeka kwa urahisi/ alinakili tuzo za Tumaini mahali, kisha bila kusema lolote, alimpigia Mwalimu Mwadime simu. Kwa bahati nzuri, alimkuta ofisini mwake. Baada ya kuhakikishiwa majibu ya mtihani wa Tumaini, aliarifiwa pia kuwa Chifu Andrea alilitoa jina la Tumaini katika orodha aliyopewa na mwalimu huyo. (Uk. 102).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili usemao; vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Mwanaume anafunzwa kuwa kila afanyacho ni sahihi kwa mwanamke na ndio maana inapokuwa kinyume huona hajatendewa haki na kuamua kulipa kisasi. Chifu Andrea aliona hawezi kukataliwa kwa sababu jamii inaamini kuwa kinachosemwa na mwanaume ni chanya hivyo hakifai kukataliwa na mwanamke ambaye kazi yake ni kutii. Mahusiano ya mwanamke na mwanaume yamejengwa kwa mwanamke kuwa msikivu kwa mwanaume na kutii. Chifu Andrea hakuelewa kuwa Tumaini alikuwa na elimu ya kiuana ambayo ilimwongoza kujisimamia katika kile alichokiamini ni haki yake. Mwanaume anapokataliwa kutoka na misingi hiyo ilijengeka katika jami, basi mwanaume huamua kufanya tendo lolote kama kumkomoa mwanamke aliyemkataa. Chifu Andrea kutoa jina la Tumaini katika orodha ilikuwa ni kumkomoa kwa kumkataa ila Tumaini ameitumia elimu yake ya kiuana kujisimamia na kwenda kujieleza kwenye jopo lililosimamiwa na D.O.

Nadharia ya mwanaume mpya, mhimili usemao: kusaidia wake zao na wanawake wengine katika jamii katika kujiendeleza kielimu na kikazi. Chifu Andrea anapaswa kubadilika na kuwa mwanaume mpya kwa kuacha kuwagandamiza wanawake kwa kuendekeza ngono. Hii ni kwa sababu alitazamwa kama muovu kwa kuwafanyia wanawake ukatili na unyanyasaji kwa kuitumia ofisi yake. Anapaswa kuwathamini wanawake wanapopata fursa za kwenda kusoma asiwabanie kwa kutaka kufanya nao mapenzi ndipo awape nafasi. Mwanaume mbaya anaweza kuacha mabaya na kubadilika akawa mzuri na ndipo anakuwa mwanaume mpya. Powers, (2002) anaeleza kuwa wanaume wanaweza kubadilika na kuwa wapya kwa nguvu zao wenyewe kwa kutumia jamii, dini au mpito wa wakati.

Vilevile, katika matukio ya kihistoria, kiyakini inaonekana kuwa mtoto wa kiume ana sauti juu ya mtoto wa kike hata awe mdogo kiasi gani. Historia hii ndiyo huwapelekea wanaume kuwa wagandamizaji wa jinsi ya kike bila kujali umri. Mzee Masumbuko baada ya kugundua kuwa Tumaini katoroka hawakutumwa dada zake Idi ambao ni wakubwa bali alitumwa Idi kwa vile ni wa kiume, wakiamini kuwa kihistoria mtoto wa kiume anaheshimika na kumtii kuliko wa kike. Idi alitumwa akafika kwa Bi Halima kwa shauku hadi akamkosea adabu kwa maana hakumsalimia bali alifikia kutoa vitisho kwa Tumaini na kumsemea kwa ukali kama alivyotumwa na baba yake. Mwandishi anaeleza:

> Baada ya kuletewa kiti na kukaa, Idi alianza kueleza, “Ma Mdogo, tulimtafuta Tuma…” “Salamu kwanza!” Bi. Halima alimkemea. “Pole, samahani. Mama Mdogo

> shikamoo, "Idi alimsabahi. "Marahabaa, mwanangu. Haya twambie yaliyokuleta kwa vishindo huku," Bi.Halima alimwitikia na kumhimiza. "Ma Mdogo, baba alinituma nije niwaulize kama Tuma yuko hapa na ikiwa yuko, nimwambie kuwa haruhusiwi kurudi nyumbani tena", alitamka Idi. "Kwanini?" Bi.Halima aliuliza. "Kwa sababu ametoroka ili asi – asi -," "Asitahiriwe," alikamilisha Bi.Halima. idi aliitikia kwa kutikisa kichwa. (Uk. 27-28).

Kihistoria baba mwenye nyumba analoamua halipaswi kupingwa na mkewe wala watoto kwa maana yeye ndiye muamuzi. Wanaume ni wenye maamuzi yanayoshindwa kuvumiliwa na watoto wao. Kwa mfano, baba yake Tumaini aliamua kuwa Tumaini atahiriwe ili aolewe bila kujali malengo ya Tumaini katika maisha yake ya kitaaluma. Tumaini aliumizwa na mawazo na kupata uchungu mwingi sana moyoni kwa maana aliona baba yake anamvurugia maisha yake kwa kumkatisha masomo na kutaka kumuingiza katika ndoa za utotoni. Tumaini aliona hakuna matumaini mbele kwani baba yake ana msimamo wa yale anayoyaamua. Mwandishi anaeleza:

> Hakuweza kufanya hivyo kwani maneno ya babake yalimgonga masikioni, yakamchoma moyoni mfano wa kisu chenye makali. Kero la uchungu lililokuwa kifuani mwake lilimchachafya, likamfanya kupukutika machozi kupu kupu pale alipokaa. Aliwaza jinsi alivyojaribu kumshawishi babake ili aweze kuelewa dhamira yake lakini akawa haambiliki hasemezeki. (Uk. 5).
>
> Macho yake yalikuwa yametumbukia ndani kidogo kutokana na masiku mengi ya kukosa usingizi. Wasiwasi mwingi kuhusu dhamira ya babake ulimfanya asipate hata lepe la usingizi. (Uk. 26).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii, mhimili usemao: ujifunzaji unahusu kuchunguza kupata habari kutokana na ule uchunguzi na kuunda maazimio kuhusu utendakazi wa tabia hiyo. Wanaume wanafunzwa kuwa wao ndio waamuzi wa mambo yote katika familia. Hata wakiwa wadogo wao ndio

wenye mamlaka ndani ya nyuma. Mzee Masumbuko alifanya yote haya na kumlea Idi hivyo ili kuweka matabaka ya kiuana katika familia yake. Malezi haya yalimpelekea Idi kuwa na jeuri kwa dada zake na hata walipomtuma kazi alikataa akisema kuwa ni za kike. Watoto wa kike katika familia hii waligandamizwa kwa kupewa kazi nyingi huku mtoto wa kiume akiwa huru.

Nadharia ya mwanaume mpya, mhimili usemao: kuwaona wanawake kama viumbe sawa na wanaume kwa kuwaheshimu na kuwapenda katika kila nyanja wanazokuwepo. Idi na mzee Masumbuko wanapaswa kubadilika kuwa wanaume wapya kwa kuwathamini wanawake na kuwashirikisha katika maamuzi ngazi ya familia. Mtunzi amewatazama kama waliotawaliwa na mfumo dume kwa kuwanyanyasa na kuwagandamiza wanawake kwa kuwanyima nafasi ya kujieleza na kutoa maoni yao. Heshima kwa wanawake iwepo kwa maana nao wanahitaji kupata heshima kama ilivyo kwa wanaume. Kiuhalisia jamii bado inapaswa kuwa na mshikamano ili kutoa elimu kwa jamii nzima ili kuyaondoa matabaka ya kiuana yanayowagawa wanajamii na kuchelewesha maendeleo. Morell, (2002) anafafanua kuwa wanaume wanajizatiti kuishi kwa amani na wanawake pamoja na watoto katika familia zao ingawa baadhi ya wanaume wanashindwa kulitekeleza hili kwa sababu ya kukosa mshikamano. Kwahiyo,wanaume wanapaswa kubadilika ili watazamwe vinginevyo zaidi ya uonevu huu na unyanyasaji wa wanawake na kuwafanya wakose raha ya kuishi. Kuwe na uwiano wa kijinsia katika maamuzi ili kuweze kuwa na maendeleo katika jamii.

## 4.4 Mtazamo Katika Riwaya ya *Dago Wa Munje*

Katika riwaya hii kidhanifu tunaona wahusika wa kiume wakifanya mambo mbalimbali ili kujipatia maendeleo. Babake Dago na mama yake walikuwa wakifanya kazi ili kupata mahitaji ya kila siku. Dago alikuwa mbunifu ili kupata meza ya kuwekea vitabu vyake. Dago alitoka familia ya kimasikini ambapo ndani kwao hakukuwa na vifaa vya msingi kama meza kwa ajili ya kuwasaidia katika matumizi ikiwemo kusoma. Alionesha ubunifu kwa kulitumia sanduku lililokuwa chumbani kwake kama meza ya kusomea na kupanga vitabu vyake. Ubunifu humfanya mtu kuibua mambo mapya na kuisaidia familia na jamii kwa ujumla. Mwandishi anaeleza:

> Dago aidha hajaliona sanduku hili likifunguliwa hata siku moja; kinyume chake, aliona kufuli kubwa ambalo lilining'inia katika bawaba ya sanduku lile kwa muda wote lilipokuwa pale. Kwa mara chache aliwahi kujiuliza ikiwa liliwahi kufunguliwa hata mara moja maishani. Lkini usiri ule haukumsumbua Dago kwani kwake lilikuwa kifaa cha kumfaa. Pale nyumbani hapakuwa na meza ambayo angetumia kufanyia kazi zake za shule. Sanduku lile lilimfaa kwani juu yake palikuwa na vitabu vyake vya shule alivyovipanga kwa safu. (Uk. 3-4).

Katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao; uyakinifu: kuelezea mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Maisha ya Dago na familia yake yalikuwa magumu sana kulingana na uwezo mdogo kiuchumi. Hali hiyo ndiyo iliyompelekea Dago kuwa mbunifu kwa maana shida huleta maarifa. Katika kuleta maendeleo wanaume wanatakiwa kubadilika kitabia. Tabia zao zilizo mbaya ambazo mpaka wanaume wenzao wanakosa ustahimilivu juu yake. Mwalimu aliamua kumuadhibu darasani ili abadilike na kuwa na mwenendo mzuri katika jamii. Mwanaume anakosa ustahimilivu kwa sababu anaona

mtoto wa kiume anawatia aibu mara zote akiambiwa habadiliki na badala yake anaendelea na yaleyale ayatendayo siku zote. Mwandishi anaeleza:

> "Nyoosha mkono mara moja!" Hasira ya mwalimu ilianza kuonekana. Licha ya kuwapenda watoto, hakustahimili watoto watundu wala wazembe. Aligeuka ghafla na kuwatazama wanafunzi wote kabla ya kuuliza kwa sauti ya radi. "Wito wa shule yetu ni upi?" "Juhudi na maendeleo!" Wanafunzi walijibu kwa pamoja………… "Dago peke yake!" Mwalimu Sifa aliamuru. "Juhudi na maendeleo," Dago alijibu kwa mnong'ono. (Uk. 46-47).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Wanaume hufunzwa kupendana kwa ukaribu na kufuatiliana ili waweze kusaidiana. Kutokana na mafunzo hayo, wanaume huwa wanakuwa wakali sana mwanaume mwenzao anapofanya mambo ya kuwatia aibu. Wanaona kama ni wanaume wote wanadhalilika hata kama aliyetenda ni mmoja, wengine hutoa ushirikiano ili kuikomesha hiyo tabia inayowatia aibu. Mafunzo haya yalikuwa chachu kwa Rashidi na Juma kumfuatilia sana Dago kuhakikisha anabadilika kitabia. Walifanya kila jitihada walizoziweza kuhakikisha wanapunguza tabia mbaya kwa Dago. Kumuacha mwenzao akajitenga nao tayari kutaweka matabaka ambayo ni hatari kwa maendeleo yao kama wanaume. Mfano, Kelegeya, (2015) anasema kuwa utabaka umekuwa mbaya zaidi kipindi cha utandawazi kwa kuwatenga wanaume kwa wanawake, wenye nacho na wasio na nacho na ndicho huturudisha nyuma kimaendeleo. Hivyo Rashidi na Juma walimkazania Dago kukwepa utengano ambao ungewaweka mbali.

Katika kuangalia madhila ya wanyonge na maslahi yao, kidhanifu inaonekana kuwa wahusika wa kiume wanapata matatizo mbalimbali ambayo yanawapelekea kupata matatizo mengine. Dago alikuwa na tatizo la kukojoa kitandani ambalo lilimpa matatizo makubwa ya kutengwa na kusakamwa na marafiki zake mara afikapo shuleni akiwa mchafu. Madhila hayo yalimpelekea Dago kuwa mjanja mara aliposhtuka na kuona kuwa nguo zake za shule zimelowa kwa mikojo na hakuwa na nguo nyingine za kuvaa. Ilipelekea awe mjanja awapo jikoni kwa mama yake akinywa uji, alizisogeza jirani na moto ndipo zikakauka na hakuonesha hali ya kulowa ingawa mkojo ulitoa harufu. Mwandishi anaeleza:

> "Na hizi ndizo nguo nitakazovaa kwenda shuleni!" Moyo ulimdunda kwa hamaki iliyochanganyika na hisia za uchungu moyoni. "Watu watasemaje leo nikifika shule?" Dago alifikiria akaiwa bado anapindukapinduka kitandani. (Uk. 10-11).
>
> Fikira za Dago zilikuwa kuketi karibu na moto, ili nguo zake zipate kukauka. Hakutaka kwenda shule akivaa nguo zilizotota, na aliomba kwamba zitakapokauka harufu pia ingetoweka.(Uk. 13-14).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume. Dago anapaswa kujikosoa matendo yake mabaya ayafanyayo kama mwanaume ili aweze kuwa mpya aaenze kuwa na bidi kwenye masomo, msafi, awe anamsaidia mama yake kazi kwa kujua kuwa kila siku anarauka kufanya biashara na kumuandalia Dago chai kabla ya kwenda shule. Dago awe mpya kwa kuacha mazoea yake mabaya ndipo atakuwa mwanaume mpya.

Katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao; usadikifu; yale yanayoibuliwa katika jamii yawe yanasadikiwa na wasomi. Ni kweli kuwa kijana anapofikia umri wa kujitegemea jamii inaamini kuwa tayari ana nyenzo za kumwezesha kufanya hivyo. Inapotokea hajajitegemea jamii nzima hubaki kujiuliza maswali kwa maana wanaona kuwa kijana anapoendelea kukaa kwa wazazi ni ishara kuwa bado anawategemea hivyo hajaweza kujitegemea. Hii huwa inaibua taswira ya tofauti kwa kijana wa kiume kutokana na mielekeo ya kijamii pamoja na tamaduni zinazowaona vijana wa kiume kuwa ndio wanapaswa kupambana zaidi kujitegemea tofauti na vijana wa kike ambao huendelea kulelewa hata wanapoolewa. Jamii inapaswa kupata elimu ya kiuana ili kuwafanya wawe na mabadiliko ya kimtazamo juu ya vijana wa kike na wa kiume. Symon, (1999) anaeleza kuhusu kubadilika kwa mambo katika jamii kuwa ni jambo lisiloepukika. Ametoa mifano ya Uingereza yaani Uropa Magharibi ambako miaka ya 1988-1995 kuwa wanaume walikuwa wakiwatawala wanawake na hata wanaume wenzao ila mambo yamekuwa yakibadilika siku hadi siku.

Madhila ya kukojoa vile vile yalimsababisha Dago achelewe kujitegemea mara baada ya balehe na kuhudhuria jando na unyago. Yeye hakuweza kujitegemea kabisa kwa sababu ya tatizo lake la kukojoa. Mwandishi anaeleza:

> Ingawa weyeji wa eneo hili huwaruhusu vijana waliobalehe kama Dago kuendelea kuishi nyumbani mwa wazazi wao, walitarajiwa kujitweka majukumu ya utu uzima wa kiume. Kumbe si watu wote waliopita jandoni wanaobahatika

> kuzivua tabia za kitoto na kuzivaa zile za kiutu uzima! (Uk. 6).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Dago alifunzwa namna ya kuanza kujitegemea kama mtoto wa kike. Hii hufanyika wawapo jandoni. Jamii ndiyo hupima hatua za makuzi ila inapokuwa kinyume chake napo jamii hutathimini na kujua tatizo liko wapi. Hapa ndipo Sengo, (keshatajwa) ndipo husisitiza suala la malezi katika kupelekea tabia za ukubwani.

Katika mtazamo wa kiyakinifu, mwandishi anaonyesha kuwa wahusika wa kiume wanaonyesha tabia mbalimbali katika maisha yao ya kila siku. Wahusika wa kiume wanaonekana wadanganyifu katika jamii. Hii imedhihirishwa na Dago alipochelewa kwenda shule. Alipofika shule akaulizwa sababu ya kuchelewa shule kila mara wakati alishaonywa kuhusu tabia hiyo isiyokoma, Dago alisema uongo ili kujinusuru na adhabu. Hata hivyo Dago alimdanganya mama yake mara zote alipochelewa kurudi nyumbani akitokea shule na vile vile alipokuwa nyumbani akagundua ameishachelewa kwenda shule. Alimwambia mama yake uongo ili asiende shule au asiadhibiwe na mama kwa kuchelewa kurudi nyumbani. Mwandishi anaeleza:

> “Sijisikii vyema mama, tumbo linaniuma,” Dago aliitikia, akifikiri kwamba uongo ungemfanya mama yake asiulize maswali mengi. Kila wakati Dago alitumia udanganyifu alipotaka kujinusuru na lawama. “Mbona umechelewa kurudi nyumbani?” Hili lilikuwa swali la kawaida kila alipochelewa. (Uk. 104).

Vile vile, mhusika wa kiume ameonekana asiyejipenda yaani siyo nadhifu. Dago alikuwa mchafu, mzembe awapo shuleni. Juma na Rashidi ambao ni marafiki zake waliyasema hayo Dago akiwa mlangoni mara alipochelewa kuingia darasani. Hata hivyo Juma na Rashidi walimpenda Dago wakawa wanamwambia kila mara ili abadilike maana alikuwa akiwatia aibu kwa kuchelewa kuja shule kila siku halafu anakuja akiwa mchafu. Mwandishi anaeleza:

> "Hana siku anayowasili shule kabla ya kengele kupigwa," Juma alimnong'onezea mwenzake. "Na nguo zake waziona zilivyo!" Rashidi aliongeza, akiashiria jinsi zilivyokunjana. Ikiwa ziliwashngaza sasa, ingekuwaje kama wangalimuona kabla ya kuzinyoosha na kuzitandaza motoni, pale alipokuwa akisherehekea kiamsha kinywa chake kwenye joto lililonoga? (Uk. 24).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kuwaona wanawake kama viumbe sawa na wanaume kwa kuwaheshimu na kuwapenda katika nyanja wanazokuwepo. Mhimili huu unamwelekeza Dago kubadilika na kuwa mwanume mpya kwa kumheshimu mama yake na kuwa mkweli awapo shuleni na kuwa nyumbani. Kuwa msafi, anayependa masomo na kusikiliza ushauri wa walimu na wanafunzi wenzake.

Mhusika wa kiume ameonekana mwenye lugha nzuri ya unyenyekevu. Hii imeonyeshwa na Dago alipotumia lugha ya unyenyekevu akiomba ruhusa kuingia darasani alipokuja amechelewa na akakuta mwalimu kaishaingia darasani. Mwandishi anaeleza:

> "Tafadhali mwalimu naweza kuingia?" Dago alisema kwa sauti iliyosikia kama ambaye alikuwa akitafuna kitu mdomoni. Haikuwa wazi ikiwa alinuia sauti hiyo iashirie unyenyekevu, ama ukakamavu. (Uk. 23).

Nadharia ya ujifunzaji mhimili usemao: vishawishi vinapimakatika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Mwanaume anafunzwa kuwa na lugha nzuri ya kujitetea pal anapofanya kosa. Dago alikosea kuchelewa darasani ndio maana alitumia lugha ya unyenyekevu ili kumshawishi mwalimu amruhusu kuingia na asimpe adhabu.

Katika nadharia ya uhalisia mhimili usemao; wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii. Kiuhalisia masuala ya kitabia huwa hayana jinsi. Kijana wa kike au wa kiume anaweza kuwa mchafu, mvivu, mdanganyifu na mengineyo kama aliyonayo Dago. Kutoka na masuala ya kihistoria kila jinsi hubambana ili kuondokana na tabia hizi zisizopendeza katika jamii. Jamii inazichukia tabia zote hizo ambazo si za mwanamke wala mwanaume bali hazipendezi katika jamii. Katika hili ndipo mshikamao unapotakiwa ili kuibadilisha jamii kwa ujumla ili kuondokana na tabia hizi zisizopendeza. Khamis, (2007) anaeleza kuwa mambo ambayo hayapendezi katika jamii huwa yanaondolewa na jamii yenyewe kwa kushikamana na kuonesha kuwa wanajamii hawayahitaji.

Vile vile, katika uyakinifu mhusika wa kiume anaoneka mkwepa majukumu. Wanaume wanakwepa majukumu kwa wanawake na kuwaachia mzigo wanawake waubebe wenyewe. Hii ilidhihirishwa na Charo alipoambiwa kuwa kampa mimba Swafiya aliamua kutoroka na kurudi kwao na kukimbia kuilea mimba na mtoto atakapozaliwa pamoja na mama yake. Charo alionekana mlaghai kwa mambo mengi katika jamii na kutambulika kwa ubaya badala ya

mazuri. Hakukaa vizuri na watu katika kijiji cha Munje na ndio maana alipogundulika kumpa mimba Swafiya kila mtu hakushangaa maana alijulikana kwa tabia mbaya. Charo alikana kabisa suala la kuhusika na ujauzito wa Swafiya. Charo alipelekea Swafiya kufukuzwa shule na kubaki mtaani anawayawaya. Mwandishi anaeleza:

> Kwa ulaghai wake naye Charo,mara tu aliposikia uvumi huo na kuthibitishiwa na Swafiya kuwa angekuwa babake mtoto wao, alikana. Hakukana tu, bali alimsingizia kuwa ni tabia yake ndiyo iliyomchongea, na angenufaika kama angemwendea babake mtoto halisibadala ya kumbandika jukumu lile!............. Charo aliona uji uko moto. Hakuweza hata kumdokeza ama kumtaka mawaidha binamu yake. Kama ilivyo desturi wapotea njia hawa, aliamua kufunga virago vyake ghafla na kurudi kwao bila kuaga. Swafiya alijikuta pekee na mimba change ambayo alijua ingekuwa dhahiri tu baada ya majuma machache. Swafiya alifukuzwa shuleni tu baada ya kujulikana ni mjamzito. (Uk. 42).

Katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao; mwanafunzi si mpokezi tulivu wa habari, utambuzi mazingira na tabia vinaathiriana katika upataji wa habari wa mwanafunzi. Charo alifunzwa kuwa kama mwanume kukubali jambo kirahisi hata kama ni kosa huo sio uanaume. Wanafunzwa kuwa wakipata magumu wapambane naye kwa namna yoyote ile na siyo kukiri udhaifu kirahisi. Hii ndo iliyompelekea kumkana Swafiya. Kijinsia anayebeba mimba tumboni ni mwanamke na ndio maana kulingana na mielekeo ya kijamii wanaume wengi hukimbia majukumu ya kulea mimba wakisingizia siyo ya kwao. Mielekeo ya kijamii dhidi ya wanawake wanaobeba mimba, wanapokimbiwa na wanaume wao ndio huonekana wahuni. Kiutamaduni mwanaume hupaswa kumlea mwanamke mpaka atakapojifungua ila wakwepa majukumu kama Charo hayo huyakimbia. Jamii inapaswa kupata elimu ya kiuana ili uleaji mimba usiwe unakimbiwa na

wanaume. Vijana wanapojihusisha na vitendo vya kingono,kosa huonekana kwa mwanamke. Hata mtu mzima kwa binti mdogo bado kosa litaonekana kwa binti. Hii inaelezwa na Nicholaus, (2011) kuwa katika jamii ya watu wazima yaani wanaume hupenda kuwa na mahusiano ya kingono hasa na watoto wadogo na haionekani jambo la aibu kwao kufanya jambo hilo.

Katika maisha, kihistoria mwanaume huitunza familia yake na kuipa mahitaji muhimu ikiwemo kumwezesha kupata elimu katika ngazi mbalimbali. Mzazi anaposhindwa kutimiza hayo kwa familia yake huishia kupata mgogoro wa nafsi. Baba Nchimoni anapata mgogoro wa nafsi anabaki kuzungumza peke yake na kuumia roho kwa kushindwa kumlipia karo Nchimoni mara baada ya kufaulu. Mwandishi anaeleza:

> Mara kwa mara alijipata akizungumza na nafsi yake; “Ya Rabi Maulana, liegeshe dau langu nisije nikadidimia.” Haikufahamika wazi ikiwa dau hali ni yule mwanawe, ama ikiwa ni hali ya maisha iliyowakumba kama familia. Aidha, maneno haya yalimtoka kila alipomkumbuka Nchimoni, kifungua mimba chake, bintiye wa kwanza, mtiifu na mwenye juhudi. Uchochole uliwafanya wasiweze kumlipia karo za shule ya upili ingawa alihitimu na kuitwa katika shule ya kitaifa. (Uk. 87).

Kiuhalisia, wasomi wanasadiki kuwa familia bora ni ile inayopatiwa mahitaji yake ya msingi kama vile elimu, malazi na chakula. Kuanzia hapo ndipo familia huanza kupanuka kimahitaji kulingana na uhitaji pamoja na uwezo. Nadharia ya uhalisia inatuelekeza katika mshikamao ambao unazipelekea jamii kuweza kupata mahitaji ya kila siku na kuleta maendeleo kwa ujumla. Jamii inapaswa kushikamana pia katika kutoa elimu ya kiuana katika kushikamana kupata mahitaji ya msingi katika familia badala ya jinsi moja

kuitegemea nyingine. Maendeleo ni mshikamano wa jinsi zote katika jamaii kwa maana umoja ni nguvu. Hii itatokomeza tamaduni zinazoendelea kuirudisha jamii nyuma. Nyambwogi, (2016) anaeleza kuwa utamaduni wa jamii ndio hutoa dira na mwelekeo wa namna mambo mbalimbali ya kijamii yanavyopaswa kuendeshwa na wanajamii wote kwa kuwa na mahusiano mazuri miongoni mwao, amani na upendo, ushirikiano na kuheshimiana katika jamii na huo ndio mshikamano. Kwahiyo, mwanaume ametazamwa kuwa na majukumu ya kuitunza familia kwa kuipatia mahitaji muhimu ikiwemo elimu. Hili si jambo la baba peke yake, familia nzima ishikamane na kutafuta mahitaji muhimu kwa familia kwa umoja, asiachiwe baba iwe ni jukumu la baba, mama na watoto wenyewe na ndipo tutakuwa na familia inayowajibika kwa pamoja.

## 4.5 Hitimisho

Katika riwaya hizi za *Kipimo cha Mizani*, *Hiba Ya Wivu*, *Tumaini* na *Dago wa Munje* waandishi wa riwaya hizi wana mitazamo hasi na chanya kwa wahusika wa kiume. Kwa vile wamewatazama wahusika wa kiume kama watenda maovu na watenda mazuri katika jamii zao. Uovu au uzuri hutofautiana baina ya jamii na jamii au familia na familia na baina ya mtu na mtu. Mitazamo iliyoibuliwa na watunzi wa riwaya teule juu ya wahusika wa kiume inawafanya wanaume waonekene katika sura mbili yaani uzuri na ubaya kama ilivyobainishwa katika uchanganuzi wa riwaya mahsusi. Waandishi wameonesha matendo mema yanayofanywa na wahusika hao lakini pia waandishi hao hawasiti kuonesha mambo au tabia mbaya

inayofanywa na wahusika wa kiume ambayo kwa ujumla hurejelea hali halisi iliyopo katika jamii. Hii inadhihirisha kuwa kupitia wahusika wa kiume tunaweza kuhitimisha kuwa binadamu anakuwa na tabia mbalimbali hivyo huweza kubadilika badilika.

# SURA YA TANO

# ULINGANISHI NA ULINGANUO WA WAANDISHI WA KIKE WA KENYA NA TANZANIA

## 5.0 Utangulizi

Sura ya nne imejadili mitazamo inayoibuliwa na wahusika wa kiume katika riwaya teule. Mitazamo hiyo ni ya aina mbili yaani mtazamo wa kidhanifu/kidini na mtazamo wa kiyakinifu. Sura hii ya tano inahusu namna waandishi wa kike wa Kenya na Tanzania wanavyofanana na kutofautiana katika usawiri wa wahusika wa kiume katika kazi zao. Hata waandishi wa nchi moja hutofautiana maana kila mwandishi huandika kwa wakati wake na anakuwa na msukumo tofauti na mwenzake wa kuandika kazi. Hata hivyo waandishi huweza kufanana kwa namna fulani kwa maana wanakuwa wanazilenga jamii zinazofanana au kukaribia kufanana. Waandishi hukulia katika familia na jamii tofauti na hicho huwa ndo kichocheo kikubwa cha waandishi hao kutofautiana (Wamitila, 2008).

## 5.1 Kulingana kwa waandishi wanawake wa Kenya na Tanzania

Waandishi wa kazi za fasihi huweza kulingana kwa kufanana katika mawazo na matendo yao. Hii ni kutokana na jamii wanazozizungumzia, zilizowakuza pamoja na tamaduni zao. Wataalamu kama (Mekacha, 1993. Mlacha, 1991. Rear, 2015) wanaoona kuwa jamii nyingi zina mfanano mkubwa na hilo hupepelekea kuwa na kazi za fasihi zinazohusiana kwa ukaribu. Wataalamu hawa huona kuwa, licha ya tofauti ndogondogo baina ya jamii hizo, mfanano wa kazi hizo ni mkubwa kuwa kutokana na falsafa zao. Vile vile wataalamu

hawa huamini kuwa jamii nyingi za Afrika, ikiwemo Kenya naTanzania, mbali na tofauti ndogondogo miongoni mwao, zina mfanano mkubwa katika mambo mengi ya kijamii (Sosoo, 2020).

Kufanana kwa waandishi wa riwaya teule kumebainika katika masuala mbalimbali waliyoazungumzia kuhusu wanaume kama vile dhamira, mtazamo falsafa,taswira, mtazamo na motifu. Vipengele hivi vimefanana katika kumpa mwanaume sifa mbalimbali kama ifuatavyo:

### 5.1.1 Kumsifu Mwanaume

Wahusika wa kiume katika riwaya teule wameweza kusifiwa kulingana na matendo wanayoyafanya. Kwa kuanza na riwaya ya *Kipimo cha Mizani*, iliyoandikwa na Zainabu Burhani wa Tanzania, mwanaume amepewa sifa nyingi nzuri. Amini alikuwa mchapakazi katika ofisi yake alikokuwa ameajiriwa na hata alipoaga kuwa anataka kustaafu afanye kazi zake mwenyewe haikupokelewa kwa uzuri maana alikuwa anapendwa kwa uchapakazi wake. Mzee Hasani alikuwa mchapakazi sana kazini kwake na hata alipostaafu aliendelea kukumbukwa kwa uchapakazi wake pamoja na uaminifu. Hii ndo ilikuwa sababu ya Amini kumtafuta ili aje afanye kazi ya kuuza duka.

Vile vile, Amini alionekana kuwa na sifa nzuri sana tangu akiwa kijana mdogo. Hata alipoenda kumposa Halima wazazi wa Halima na familia nzima

akiwemo nyanya wa Halima alimkubali sana kwa sifa nzuri. Nyanya yake alimweleza Halima kwa uwazi. Mwandishi anasema:

> Mjukuu wangu umebahatika! Maana katika dunia hii ya leo ni wachache sana walio na tabia nzuri za kijana huyo. Fikiri vizuri. Mimi ningekushauri umkubali! (Uk. 29).

Selemani alikuwa mshauri mzuri sana kwa Amini na wala hakutegemea malipo yoyote hata alipotoa ushauri wa kitaalamu. Alikuwa mtu wa kujitoa kwa ajili ya familia ya Amini. Hata Amini alipofariki, Selemani aliendelea kuwa karibu na hiyo familia kwa kila hali.

Bakari alisifiwa sana kwa kuwa alikuwa mtu wa kujitoa sana kwa kufanya biashara yake mwenyewe ya duka anafanya kila kitu mwenyewe kwa kufanya manunuzi, kuuza na kufanya kazi zake za nyumbani. Duka lake ndilo lilikuwa ofisi yake na mahali pa kuishi. Hata Ali na wadogo zake walipofukuzwa na Maryamu walipokelewa na Bakari hapo dukani akakaa nao huku akiendelea na shughuli zake hadi alipowaombea makazi kwa Bi Rehema. Hata hivyo jamii hii ilifurahia sana watoto wa kiume wakiamini kuwa wao ni wachapakazi. Amini alipopata mtoto wa pili wa kiume alifurahi sana. Ndiyo maana watoto wa kiume wanasifiwa na kuthaminiwa sana kuliko wa kike. Mwandishi anasema:

> Wakati huu, Halima alizaa mtoto wa pili wa kiume. Amini alifurahi sana, akampa jina “Uledi”. (Uk. 33).

Kama inavyoelezwa na nadharia ya ujifunzaji wa kijamii katika mhimili wa pili kuwa ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza

matokeo ya hiyo tabia. Inamaanisha kuwa mfumo unaomlea mtoto ndizo tabia anazokua nazo. Hata Amini alilelewa katika jamii hizo. Jamii zinazomthamini mtoto wa kiume zinaendelea kurithisha tabia hizo vizazi na vizazi. Hii inaelezwa na Mnenuka, (2012) kuwa jamii nyingi za Kiafrika hupendelea zaidi wanawake wanaozaa watoto wa kiume.

Sefu ambaye ni mhusika katika riwaya ya *Kipimo cha Mizani*, alijitoa kufanya utafiti bila malipo kuhakikisha Halima anasakwa kwa kila njia na kujua mahali alipo kama yuko hai au alishakufa. Alifanya utafiti mpaka akajua kuwa yuko hospitali na anaishi huko kama mgonjwa wa kichaa. Alirejea na kuwajuza akina Bi. Riziki, Selemani na mzee Hasani na ndipo safari za kwenda kumwona hospitali zilipoanza hadi alipoweza kutoka na kuja kuonana na wanae waliokuwa wakipata malezi mazuri na kila huduma kwa Bi. Rehema ikiwemo kusoma shule. Bi. Rehema aliwapenda sana maana wale watoto wa kiume hawakuwa na kiburi na walikuwa watii kila walichoambiwa. Mwandishi anasema:

> Rehema aliwaangalia vizuri na kusema nao kwa upole, na wao walimsikiliza na kumtii. Walikubali kwenda shule kuendelea na masomo yao. (Uk. 191-192). Katika riwaya ya *Kipimo cha Mizani*.

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao:ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Tabia hizi zinazofanywa na wahusika wa kiume si kwamba walizaliwa nazo bali wanajifunza katika jamii. Jamii ndiyo hutathmini kama kweli wanafuatilia waliyofunzwa na kuyatenda. Chomsky, (k.h.j) katika

makala yake inayomhusu Skinner na tabia yake ya uzungumzaji katika lugha, anaeleza kuwa tabia anazokuwa nazo binadamu zinatokana na alivyofunzwa.

Issa alikuwa aliyetambua maadili ya kazi yake. Aliifanya kwa kufuata taratibu na kanuni na kila alipokuwa akiwahudumia wagonjwa walifurahi sana. Hata wauguzi waliofanya naye kazi walimfurahia sana kwa nidhamu yake kazini. Hii ndiyo ilipelekea Salama baada ya kupata matatizo kazini kuanza kumsaka ili aweze kumpa ushauri wa namna ya kumpa huduma stahiki Halima ambaye alikuwa haongei. Issa alimwelekeza Salama hatua mbalimbali za kupitia ili aweze kupata taarifa za mgonjwa na kweli alifanikiwa.

Katika riwaya ya *Hiba ya Wivu* iliyoandikwa na Zainabu Mwanga wa Tanzania, nako wahusika wa kiume wamepewa sifa nzuri ambazo zimedhihirshwa kwa matendo ya wahusika mbalimbali wa kiume. Ihucha alikuwa mchapakazi katika biashara yake ya kuuza saa. Alikuwa na ushrikiano na Feruzi pamoja na wenzao. Walikuwa wakifanya mikutano ya mara kwa mara ili kupeana mikakati ya mafanikio. Hata mmoja wao alipoonekana kutofanya vizuri aliitwa na kuambiwa ajieleze kwanini hapigi hatua. Wanaume wanakuwa na mshikamano hata wakati wa shida hasa mwenzao anapopata matatizo wanajitoa kumsaidia. Mfano Ihucha, mkewe alipopotea na ikajulikana kuwa katekwa na wateka nyara. Feruzi alishirikiana na Ihucha kutoa taarifa polisi na kuwa karibu na Ihucha kumpa ushauri wa kutangaza gazetini na kuendelea kuwa na subira. Wateka nyara walipopiga simu kutaka pesa, bado akina Feruzi walimtia moyo Ihucha na kumpa gari la

kwenda nalo bonde la mkwajuzi kupeleka elfu hamsini walizozitaka wateka nyara ili kumuachia Farida arejee nyumbani kwa mumewe. Feruzi alikuwa mtu mkubwa yaani meneja masoko wa kiwanda cha saa ila alikuwa karibu sana na watu na kuwasaidia wakati wa shida. Ihucha alichanganyikiwa kujua mkewe katekwa nyara ndipo akampigia simu Feruzi. Mwandishi anasema:

> "Mke wangu yuko hatarini,nifanyeje?" "Loh! Pole sana. La muhimu ni kumwokoa huyo binti kwanza. Lakini angalia usalama wako. Ningekushauri utafute ulinzi,usiende peke yako kupeleka hizo pesa." "Ni sawa bastola ninayo…. nitakuwa na mtu wa kufuatana naye awe kama mlinzi". "Mimi ningekuwa radhi kabisa kuandamana nawe, lakini kesho asubuhi saa mbili nina kikao cha Bodi ya Wakurugenzi ya Kiwanda". (Uk. 25).

Wanaume wamepewa sifa ya uwajibikaji. Kwa mfano Ray alikuwa akiendesha teksi yake mwenyewe usiku na mchana akijipatia pesa na huku alikuwa akifanya biashara ya magendo ambapo alikuwa anafuata bidhaa mpakani na kuvivusha na kuja kuuza Tanzania. Alikuwa na maendeleo mazuri maana alijenga nyumba yake mwenyewe huko Ilala Sharifu shamba na kwao Moshi alikuwa na nyumba nzuri. Sikujua na Chaurembo wote walikuwa wakifanya kazi za kuendesha teksi ili kujipatia kipato na walifanya kazi yao kwa bidii usiku na mchana bila kuchoka. Ray alieleza mali zake kwa Farida anazomiliki na mipango yake ya baadae hadi Farida akashangaa uchapakazi ule na maendeleo makubwa katika umri mdogo. Mwandishi anaeleza:

> "Hapana, sikupanga. Nyumba hii ni mali yangu. Teksi ni mali yangu. Sina mke, sina mchumba. Baba na mama wako Moshi, wanajiweza; hawahitaji msaada wangu. Nimejijenga nimejengeka. Niko mbioni kununua benzi sasa. (Uk. 27).

Mzee Kimambo ambaye ni baba mzazi wa Farida, alikuwa na busara sana. Hakupewa taarifa za kupotea kwa Farida hadi alipoziona gazetini. Hakuwa mkali kwa Ihucha wala mjomba wake Farida aliyemlea. Hawa walikuwa na taarifa za kupotea kwa Farida ila hawakumjuza baba mzazi. Alipopata habari, alipiga simu kuhakikisha kama taarifa ni za ukweli. Baada ya kuujua ukweli alishtuka ila bado aliwatia moyo akina Ihucha na mjombake Farida kuwa wasikate tamaa atapatikana. Alipopigiwa simu Ihucha alijieleza mzee akamwelewa. Mwandishi anasema:

> “Mwanangu! Imekuwaje mambo kama haya yanatokea hamtupi taarifa mpaka tunayaona kwenye magazeti? Au sio Farida mtoto wetu tuliyemwona kwenye gazeti anatangazwa kuwa kapotea?” Ilikuwa sauti yam zee Kimambo,baba yake Farida. (Uk. 38).

Nadharia ya uhalisia katika mhimili usemao: uyakinifu:kueleza mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Wahusika wamepewa sifa kulingana na hali halisi ya masiha yao kazini pamoja na majumbani mwao na katika biashara walizozifanya kwa ajili ya kujipatia kipato. Uwajibikaji ndiyo nguzo kuu katika hali halisi ya masiha ya binadamu. Kila mmoja anapaswa kufanya kazi ili ayasongeshe maisha.

Sengo, (2009) anaeleza kuwa jamii ina mgawanyo wa majukumu ili kuhakikisha kila mtu anafanya kazi ili kujipatia riziki. Mwanaume kwa mwanamke wote wanatekeleza wajibu kwa kufanya kazi. Mwanaume anaenda kazini kutafuta riziki kwa ajili ya kulisha familia na mama anabaki nyumbani kutekeleza majukumu yake ya kifamilia. Katika riwaya ya *Tumaini*, wanaume pia wamesawiriwa kwa kupewa sifa nzuri kulingana na matendo yao. Shabani

ambaye ni babake mdogo wa Tumaini ana sifa nzuri za kujitoa kuwasaidia watoto wa kike bila kuwakatisha tamaa. Alikuwa akipenda wanae wasome hata kama yeye hakupata elimu ya juu. Alimhamasisha mwanae Riziki kuwa asome mpaka atakapochoka,yeye yuko tayari kumhudumia. Hata Tumaini alipokimbilia kwake akitoroka wazazi wake wasimfanyie tohara na kumwozesha, alitiwa moyo kuendelea na masomo. Tumaini alisomeshwa na mzee Shabani kwa kushirikiana na mkewe Halima hadi chuo kikuu na akafaulu vizuri masomo. Mwandishi anaeleza:

> Shabani na mkewe hawakuona umuhimu wa kuyapeleka mashtaka dhidi ya mzee Masumbuko kwa Chifu Andrea. Walifahamu njama za mzee huyo na Chifu. Kwahiyo waliamua kumsomesha Tumaini hadi akamilishe elimu yake ya shule ya msingi. (Uk. 67).

Sifa ni kijana mchapakazi na mpenda masomo. Alikuwa mshauri mzuri wa Tumaini juu ya masomo na kumhimiza kutia bidi katika kusoma. Alikuwa mstaarabu hata alipofika nyumbani kwa mzee Shabani, wote walimpenda kwa namna alivyojitambulisha kwao.

Mwandishi anaeleza:

> Tumaini alimheshimu Sifa ambaye nyaraka alizomwandikia hazikuwa na uchokozi wowote au hila za kumtaka kimapenzi. Alitambua kwamba barua zake hazikuwa na lengo baya.  (Uk. 117).

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: mwanafunzi si mpokezi tulivu wa habari, utambuzi mazingira na tabia vinaathiriana katika upataji wa habari wa mwanafunzi. Hii inaonyesha kuwa wanaume hawa katuka jamii zao walifunzwa kuwa na sifa nzuri ambazo wanaziakisi katika utendaji wao wa mambo mbalimbali katika jamii. Wahusika wanaonesha matendo haya mazuri

waliyatenda kwa ajili yao,wenzao walio karibu nao pamoja na jamii kwa ujumla. Hii ndiyo huwa faida ya malezi kwa wanajamii. Ngaiza, (2002) anaeleza kuwa matatizo mengi yanayozikumba jamii kutosonga mbele kimaendeleo, yanatokana na kosa lililofanyika kwenye malezi na hivyo kuwapelekea watu kutokuwa wapenda kazi, wapenda kubagua gazi na kutomakinikia kazi mara wanapozipata.

Mzee Majaliwa ni baba mzazi wa Sifa. Alithamini sana elimu na kuitilia mkazo. Alikuwa akimpa zawadi Sifa kila alipokuwa akifaulu vizuri masomo yake ili kumjengea motisha ya kutia bidi zaidi ili afanikiwe. Mzee Majaliwa alifahamika sana kwa busara yake katika jamii. Hata Shabani alipojua kuwa Sifa ni mtoto wa mzee Majaliwa walifurahi sana.

Mwalimu Johnson ni mwalimu wa Tumaini ambaye alikuwa na maadili ya kazi yake. Alikuwa akijituma sana kufanya kazi na kuhakikisha wanafunzi wake wanafaulu vizuri masomo yao. Tumaini alipodondokewa na nyoka akiwa anajisomea chini ya mti, mwalimu huyu alitumia muda mwingi kumpa ushauri nasaha Tumaini ili aweze kurudia hali yake ya kawaida na kupata nguvu za kufanya mtihani. Alijitahidi sana mpaka Tumaini akawa vizuri,akaacha uoaga na kulia ndipo akaweza kufanya mtihani siku hiyo. Mwandishi anasema:

> Hapo mwalimu Johnson wa somo la Fizikia alimkabili Tumaini na kutishia kumpiga kofi kali jambo lililomshtua na kumrejesha katika hali ya utulivu. Mwalimu aliamini hiyo ndiyo njia nzuri ya kumfanya

> aone mambo katika uhalisi, na sio ule wehu aliokuwa nao wakati huo. (Uk. 120).

Vile vile katika riwaya ya *Dago wa Munje*, tunaona pia wahusika wa kiume walivyopewa sifa nzuri. Baba Dago alikuwa mchakalikaji kweli. Kila siku aliamka mapema kwenda kutafuta vibarua ili apate pesa kwa ajili ya kuitunza familia yake. Vilevile baba Dago aliwapenda sana wanae wa kike na kuwapa elimu. Aliwasisitiza kuwa wasome na atajitahidi kuwapatia matumizi ya shule licha ya kuwa na uwezo mdogo. Aliumia sana Nchimoni kushindwa kuendelea na masomo ya sekondari sababu ya kukosa pesa za kumlipia. Alijieleza kwa mwalimu mpaka Nchimoni akapata nafasi ya kwenda chuo cha ualimu na akafanikiwa kupata kazi. Baba Dago ni mzazi wa kiume anayewathamini watoto wa kike. Aliumizwa sana na Swafiya kuachishwa masomo kwa kubeba mimba akiwa mwanafunzi. Hakuwa na la kufanya ikabidi tu Swafiya atulie kwa nyanya yake akisubiri kujifungua.

Mwalimu Sifa alikuwa mwalimu wa Dago ambaye alikuwa akimfuatilia kila mara ili aweze kujua tatizo linalomfanya achelewe kuja darasani kila siku na pia kwanini anakuwa mchafu muda wote na hatilii maanani masomo. Mwalimu Sifa alitumia muda wake mwingi kutafuta taarifa za Dago na ndipo alianza kumuadhibu bila kuona mabadiliko. Aliamua kuwajuza wazazi wake taarifa hizo ili washirikiane na mwalimu kujua kinachompelekea Dago kuwa vile. Mwalimu Sifa alifanya kazi yake kwa moyo na uadilifu pia.

Juma na Rashidi ni marafiki zake Dago ambao wana upendo wa kweli kwa Dago. Walikuwa wakimfuatilia kwa kila hatua ilinwajue ni kwanini anachelewa kuja darasani na kwanini anapofika anakuwa mchafu. Walikuwa wakienda hadi nyumbani kwao kumfuatilia endapo hajaonekana shuleni. Walikuwa wakimpitia mara kwa mara ili waende kuoga na kufua mtoni mama Dago hakupenda kufua wala kuoga. Hata wazazi wa Dago waliwatambua Juma na Rashidi kama marafiki wa kweli wa Dago maana walijitoa kumsaidia mengi ili kubadilisha tabia yake.

Nadharia ya uhalisia mhimili usemao:wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii. Hapa tunawaona wahusika wa kiume namna walivyochorwa kutokana na historia za familia pamoja na jamii zao ndizo zilizowapelekea kuwa kama walivyoainishwa. Jamii ndiyo chombo kinachomkuza mhusika na ndicho huona kuwa kinachotendeka siyo sawa au vinginevyo. Paik, (1994) anaeleza kuwa mambo yaliyomo katika jamii kama vile runinga ndiyo huleta athari za kitabia na ndipo jamii huanza kufanya tathmini ya tabia hizo.

### 5.1.2 Kumdunisha Mwanaume

Waandishi wanawake wa Kenya na Tanzania pia wamefanana katika kumdunisha mwanaume katika matendo mbalimbali ambayo mwanaume amechorwa kwayo. Kwa kuanza na riwaya ya *Kipimo cha Mizani* ya Zainabu Burhani wa Tanzania, tunawaona wanaume wakifanya yafuatayo:

Umari alionekana akiwa mbabe sana na mtovu wa nidhamu kwa kaka yake Amini kuhusiana na mali za urithi. Amekuwa ni kijana ambaye hajui mipangilio ya maisha kulingana na kipato alichonacho. Amekuwa ni mtovu wa nidhamu pia kwa mzee Hasani ambaye ana umri sawa na baba yake kwa kumsemea vibaya ili aweze kupata mwanya wa kuchukua pesa dukani kwa Amini. Umari ameishi maisha ya utegemezi kwa kaka yake ilhali yeye na mkewe wanafanya kazi na wanapata mishahara yao. Kila mara alikuwa akizozana na kaka yake Amini ila Halima ndiye alikuwa akiepusha ugomvi baina yao. Mwandishi anasema:

> Halima anastahili hayo kwani hakupenda kugongana naye wala hakupenda kuona ugomvi baina ya Amini na ndugu yake. (Uk. 42).

Vile Umari amekuwa mdhaifu sana kwa mkewe kwa kumsikiliza kwa kila alichokipanga bila kumkosoa. Umari anaujua uwezo wake wa kipesa ila bado Maryamu anaamua wahamie nyumba mpya ghorofani, wanunue kila kitu kipya ndani ya nyumba na kufanya sherehe kubwa ya kualika watu kama harusi, bado anamkubalia bila kujua hizo pesa zitatoka wapi. Aliishi kwa kudaiwa na kuwa ombaomba kwa Amini na wakati mwingine kuibua ugomvi baina yao alimradi tu atekeleze alichokipanga Maryamu.

Umari amekuwa mdhaifu kwa Maryamu hata pale alipotenda matendo yasiyofaa alishindwa kumkanya au kumwambia ukweli. Mfano, Ali na wadogo zake walikuwa wakinyanyaswa sana kwa kunyimwa chakula na kufanyishwa kazi ngumu kuliko umri wao. Ilifikia wakati wakazuiliwa kwenda shule wakawa wanabaki tu nyumbani ila watoto wa Umari pekee ndo

wanaenda shule. Yote haya aliyaona ila hakuweza kuyakemea. Kilichoshangaza zaidi, Maryamu aliwafukuza watoto hawa kuwa wamfuate mama yao ilhali hawajui halipo na wala hawajui popote kiuelekeo. Aliporejea nyumbani hakuwaona ndipo akaulizia watoto walipo.

Maryamu akamjibu kuwa walikuwa wakisumbua wanamtaka mama yao akaamua awafukuze wamfuate huko aliko watoe kelele. Umari alisikitika tu na kusema kuwa kwa umri wao ni lazima wamhitaji mama yao. Hata hivyo hakumsema Maryamu kuonesha kakosea kufanya kitendo hicho. Umari hakuangaika hata kidogo kuwatafuta wale watoto wa kaka yake.

Mwanaume anaonekana mtumia lugha mbaya awapo ofisini. Mfano, Dr Juma anatumia lugha kali mno na ya kiburi akiwa kazini kumbe anatetea uovu uliopelekewa na rushwa aliyopewa na Umari ili kumnyanyasa Halima. alimjibu Halima baada ya kuona anafuatilia taarifa za Halima. Mwandishi anaeleza.

> Wewe mpya hapa, sivyo? Alipoitikia aliendelea. Sikiliza! Mimi ndiye hapa, sio wewe! Nitakapohitajia ja1ada 1a mgonjwa yeyote nitakuarifu ....(Uk. 9).

Vile vile mwanaume anaonekana kuwa pale anapojitoa sana kunakuwa na kitu anachokiwinda kama malipo mbele yake. Hawafanyi kitu kizuri bila kutegemea malipo Fulani ya jambo. Kwa mfano, Selemani alikuwa rafiki yake mkuu na Amini na akawa anawashauri familia kwa kujitoa. Cha ajabu baada ya Amini kufariki yeye ndiye alikuja kumposa Halima. Daktari Isa alikuwa akifanya kazi vizuri na Salama na kumpa ushirikiano mzuri katika

kuwahudumia wagonjwa. Salama alifurahia ushirikiano wa huyu. Mwishoni mwa kitabu yeye ndo alikuja kumposa Salama. Mwandishi anasema:

> Mzee Hasani alimletea habari za furaha, kuwa Halima amekubali posa za Selemani lakini hakutaka sherehe wala ghasia zozote. (Uk. 231).

Salama alimwambia Halima habari za uchumba wake na Daktari Isa.

Mwandishi anaeleza:

> Kweli,basi ameniposa, na harusi itakuwa karibu. Baada ya miezi mitatu tu. (Uk. 232).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kutoonesha udikteta katika familia zao na jamii inayowazunguka. Mhimili huu unawataka wanaume kubadilika na kuacha tabia mbaya ambazo zinawafanya waonekane dhaifu katika jamii na badala yake kuwa washaurianaji na wake zao. Haimtaki mwanaume kuwa mtii wa kila kitu bali kuwa mtu wa kushauriana kimaamuzi. Masingele, (2012) anaeleza kuhusu mabadiliko ya riwaya katika miaka ya 1970 hadi 2011 ambapo anafafanua kuwa riwaya ya kiswahuli huwa na mabadiliko ya kidhamira ambayo yanasungamana na matukio yanayoibuka kutokana na binadamu kupitia changamoto katika nyanja mbalimbali za maisha. Madiliko hayo huwa ni dhamira zinazowahusu wahusika ili kuweza kubadilika kwa kutenda matendo mazuri na kuacha mabaya yanayowakwamisha kimaendeleo.

Mzee Hasani pia amedunishwa katika maisha aliyokuwa akiyaishi. Huyu mzee alikuwa na wasifu mzuri sana alipokuwa kazini maana alipendwa na kuthaminiwa kazini kwa uchapakazi wake pamoja na uaminifu. Mzee huyu alifanya biashara ndogo ndogo nje ya ajira yake na akawa akijipatia kipato.

Cha kushangaza mzee Hasani alikuwa akiishi mazingira magumu sana kwenye nyumba yake duni. Baada ya kustaafu, licha ya kupata kiinua mgongo, hali ikawa mbaya sana kiuchumi ndipo akakubali kumfanyia kazi Amini dukani. Kwa wasifu wa mzee Hasani akiwa kazini alipaswa kuwa na maisha mazuri ya kuweza kujikimu badala ya kurudi kuwa muuza duka wa kupambana na matusi ya akina Umari.

Katika riwaya ya *Hiba ya Wivu*, mwanaume pia amedunishwa katika mambo kadhaa kulingana na matendo yake. Ihucha anakuwa mtii kwa wateka nyara na kusalimisha pesa zake kwa namna ambayo walimwambia bila kuzitaarifu mamlaka za kiusalama ili huyo mtu aweze kukamatwa. Kitendo cha mtekanyara kupiga simu na kujitambulisha anachokitaka kwa Ihucha, hiyo ndo ilikuwa njia nzuri ya kumkamata haraka. Ihucha alitii na kupeleka pesa bonde la mkwajuni huku roho ikiwa inamuuma maana elfu hamsini ilikuwa pesa nyingi.

Ray ambaye ni mwendesha teksi, anakuwa muongo kwa Ihucha kuwa yeye ni mteka nyara kumbe alikuwa katika mbinu za kumshawishi Farida aridhike kurudi kwa Ihucha bila matatizo na kisha waanzishe mahusiano ya kimapenzi. Anakuwa huru kabisa kumrubuni mke wa mtu ili aachane na mumewe aje kuoana na yeye. Ray ni kijana mdogo ambaye anajua kupambana kiutafutaji ila anakuwa na udhaifu wa kupenda wake za watu. Alipomwona Farida mwili ukawaka tamaa na ndipo mawazo ya kumtoa kwa Ihucha yakaja na mbinu

mbalimbali za uongo zikaanza kufanyika ili afanikishe hazima yake hiyo mbaya. Ray anapanga kuoa mke wa mtu. Mwandishi anasema:

> “Mwishowe nije kushikwa wizi,wizi ambao huitwa ugoni. Sitaki! Japo Farida namtaka. Namtaka sana, tena sio awe rafiki tu, bali namtaka awe mke wangu. Kaolewa ndio, lakini hata mie pia ni mwanaume.naweza kuoa. Kati ya wasichana waote niliowahi kuwaona, mtoto huyu wa kwetu kanimaliza. Nimempenda, nimemchagua, nitamwoa”. (Uk. 29).

Vile vile Ray anatumia mbinu hafifu sana ya kumshawishi Ihucha pamoja na jamii kuwashawishi waamini kuwa Farida alitekwa nyara. Kumnyoa Farida nywele akabaki na kipara yeye aliona ni kishawishi kikubwa kwa Ihucha na jamii kwa ujumla kuamini ilhali kunyoa nywele ni jambo la kawaida. Mwandishi anaeleza:

> “Utawaonyesha jinsi ulivyotendewa na majambazi,wataamini kweli ulitekwa nyara. Watabaki kukupa pole tu, maswali mengine yatawaishia”. “Nijiumbue vipi? Ninyoe kipara labda. kujiumiza siwezi………. “Uamuzi ni wako. Kalete wembe tuanze kukunyoa kipara. Saa kumi na moja sasa, saa zinakwenda”. Ray aliinuka akauendea wembe chumbani kwake. Kama utani, Farida alikaa chini, na Ray kwenye kiti,kazi ikaanza. Saa kumi na mbili na nusu, kichwa cha Farida kilikuwa cheupe, kama kafiwa. (Uk. 46-47).

Nadharia ya uhalisia mhimili usemao: usadikifu: yale yanayoiibuliwa katika jamii yawe yanasadikiwa na wasomaji. Inaonesha kuwa wahusika hawa wa kiume kwa namna walivyochorwa na waandishi ni kama walivyo katika jamii. Jamii nyingi za Kenya na Tanzania zina akina Ray wanaoendekeza tamaa za mwili mara wawaonapo wanawake. Wapo akina Ihucha ambao wanatii mambo bila kuyatafakari na wakati mwingine kujitia matatizoni. Mambo haya

huweka wazi ili jamii iweze kubadilika. Selemani, (2012) ambaye ametafiti kuhusu riwaya mpya ya Kiswahili na masuluhisho ya changamoto zake, anaeeleza kuwa mwandishi wa kazi ya fasihi huambua kuweka mambo kihalisia katika ulimwengu halisi ili kuwasilisha wazo hilo kwa hadhira iweze kulifanyia mabadiliko chanya.

Riwaya ya *Tumaini* iliyoandikwa na Clara Momanyi wa Kenya, tunawaona wahusika wa kiume kadhaa wakitenda matendo mbalimbali ya kuwadunisha. Mzee Masumbuko anakuwa mlevi kupindukia hadi anaogopwa katika familia na jamii nzima kwa vurugu anazozifanya nyumbani kwake na mtaani. Anaifanya familia inamuona mbogo hata mkewe Amina anashindwa kuwa huru kwa mumewe hata kumueleza jambo. Anaishi maisha ya kipekepeke kwa kujiamulia jambo bila kutaka kushauriwa. Mfano, suala la kumwozesha Tumaini lilipogonga mwamba baada ya Tumaini kutoroka nyumbani, mzee Masumbuko anawaozesha wadogo zake Tumaini wawili yaani Rehema na Mashaka bila wao kupenda. Alishauriwa na marafiki zake kuwa wale watoto ni wadogo wanaozeshwa kwa umri mdogo, wataishi maisha ya shida. Rehema anaozeshwa kwa mzee ambaye ni makamo ya mzee Masumbuko, bado huyu baba hakujali wala kuwasikiliza waliomshauri juu ya hili.

Mzee Masumbuko anawapelekea wanae kuishi maisha magumu katika ndoa zao na kumtwisha mzigo Tumaini wa kuwatunza wadogo zake ilhali wako kwa waume zao ambao hawana uwezo hata wa kuwapeleka hospitali. Mzee

huyu anakuwa kielelezo kibaya kwa familia yake na jamii kwa ujumla kutokana na hizi tabia zake. Mwandishi anaeleza:

> Rehema sasa alikuwa na watoto wawili akiwa bado ana umri mdogo. Je, baada ya miaka kumi , amgekuwa na watoto wangapi? Swala kama hili na mengineyo yalimtia hofu Tumaini ,hasa alipoelewa kuwa mumewe Rehema hakuwa na uwezo wa kumkimu yeye na wanawe. (Uk. 114).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kusaidia wake zao na wanawake wengine katika jamii katika kujiendeleza kielimu na kikazi. Mzee Masumbuko anapaswa kubadilika na kuwa mwanaume mpya kwa kuwathamini wanawake akianza na mkewe pamoja na watoto wake wa kike. Aachane na tabia mbaya hata alizokuwa akimfundisha Idi kuwadharau dada zake. Aanze kuwapa nafasi katika maamuzi na kuwaruhusu kusoma mpaka elimu za juu badala ya kuwakatiza masomo na kuwaozesha bila ridhaa yao. Mabadiliko ndio msingi wa mabadiliko. Gromov, (2004) anaeleza kuwa riwaya ya Kiswahili imeweza kuchunguza jamii kwa kutumia mbinu mpya ikiwemo kueleza matatizo ya kijamii. Matatizo hayo huwaweka wanajamii katika hali ya kuwataka kubadilika na kuwa wapya kama mbinu mpya zitumikazo kueleza matatizo hayo.

Mzee Okwemba anaishi maisha magumu katika mji wake hana mtu wa kumsaidia hata anapougua. Anadunishwa kwa kujifungia peke yake nadani ilhali anajua hana uwezo. Alipaswa kutoka nje na kuomba msaada kwa watu na badala yake anajifungia ndani kwa kulala na kushinda njaa. Anadunishwa kwa kujitenga na watu wakati shida humalizwa na watu. Hakuwahi kuoa wala

kuwa na mtoto. Jamii nzima ilikuwa ikimshangaa kwa kuishi maisha ya upweke wakati alipaswa kuwa na familia yake. Tumaini alikuwa akipita njia hiyo na kumjulia hali huyu mzee maana alikuwa karibu na nyumba ya mzee Shabani. Mwandishi anaeleza:

> Mara nyingi Tumaini alimsaidia mzee huyu kusafisha kijumba kile,mbali na kumtekea maji na kumchanjia kuni. Kwa sababu ya usaidizi wake, mzee Okwemba alimpenda sana Tumaini. (Uk. 81).

Mwalimu mkuu Bwana Majaaliwa alikuwa akiwapangia wanafunzi wake hasa wa kike masomo ya kuendelea nayo. Aliwanyima nafasi watoto wa kike kujisomea masomo ya sayansi akihisi hawatayafanya vizuri. Huu ni udhaifu mkubwa kwa mwalimu maana yeye ndiye anapaswa kuwajengea mbinu za kufaulu masomo hayo badala ya kujikita katika dhana za kusadikika kuwa wasichana hawawezi masomo ya sayansi. Tumaini alimdhihirishia kuwa hiyo dhana haina ukweli. Mwandishi anasema:

> "Nimesema masomo ya sayansi yasijazwe. Nyie wasichana ni vigumu sana kufuzu katika masomo haya. Kwanza ni wasichana wangapi ambao umesikia hufuzu u chuo kikuu, enh? Wewe unataka kuiletea shule yangu aibu?" Mwalimu alitamka kwa hamaki ili kumvunja moyo Tumaini. (Uk. 115).

Nadharia ya uhalisia mhimili usemao: Mshikamano. Inaonesha kuwa dhana ya wanaume kuwadharau wanawake katika mambo mbalimbali ya kijamii ni jambo ambalo lipo. Kulimaliza hili jambo ni lazima jamii iwe na mshikamano. Wanaume huwadharau wanawake katika mambo mengi ikiwemo masomo. Jamii inaamini kuwa masomo ya sayansi ni ya wanaume ingawa wako wanawake wanaikataa hiyo dhana na kufanya vizuri katika masomo ya sayansi kama alivyofanya Tumaini ila bado jamii haijakubaliana na hilo hasa

wanaume. Mshikamano ndio utakaowawezesha wanajamii kukubali mabadiliko. Ponera, (2010) anaeleza kuwa kazi za fasihi zinasaidia kumaliza matatizo mengi yaliyomo katika jamii zikiwemo kazi za Shaban Robert zinazoeleza malezi kwa familia,kujenga maadili na kuimarisha mshikamano ili kuleta mabadiliko chanya katika jamii.

Chifu Andrea anaonyesha udhaifu mkubwa wa kuendekeza ngono kwa wanafunzi badala ya kuwasaidia shida zao kwa mujibu wa taratibu za kazi yake. Alimtaka Tumaini kimapenzi baada ya kukataliwa aliamua kutoa jina lake kwenye orodha ya wanafunzi walio na uwezo mdogo wanaostahili kufadhiliwa. Kosa hili lilimpelekea Chifu Andrea kusimamishwa kazi baada ya kubainika maana alikuwa hana la kujitetea kwa vile upuuzi huu alikuwa akiufanya kweli wakati naye ni mzazi. Mwandishi anasema:

> D.O alimvaa Chifu Andrea kwa hasira,akamtia kwenye mizani ya ukweli. Kwa upande wake, chifu huyu hakupenda kuutaja ukweli ,hali hakuwa na budi kutamka kwa kinywa chake. Ukweli ukidhihiri, uongo hujitenga. “Kusema kweli Bwana D.O –eeer,” chifu alianza kubwabwaja, lakini D.O akawa anamhimiza huku macho yamemtoka kwa wingi wa hamaki, “Ukweli chifu sema ukweli.”. (Uk. 102).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao: kuwaona wanawake kama viumbe sawa na wanaume kwa kuwaheshimu na kuwapenda katika kila nyanja wanazokuwepo. Chifu Andrea anapaswa kubadilika awe mwanaume mpya kwa kutowang’ang’aniza wanawake katika mahusiano ya mapenzi. Hili limeelezwa na Khatibu, (2011) ambaye ametafiti juu ya chanjo ya matakwa ya mwanaume katika mwili wa mwanamke akilinganisha mashairi ya Muyaka

Bin Haji nay a Shaban Robert. Ameeleza kuwa waandishi wengi wamekuwa na matatizo katika kumjadili mwanamke hasa mwili wake. Amehitimisha kuwa chanjo ya hili ni kumweleza mwanamke ukweli ambao utamfanya awe mkali na kuwa na msimamo ili mwanaume aweze kubadilika katika kumtazama kwa jicho la tamaa. Wanaume huyu anapoacha haya juu ya mwanamke ndipo anakuwa mwanaume mpya.

Katika riwaya ya *Dago wa Munje* pia wahusika wa kiume wamedunishwa kwa namna mbalimbali. Dago anakuwa na tabia mbaya nyingi kiasi kwamba jamii nzima inamshangaa na kuhisi ana matatizo. Hapendi kusoma, hapendi kuoga, kufua, wala kumsaidia mama yake kazi na ni kijana mkubwa. Dago amekojoa kitandani mpaka anapoishia kusoma. Kwa kawaida tabia zote hizi kwa mtoto mkubwa wa vile lazima jamii ihisi kuna tatizo.

Baba Dago anakuwa na pilika za utafutaji pesa badala ya kumkalisha chini mwanae Dago ili kujua ni matatizo gani yanampelekea kuwa na tabia zote hizo mbaya. Hata alipotakiwa mzazi kwenda shule,alienda mama yake mara zote. Mwandishi anaeleza:

> Alipoamka leo asubuhi alijikuta taabani katika shida nyingine. Nguo zake alizozilalia jana usiku zilikuwa zimetota. Hazikutota kwa kunyeshewa na mvua tu, zilitota pia kwa mikojo. “Nthsye”, Dago alitoa sauti kwa hisia za uchungu aliouhisi. (Uk. 4-5).

Mama Dago alilalamika kwa mumewe jinsi alivyomuachia suala la malezi peke yake. Mwandishi anasema:

> “Naam, wanapokuwa na tabia njema tuwatie moyo wa Imani waendelee na wanapozibua tabia mabaya,tuwaongoze sote wawili. Lakini wewe kazi yako iko mbele. Umeniachia peke yangu, wavulana kwa wasichana”! Alisema mama akijiondolea lawama. (Uk. 116).

Nadharia ya mwanaume mpya mhimili usemao; kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume. Mhimili huu unamtaka Dago na baba yake kubadilika na kuwa wanaume wapya. Baba Dago anapaswa kujua majukumu yake katika malezi na siyo kumwachia mke wake pekee kupambana na tabia za Dago za utoro shuleni na uchafu. Anapaswa ajue kuwa pamoja na kutafuta pesa kuwahudumia wanae na masomoni , kuwafuatilia kitabia nalo ni jukumu lake. Dago anapaswa kubadilika kuacha tabia za kukojoa kitandani na kuhudhuria masomo, kumsaidia mama yake kazi ndipo atakuwa mwanaume mpya. Hapa suala la malezi linahusika kumfanya kijana awe na tabia mbaya au mzazi aonekane hakuwajibika ipasavyo. Daudi, (2013) anaeleza kuwa dhihaka na kejeli ni vipengele ambavyo watunzi wa kazi za fasihi huvitumia kufikisha ujumbe. Mbinu hii hufikisha ujumbe kwa wasomaji na hadhira lengwa kwa ujumla kupitia dhamira mbalimbali ikiwemo kubadilika kimalezi pamoja kuacha tabia zisizofaa.

### 5.1.3 Mfanano wa Mwanaume katika Kukabiliana na Mitihani ya Maisha

Katika riwaya ya *Kipimo cha Mizani* tunaona mwanaume anaonyesha udhaifu katika kukabiliana na mitihani inayomkumba katika maisha. Mzee Hasani baada ya kustaafu uchumi uliyumba mno akawa anaishi maisha ya shida. Badala ya kutafuta namna ya kujikwamua, aliamua kujitenga na watu akaishi

kipekepeke nyumbani kwake. Hii ilidhihirika wakati Amini akitafuta taarifa zake ili kujua alipo aweze kuongea naye aje kuuza duka. Amini aliulizia sana ila alikosa mwenye taarifa za wapi alikokuwa mzee Hasaani na ndipo aliamua kwenda nyumbani kwake akamkuta akiwa na maisha magumu mno. Mtu anapokuwa na anwani ya kupatikana linakuwa jambo jema hasa anapohitajika. Hili linadhihirishwa na Bi Riziki baada ya Rajabu kupata kazi. Mwandishi anasema:

> Umeniondoshea wasiwasi mkubwa, maana sasa nitajua Rajabu yuko wapi wakati wote. Na pia atakuwa ameshughulika, ataepukana na ule uibilisi wa vijana wengine (Uk. 39).

Katika riwaya ya *Hiba ya Wivu* tunamwona Sikujua baada ya kutoka gerezani kwa kosa la kumuua rafiki yake, anaamua kujitenga na wenzie katika jamii. Hakutaka kukaa na wanaume wenzie bali alikaa na marafiki wa kike tu ambao alikuwa na mahusiano nao ya kimapenzi hasa Fatuma. Wanaume wenzie alikuwa kama anawakimbia nao wakakosa namna ya kumshauri kuhusu mbinu mpya za kuishi mtaani.

Riwaya ya *Tumaini* tunawaona wahusika wakikabiliana na mitihani kadha wa kadha katika maisha yao. Mwalimu Johnson alikabiliana na tatizo la mwanafunzi kudondokewa na nyoka huku akijiandaa kuingia kwenye mtihani. Mwalimu alipomkuta Tumaini akilia kwa nguvu alishindwa kujua ni nini kimempata. Alikabiliana na hilo tatizo lililotokea akiwa kazini mpaka akahakikisha amelimaliza. Chifu Andrea alipotaka kufukuzwa kazi kwa kosa la kumwondoa jina lake Tumaini katika orodha ya wafadhiliwa, alikana kabisa

hilo jambo na kusema yuko tayari kukabiliana na hali yoyote alimradi tu asikubali kosa. Mzee Masumbuko alijitia matatizoni kwa kwenda kumwomba mzee Suleimani ili mwanae aitwaye Mbarouk aje kumposa Tumaini. Walikuabaliana yote hayo ila Tumaini akatoroka kabla wageni hawajaja. Siku ya akina Suleimani kuja kuleta posa, Mzee Masumbuko badala ya kueleza tatizo ili wamsaidie kulitatua anakuwa mkali kupita kiasi na kuwafukuza ambao wangemsaidia. Mwandishi anasema:

> Mzee Masumbuko alimkatiza kwa kusema, “Semeni mliyoyajia , na kama hamna la muhimu , inukeni mwende zenu. Mimi najua mipango yenu yote. Majungu mliyapika yakapikika. Sasa mwajitia hamnazo. Mmenitia izarani,kisha mwaja hapa kunicheka. Tokeni! Nasema tokeni!” Alipaaza sauti huku midomo ikichezacheza na macho yamemtoka pima kwa wingi wa hamaki. (Uk. 40).

Vile vile riwaya ya *Dago wa Munje* tunawaona wahusika wakiume wakikumbwa na mitihani ya maisha. Kijana (Charo) aliyempa Swafiya mimba alisongwa sana na jamii kuwa anapaswa awajibike kumtunza na kumhudumia Swafiya mpaka ajifungue. Kijana alikataa katakata na kuamua kuhama eneo hilo ili akwepe jukumu hilo. Baada ya kijana kukataa ilibidi Swafiya apelekwe kwa nyanya yake kwa ajili ya kujifungulia huko. Mwandishi anaeleza:

> Jambo lililokuwa gumu zaidi na la kuwabugudhi wazai hawa ni kwamba mvulana aliyemhadaa Swafiya, alimkana binti yao. Mvulana huyu aliitwa Charo, na alikuwa tayari amerudi kwao wilaya ya Kilifi. (Uk. 40).

Vile vile Swafiya baada ya kufukuzwa shule, baba Dago aliona kukaa naye pale kwao itazidi kuwa aibu kubwa kwa familia na ndipo aliongea na mama Dago ili ampeleke kwa nyanya akajifungulie huko. Yule ni binti yao ila

hawakuwa tayari kukaa naye kumhudumia hadi kujifungua ilhali shule kaishafukuzwa. Mwandishi anaeleza:

> Dada yake kitinda mimba,alikuwa akiitwa Swafiya. Huyu hakuishi pale nyumbani na wazazi wake, bali alikuwa amesafirishwa kwenda kuishi na nyanya mzaa mama, aliyeishi mbali na pale kwao nyumbani. Alihamishwa pale nyumbani kwa sababu alikuwa mjamzito. (Uk. 34).

Kufanana kwa waandishi hawa kunatokana na sababu kadhaa, kwanza wote ni waafrika na zaidi kuna mwingiliano mkubwa kati ya jamii za Kenya na Tanzania. Kazi zao zimeandikwa katika nyakati zinazokaribiana hivyo mfanano lazima uwe ni mkubwa kuliko utofauti.

## 5.2 Kutofautiana kwa Waandishi Wanawake wa Kenya na Tanzania

### 5.2.1 Kukabiliana na Mitihani ya Maisha

Waandishi hawa wametofautiana kwenye jambo la wahusika wa kiume katika kukabiliana na mitihani ya maisha inayowakumba. Waandishi wa Kenya wameonesha kuwa wahusika wa kiume wanavyokumbana na mitihani ya maisha huikimbia na kuhamia kwingine kama njia ya kuitatua mitihani hiyo. Wengine hukataa kabisa jambo lililotokea kuhusika nalo na wachache hukabiliana na tatizo.

Kwa mfano,katika riwaya ya *Dago wa Munje* iliyoandikwa na Sheila Ryanga wa Kenya, kijana aliyempa mimba Swafiya aitwaye Charo, ili kukimbia jukumu la kumtunza Sawafiya aliamua kutoroka lile eneo na kukimbilia kwingine ambako ni wilayani kwao ili asilibebe lile jukumu. Hata hivyo alikana kuhusika na ule ujauzito. Katika riwaya ya *Tumaini* iliyoandikwa na

Clara Momanyi wa Kenya, Chifu Andrea alikana kabisa suala la kumtaka Tumaini kimapenzi na kuhusika kutoa jina lake kwa kutaka binti huyo akubali ombi lake. Waandishi wa Tanzania wamewasawiri wahusika wa kiume kuwa ni wasiri mno na hawataki kuweka matatizo yao hadharani kama njia ya kutatuliwa kwa tatizo. Hujitenga peke yao na kuendelea kuishi kwa kuumia na hayo matatizo.

Kwa mfano mzee Hasani katika riwaya ya *Kipimo cha Mizani* ya Zainabu Burhani wa Tanzania aliona ni bora atulie nyumbani kwake huku akiendelea kuumia na matatizo yake ya shida za kiuchumi. Aliteseka huko mpaka Amini alipomleta kuja kuuza dukani. Vilevile Sikujua katika riwaya ya *Hiba ya Wivu* ya Zainabu Mwanga wa Tanzania alipotoka gerezani alikuwa hana pesa na alikuta maisha yamebadilika kijijini akawa hajui wapi pa kuanzia. Badala ya kuchangamana na wenzie wamsaidie kumpa mbinu ya kujinasua kwa tatizo hilo, aliishi kwa kutumia pesa za benki akiwa na mpenzi wake Fatuma bila kujua zikiisha ataishije. Hata mzee Okwemba katika riwaya ya *Tumaini* ya Clara Momanyi wa Kenya, aliishi peke yake akijitafutia mahitaji kwa kuchuuza samaki licha ya kuwa mzee hakutaka kuweka wazi shida zake ili asaidiwe.

### 5.2.2 Mtazamo wa Waandishi kuhusu Ushujaa wa Wahusika wa Kiume

Waandishi pia wametofautiana kimtazamo. Tunapomuangalia mwandishi wa Kenya Clara Momanyi, licha ya kuwa mwanaharakati wa mtazamo kike, bado kuna wanaume amewatazama kichanya zaidi katika kazi yake. Kwa mfano,

mzee Shabani amechorwa kuwa ni shujaa katika kuwapambania wanawake ili kupata elimu. Anawasomesha Riziki na Tumaini hadi chuo kikuu na anakaa vizuri kwa kusikilizana na mkewe Bi Halima. Hata hivyo anamchora mzee Masumbuko hasi zaidi. Ana mtazama kama mbeba maovu mengi katika familia yake katika jamii. Anaogopwa katika familia na nje ya hapo kwa namna anavyokuwa mbogo kuutetea uovu wake anaoufanya kwa kujificha katika mwavuli wa ulevi. Familia inakuwa ya kunyanyasika bila kuwa na matumaini ya mzee huyu kubadilika. Mfano, Uk. 51 mzee Masumbuko anasafiri kwenda Maunguja huko Mombasa kwa mzee Suleimani kumtaka mwanae Mabruk amwoe Tumaini ila anamficha mkewe lengo la safari. Anawasababishia wanae kuishi maisha ya shida kwenye ndoa zao kwa kuwaozesha kwa wazee sana na familia zisizo na uwezo kiuchumi mfano, Rehema na Mashaka wanaishi ndoa za shida sana hadi Rehema anapougua inabidi Tumaini ndiye atoe pesa ya kumpeleka hospitali kwa vile mumewe hana pesa kabisa.

Nadharia ya ujifunzaji, mhimili usemao:ujifunzaji hutokea kwa kuchunuza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Mhimili huu unaonesha kuwa tabia za ubabe au upole hufunzwa katika familia na jamii alimokulia. Matokeo ya mafunzo hayo hujidhihirisha katika tabia za mtu awapo mtu mzima.

Hata hivyo uhalisia unatueleza kuwa na mshikamano katika kuziondoa tabia zisizofaa katika jamii. Na nadharia ya mwanaume mpya inamtaka mtu kama mzee Masumbuko kubadilika na kuwa mwanaume mpya anayemthamini

mkewe na watoto wake wa kike kama walivyo wanaume.hili limefafanuliwa na Ndungo, (1998) akizungumzia suala utamaduni na malezi kwa mtoto wa kike. Anafafanua kuwa,jamii hukuza msingi wa tabia na mtazamo wa watu wake. Mwanamke huzingatia mielekeo na itikadi za jamii anamoishi hata kama ni mfumo wa kuumeni.

Sheila Ryanga, anakuwa na uvumilivu kidogo kwa namna anavyowachora wahusika wake wa kiume. Anamtazama mhusika wa kiume kama mtenda makosa ila ambayo yanashaurika na kubadilika. Baba Dago anawajibika kutafuta pesa kwa ajili ya kuwasomesha watoto wake wa kike. Nchimoni anapokosa kwenda sekondari sababu ya babake kukosa pesa ya kumlipia, bado anachukua jukumu la kujieleza kwa mwalimu na Nchimoni anatafutiwa chuo cha ualimu anakwenda kusoma. Baba Dago anakuwa mbali na malezi ya watoto na kumuachia mama Dago ila anakuwa katika shughuli za kuangaika kupata pesa kwa maana alikuwa akifanya kazi za nguvu mno. Haya hujikita katika mifumo ya jamii zao zilizowakuza kama tuonavyo katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii mhimili usemao: ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Jamii zinazotukuza ndizo zinatupelekea kuwa kama tulivyo.

Waandishi wanawake wa Tanzania nao wanawaona wanaume kuwa ni mashujaa wa aina yake ila ushujaa wao ni wa kificho. Hawataki kujionyesha kuwa nao wanakumbwa na mitihani kama wanadamu wengine. Wanadhani kwa vile ni wanaume basi mitihani inawapita mbali. Kwa mfano, mzee Hasani

anaamua kukaa nyumbani kwake bila kueleza popote shida yake. Na Sikujua anakufa na tai shingoni huku anakabiliwa na shida ya kiuchumi. Hataki kuonesha kuwa naye ana mkwamo mahali. Hata Daktari Juma baada ya kuona suala la yeye kumnyanyasa Salama ilhali ana haki ya kupata huduma kama wagongwa wengine pale hospitali, anaamua kumshitaki Salama ambaye analichokonoa hili. Lengo ni kutaka asionekane kuwa naye anatenda maovu kwa shinikizo la rushwa. Hii inaoneshwa Uk.176 katika *Kipimo cha Mizani*.

### 5.3 Hitimisho

Wanawake wa Tanzania na Kenya wamewachora wahusika wa kiume kwa namna tofauti na pengine wamefanana. Hii ni kwa sababu ya jamii zilizowakuza kutofautiana kitamaduni.

Kutokana na matokeo ya utafiti inaonesha kuwa usawiri wa wahusika wa wahusika wa kiume na waandishi wanawake katika dhamira, taswira na mitazamo inayoibuliwa kuhusu wahusika wa kiume, uandishi wao haufanani,wako ambao wanakuwa hasi zaidi na wengine chanya zaidi. Hii hutofautiana kulingan na tamaduni zilizomkuza mwandishi na mazingira aliyomo mwandishi. Wako ambao wamekabiliana na mazingira yote hasi na chanya. Kwa mfano mwandishi anaweza kulelewa na mzazi wa kiume mkali sana ila akaolewa na mwanaume anayemjali na kumthamini, huyo ataakisi hali zote katika uandishi wake. Katika kazi hizi nne za waandishi wanawake wa Kenya na Tanzania zote zimeibua taswira hasi na chanya kwa wahusika wa kiume ambazo zimo katika jamii za Kenya na Tanzania. Pamoja na

kutofautiana ila kazi zao sehemu kubwa zinafanana kwa maana jamii nyingi za Afrika Mashariki mambo wayatendayo yanashabihiana kama siyo kufanana kabisa. Schermerhorn, (1960) anaeleza kuwa dunia yoyote ile ina watu wa aina zote yaani watendao mambo hasi na watendao chanya na hiyo ndiyo jamii. Wanajamii ni wamoja ila huweza kutofautiana kutokana na tamaduni zao zilizowakuza na kuwaongoza.

# SURA YA SITA

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 6.0 Utangulizi

Sura ya tano imehusu ulinganishi na ulinganuo wa waandishi wa kike wa Kenya na Tanzania kwa mujibu wa kazi teule. Katika ulinganishi tumejadili vipengele vya kumsifu mwanaume, kumdunisha na mfanano wa mwanaume katika kukabiliana na mitihani ya maisha. Vile vile, katika kuwatofautisha vimejadiliwa vipengele vya kukabiliana na mitihani ya maisha pamoja na mtazamo wa waandishi kuhusu ushujaa wa wahusika wa kiume sura hii ndiyo ya mwisho, hivyo inatoa muhtasari, hitimisho na mapandekezo ya utafiti huu. Sura hii inazo sehemu nne ambazo ni utangulizi, muhtasari, hitimisho pamoja na mapendekezo mbalimbali ya utafiti huu ambayo yatashughulikiwa katika tafiti zijazo.

## 6.1 Muhtasari

Lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchambua na kuhakiki riwaya nne zilizoandikwa na waandishi wanawake wa Kenya na Tanzania. Riwaya hizo ni *Tumaini* ya Clara Momanyi na *Dago wa Munje* ya Sheila Ryanga ambazo zimeandikwa na waandishi wa Kenya na *Hiba ya Wivu* ya Zainabu Mwanga na *Kipimo cha Mizani* ya Zainabu Burhani zilizoandikwa na waandishi wa Tanzania.

Lengo kuu lilikuwa ni kuangazia katika usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya hizo zilizoandikwa na waandishi wanawake wa Kenya na Tanzania

kwa kutumia nadharia ya ujifunzaji wa kijamii iliyoasisiwa na Albert Bandura, (1963) ya mwanaume mpya iliyoasisiwa na John Beynon, 2002 na ya uhalisia ya Georg Lukacs na wenzake, (1972). Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii imetumika kuangazia masuala ya kiuana namna watu wanavyojifunza tabia na chanzo cha tabia mbalimbali kama yalivyobainishwa katika utafiti huu kwa kujikita katika mihimili yake. Nadharia hii metumia pia kuonesha ufaafu wa matendo yanayofanywa na jinsia fulani dhidi ya jinsia tofauti. Nadharia ya mwanaume mpya imetumika kuonesha matendo yasiyofaa yanayofanywa na wahusika wa kiume yanayofaa kubadilishwa na kuwafanya wawe wapya kimatendo.Vile vile nadharia ya uhalisia inatumika kuakisi matukio halisi ya kila siku kwa jinsi yaliyoibuliwa na waandishi wa riwaya teule. Imetumika pia kuonesha kama matendo yanayofanywa na wahusika kama yanaendana na hali halisi ya jamii husika. Kazi hii haikuwa rahisi ila kwa kuongozwa na wasimamizi wabobezi katika fani hii, utafiti huu umewezekana kukamilika.

Msukumo wa utafiti huu ulitokana na kazi zilizoandikwa na waandishi wanaume namna wanavyowasawiri wanawake kwa mtazamo hasi zaidi kuliko chanya na wanawasawiri wahusika wa kiume chanya zaidi kuliko hasi. Kutokana na tafiti tangulizi, tumeona kuwa waandishi hao wanawasawiri hivyo wahusika wa kike na wa kiume hawajazungumziwa. Usawiri wa waandishi hao ndio umetoa chachu kwa utafiti huu kuchunguza namna waandishi wa kike wanavyowasawiri wahusika wa kiume katika kazi teule ambazo ni riwaya licha ya kwamba tafiti nyingi zimefanywa kuhusu usawiri wa wahusika wa kike, ilikuwa ni muhimu kutafiti usawiri wa wahusika wa

kiume kwa namna walivyochorwa na waandishi wanawake. Tasnifu hii imegawanywa katika sura sita ambazo ni:

Sura ya kwanza imetoa maelezo juu ya mada, malengo ya utafiti na sababu za kuchagua mada ya utafiti. Upeo na mipaka ya utafiti vimeelezwa pamoja na udurusu wa yaliyoandikwa kuhusu mada yameonyeshwa, nadharia za utafiti pamoja na mihimili yake imebainishwa na mbinu za utafiti huu. Sura ya pili imebainisha dhamira zinazoibuliwa na wahusika wa kiume katika riwaya teule. Sura ya tatu inahusu taswira zinazotumiwa na waandishi kuwasawiri wahusika katika riwaya teule. Sura ya nne imeeleza mitazamo inayoibuliwa na wahusika wa kiume katika riwaya teule. Sura ya tano inahusu kufanana na kutofautiana kwa waandishi wanawake wa Kenya na Tanzania. Sura ya sita ni muhtasari, matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

### 6.2 Matokeo ya Utafiti

Kutokana na utafiti huu imebainika kuwa wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake wamesawiriwa kwa namna mbalimbali kutegemeana na tamaduni na mazingira aliyomo mtunzi. Mfumo wa kuumeni unaendelea kushika kasi katika jamii nyingi walizozizungumzia waandishi hawa ingawa mabadiliko yapo na mengine yanaendelea. Masuala ya kiuana yanatofautiana namna yanavyowasilishwa na mtunzi mmoja baina ya mwingine kulingana na jamii inayozungumziwa. Katika utafiti huu, tumeona kuwa waandishi wengi wanajikita katika mtazamo wa kidini ambao unaendelea kumuweka juu mwanaume, jambo ambalo humfanya awe na

mamlaka nyingi katika ngazi ya familia na jamii kwa ujumla. Wamitila (2003) anaeleza kuwa jamii nyingi za Kiafrika zinaendelea kujikita katika mfumo wa kuumeni ambao huendelea kumpa mamlaka katika nyanja zote za maisha.

Majukumu mengi ya kiuana yanaendelea kumwelemea mwanamke. Katika utafiti huu tumeona kuwa katika masuala ya kiuana mwanaume anaangazwa zaidi katika nafasi yake kijamii hasa katika mamlaka. Suala hili limejitokeza sana katika kazi nyingi zilizoandikwa na wanaume na kuwaweka wanawake chini ya mwanaume ndipo ukaonekana umuhimu wa kuliangaza suala la usawiri wa wahusika wa kiume kama wanavyosawiriwa na wanawake. Wanawake wanawasawiri wahusika wa kiume kwa mtazamo chanya na hasi kutegemeana na jamii inayozungumziwa.

Kuna dhamira nyingi zilizoibuliwa ila zilizojadiliwa katika utafiti wetu ni: ndoa; katika riwaya teule zimezungumziwa ndoa za aina mbali mbali ikiwemo zinazogubikwa na ushindani, ubabe na kupoteza upendo na amani katika ndoa pamoja na ndoa zilizojaa wivu na uvivu kwa baadhi ya wanandoa na kupelekea majukumu ya familia kuegemea upande mmoja na mwingine kuelemewa.

Dhamira nyingine ni uchapakazi. Katika riwaya teule, wapo wahusika wa kiume waliochorwa kama wachapakazi katika ajira zao na wengine hawajaajiriwa ila ni wachapakazi katika shughuli za kijamii ili kupata mahitaji yao ya kila siku. Wako wahusika wa kiume ambao pia si wachapakazi na

badala yake huishia kuwa walevi na wakorofi katika familia zao. Maadili ya kazi pia ni dhamira iliyoibuliwa na wahusika wa kiume. Wako wahusika wanaofuata maadili ya kazi zao na wengine hawayafuati kabisa na kuwapelekea kuwa wadhulumaji, wanyanyasaji na wapokea rushwa. Kutofuata maadili ya kazi zao ndiko kunawapelekea kutotenda haki. Urafiki wa kweli pia ni dhamira nyingine ambapo tunawaona wahusika wa kiume wakisaidiwa na marafiki zao ambao ni wa kiume pia. Wanajitoa kwa ajili ya marafiki zao, jambo hili linaleta undugu na mshikamano na upendo wa kweli katika jamii.

Ukosefu wa haki pia ni dhamira iliyowasilishwa na wahusika wa kiume. Kuna wahusika wa kiume wanaowanyima haki zao wanajamii kwa malengo yao binafsi na kuwafanya wapate maumivu makali katika mioyo yao na kuwakatisha tamaa ya kuendelea kupambana kuyatafuta maendeleo. Malezi pia ni dhamira nyingine ambapo wahusika wa kiume wanalelewa kwa namna tofauti kulingana na mitazamo ya jamii husika. Malezi hayo huwapelekea wahusika hao wa kiume kuwa na tabia zinazofaa na zisizofaa kutokana na namna walivyolelewa katika familia zao na wazazi wao au walezi. Malezi huwafanya wawezi kukubalika au kukataliwa katika jamii.

Dhamira ya mwisho katika utafiti wetu kwenye sura hii ni migogoro. Wahusika wa kiume katika riwaya teule wamekumbwa na migogoro ya kijamii, kiuchumi na ya kinafsi. Wahusika walipata ukinzani wa mambo katika jamii zao na kuifanya jamii kuingia katika mgogoro. Kwenye mgogoro

wa kiuchumi ni kuwa wahusika wa kiume wanapata migogoro hii kulingana na hali za vipato vyao na kuibua matabaka na hatimaye migogoro miongoni mwao kuhusiana na uwezo wa kipato kupanda na kushuka au kutofautiana. Katika mgogoro wa nafsi, tumeona wahusika wanapatwa na mambo kadha wa kadha katika nafsi zao na kushindwa kufanya maamuzi ya namna ya kutatua yanayowakabili. Mambo haya hupelekea wahusika kuumia nafsini mwao bila kujua ni nini cha kufanya.

Waandishi wamewachora wahusika wa kiume kwa taswira mbalimbali. Kuna taswira hasi yaani zile mbaya ambazo hazina muonekano mzuri katika familia na jamii kwa ujumla. Kwa mfano wamechorwa kama walevi, wababe, wavivu, katili, wadanganyifu na wenye maringo, wapenda rushwa, wadhulumaji, wakorofi, wenye tamaa na washari. Taswira hizi zinaibuliwa na waandishi kulingana na walivyoichunguza jamii husika. Lengo la waandishi kuyaweka bayana haya ni kutaka jamii ibadilike na kuwa na matendo mema na mazuri hasa kwa hao wahusika wa kiume tuliowaangazia katika utafiti wetu.

Katika taswira chanya, waandishi wanaonesha matendo mema au mazuri yanayotendwa na wahusika wa kiume ili yaweze kuendelezwa au kuboreshwa zaidi ili jamii iweze kuwa na uwianao sawa wa kiuana kulingana na uhalisia uliopo katika jamii zetu. Taswira chanya wanazoziibua waandishi wanawake katika riwaya teule juu ya wahusika wa kiume ni: wenye bidii, wachapakazi, wenye upendo na mshikamano kwa kujitoa kwa ajili ya wengine,wakweli na

wawazi. Waandishi wameyasawiri hawa juu ya wahusika wa kiume ili jamii iweze kupata kujifunza zaidi juu ya mahusiano ya kiuana ili kuleta maendeleo.

Wahusika wa kiume wanaibua mitazamo mbalimbali ambayo hutofautiana kulingana na tajriba za jamii husika. Kuna mtazamo wa kidhanifu na mtazamo wa kiyakinifu. Katika udhanifu kuna vipengele viwili ambavyo ni usawiri wa wahusika kimaendeleo na kuangaza madhila ya wanyonge na maslahi yao. Katika mtazamo wa kiyakinifu tumejikita katika kuangazia matukio ya kihistoria na mambo yatendwayo na wahusika kuendana na hali halisi iliyopo katika jamii husika.

## 6.3 Mchango kwa Utafiti

Kutokana na utafiti huu, kuna masuala ya kiuana yanayoibuliwa na wahusika wa kiume kwa namna walivyosawiriwa na waandishi wa kike. Masuala ya kiuana yanapaswa kuwekwa bayana kwa kila jamii ili jinsi zote ziweze kuwa na usawa katika masula ya kiutendaji wa kijamii na kiuchumi kwa ujumla. Maendeleo yanaanzia ngazi ya familia hasa katika masuala ya uwajibikaji na mgawanyo wa kazi.

Imebainika kuwa waaandishi wanawachora wahusika kutokana na jamii zilizowakuza. Mwandishi wa kike kama amekulia katika jamii ya ubabedume lazima tajriba hiyo iliyomkuza itajidhihirisha katika utungo wake. Kuna dhamira na taswira zilizowekwa wazi kuhusu wahusika wa kiume ili wajue namna zinavyowaathiri kwa kuleta picha mbaya katika jamii. Dhamira na

taswira hasi ndizo hazileti picha nzuri katika jamii. Mambo hayo ni kama uonevu, unyanyasaji, kiburi, ukatili, rushwa, ushari, fitina, ulevi, ugomvi, uchafu, uvivu, uchu wa mali, kuombaomba, kupenda starehe, kero, ukali na ugomvi. Kuonesha kuwa mambo hayo hayafai, watunzi wamemaibua taswira na dhamira chanya kama vile kuwa na bidii, kupenda maendeleo, kujiamini, ujasiri, hekima, wenye kujitambua, bidii, upole na wabunifu. Hivyo kupitia mitazamo hii, waandishi wanaibua matatizo na kupendekeza namna ya kuyatatua.

Utafiti huu umeonesha kuwa waandishi wanayaibua mambo mbalimbali yaliyomo katika jamii kwa kuyashughulikia na kuonesha namna yanavyowaathiri wahusika wa kiume. Haya ni mambo yaliyomo katika jamii halisi na yamedadavuliwa kwa kutumia nadharia ya uana na uhalisia ili kuyaweka bayana katika jamii zetu.

Utafiti huu umesaidia kueleza mambo mbalimbali katika riwaya teule ambazo ni *Tumaini*, *Dago wa Munje*, *Hiba ya Wivu* na *Kipimo cha Mizani*. Tumeona kuwa wahusika wa kiume wanachorwa na wahusika wa kiume kwa maana wanawakilisha jumbe mbalimbali. Tumeona masuala mbalimbali yanayotendeka katika jamii za waandishi hawa walizoziandikia yanategemea jinsi husika inavyochukuliwa katika jamii hiyo. Kwa maana hiyo elimu ya masuala ya kiuana imetolewa katika jamii husika kupitia utafiti huu.

Kulingana na utafiti huu pia tunaona kuwa utafiti huu una faida kwa taaluma ya fasihi na jamii kwa ujumla kwa kuchochea ari wa watafiti wengine kufanya utafiti katika masuala mengine ya kifasihi kwa kujikita katika diwani zinazozungumzia masula ya kiuana kwa kuegemea katika tanzu za tamthiliya, ushairi na hadithi fupi kwa maana utafiti huu umejikita katika riwaya. Dhana ya uana ni pana na inahitaji elimu pana ili kuleta uwiano wa kiuana katika jamii zetu.

Matokeo ya utafiti huu yatawafaa wasomi na hata waandishi wa fasihi. Wanaume watafaidika kwa kuwa watagundua kuwa mabadiliko ndicho kitu cha kudumu maishani kwa maana yanatusaidia kujifanyia tathmini katika mambo mengi katika jamii. Hivyo, ikiwa mabadiliko yana manufaa hayafai kukataliwa. Aidha, si vyema wanaume kufa na tai shingoni kwa kuelemewa na mambo yanayotokana na tamaduni zilizopitwa na wakati. moyo wakikumbwa na changamoto. Pia, wasomi kama vile vijana watafaidika kwani wataanza kutathmini na kupima mambo mageni kabla ya kuyakubali au kuyakataa. Watafiti wa fasihi nao watafaidi maarifa mapya kutokana na utafiti huu.

Kupitia utafiti huu pia,kutakuwa na faida kwa watafiti wajao kupata rejea na tafiti tangulizi kuhusu wahusika na dhana za kiuana kwa kutumia nadharia za ujifunzaji wa kijamii, mwanaume mpya na uhalisia ili kuwapatia maarifa watakaotembelea maktaba utakapokuwa utafiti huu baada ya kukamilika ikiwemo chuo Kikuu cha Kenyatta na Chuo kikuu cha Dar Es Salaam ambako ni eneo mojawapo la utafiti wa kazi hii.

Utafiti huu umesaidia kuongeza maarifa na kupanua wigo wa mtafiti juu ya vipengele mbalimbali vya kiuna, dhamira, taswira na mtazamo. Utafiti umesaidia pia kujikita katika mihimili ya nadharia zilizotumiwa ambazo zinajibu maswali ya utafiti. Kwa mfano nadharia ya ujifunzaji wa kijamii tumejikita katika mihimili ifuatayo: moja; Ujifunzaji si hali ya tabia peke yake bali ni mchakato wa utambuzi unaofanyika katika muktadha wa kijamii. Pili; Ujifunzaji hutokea kwa kuchunguza tabia na pia kuchunguza matokeo ya hiyo tabia. Tatu; Ujifunzaji unahusu kuchunguza kupata habari kutokana na ule uchunguzi na kuunda maazimio kuhusu utendakazi wa tabia hiyo. Nne, Vishawishi vinapima katika ujifunzaji lakini havisababishi ujifunzaji wote. Tano, Mwanafunzi si mpokezi tulivu wa habari, utambuzi mazingira na tabia vinaathiriana katika upataji wa habari wa mwanafunzi.

Nadharia ya mwanaume mpya tumetumia mihimili ifuatayo: Moja; kusaidia wake zao na wanawake wengine katika jamii katika kujiendeleza kielimu na kikazi. Pili; Kukubali majukumu yoyote ya kiuana bila kujali jinsia na bila kujali nwatu waliowazunguka. Tatu; Kutoonesha udikteta katika familia zao na jamii inayowazunguka. Nne; Kuwaona wanawake kama viumbe sawa na wanaume kwa kuwaheshimu na kuwapenda katika kila nyanja wanazokuwepo. Tano; Kukosoa nafasi zao na mazoea yao kama wanaume.

Katika nadharia ya uhalisia tumetumia mihimili ifuatayo: moja. Uyakinifu; kuelezea mambo kulingana na hali halisi ya maisha. Pili; wahusika waonyeshwe kama walivyo katika muktadha wa kihistoria na kijamii. Tatu;

usadikifu; yale anayoyaibua katika jamii yawe yanasadikiwa na wasomi. Nne, mshikamano. Tano; itumie sajili ambazo ni za kawaida.

Utafiti huu ni muhimu kwa wanafasihi kwa ujumla na wapenzi wa masuala ya kiuana na mabadiliko ya kijamii. Kupitia utafiti huu, jamii itapata elimu kuhusu masuala ya kiuana na uhalisia kwa ujumla.

**6.4 Changamoto**

Utafiti huu ulipitia changamoto mbalimbali ikiwe ukosefu wa vitabu vya Kiswahili vya kusoma. Ilimbidi kusomea vitabu na makala nyingi ziliyoandikwa kwa lugha ya Kingereza na baadae kuzitafsiri kwa Kiswahili.Kuna wakati, ilikuwa ni vigumu kupata istilahi mwafaka na kutumia zinazokaribiana kimaana. Vile vile kulikuwa na changamoto ya safari ndefu ya Tanzania na Kenya kuingia maktabani, kuonana na wasimamizi kwa ajili ya maelekezo pamoja na gharama za maktabani kupiga chapa na kutoa nakala. Hata hivyo ugonjwa wa corona umepelekea masomo kusimama kwa muda kwa vyuo kufungwa na mipaka kufungwa, ikawa ni vigumu kusafiri kuja Kenya kutembelea maktabani, ilibidi kusoma kwa kutumia mtandao tu. Hili lisingeweza kutosheleza kukamilisha hatua zote na kupelekea kuchelewa kukamilisha kazi hii ya utafiti. Pamoja na hayo yote, kwa neema ya Mungu, mtafiti aliweza kufanikisha kuukamilisha utafiti huu.

## 6.5 Hitimisho

Wandishi wanamke wa Kenya na Tanzania wamelijadili swala la usawiri wa wahusika wa kiume kwa namna tofauti. Wameonekana wanafanana kwa namna Fulani na kutofautiana kwa namna nyingine. Hii ni kutokana na jamii zilizowakuza waandishi. Kwa kiwango kikubwa, mwanaume anaonekana kukwezwa na jamii nyingi zilizowakuza waandishi. Kuna mahali anakandamizwa kisaikolojia na kiuchumi hadi kushindwa kumudu mahitaji ya kila siku,mfano baba Dago. Wapo wanaotumia ubabe kujilimbikizia mali zote za familia na kuwaacha wanafamilia yaani mke na watoto wanaangaika. Mfano, Mzee Masumbuko. Japo kwa kiwango kikubwa waandishi wameonekana kulikemea suala la ukandamizaji wa kijinsia na kuitaka jamii kubadilika kutoka katika lindi hilo la kitabaka.

Katika jamii walizozizungumzia waandishi zinaonekana kuwa na wahusika wa kiume wa aina nzuri na mbaya katika matendo wayatendayo katika jamii zao. Hii ndiyo jamii maana haiwezi kuwa na watu wanaofanana kitabia na kimienendo. Hii hutofautiana kulingana na mielekeo ya jamii husika. Wako wanaume wanaotimiza wajibu wao na wasiotimiza na badala yake kujikita katika kumomonyoa maadili na kuwa na sifa mbaya. Kwa mfano, Andrea. Haya yote yameibuliwa na waandishi wa riwaya teule ili kuyaweka bayana kwa ajili ya kuleta usawa wa kijinsia katika jamii kwa maana hakuna jinsia inayopaswa kuwa chini ya nyingine wala kutenda matendo yasiyofaa katika jamii.

## 6.6 Mapendekezo

Utafiti huu umeshughulikia usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili zilizoandikwa na wanawake. Kutokana na jamii kubadilika, wanaume wanaibua taswira mbalimbali ambazo huonekana kuwa ni za kawaida katika jamii na wakati mwingine zisizofaa nazo huibuliwa na waandishi kupitia wahusika wao. Utafiti huu umeibua mjadala wa mambo kadhaa na kupendekeza namna ya kuyaweka kulingana na sababu za usawiri wawahusika tajwa uliobainishwa kupitia dhamira, taswira na mitazamo ya wahusika wa kiume katika utafiti huu.

i. Wahusika wa kiume wanachorwa kwa namna mbalimbali kutokana na sababu za kitamaduni. Wanaume katika tamaduni nyingi za Kiafrika wanaonekana kuthaminiwa na wanawake na hata wanaume wenzao katika miktadha fulani. Suala la kiutamaduni hata kidini liangaliwe upya ili kuwepo na uwiano wa kiuana baina ya wanaume na wanawake.

ii. Sababu za kiuchumi. Wanaume wengi Kenya na Tanzania huwa wa kiwango cha juu kiuchumi wakilinganishwa na wananawake. Hata katika matajiri wanaoongoza katika nchi hizo ni wanaume au makampuni yanayomilikiwa na wanaume. Katika kipengele cha uchumi, ni muhimu jambo hili litiliwe msisitizo ili kuleta uwiano wa kiuana katika uchumi.

iii. Siasa. Kisiasa wanawake wanaonekana kuwaachia wanaume kugombea vyeo mbalimbali vya kisiasa. Kwa upande wa Kenya kuna nafasi wa uwakilishi wa wanawake bungeni kwa maana hawakuwa na nafasi za

kutosha huko bungeni kupitia kugombea. Kwa upande wa Tanzania kuna viti maalum ambavyo hutolewa kwa wanawake ili waweze kupata uwakilishi huko bungeni. Itolewe elimu ya kutosha kwa wanawake ili waelewe umuhimu wa kushiriki katika nafasi za kisiasa.

iv. Mfumo dume. Huu hutawala katika jamii nyingi za Kenya na kuwakweza wanaume katika kila kipengele na kumuona mwanamke hawezi kusimama katika nafasi fulani au kutenda jambo la maana isipokuwa mwanaume. Jambo hili huwapelekea wanawake wenyewe kujidunisha kiasi cha kuwatukuza wanaume. Jambo hili limepelekea kuwa na ombwe katika fani mbalimbali hata uandishi. Kazi nyingi za fasihi na isimu zinaandikwa na wanaume ambapo wanawake hawaandiki kwa kiasi kikubwa kama ilivyo wanaume na wanaona ni sawa tu. Jamii ipate hamasa ya kuwafanya wanawake waweze kuonyesha vipaji vyao katika fani mbalimbali ikiwemo uandishi wa kazi. Ndio maana nadharia ya mwanaume mpya inamtaka mwanaume kuwa mpya pale anapotambua wajibu wake katika familia na jamii kwa ujumla kwa kumthamini mwanamke na kumuona kiumbe sawa na mwanaume. Hii ni pamoja na kumjali mkewe kwa kumsikiliza, kumsaidia kazi, kumhudumia na kumpa hamasa katika kufanya mambo mbalimbali ya kifani. Vile vile mwanaume mpya huthamini yale ayafanyayo mkewe na kujifunza mengi kutoka kwa mkewe ikiwemo kupika, kufua, kufanya usafi nyumbani, kulea watoto, kuchota maji n.k. kazi zote zilizoaminiwa na jamii yenye ubabe dume kuwa ni za

mwanamke zote anazifanya kwa ajili ya kuleta maendeleo na uwiano wa kiuana.

**Mapendekezo ya utafiti wa baadae:**

Utafiti huu umeshughulikia usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya zilizoandikwa na wanawake. Wahusika ni dhana pana hivyo inapendekezwa kuwa utafiti ufanyike zaidi ili kuboresha na kutoa ufafanuzi zaidi juu ya dhana ya wahusika. Utafiti huu ulihusisha vitabu vinne yaani riwaya vya waandishi wanawake wawili wa Kenya na wawili wa Tanzania. Utafiti zaidi unaweza kufanywa katika waandishi wengi zaidi wa nchi mbalimbali ili kupata utofauti wa kimaeneo na kitamaduni. Tafiti pia zinaweza kufanywa katika tanzu nyingine kama vile tamthiliya, ushairi na hadithi fupi ili kuona waandishi wanavyoshughulikia masuala ya kiuana katika kazi zao.

Utafiti huu ni wa maktabani, hivyo tafiti zijazo zinaweza kwenda nje ya maktaba hadi uwanjani kwa wasomaji wa kazi za fasihi na waandishi wa kazi hizo kwa maana wote wamo katika jamii. Utafiti pia unaweza kutumia nadharia tofauti na zilizotumika katika utafiti huu ili kubaini kama kutakuwa na utofauti wa matokeo ya utafiti. Vile vile zinaweza kutumika mbinu za utafiti tofauti na zilizotumiwa katika utafiti huu.

Vile vile tafiti za baadae zinaweza kuangazia namna wahusika wa kiume wanavyozipokea taswira wanazopewa na waandishi wa kike na wa kiume.

**MAREJELEO**

Abourweeshah, A.M (2017). “Kuchunguza matumizi ya mbinu za kiasanaa na dhamira katika tamthiliya ya Morani”, Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Abram, D. (1993). “Context and the Social Self- regulations of ASteriotyping : perception”, Judgement and Behavior, In R.S Wyer(Ed.), advanced in social recognition vol.11: 53-67

Adam, O.A (2014). “Kuchunguza dhamira zan kijamii na kiutamaduni katika riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka Kuli na Vuta N’kuvute, Tasnifu ya uzamivu, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.( Haijachapishwa)

Ali, J.A.E (2017). “Kuchunguza dhamira katika riwaya ya Kiu ya Mohamed Suleiman Mohamed”, Tasnifu ya uzamili,Chuo kikuu Huria cha Tanzania Amadiume, I. (1987). *Male Daughters, Female Husbands: Gender and Sex in an African Society.* London: Zed Publishers Ltd.

Ambrose, J. na Palm, S. (2015). Dating in the 21st Century. *The Real Truth Magazine.* Ohio, The Restored Church of God.

Ambrose, V.L.G.M (2018). “Mtazmo wa jamii juu ya sera ya elimu na mafunzo 2014 kuhusu kutumia Kiswahili kufundishia na kujifunzia elimu ya juu katika vyuo vya kati” Tasnifu ya uzamili, chuo kikuu Huria cha Tanzania.

Anfred, M. (2004). *Culture and Social Norms*. New York: Dove Publishers.

Anivery, S.(1970). The Social and Political Tought of Karl Marx, Cambridge University Press.

Ayang, S.G. (1970). *A History of Zanzibar*. Nairobi: East Africa Literature Bureau.

Ayisi, E.O. (1972). An Introduction to the Study of African Culture, Nairobi, East African Educational Publishers.

Armet, D. (1999). Developing Adolescent. New York, American Psychological Association.

Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research*, Belmont, Wadsworth Publishing Company.

Bakari, M.M. (2016). “Usawiri wa mhusika mama wa kambo ndani ya ngano za Kiswahili za Kizanzibari”, Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Bakhtin, M.M. (1986). *The problems of Speech Genres*. Austin. University of Texas Press.

Balisidya, M. L (1982). “The Image of the woman in Tanzania Oral Literature”, Katika Jarida la TUKI Juzuu 49/2, Uk.1-25, Dar es Salaam, TUKI.

Balisidya, M. L. (1987). “The Construction of Sex and Gender Roles in Penina Muhando’s. Plays” Jarida la TUKI, Juzuu54/1 na 54/2, uk.34-48, Dar es Salaam. TUKI.

Bandura, A. (1972). Modeling Theory : Some Traditions, Trends and Disputes, Academic press,INC

Bandura, A. (1977). Self-E fficacy: Toward a Unifying Theory of Behavioral Change. Psychological Review, 84(2)

Basow, S.A. (1992). Gender Stereotypes and Role, California, Brooks/Cole Publishing Company.

Berlin, L.J. (2009). Research on Adolescent Development, Competence and Character. Durham, University of Duke.

Beynon, J. (2002). Masculinities and Culture. Philadelphia, Open University Press.

Blackbeard, D. R., and G. Lindegger. (2014). “Dialogues through autophotography: young Masculinity and HIV identity in KwaZulu-Natal.” European Journal of Social and Behavioural Sciences 10:1466–1477.

Bourgois, P. (1996). “In Search of Masculinity - Violence, Respect and Sexuality among Puerto Rican Crack Dealers in East Harlem.” British Journal of Criminology 36: 412–427.

Bressler, C.E. (2011). Literery criticism : An Introduction to Theory and Practice.5th ed. Boston, Pearson Education.

Brittan, A. (2001). “Masculinities and Masculinism”. The Masculinities Reader. Eds.Stephen M. Whitehead and Frank, J. Cambridge: Policy Press. Barrett.

Brown, B.B, Larson, R.W (Eds) (2002). *The World’s youth adolescence in Eight Regions of the Globe*: United Kingdom. Cambridge University Press.

Bukenya, A.S. (1988). Notes on Marjorie Oludhe Macgoye's Coming to Birth, Nairobi Heinemann Kenya Ltd.

Bukenya, A.S.et al (2000). Understanding Oral Literature, Nairobi,Longhorn Publishers (K) Ltd.

Buliba na wenzake (2014.). *Misingi ya nadharia na mbinu za utafiti*. Dar es Salaam: Serengeti Educational Publisher limited.

Burgess, P.M. (1966). A Differential Reinforcement Theory of Criminal Behavior, Hein Online

Burhani, Z. (2004). *Kipimo cha Mizani,* Nairobi, Longhorn Publishers Ltd.

Butler, J. (1990). Gender Trouble: Feminism and Subversion of Identity. NewYork: Routledge.

Caleb, C.W (2013). "Taswira ya mwanamke katika tamthilia za Nguzo Mama na Mama Ee, Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.

Cancian, F.M. (1990). Love in America: Gender and Self-development, Cambridge University Press.

Chaterji, S. A. (2004). Signs of Change in Patriarchal Ideas about Men and Women's Status and Role in Indian Society. Katika *Gender and Conflict Transformation.* Irenees.net.

Carole, B. O. (1986). *Is there a Female Voice? Joyce Carol Oates Replies* in 'Feminist Literary Theory: A Reader'. Cambridge: Basil Blackwell Ltd.

Carton, B.(2001). "Locusts Fall From the Sky: Manhood and Migrancy in Kwazulu" Changing men in Southern Africa. Ed. R. Morrell. South Africa. Natal University Press.

Chesaina, C. (1987). 'Women in African Drama:Representation & Role'. PhD Thesis, University of Leeds.

Chesaina,C. (1994). "Images of women in African Oral Literature: Kalenjin and Maasai Oral Narratives as case studies". In Bukenya, A. Kabira, W. and Kombo, O. (eds) *Understanding Oral literature*. Nairobi University Press.

Childs na Wiliam, (1997). *An introduction to Post-colonial Theory*. New York:Routledge.

Chomba, M.L.D (2018). Organizational Motivational for Collaboration Theory and Evidence, New York, Lexington Books

Cohen, L. et.al (2000). Research Methods in Education, (5th ed.), London, Routledge.

Connell, R.W (1987). Gender and Power Society : The Person and Sexual Politics, Stanford University Press.

Connell, R. W., and J. Messerschmidt. (2005). "Hegemonic Masculinity: Rethinking the Concept." Gender & Society 19 (6): 829–859.

Kothari, C. R (2008), Research Methodology; Methods and Technique, New Age International (P) Limited: New Delhi.

Crous, M. L. (2005). *Presentation of Masculinity in a Selection of Male-Authored Post- Apartheid Novels*, University of Stellenbosch.

Creswell, J.W. (2009). Research Design: Qualitative, Quantitative, and Mixed Methods Approaches, SAGE Publications.

De' Beauvoir, (1949). *The Second Sex*. London: Pan books publishers.

Dhahabu, L. (1994). 'Uumbaji na Uendelezaji wa Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Penina Muhando'. Tasnifu ya uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Erikson, H. E. (1961). *Youth Change and Challenge.* New York: America Academy of Art and Science.

Finnegan,R. (2007). *The Oral and Beyond: Doing Things with Words in Africa*, The University of Chicago Press.

Flaubert, B.M (1990). Landmarks Of World Literature, New York, Cambridge auaniversity Press.

Flood, M. (2011). "Involving Men in Efforts to End Violence against Women." Men and Masculinities14 (3): 358–377.

Furlong, N. et.al (2000). *Research Methods and Statistics: An Intregrated Approach*. New York, HartCourt Colledge Publishers.

Gagiano, A. (2000). *Achebe, Head, Marechera: On Power and Change in Africa***.** Boulder: Lynne Rienner.

Gill,R. (2003). Change Management, Journal of Change Management vol.3: 307-318.

Gitau, E. N. (2005). “Unyanyasaji Dhidi ya Waume katika Fasihi Andishi ya Kiswahili” Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Gramsci, A. (1971). Selections from a Prison Notebook. London: Lawrence & Wishart.

Gromov, M. D. (2002). *Post Modernistic Elements in Recent Kiswahili Novels*, Nairobi.

Haji, A. (2015). Matumizi ya Utanzia Katika Riwaya Teule za Said Ahmed Mohamed, Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dodoma.( Haijachapishwa)

Hassan, H.H. (2013). “Taswira zinzzojitokeza katika nyimbo za mwakakogwa”, Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Harvey, D. (2003). *The New Imperialism*. Oxford, Oxford University Press.

Hawthorn, J. (1985). Studying the Novel: An Introduction. New Delhi, Universal Book Stall.

Hearn, J. (2004). “From Hegemonic Masculinity to the Hegemony of Men.” Feminist Theory 5 (1): 49–72.

Hegel, G. W. F. (1971). *Introduction to Aesthetics.* Oxford: Clarendon.

Held, D. and D. MacGrew (2007). The Global Transformation Reader, Cambridge, Cambridge Polity Press.

Herek, G.M. (1987). “On Heterosexual Masculinity: Some Psychological Consequences of the Social Construction of Gender and Sexuality.” In Changing Men: New Directions in Research on Men and Masculinity, edited by M. S. Kimmel, 365–374. Beverly Hills, CA: SAGE.

Herman, B. (2007). Moral Literacy, London, Harvard auaniversity Press

Hill, J. S. (1977). *The Romantic Imagination*. London: Macmillan Press Ltd.

Hug, H. (1986). *A handbook to Literature*, New York Mcmillan Publishing Company.

Isiaho, J. K. (2001). “Taswira ya Mwanamke katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed” tasnifu ya M. Phil. Eldoret. Chuo Kikuu cha Moi, Eldoret.

Issa, I. (2013). “Usawiri wa mhusika mwanamke katika ushairi wa Mathias Mnyampala: mifano kutoka Diwani ya Mnyampala (1965) na Waadhi wa Ushairi (1965)”, Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Jessee, M.J. (2018). “Uhusiano wa Itikadi na mtazamo wa mtunzi” IOSR Vol.23 ver.4 sept 2018-JHSS.

Jessee, M.J Na wenzake (2019). “Mabadiliko ya maudhui katika riwaya teule za S.A.Mohamed” Katika Koja la Taaluma za Insia. DSM, Karljammer Ltd.

Jewkes, R., and R. Morell. (2012). “Sexuality and the Limits of Agency among South African Teenage Women: Theorising Femininities and Their Connections to HIV Risk Practices.”Social Science & Medicine 74 (11): 1729–1737.

Jick,K.H & Nkweteyim, P.T. (2016). Alternative Vision of Gender in the New Literatures of Africa in English: An Appraisal of Bole Butake’s Dramaturgy, Journal of Education and Practice (online).

Jilala, H. (2011). “Lugha na Jinsia Katika Ushairi: Uchunguzi wa Sitiari za UKIMWI na Mapenzi Katika Mashairi ya Bongo Fleva”, Katika Jarida la Mulika, Toleo Na. 29 & 30, Uk.55-67 Dar Es Salaam, TATAKI.

Jilala, H. (2016). *Misingi ya Fasihi Linganishi, Nadharia, Mbinu na Matumizi*. Dar es Salaam: Daud Publishing Company.

Johansson, T., and R. Klinth. (2008). “Caring Fathers: The Ideology of Gender Equality and Masculine Positions.” Men and Masculinities 11 (1): 42–62.

Julian, J. (2017). Planned Parenthood and the Novel, New York, Vintage Books.

Kanana, A.S. (2000). Changing the Patriarchal Attitude of Ovawambo Men: Can the Bible help? M.A Thesis.University of Natal,Pietermaritzburg.

Kanwa, O. (2011). “Usawiri wa wahusika wa kiume katika riwaya za Kiswahili: mkabala Linganishi”, Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.( Haijachapishwa)

Kawira, S. na Kisurulia, S. (2017). “Wahusika,uhusika na mtazamo katika riwaya ya Kiswahili” Katika jarida la taasisi ya taaluma za Kiswahili, Mulika toleo maallum, makala ya kongamano la CHAUKIDU 2016. TATAKI. Chuo Kikuu cha Dares Salaam.

Kelly, L. (1988). Surviving Sexual Violence. Cambridge: Polity.

Kezilahabi, E. (2003). “Utunzi wa Riwaya na Hadithi fupi”, katika makala za semina za kimataifa ya waandishi wa Kiswahili namba 3, Dar Es Salaam, TUKI.

Khamis, M. H. (2007). Taswira za Wahusika Wakuu katika Riwaya Tano za Shaaban Robert. Tasnifu ya Shahada ya kwanza, Chuo kikuu cha Taifa cha Zanzibar SUZA.(Haijachapishwa)

Khamis, S. (2007). “Vionjo vya Riwaya Mpya ya Kiswahili” katika *Kioo cha Lugha* no. 5, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu Dar es Salaam.

Khamis, S.A.M. (2008). “Nadharia, Ubunifu, Uchambuzi na Taaluma ya Kiswahili”. Katika: Nathan Ogechi, Naomi Shitemi & Kenneth Simala (eds), *Nadharia katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika.* Eldoret: Moi University Press. Uk. 3-24.

Khatib, M. (2011). “Chanjo za Matakwa ya Mwanaume katika Mwili wa Mwanamke Ulinganisho wa Ushairi wa Muyaka bin Haji na Shaaban Robert”, Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma.

Kiango, S. D (1992). “Taswira ya Mwanamke Katika Tamthiliya za Kiswahili za Kenya”, Katika Jarida la Kiswahili, Baragumu, Juzuu 1ToleoNa 2, Uk.32-58 Maseno University College.

Kimani, C. W. (2003). “Swala la Dhuluma Dhidi ya Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili.” Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu, Kenyatta.

King’ei, G.K (2002). “Swala la uana katika fasihi ya Kiswahili: Uhakiki wa utafiti kutoka Kenya”.Katika utafiti wa Kiswahili. Eldoret: Moi University Press.

Kitanga, F. (2016). “Usawiri wa mwanamke katika majigambo ya wahaya”, Tasnifu ya uzamili,Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Kobia, J. M (2011). “Taswira za Kiuana katika Nyimbo za Tohara za Wanaume miongoni mwa Waigembe nchini Kenya”, Tasnifu ya uzamivu, Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Koda,B. (2000). “The Gender dimension of Land Rights in Thanzania: The case of Msindo village Same District”, Tasnifu ya uzamivu,Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Kothari, C. R (2004). *Research Methodology*; *Methods and Techniques*, New Delhi New Age Internatinal (P) limited.

Kothari, C. R (2008). *Research Methodology*; *Methods and Technique*, New Delhi, New Age International (P) Limited.

Kweka, N.E. (2013). Uchambuzi wa dhamira katika nyimbo za muziki wa injili, Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Lamb, M.E. (2004). *The Role of the Father in Child Development*.Eth ed. New York: John Wiley & Son.

Larkin, M. (1977). *Man and Society in the Nineteenth Century Realism*. London; London Macmillan Press.

Ligopola, M.S (2003). "Nafasi ya Mwanamke katika Nathari teule za S.A. Mohamed", M.A Thesis,UDOM

Lukacs, G. (1972). *Studies in European Realism*, London: The Marlin Press.

Lyatuu, J. (2011). "Usawiri wa Wanawake katika Riwaya ya Kiswahili: Ulinganifu wa waandishi wa kike na wa kiume: Uchaguzi katika Riwaya Teule. Tasnifu ya uzamili.Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Mabala, R. S. (1993). *"Mchango wa Waandishi wa Riwaya", ktk: Fasihi, Uandishi na Uchapishaji.* Dar es Salaam: DUP.

Maddison, S. (1999). "Private Men, Public Anger; The Men's Rights Movement in Australia." Journal of Interdisciplinary Gender Studies 4 (2): 39–52.

Madumulla, J. S (1987). "Maendeleo ya Wahusika Katika Riwaya ya Kiswahili Tanzania", Jarida la TUKI, Juzuu 54/1 na 54/2, Uk.66-75,Dar es Salaam, TUKI.

Madumulla, J. S. (1988). "Riwaya ya Kiswahili (Tanzania) Katika Miaka ya Themanini", Mulika na. 20, uk.9-24, Dar es Salaam, TUKI.

Madumulla, J.S. (2009). Riwaya ya Kiswahili; Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi, Dar Es Salaam, Mture Educational Publishers.

Mair, L. (1979). African Societies, Cambridge, Cambridge University Press, Cambridge.

Makarani, H.S. (2018). "Usawiri wa mhusika mtoto wa kike katika ngano za Kingoni", Tasnifu za uzamili, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Marx, K.na F. Engels (1973). On Literature and Art,International General.

Masamba, D.P.B Na wenzake (1999). Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu, Dar Es Salaam,TUKI.

Masamba, D.P.B. (2009). Kiswahili Origins and the Bantu Divergrnce-convergence Theory, Dar Es Salaam, TUKI.

Mascarenhas, R.M, etal (2005). Globalization and Workers Rights in Tanzania, a report on The Finding of the Field Research on the Impact of Globalizationon the Rights of Workers in Tanzania, Dar Es Salaam, Local and Human Rights Centre.

Masinde, E. (2003). "Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui Katika Ushairi-andishi wa Kiswahili" Tasnifu ya Uzamivu: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Matteru, M. (1982). "The Image of the Woman in Tanzanian Oral literature. A survey". Kiswahili Journal of the Institute of Kiswahili Research. University of Nairobi.

Matundura, B.(2007). Taswira Dumifu za Uana katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto. M.A. Thesis University of Nairobi.

Mavisi, R. (2007). "Usawiri wa Wahusika wa Kike Katika Kazi za Zainabu Burhani", Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta.(Haijachapishwa)

Mazingwa, S. A. (1991). *Fasihi ya Kiswahili,* Paramilo BPN.

Mbatiah, M (2001). *Kamusi ya Fasihi,* Nairobi: Standard Textbooks and Graphics and Publishing Ltd.

Mboya, T. M. (1997). "The Woman and History in Marjorie Oludhe Macgoye's Fiction" M. Phil Thesis. Moi University.

Mbuthia,M.E (2007). The Role of Kiswahili Children's Literature in Formulating own View. International Journal of education and araesearch,Vol.6. Kenya.

Mekacha, R. (1993). 'Mwanamke ni Ibilisi' katika mulokozi et.al (Wahariri) Fasihi, Uandishi na Uchapishaji, Dar es Salaam University Press.

Messerschmidt, J. (1993). *Masculinities and Crime: Critique and Reconceptualization of Theory*. Lanham: Rowman & Littlefield.

Mlacha, S. A. K, (1985). “Wahusika katika Riwaya za Kiswahili (1970-1982)”, Katika Jarida la Mulika, Toleo na.17, uk.29-44, Dar es Salaam, TUKI.

Mlacha, S.A.K.(1991). “Point of view as Stylistic Device in Kiswahili novels” in Kiswahili vol.58, TUKO. Dar Es Salaam.

Mlacha, S.A.K na J.S Madumulla (1991). Riwaya ya Kiswahili, DSM,Dar Es Salaam university Press.

Mlacha S.A.K. (2003). “Wahusika Katika Riwaya za Kiswahili Tanzania”. *Mulika*. Dar-es- Salaam: TUKI.

Mlama, P. (1983). “Hali ya Sanaa za Maonyesho Tanzania”, katika Makala za semina ya Kimataifa ya waandishi wa Kiswahili-iii, DSM: TUKI.

Mnenuka, A. (2011). “Taswira ya Mwanamke Katika Muziki wa Bongo Fleva: Mifano Katika Nyimbo Teule”, Katika Jarida la Mulika na. 29&30, Uk.69-93 Dar Es Salaam, TATAKI.

Mnenuka, A. (2012). “Tofauti ya Dhana ya Mwanamke katika jamii: mifano kutoka Taarabu(mipasho) na Nyimbo za Kibena”, Swahili Forum 19:23-44.

Mogere, O.G (2003). “Uhakiki wa riwaya za Ahmaed Mohamed katika Misingi ya Kifeministi”. Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa)

Mo’d, M. (2017). “Ulinganishi wa tabia za wahusika wakuu na dhamira katika riwaya za Kusadikika na Utengano”. Tasnifu ya Uzamili, Chuo kikuu Huria cha Tanzania.

Momanyi, C. (2001). “Nafasi ya Mwanamke Katika Ushairi wa Shaaban Robert”, Jarida la TUKI, Juzuu 64, uk.53-63, Dar es Salaam, TUKI.

Momanyi, C. (2006). *Tumaini*. Nairobi: VIDE-MUWA.

Mooka, E. (2019). “Masculinity, in Selected Realistic Young Adult Novels by Kenyan Writers,PHD Thesis, Kenyatta University.

Morell, R. (2002). “Mutations in a novel Genre Are Associated With Hearing Loss, Linked to the DFNB 6 Locus vol.7.

Morell, R. (2005). Foreword to Men Behaving Differently.In: Reid, Graeme and Liz Walker (eds) *South African Men Since 1994*. CapeTown: Double Storey.

Morris, P. (2003). *Realism*. London. Routledge and Keegan Paul Ltd.

Msokile, M. (1992). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*, Dar Es Salaam,Educational Publishers and Distributors Ltd.

Mugenda, O. M & Mugenda A.G. (1999). *Research Method: Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Centre for Technology.

Muleka, J. (2000). "Portrayal of Girl Characters in Selected Children‟s Books in Kenya". M.A Thesis, Kenyatta University.(Haijachapishwa)

Mulokozi, M.M na T.S.Y. Sengo (1995). *History of Kiswahili Poetry A.D.1000-2000*, Dar Es Salaam, Institute of Kiswahili Research.

Mulokozi, M.M (mh) (1999). *Tenzi Tatu za Kale*, TUKI, Dar Es Salaam.

Mutua, J. (2007). "Mitazamo ya Vijana na Wazee kuhusu Ukombozi wa Mwanamke". Tasnifu ya uzamili: Chuo Kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa)

Mutua, M.J. (2017). Mitazamo ya waandishi wa kike na wa kiume kuhusu usawiri wa wahusika wa kike katika tamthilia za Kiswahili, Tasnifu ya uzamifu, chuo kikuu cha Pwani

Mutungi, B. (2008). "Usawiri wa Wahusika wa Kiume Kama Kielelezo cha Udume", Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Makerere. (Haijachapishwa)

Mutungi, B. (2019). " kilongo cha unyanyasaji wa Kiusemi katika mahusiano ya vijana katika tamthiliya ya Hatia: mkabala wa uchanganuzi tunduizi Kilongo wa kifeministi", Jarida la Taasisi za Taaluma za Kiswahili, Juz. 17: 151-163.

Mutungi, B. (2021), " Uchanganuzi Tunduizi kilongo wa unyanyasaji wa kiusemi baina ya wanandoa katika tamthiliya teule za Kiswahili", PHD Thesis, UDSM.(Haijachapishwa)

Mwaifuge, E.S. (2006). "Fasihi ya Kiswahili na Rushwa Tanzania: Thomas, A.R. Kamugisha na Kitu Kidogo Tu, katika Kioo cha Lugha, Juzuu namba 4, Dar Es Salaam, TUKI.

Mwanga, Z. (1997). *Hiba ya Wivu*, Dar Es Salaam, Ruvu Publishers Ltd.

Nassoro, B.M. (2017). “Dhima ya taswira katika hadithi za watoto: uchambuzi wa vitabu vya hadithi vinavyosomeshwa Zanzibar”. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Ndungo, C.M. (1998). “Images of Women in African Oral Literature” PHD thesis, Kenyatta University.

Newmna, M.C.J (2012). Community Food webs Data and Theory, USA, International union for Conservation of Nature, University of Arizona

Ngaiza, M.K. (2002). “Gender Dynamics in Poverty Alleviation in Tanzania: Ngara District Case Study,Tasnifu ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.

Ngaiza, M.K. (2003). “Gender and Political Empowerment in the Third Millenium: A conceptual Frame Work”, In Tanzania Journal of Development Studies, Vol.4.

Ngaiza, M.K. (2004). “Harmonization and Mainstreaming Gender in Local Government.

Ngugi Wa Thiong’o, (1986). *Decolonising The Mind: The Politics of Language in African Literature*, London, Jamesm Currey.

Njogu, K. na Wafula, M. (2007). Nadharia za Uhakiki wa Fasihi, Nairobi,The Jomo Kenyatta Publishers.

Nkwera, F.V. (1978). Sarufi na Faihi: sekondari na Vyuo. Dar Es Salaam, Tanzania Publishing House.

Ntarangwi, M. (2004). Uhakiki wa kazi za Fasihi, Augustane College, Rock Island.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). Ufundishaji wa Fasihi, Nadharia na Mbinu. Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation.

Nyambwogi, J.M. (2016). “ Mikakati ya Upole na Uana: Tathmini ya Natala, Tasnifu ya uzamili, Chuo kikuu cha Moi. ( Haijachapishwa)

Ponera, A.S. (2010). “Ufutuhi katika Nathari za Shaaban Robert: Maana Yake, Sababu za Kutumiwa na Athari Zake kwa Wasomaji”, Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Dodoma.

Ponera, A.S. (2014). *Utangulizi wa Ndharia ya Fasihi Linganishi*, Dar es Salaam, Karljamer Print Technology.

Powers, K.T. (2002). Attaining Personal Goals: Self- concordance plus Implementation Intentions Equals Success, Journal of personality and social Psychology. Apa.org.doi Landing.

Rear, et al. (2015). “Molecula Evidence of Sexual Transmission of Ebola Virus”, London, New England Journal of Medicine vol.373: 2448-2454.

Renzette, S. (2012). The Economics of Water Demands: springer science and Business Media, New York, Academic Publishers.

Ricardo, C., M. Eads, and G. Barker. (2012). Engaging Boys and Young Men in the Prevent of Sexual Violence: A Systematic and Global Review of Evaluated Interventions. Pretoria: Sexual Violence Research Initiative.

Richards, I. A. (1970). *Principles of Literary Criticism*. London.Routledge and Keegan Ltd.

Rotter, J.B.(1954). Social Learning Clinical Psychology,U.S.A, American Psychological Association.

Ryanga, S. (2008). *Dago wa Munje,* Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation.

Samwel, M. (2012). Mabadiliko katika majigambo; uchunguzi wa majigambo ya jadi na ya bongo fleva, Tasnifu ya uzamivu. Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.(Haijachapishwa)

Samwel, M. (2013). Ushairi wa Kiswahili; Nadharia Maendeleo na Mwongozo kwa Walimu wa Kiswahili, Dar Es Salaam, MEVELI Publishers.

Schauk, P.C. and Burkart, M.J. (2011). Social Learning and Evolution; the Cultural Intelligence Hypothesis, online library

Saunders, M., P. Lewis na A. Thornhill (2003). *Research Methods for Business Students*, London, Prentice Hall.

Sedgwick, E.K. (1990). Epistemology of the Closet. Berkeley: University of California Press.

Sengo, T.S.Y.M. (1987). *Fasihi Simulizi,* Sekondari na Vyuo, Dar Es Salaam, Nyanza Publications Agency.

Sengo, T.S.Y.M na Kiango, S.D. (2012). *Hisiya Zetu*, Dar Es Salaam, TUKI.

Senkoro, F. E. M. K. (1976). Utamaduni katika Riwaya ya Kiswahili. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, 46(2): Uk.74-97.

Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi*, Dar Es Salaam Press and Publicity Centre.

Shao, I.F. (2003). "Beyond Rhetoric: The Role and Experience of the University of Dar Es Salaam the Involvement of Men in Gender and Development Practice", in Tanzania Journal of Development Studies, Vol.4 na 1.

Shao, I.F. (2004). "Conext of Gender Mainstreaming, Internationally, Regionally and Nationally", Paper presented at a Gender Sensitization Workshop for UDSM Council Members, Zanzibar.

Shao, I.F.(2010). "Gender Rural Development Governance: An Overview", In Tanzania Journal of Development Sudies,Vol.10 na 1&2.

Sosoo, E.C. (2020). The Influence of Interalized Racism on the Relationship between Discrimination and Anxiety, Psycret.apa.org

Skeggs, B. (1997). *Formation of Class and Gender*, London: Routledge.

Steady, R. (2004). GMAT Studies. New York: NHS Publishing House.

Stern, J. P. (1973). *On Realism*, London: Routledge and Kegan Paul.

Stromberg, R. N. (1968). *Realism, Naturalism and Symbolism*: Modes of Thought and Expression in Europe 1848-1914, New York: Walker and Company.

Stromquist, N. P. (2014). "Freire, Literacy and Emancipatory Gender Learning." International Review of Education. 60 545–558.

Suzan, Z.A (1994). *Contemporary African Literature and the Politics of Gender*: Book Review by Florence Stratton, Indiana University Press.

Symon, N. (1999). "Men and Masculinity- The Presentation of Men and Relationships in Three Contemporary British Novels". M.A.Thesis.University of Berlin. Munich:GRIN Publishing.

Talbot, K., and M. Quayle. (2010). "The Perils of Being a Nice Guy: Contextual Variation in Five Young Women's Constructions of Acceptable Hegemonic and Alternative Masculinities." Men and Masculinities 13: 1–24.

Tannen, D. (1990). *You Just Don't Understand:Women and Men in Conversation*. New York: Harper Collins Publishers.

Taylor, R. (1991). Understanding The Elements of Literature, London, Macmillan.

Toots, V. (1984). “Ufafanuzi wa Riwaya ya Kurwa na Doto”, Lugha, Juzuu 3, Uk.37-62. Sweden, Uppsala University.

TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu Toleo la Pili*, Kenya,Oxford University Press.

Vasquez, A. (1973). *Art and Society*. New York: Monthly Review Press.

Wafula, R.M (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake*, Nairobi, Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Walby, S. (1990). *Theorising Patriarchy*. London: Basil Black Well.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*, Nairobi, Focus Publications LTD.

Wamitila, K.W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*, English Press, Nairobi.

Wamitila, K.W (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi, Phoenix Publishers.

Wamitila, K.W. (2008). Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi, Nairobi, Vide- Muwa Publishers.

Wandera, S. (2002). **“**Utafiti wa maswala ya Kijinsia Katika Kiswahili**.”** Katika *Utafiti wa Kiswahili*. Eldoret: Moi University Press.

Wanjala, F.S (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi Kwa Shule, Vyuo na Ndaki*, Mwanza Serengeti Bookshop.

Wanjiku, M.J (2018). “Mabadiliko ya nafasi ya mtazamo wa wahusika wanaume katika riwaya za Said A. Mohamed: Utengano (1980) na Dunia Yao (2006), Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Webster, F. (2006). *Theories of the Information Society*: London: Routledge.

Wegesa, B. B. N. (1996). “Mwanamke katika Tamthilia za Ebrahim Hussein,” Tasnifu ya M. Phil. Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa)

Wellek, R. na Warren, A. (1949). *Theory of Literature*. Harmondsworth: Penguin Books.

Wellek, R. (1961). *"The Concept of Realism in Literary Scholarship".* Neophilologus. London: J Cape.

West, C., and D. Zimmerman. (1987). "Doing Gender." Gender & Society 1 (2): 125–151.

Winerman, D.N. (2005). Counselling Aging men: Best Practice for Group Counselling, adult Pan Journal; online library

Yin, R. K. (1994). *Case Study Research: Design and Methods*, (2nd eds.) thousand Oaks Calif: SAGE Publishers.

Young, P.V., (1984). *Scientific Social Surves and Research*, Englewood Chiffs: Prentice Hall. Inc.

Zola, W.P (2010). The Depiction of Female Characters by Male Writers in Selected Isixhosa Drama Works, PHD Thesis, South AfricaNelson Mandela Metropolitan University.

Zulfiqar, S. (2016). African Women Writers and the Politics of Gender, U.K. Cambridge Scholars Publishing.

http:// grad works.umi/14/81/1481340.html.The Depiction of Male Characters in Selected Short Fiction of Kate Chopin by Elkins- Livingstone, Miranda, M.A. 28/10/2019.

http://www.directessays.com/viepaper/1431.html.The Portrayal of Male Characters by Ernest Hemingway. 28/05/2020.

http://www.jstor.org/stable/189829. Bird, S.R. (1996). "Welcome to Men's Club: Homosociality and the Maintenance of Hegemonic Masculinity" Gender and Society. 15/06/2021.

.